

# Mwongozo wa Mdadisi

Utafiti wa Kufuatilia Kaya Tanzania (NPS 2014-15)

2014-2015



## **Yaliyomo**

<b>I. Dodoso la Kaya .....</b>	<b>4</b>
Utangulizi .....	5
Mwongozo kwa Ujumla Jinsi ya Kujaza Dodoso la Kaya .....	10
Orodha ya Wanakaya Iliyochapishwa .....	14
Sehemu A-1: Utambulisho wa Kaya.....	14
Sehemu A-2: Taarifa za Mdadisi na Msimamizi.....	16
Sehemu B: Taarifa za Wanakaya .....	16
Sehemu C: Elimu .....	19
Sehemu D: Afya .....	22
Sehemu E: Maswali ya Ajira na Kazi.....	27
Sehemu F: Matumizi ya Chakula Nje ya Kaya.....	33
Sehemu G: Mwonekanu Wa Ustawi Wa Maisha .....	34
Sehemu H: Uhakika wa Chakula .....	35
Sehemu I: Makazi, Maji na Usafi .....	36
Sehemu J: Matumizi ya Chakula kwa Wiki Moja Iliyopita .....	39
Sehemu K: Matumizi Yasiyo ya Chakula – Wiki Moja na Mwezi Moja .....	42
Sehemu L: Matumizi Yasiyo ya Chakula Miezi 12 Iliyopita .....	42
Sehemu M: Rasilimali za Kaya.....	43
Sehemu N: Shughuli za Kibiashara za Familia/Kaya Zisizo za Kilimo .....	43
Sehemu O: Misaada na Vikundi vya Kusaidiana .....	49
Sehemu P: Mikopo.....	50
Sehemu Q: Fedha.....	51
Sehemu R: Mishtuko/Maafa ya Karibuni kwa Ustawi wa Kaya.....	53
Sehemu S: Vifo katika Kaya.....	54
Sehemu U-1: Taarifa za Kuifuatilia Kaya.....	55
Sehemu U-2: Maswali ya Mchujo wa Sehemu ya Kilimo .....	55
Zawadi kwa Mhojiwa .....	56
Sehemu V: Vipimo vya Uzito na Urefu na Mzunguko wa Mkono wa Juu.....	56
BAADA YA KUMALIZA MAHOJIANO .....	59
<b>II. Dodoso la Kilimo .....</b>	<b>60</b>
Utangulizi .....	61
Sehemu A – 1: Utambulisho .....	61
Sehemu 1: Taarifa za Wanakaya.....	61
Sehemu 2: Orodha ya Mashamba .....	61
Maelezo ya Sehemu 2 – 7 .....	65
Watoa Huduma .....	69
Sehemu 3: Taarifa za Mashamba .....	70
Sehemu 4. Mazao Katika Shamba.....	82
Sehemu 5: Jumla ya Mauzo na Hifadhi ya Mazao katika Kaya.....	85
Sehemu 6. Mazao ya Kudumu & Miti ya Matunda katika Shamba .....	89
Sehemu 7. Mazao ya Kudumu na Miti ya Matunda .....	91
Sehemu 10. Bidhaa na Mabaki ya Mazao .....	94
Sehemu 11. Vifaa na Mitambo ya Kilimo.....	95

<b>Sehemu 12. Huduma za Ushauri wa Kilimo na Mifugo.....</b>	<b>96</b>
<b>III. Dodoso la Mifugo na Uvubi .....</b>	<b>98</b>
<b>Sehemu A1: Utambulisho wa Kaya .....</b>	<b>99</b>
<b>Sehemu 1: Taarifa za Mwakaya .....</b>	<b>99</b>
<b>Orodha ya Watoa Huduma .....</b>	<b>99</b>
<b>Sehemu ya 2: Mifugo .....</b>	<b>99</b>
<b>Sehemu ya 3: Afya ya Wanyama .....</b>	<b>104</b>
<b>Sehemu ya 4: Chakula cha Mifugo, Maji, Makazi na Uzalishaji.....</b>	<b>108</b>
<b>Sehemu ya 5: Nguvu Kazi kwa Wanyama .....</b>	<b>111</b>
<b>Sehemu ya 6: Maziwa .....</b>	<b>111</b>
<b>Sehemu ya 7: Wanyama Kazi na Kinyesi cha Wanyama .....</b>	<b>114</b>
<b>Sehemu ya 8: Bidhaa/Mazao Mengine Yatokanayo na Wanyama .....</b>	<b>114</b>
<b>Sehemu ya 9: Wanakaya Walioshiriki katika Uvubi .....</b>	<b>116</b>
<b>Sehemu ya 10: Nguvu Kazi ya Uvubi .....</b>	<b>117</b>
<b>Sehemu ya 11: Zana za Uvubi.....</b>	<b>119</b>
<b>Sehemu ya 12: Uzalishaji wa Samaki .....</b>	<b>121</b>
<b>Sehemu ya 13: Biashara ya Samaki.....</b>	<b>124</b>
<b>IV. Fomu ya Ufutiliaji.....</b>	<b>125</b>
<b>Itifaki za ufutiliaji .....</b>	<b>125</b>
<b>Fomu ya T-0 Iliyochapishwa Orodha ya Wanakaya .....</b>	<b>125</b>
<b>Fomu ya Kufutililia Kaya, T-1.....</b>	<b>132</b>
<b>Fomu ya Kufutililia Wanakaya, T-2.....</b>	<b>134</b>
<b>Mifano ya Ufutiliaji wa Kaya / Wanakaya.....</b>	<b>137</b>
<b>V. Dodoso la Jamii .....</b>	<b>143</b>
<b>Utangulizi .....</b>	<b>144</b>
<b>Sehemu CB: Upatikanaji wa Huduma Muhimu.....</b>	<b>144</b>
<b>Sehemu CC: Miradi ya Uwekezaji .....</b>	<b>144</b>
<b>Sehemu CD: Matumizi ya Ardhi .....</b>	<b>144</b>
<b>Sehemu CE: Demografi, Ardhi na Mifugo.....</b>	<b>145</b>
<b>Sehemu CF: Bei za Bidhaa .....</b>	<b>145</b>
<b>Sehemu CG: Vipimo vya Kienyeji.....</b>	<b>145</b>
<b>VI. Vipimo vya GPS.....</b>	<b>146</b>
<b>Jinsi ya Kuwashaa na Kutumia GPS .....</b>	<b>147</b>
<b>Matumizi ya Msingi .....</b>	<b>148</b>
<b>Jinsi ya Kuandika Majina ya Faili kwenye GPS.....</b>	<b>150</b>
<b>VII. Viambatanishi .....</b>	<b>152</b>
<b>Mageresho ya TASCO .....</b>	<b>153</b>
<b>Mageresho ya ISIC .....</b>	<b>157</b>
<b>Ubabilishaji wa Vipimo .....</b>	<b>160</b>
<b>Picha za Aina ya Vyoo .....</b>	<b>163</b>
<b>Picha za Utengenazaji wa Maji Salama ya Kunywa ya Kaya.....</b>	<b>171</b>
<b>Picha za Namna ya Kudhibiti Mmomonyoko wa Udongo / Njia za Uvunaji wa Maji ya Mvua .....</b>	<b>172</b>
<b>Picha za Aina ya Visima .....</b>	<b>168</b>
<b>Picha za Nembo za Urutubishaji .....</b>	<b>168</b>

# I. Dodoso la Kaya

---

# Utangulizi

---

Katika shughuli zozote za mipango, kwa mfano kutathmini maendeleo, kupima kiwango cha umaskini, kuweza kufutilia miundo iliyowekwa, n.k. takwimu zinahitajika. Utafiti wa kufutilia kaya ni mojawapo ya njia za kuweza kupata takwimu hizo. Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi una dhamira ya kukusanya na kuchanganua taarifa za kipato cha kaya kinachotumika kwa chakula na matumizi mengine. Kutokana na taarifa hizi tunaweza kutathmini matokeo ya sera mbalimbali zinazohusiana na watu.

## Madhumuni ya Utafiti

Lengo kuu la Utafiti wa kufutilia Kaya Tanzania bara na visiwani wa mwaka 2014/2015 ni kukusanya taarifa kutoka katika kaya binafsi zinazohusu Taarifa za Kaya, Elimu, Afya, Ajira na Kazi, mwonekano na ustawi wa maisha, Makazi, Maji na Usafi, Matumizi ya Chakula Ndani na Nje ya Kaya kwa Siku Saba, Matumizi Yasiyo ya Chakula (kwa wiki moja na mwezi mmoja na miezi 12 iliyopita) Rasilimali za Kaya, Shughuli za kaya, Vikundi vya Kusaidiana na Misaada, Mikopo, Fedha, Mshtuko/Maafa ya Karibuni kwa Ustawi wa Kaya, Vifo Katika Kaya, Taarifa za kusaidia kuifutilia kaya, Taarifa za kusaidia kutambua kaya, Maswali yahusuyo wanawake tu na vipimo vya uzito, urefu na mzunguko wa mkono wa juu kwa watoto chini ya miaka 5.

Aidha, madhumuni makuu ya Utafiti wa kufutilia Kaya wa mwaka 2014/15 Tanzania Bara na Visiwani ni yafuatayo:

- Kupata takwimu/taarifa sahihi juu ya kiwango cha matumizi ambapo takwimu hizi zinatumika katika kupima umaskini na uchambuzi wa kiwango/hali ya maisha kwa kipindi husika hususani katika ngazi ya kaya.
- Kuweka msingi katika kutambua viashiria vya msingi vya kiuchumi, ajira na ustawi wa jamii ambavyo vinatakiwa kufutiliwa kwa kipindi husika.
- Kupata makadirio ya jumla ya mwenendo wa matumizi ya kaya ili kuandaa bei óweighting systemö kwa ajili ya Fahirisi za bei (Consumer Price Index).
- Kutoa makadirio ya uchumi jumla (macroeconomic), hususani matumizi ya kaya kwa ajili ya takwimu za Pato la Taifa (Gross Domestic Product ó GDP).
- Kupata mwenendo wa matumizi ya moja kwa moja ya kaya ili kuwezesha uchambuzi wa hali ya soko.
- Kupata taarifa za umilikaji wa vifaa vya kudumu pamoja na nyenzo za uzalishaji wa kipato.

## Takwimu za Tafiti za Ufutiliaji (Panel)

Tafiti nyingi za kaya takwimu zinakusanya kwa kuhoji kaya tofauti kila mwaka wa utafiti. Hii kitaalamu inaitwa ócross-sectionalö. Katika utafiti huu ni tofauti kwa sababu kaya zilezile zitatemelewa kila mwaka wa utafiti. Kwa maana hiyo tutakusanya taarifa za hali ya maisha ya watu, na mabadiliko yake. Hii inatafanya utafiti kidogo kuwa mgumu, itachukua muda kutafuta kaya zilezile tulizohoji na kutafuta walipo baadhi ya kaya au wanakaya waliohama. Hii itafanya uchambuzi wa takwimu kuwa wa kina na kutambua ni jinsi gani baadhi ya matukio yana athiri kaya. Ni muhimu kufanya kila linalowezekana kumtafuta kila mwanakaya aliyepo kwenye orodha ya kaya. Si rahisi kutafuta kaya mbadala katika utafiti huu.

## Usiri

Taarifa zinazokusanya kutoka katika kaya pamoja na wanakaya zinatunzwa kwa usiri mkubwa kama inavyotakiwa kwa mujibu wa **Sheria ya Takwimu namba 1 ya mwaka 2002** na hazitakiwi kuonekana

na/au kutolewa kwa mtu ye yeyote asiyehusika na utafiti huu. Taarifa za kaya zote zitajumuishwa kwa pamoja na kuwekwa katika mchakato wa kuandaa ripoti ya kitakwimu ambayo inatumika kwa madhumuni ya kutayarisha mipango ya maendeleo.

**Ni muhimu sana mhojiwa kuhakikishiwa kwamba kila taarifa atakayotoa itatunzwa kwa usiri mkubwa na kutumika kwa ajili ya shughuli za kitakwimu pekee.**

## **Maana, Ufanuzi na Matumizi ya Baadhi ya Maneno**

Sehemu hii inaeleza na kufafanua maana ya baadhi ya maneno yaliyotumika katika madodoso pamoja na utafiti huu kwa ujumla:

- KAYA ó Kaya inahusisha watu wanaoishi pamoja, kuchangia mapato na kula kutoka katika chungu kimoja cha chakula.
- MKUU WA KAYA ó Mkuu wa kaya ni mwanakaya ambaye huwa ndiye anachukuliwa kama mtoa ushauri au uamuza muhimu katika kaya, na kwa kawaida hutambuliwa na wanakaya wengine kama mkuu wao wa kaya. Mara nyingi huyu huwa ni mtu ambaye ana jukumu la kuiangalia kaya kifedha pamoja na ustawi wa wanakaya kwa ujumla.
- MAKAZI YA KAYA ó Hii ni sehemu yote inayokaliwa/milikiwa na kaya moja bila kujali muonekano wa makazi hayo kwa nje. Inaweza kuwa ni chumba kimoja kinachokaliwa na wapangaji au inaweza kuwa ni jengo moja, mawili au zaidi yanayokaliwa na kaya.
- KIPATO CHA KAYA ó Hii inajumuisha:
  - a. Ujira, mishahara, bakshishi, n.k.
  - b. Faida kutokana na shughuli za kilimo na zisizo za kilimo.
  - c. Kipato kutokana na umilikaji wa rasilimali kama kodi, riba, gawiwo na mrabaha.
  - d. Uhamishaji wa fedha uliopokelewa kwa mfano misaada iliyopokelewa, malipo ya uzeeni, n.k.
  - e. Kipato kwa njia ya bidhaa/huduma: thamani ya bidhaa na huduma zilizopokelewa na kutumiwa (ikijumuisha thamani ya kodi kwa makazi binafsi au makazi ya bure kutoka kwingineko).
  - f. Pesa nyingine zinazopokelewa kama vile fidia ya bima, bahati nasibu pamoja na mapato mengine ya namna hiyo.
- MATUMIZI YA KAYA ó Hii inajumuisha:
  - a. Kiasi kilichotumika kununulia bidhaa na huduma kwa ajili ya maisha ya kila siku.
  - b. Thamani ya bidhaa na huduma zilizopokelewa na kutumiwa (ikijumuisha thamani ya kodi kwa makazi binafsi) matumizi ya bidhaa zilizozalishwa na kaya.
  - c. Kiasi kilichotumika kwa ajili ya kodi, michango, malipo ya bima, tiketi za bahati nasibu, riba juu ya mikopo pamoja na matumizi ya bidhaa zisizo za mlaji.

## **Utaratibu wa Kazi katika Vijiji/Maeneo ya Kuhesabia Watu**

Sehemu hii inatoa maelezo ya utendaji kazi ya Utafiti wa Kufuatilia Kaya Tanzania, 2014/15. Maelekezo na maelezo yanayotakiwa katika maeneo ya kazi (vijiji na maeneo ya kuhesabia) yanayotolewa hapa yanahusiana na utaratibu/mpangilio wa kazi, umuhimu wa kazi pamoja na vitendeza kazi, n.k. Wakati wa utekelezaji wa kazi hii na kama ilivyo katika kila kazi, matatizo mengi yanaweza kujitokeza na ambayo hayakuelezw hapa. Njia bora ya kushughulikia matatizo kama hayo

ni kwa wasimamizi wote kuwa na mawasiliano mazuri na ya mara kwa mara na Makao Makuu ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Dar es Salaam.

## **Vitu/Vifaa Muhimu kwa Utafiti**

Kila mdadisi atatakiwa kuwa na vitu/vifaa vifuatavyo:

- i. Kitambulisho.
- ii. Barua ya utambulisho.
- iii. Kitabu cha maelekezo kwa mdadisi na madososo.
- iv. Orodha ya kaya zilizochaguliwa katika kijiji/eneo la kuhesabia watu
- v. Dodoso.
- vi. Orodha iliyochapishwa taarifa za kaya.
- vii. Kalamu ya risasi, kifutio, kichongeo cha kalamu ya risasi.
- viii. Kibao cha kuandikia.
- ix. Daftari ya mazoezi.
- x. Mfuko wa nguo wa kupimia vitu.
- xi. Mzani wa kuningāiniza.
- xii. Mzani wa kupimia uzito.
- xiii. Mzani wa kupimia urefu.
- xiv. Mkeka mdogo wakulaza watoto wakati wa kupima.
- xv. Kipimo cha kupima sehemu ya juu ya mkono.
- xvi. Viatu vya mvua pamoja na koti la mvua (kwa ajili ya mdadisi).
- xvii. Wasimamizi pia watapewa baadhi ya vifaa hivi. Msimamizi atakuwa pia na orodha ya kaya za ziada.

Wadadisi na wasimamizi wanajukumu la kuhakikisha vifaa hivi vinatunzwa kwa kuwa havipatikani kiurahisi na hakutakuwa na vifaa vya ziada pindi vikiharibika.

### **Namna ya Kuingia Katika Kaya kwa Mara ya Kwanza**

Kabla ya kuanza mahojiano, mtendaji wa kijiji au wa mtaa atafahamishwa kuhusu utafiti. Kabla ya kuingia kwenye kaya, msimamizi atawatembelea watendaji wa kijiji/mwenyekiti/sheha na atawaonesha barua ya kujitambulisha pamoja na kitambulisho chake. Msimamizi atawaonyesha orodha ya majina ya kaya zilizohojiwa kipindi kilichopita. Kwa maeneo mapya ya utafiti kutakuwa na ramani za maeneo haya. Watendaji wa vijiji na mitaa wataambatana na mdadisi kwenda kumtambulisha katika kaya. Mdadisi atakuwa na jukumu la kujieleza mwenyewe kilichompeleka katika kaya ile. Kumbuka kuva nguo za heshima, na kuwa msafi na mwenye mwonekano mzuri. Wanawake/wasichana wanatakiwa kuwa na khanga au kitenge kwa ajili ya kujisitiri pindi ikibidi kuketi chini kwa kuwa si kaya zote zinakuwa na viti vya kukalia.

### **Nini cha Kufanya Ikiwa Kaya Haipatikani?**

Katika ufafiti huu tunahoji pia kaya zilezile zilizohojiwa katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita. Inawezekana kaya au mwanakaya asiwepo tena katika eneo la utafiti la awali. Kaya hii itafahamika kama ōkaya ya kufuatiliaö au ōkaya iliyogawanyikaö. Taarifa zaidi zitapatikana kuhusiana na kaya na kumweleza msimamizi/mdadisi nini cha kufanya.

### **Nini cha Kufanya Ikiwa Kaya Inakataa Kuhojiwa?**

Mdadisi anawajibika kufanya kila linalowezekana kuishawishi kaya kutoa ushirikiano unaotakiwa katika utafiti huu. Kaya zinatakiwa kufahamishwa kwamba utafiti huu ni kwa manufaa ya taifa. Ikiwa kaya bado inakataa kutoa ushirikiano jaribu kupata msaada kutoka kwa uongozi wa eneo husika katika eneo la utafiti. Kama kaya bado inakataa, mdadisi anatakiwa amfahamishe msimamizi wa kazi hii na ahakikishe anajaza taarifa za utambulisho wa kaya hiyo katika dodoso kama ambavyo inafanyika katika kaya inayotoa ushirikiano. Mdadisi anapaswa kuweka alama ya X katika kisanduku husika katika fomu ya T-0 kuonyesha kwamba kaya imekataa kuhojiwa.

### **Namna ya Kuhoji**

Jaza utambulisho wa kaya katika sehemu A-1: UTAMBULISHO WA KAYA. Mageresho ya Mkoa, Wilaya, Kata/Shehia na Eneo la kuhesabia (EA) utayapata kutoka kwa msimamizi wako, vilevile namba ya kaya, jina la mkuu wa kaya na orodha ya kaya nane zitakazohojiwa utapewa na msimamizi wako. Kumbuka NAMBA YA KAYA inapatikana kutoka orodha za kaya(katika fomu ya kuorodhesha kaya) katika kijiji au Eneo la kuhesabia (EA).

Ili kuufanya Utafiti wa Kufuatilia kaya (NPS) 2014/15 uwe wa mafanikio, utendaji na kujituma kwa wadadisi katika vijiji na maeneo pamoja na usimamizi wa karibu vinatakiwa kuzingatiwa. Jaribu kila linalowezekana kupata takwimu zilizo sahihi. Jitahidi kujenga uhusiano ulio mzuri na kaya zinazohusika. Jitahidi kuwa mwaminifu na kuonesha uaminifu wako katika kaya. Ikiwa unaahadi na kaya, hakikisha kufika katika kaya kwa muda mliokubaliana. Hakikisha unafanya kama ulivyo elekezwa kwa kuzingatia kuwa utatakiwa kurudi mara kadhaa katika kaya hii.

### **Majukumu ya Mdadisi**

Kama ilivyo kwenye miradi mingine ya utafiti, mdadisi ana jukumu muhimu sana katika utafiti huu. Jukumu la mdadisi ni kukusanya taarifa/takwimu zinazohitajika na ubora wa kazi yao unaonekana katika ubora wa taarifa anazokusanya. Hivyo, hatima ya utafiti inategemea zaidi jinsi mdadisi atakavyofanya/atavyotekeleza majukumu yake.

- i. Mdadisi anatakiwa kufuata kikamilifu maelekezo ya kazi yanayotolewa ili kufanikisha kazi hii.
- ii. Jenga mazingira ya kukubalika baina ya mdadisi na wahojiwa kwa lengo la kupata majibu yaliyo sahihi na kwa ukamilifu. Jaribu kujijengea mazingira ya kujiamini, na hili linawezekana kwa kuyazoea mazingira pamoja na tamaduni na tabia za jamii anayofanyia kazi.
- iii. Namna atavyoonekana kwa mara ya kwanza pamoja na kile atakachosema kwa mara ya kwanza vina uzito mkubwa katika namna mhojiwa atakavyotoa ushirikiano kwa utafiti huu.
- iv. Mdadisi anatakiwa kuwa mwenye ushawishi kwamba anafahamu sawia kile anachokifanya na ni kwa manufaa ya jamii/taifa. Usitaje au kuahidi msaada/manufaa ya mapema kabisa kutokana na utafiti huu, kwani kwa kufanya hivyo kutaathiri taarifa zitakazotolewa.
- v. Mdadisi anatakiwa kutamka na kusisitiza juu ya usiri wa utafiti huu. Mahojiano yanatakiwa kufanyika baina ya mhojiwa na mdadisi pekee. Kusiwe na mtu mwengine wa nje ya kaya husika wakati wa mahojiano isipokuwa kwa sababu za msingi na kwa ruhusa ya mkuu wa kaya/mhojiwa.
- vi. Mdadisi anatakiwa kufahamu kwamba katika mahojiano, tofauti na mazungumzo ya kawaida, kunakuwa na mtu anauliza maswali na mwengine anajibu maswali hayo, hivyo anatakiwa kujiepusha kutoa maoni yake binafsi. Mdadisi hatakiwi kukasirika au kutookubaliana na kile anachosema mhojiwa, mdadisi anatakiwa kutokuegemea upande wowote.
- vii. Ikiwa mhojiwa anasita kujibu swali, jaribu kuikabili hali hiyo kwa kueleza upya madhumuni ya utafiti pamoja na usiri unaoambatana na taarifa zinazotolewa. Mdadisi hatakiwi kulazimisha sana kupatiwa jibu. Kumbuka mhojiwa hatalazimishwa kutoa majibu.
- viii. Kutakuwa na msururu wa maswali, kwa hiyo unapaswa kufuata mtiririko wake na kuumudu ipasavyo. Hii ina maana kwamba unapaswa kumiliki shauku au matakwa ya mhojiwa katika muda wote wa mahojiano. Kama mhojiwa anakupa majibu yasiyolingana na swali au anakupa maelezo marefu, usimkatishe kauli haraka, msikilize mpaka mwisho, halafu jaribu kumrudisha kwa upole katika swali kama ilivyo katika dodoso.

- ix. Unatakiwa kuripoti kwa msimamizi mara unapohitajika kurudi kwenye kaya ili kumwezesha msimamizi kupanga vizuri ratiba ya siku inayofuata.
- x. Mapatano ya awali juu ya muda wa kufanya mahojiano na mhojiwa ni muhimu. Mdadisi ajitahidi kuwaona wahojija katika muda ambao wameuona unafaa kwao.

Usisahau kuwa kama mdadisi utashindwa kabisa katika jambo lolote, basi uombe msaada wa msimamizi ambaye mara nyingi atakuwa karibu nawe. Kumbuka usimamizi kwa kazi ya mdadisi ni kiungo muhimu na cha lazima ili kuweza kupata takwimu bora na sahihi.

**Kumbuka:-** yaliyoelezwa hapo juu ni wajibu wa wadadisi, shughuli na hatua za utafiti wa Kufuatilia kaya Tanzania (NPS 2014/2015) pamoja na tafiti nyingine zinazohusisha kaya binafsi.

## Dodoso

Madodoso yatakayohusika ni manne:

- 1: Dodoso la Taarifa za Kaya.
- 2: Dodoso la Kilimo.
- 3: Dodoso la Mifugo na Uvuvi.
- 4: Dodoso la Jamii (Dodoso hili litahojija na msimamizi mwenywewe).

**Aina ya Kwanza:** Taarifa za Kaya zinazohusu Jamii, Elimu, Afya, Ajira na Kazi, Chakula Nje ya Kaya, Makazi, Maji na Usafi, Mwonekano wa Ustawi wa Maisha, uhakika wa chakula, Matumizi ya Chakula kwa Wiki Moja Iliyopita, Matumizi ya Chakula Nje ya Kaya, Matumizi Yasiyo ya Chakula(wiki moja iliyopita & mwezi mmoja uliopita), Matumizi Yasiyo ya Chakula (miezi 12 iliyopita), Rasilimali za Kaya, Shughuli za kaya, Misaada na Vikundi vya Kusaidiana, Mikopo, Fedha, Mshtuko/Maafa ya Karibuni kwa Ustawi wa Kaya, Vifo katika Kaya, Maswali Yahusuyo Wanawake, Vipimo vya Uzito na Urefu. n.k.

**Aina ya Pili:** Taarifa za shughuli za kilimo za kaya binafsi. Ina maswali yanayohusu shughuli za kilimo kama ramani ya shamba, idadi ya mashamba, mazao katika shamba, uzalishaji na uuzaji mazao, pembejeo, vifaa na mitambo ya kilimo, mikopo n.k.

**Aina ya Tatu:** Dodoso la Mifugo na Uvuvi limegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza ya dodoso ina maswali yanayohusu kiasi cha mifugo inayomilikiwa na kaya, afya ya wanyama, chakula, nguvu kazi na mazao yatokanayo na wanyama. Sehemu ya pili inahusu shughuli za uvuvi, utayarishaji wa samaki na biashara ya samaki. Pia inajumuisha maswali ya pembejeo, ajira, mauzo na matumizi.

**Aina ya Nne:** Taarifa za upatikanaji wa huduma muhimu za jamii, miradi ya uwekezaji katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, matumizi ya ardhi, kilimo kijijini, demografia na taarifa za bei.

# Mwongozo kwa Ujumla Jinsi ya Kujaza Dodoso la Kaya

## Mwongozo kwa Ujumla

Kitu muhimu cha kukumbuka wakati wa kujaza dodoso ni kuandika kwa usahihi na uangalifu. Taarifa hizo zitamwezesha muingiza data kuingiza kwa usahihi katika computer. Kama taarifa zilizokusanya haziko sahihi hii itafanya programu kuzikataa na kufanya timu nzima kusimama mpaka makosa yarekebishwe, na itaharibu ratiba nzima.

Maswali yote yasomwe kama yalivyoandikwa. Mdadisi asiulize anavyotaka yeye labda pale mhojiwa asipoelewa mdadisi anatakiwa kutoa maelezo ya kumuelewesha mhojiwa. Katika hali hii unatakiwa kutoa maelezo pasipo kubadilisha maana ya swali. Hii ni muhimu kuwa kila mhojiwa atajibu maswali kwa mujibu wa utafiti.

## Muundo wa Dodoso

Dodoso la kaya lipo katika muundo ufuatao:

**Safu wima:** Katika muundo huu maswali na majibu yake ya kila swali yanapatikana katika safu wima husika. Mfano wa huu ni sehemu I: Makazi, Maji na Usafi majibu yanahu kaya nzima.

**Safu wima na safu mstari:** katika muundo unatumika kupata majibu ya kila mtu katika kaya. Swali lipo katika safu wima na majibu yanaandikwa katika safu mstari. Mfano ni sehemu D: Afya majibu yote ya wanakaya yanaandikwa katika safu mstari ya kila mwanakaya kwa swali.

### Karatasi ya Kukunja (Flap)

Kila dodoso kuna kikaratasi cha kukunja unatakiwa kuandika jina, jinsi, umri wa kila mwanakaya kama ilivyo katika sehemu B: Pia kikaratasi hiki cha kukunja kina maswali manne ambayo yatasaidia kujaza baadhi ya maswali ya sehemu E: Ajira, maelezo zaidi yatasolewa namna ya kujaza maswali haya manne. Taarifa za wanakaya yaani safu mlalo 12 katika sehemu B ziwe sawasawa na katika karatasi ya kukunja. Unapokunjua kikaratasi namba zake ziwe sawa na safu mlalo nydingine. Dodoso la kilimo lina karatasi za kukunja kwa sehemu ya 3, 4 na 5. Tumia vizuri kikaratasi cha kukunja kila unapo jaza dodoso ili uweze kujibu mswali kwa kila mwanakaya.



## Maswali ya Kuruka

Popote katika dodoso utakutana na geresho lenye kukuhitaji kwenda swali njingine badala ya swali linalofuata, zingatia hilo kwa mfano mhojiwa hakuwahi kwenda shule huitaji kumuuliza alianza shule akiwa na umri gani au amefika kiwango gani cha elimu. Kwahiyoo utahitajika kuruka baadhi ya maswali, kulingana na mfano wetu upande wa kulia kama mhojiwa hakuwahi kwenda shule jibu ni hapana unatakiwa kwenda swali la 29. Kwahiyoo maswali baada ya swali la 3 yatakuwa wazi. Hii ni aina ya kwanza ya maswali ya kuruka.

3. Je, [JINA] amewahi kusoma shule?	4. Je, [JINA] alianza shule akiwa na miaka mingapi?	3. Je, [JINA] amewahi kusoma shule?	4. Je, [JINA] alianza shule akiwa na miaka mingapi?
NDIYO..1 HAPANA..2 (►29)		NDIYO..1 HAPANA..2 (►29)	
	UMRI		UMRI

Aina nyingine ya kuruka utakayokuta kwenye dodoso ni ōmiruko isiyo na masharti.ö Mageresho haya ni rahisi kuyaona kwa sababu yana visanduku. Katika miruko isiyo na masharti, bila kujali chochote anachosema anayehojoja, unapaswa kwenda swali lilionyeshwa. Katika mfano wetu, unapaswa kwenda swali la 22, kwa mwaka wowote anaosema unayemhoji. Maswali yote ambayo hayajibowi kutokana na kuyaruka, au mtiririko wa maswali yanapaswa kuachwa wazi ó hakuna taarifa zitakazoandikwa.

## Jinsi ya Kujaza Sehemu C – F:

Maswali katika sehemu hizi asomewe mwanakaya mmoja mmoja kwa kila swali kabla ya kuhamia mwanakaya mwingine. Kwa mfano, katika kaya kuna wanakaya watatu (3): Julius, Mary na Alli. Utaanza kumhoji Julius baada ya kuorodhesha majina ya wanakaya wote.

- Kamilisha maswali yote katika Sehemu C kwa ajili ya Julius
- Kamilisha maswali yote katika Sehemu D kwa ajili ya Julius
- Kamilisha maswali yote katika Sehemu E kwa ajili ya Julius
- Kamilisha maswali yote katika Sehemu F kwa ajili ya Julius

Kisha kama utaweza kumpata na kumhoji Mary:

- Kamilisha maswali yote katika Sehemu C kwa ajili ya Mary
- Kamilisha maswali yote katika Sehemu D kwa ajili ya Mary
- Kamilisha maswali yote katika Sehemu E kwa ajili ya Mary
- Kamilisha maswali yote katika Sehemu F kwa ajili ya Mary
- Angali kama Mary anastahili kuulizwa sehemu G & I. Kama hastahili kamilisha sehemu anazostahili.

**ONYO:** Usikamilishe ukurasa wa kwanza sehemu C (Swali 1-9) kwa Julius, kisha ukamhoji Mary ukurasa huohuo wa kwanza sehemu C! Kukamilisha sehemu kwa mtu kabla au kwenda sehemu kwa mtu huyo au kuuliza sehemu hiyo kwa mtu tofauti, Ni kuchanganya mhojiwa na mdadisi!

**Majibu ya Nyingine:** Ikiwa muhojiwa amesema öNyingineö unatakiwa kujaza geresho la nyingine katika swali hilo na kuandika alichosema muhojiwa: Kwa mfano Sehemu C swali la 18. Kwa sababu gani [JINA] hakuhudhuria shulen? Muhojiwa amejibu alisafiri na familia kimatembezi Dar es Salaam!



**1994**

Sehemu C	
18. Kwa sababu gani [JINA] hakuhudhuria shulen?	
SIKUKUU . . . . .	1
SHULE ILIFUNGWA KWA	
DHARURA . . . . .	2
SHULE ILIFUNGWA KWA	
KAWAIDA . . . . .	3
WALIMU HAWAKUWEPO . . . .	4
ALIKUWA MGONJWA . . . . .	5
MWANAKAYA MGONJWA . . . .	6
MAZISHI . . . . .	7
HATUA YA NIDHAMU . . . . .	8
HAKULIPA GHARAMA . . . . .	9
ALIKATAA KWENDA . . . . .	10
ALIKUWA NA KAZI . . . . .	11
NYINGINE (TAJA) . . . . .	12
<b>12 amekwenda kimatembezi Dar</b>	

**Majibu ya sifuri:** Kwa majibu ambayo yanahitaji kutaja kiasi cha fedha na kama hakuna kiasi chochote kilichotumika kwa swali hilo weka õoõ.

Mfano: Mr. Ali amejibu hajatumia kiasi chochote kwa ajili ya kupumzishwa kwenye sehemu ya kutolea huduma za kiroho au kwa mganga wa jadi. Andika õoõ.

Hairuhusiwi kamwe kuacha maswali wazi kwa maswali ambayo hayapaswi kuacha wazi kwa sababu ya mruko. Kama mhojiwa hafahamu, dadisi kupata taarifa zinazotakiwa. Kama baada ya kuhoji mhojiwa bado anasema hafahamu, andika -99ø katika dodoso kuliko kuacha wazi. Tambua kuwa, -99ø haiwezi kutumika kwenye uchambuzi wa taarifa, hivyo juhudhi zote lazima zifanyike ili kupunguza majibu ya aina hii.

**SAHIHI:** Weka O

**SI SAHIHI :** õ õ

**SI SAHIHI :** õô õ

Sehemu D	Sehemu D	Sehemu D
15. Katika kipindi cha miezi 12 iliyopita ni kiasi gani cha gharama kwa ujumla kilitumika kwa ajili ya [JINA] kupumzishwa kwa mganga wa jadi au mtoa huduma za kiroho/kiimani? <b>JUMUISHA</b> <b>MAKISIO YA</b> <b>THAMANI YA</b> <b>MALIPO KWA</b> <b>NJIA</b> <b>YA VITU AU</b> <b>HUDUMA.</b>  <b>SHILINGI</b>	15. Katika kipindi cha miezi 12 iliyopita ni kiasi gani cha gharama kwa ujumla kilitumika kwa ajili ya [JINA] kupumzishwa kwa mganga wa jadi au mtoa huduma za kiroho/kiimani? <b>JUMUISHA</b> <b>MAKISIO YA</b> <b>THAMANI YA</b> <b>MALIPO KWA</b> <b>NJIA</b> <b>YA VITU AU</b> <b>HUDUMA.</b>  <b>SHILINGI</b>	15. Katika kipindi cha miezi 12 iliyopita ni kiasi gani cha gharama kwa ujumla kilitumika kwa ajili ya [JINA] kupumzishwa kwa mganga wa jadi au mtoa huduma za kiroho/kiimani? <b>JUMUISHA</b> <b>MAKISIO YA</b> <b>THAMANI YA</b> <b>MALIPO KWA</b> <b>NJIA</b> <b>YA VITU AU</b> <b>HUDUMA.</b>  <b>SHILINGI</b>
0		--

**Kusoma Dodoso:** Mdadisi hatakiwi kuuliza sentensi/maneno yaliyoandikwa kwa HERUFI KUBWA. Haya ni maelekezo kwa mdadisi au ni majibu ya swali. Kwa mfano: Usisome yafuatayo kwa mhojiwa. Badala yake angalia orodha ya wanakaya na andika jibu sahihi kwa swali hili.

Kwa mfano: Kwa Sehemu B Swali la 28, unatakiwa kusoma swali tu, sio

kusoma majibu yake kwa mhojiwa.

1. JE, MHOJIWA ANAJIBU MASWALI MWENYEWE?	21. JE, [JINA] NI MWANAMKE WA UMRI KATI YA MIAKA 12 HADI 49?
NDIYO..1 HAPANA..2  (►Sw. 27)	NDIYO..1 HAPANA..2

**SEHEMU B**

28.
Je, ni nini sababu za [JINA] kuhamia hapa?
KIKAZI.....1
MASOMO.....2
NDOA.....3
SABABU
NYINGINE ZA
KIFAMILIA...4
MAKAZI/HUDUMA
NZURI.....5
ARDHI.....6
NYINGINE
(TAJA).....7

**Majibu yanayohusu terehe:** Wakati wa kuandika matukio ya mwezi au mwaka. Sheria zifuatazo zinatumika:

- Kalenda ya mwezi: andika tarakimu 1-2. Usiandike jina la mwezi.
- Kalenda ya mwaka: kwa kawaida ni tarakimu 4 .

SAHIHI		SI SAHIHI	
SEHEMU O		11.	
13.		Je, Ni lini mara ya mwisho [JINA] alichukua mkopo?	
MWEZI	MWAKA	MWEZI	MWAKA
7	2012	July	Mwaka huu

**Siku 7 zilizopita:** Kwa maswali yanayouliza taarifa za siku 7 zilizopita, rejea katika siku 7 za karibuni. Kwa mfano: Kama mahojiano ni jumattu, siku 7 zilizopita ni kuanzia Jumatatu mpaka Jumapili (jana).

**Desimali:** Kama utatakiwa kuandika kiasi chini ya 1, inabidi kuandika katika decimali. Hakikisha kuandika katika decimali dodoso vizuri kama 3.5. Usiandike katika sehemu. Kwa mfano usiandike  $3\frac{1}{2}$ .

**Kiasi cha pesa:** Wakati majibu yanayohitaji kiasi/viwango, andika kiwango kilichosahihi panapostahili. Viwango vyote vya kiasi/fedha viwe katika shillingi ya Tanzania. Kwa mfano amejibu \$50 (US dollars), tumia viwango vya fedha vya karibuni kubadilisha kwenda shillingi za Kitanzania. Kama huna uhakika muone msimamizi wako. Andika kiasi cha fedha katika kiwango cha Tanzania shillingi usiweke decimali. Usiweke senti. Kwa kiwango chini ya shillingi 1 weka katika makadirio ya karibu. Kwa kiwango zaidi ya 1,000 weka koma.

SEHEMU 'K'			
GERESHO	1. Je, katika kipindi cha siku 7 zilizopita, mlinunua au kugharamia vitu vifuatavyo?	NDIYO....1 HAPANA....2 (►KITU KINGINE	2. Je, ni kiasi gani mlilipa kwa jumla?
101	Sigara au tumbaku	1	SHILINGI
			SAHIHI
101	Sigara au tumbaku	1	3,400
101	Sigara au tumbaku	1	3,400/=
101	Sigara au tumbaku	1	3,400 Tsh
			SIO SAHIHI

**Maoni Juu ya Mahojiano:** Unatakiwa kuandika vidokezo muhimu kuhusu mahojiano yalivyokwenda katika kisanduku cha maoni ukurasa wa pili wa dodoso. Unaweza kuandika vidokezo muhimu kwa ajili yako pembeni mwa ukurasa ili kukusaidia katika kusahihisha dodoso baadae. Yale Maoni muhimu ambayo unataka msimamiziayaone andika ukurasa wa pili katika kisanduku cha Maoni.

# Orodha ya Wanakaya Iliyochapishwa (T-0)

---

Kwa kila kaya iliyotembelewa wakati wa utafiti uliopita, kutakuwa na fomu ilichapishwa yenyе taarifa za kuweza kutambua mahali kaya ilipo, fomu hii inaitwa T-0. Fomu hii itakuelekeza namna ya kujaza wanakaya waliopo kwenye kaya na jinsi ya kujaza fomu nyingine kwa wanakaya waliohama kwenye kaya hiyo. Sehemu ya kufuatilia kaya au wanakaya imemeleza kurasa za mbele katika muongozo huu. Cha muhimu ni utambulisho wa kaya wa kaya ya awali. (andika kwa usahihi na uangalifu katika dodoso la kaya) na orodha ya awali ya wanakaya (unachotakiwa kujaza mpaka swali la 6 sehemu B).

## Kaya Mpya

**Katika awamu hii ya utafiti wa ufatiliaji wa kaya, sio kaya zote zitakuwa na wanakaya ambao walifanyiwa mahojiano katika awamu iliyopita ya utafiti huu. Kutakuwa na ongezeko la kaya mpya ambazo kamwe hazijawahi kuhojiwa katika awamu yoyote iliyopita ya utafiti huu. Kaya hizi mpya hazitakuwa na fomu za T-0. Kaya mpya zitachaguliwa kwa kutumia bahati nasibu kutoka kwenye orodha ya kaya ndani ya eneo la kuhesabia watu (EA/Cluster). Timu itatengeneza orodha hii ya kaya kupitia zoezi la uorodheshaji pindi wanapoanza eneo jipy a mbalo halikuwa katika awamu iliyopita ya Utafiti wa Kufuatilia Kaya.**

## Sehemu A-1: Utambulisho wa Kaya

---

Katika utambulisho tunaanza na jina la mkoa na geresho lake, (geresho la mkoa lina tarakimu mbili, mfano mkoa wa Dodoma geresho lake ni  $0^{\circ}01^{\prime}$ , Arusha ni  $0^{\circ}02^{\prime}$  hadi mkoa wa mwisho amba ni Geita geresho lake ni  $0^{\circ}21^{\prime}$  kwa Tanzania Bara na Kaskazini Unguja  $-51^{\prime}$  hadi Kusini Pemba  $-55^{\prime}$ ). Yanafuata majina ya wilaya, kata na kijiji/EA na mageresho yake. Mageresho yote haya ni kama yalivyoorodheshwa kwenye Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 Tanzania.

Utambulisho wote kuanzia mkoa hadi vijiji unategemea jinsi ulivyoandikwa katika Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 ukiacha namba ya kaya na jina la mkuu wa kaya ambayo mdadisi atapewa na msimamizi wake.

Mageresho ya vijiji/mtaa yatakuwa na tarakimu 2 na maeneo kuhesabia watu (EAs) yana tarakimu 3 na katika hali ya kawaida geresho la kijiji linaanza na tarakimu 0 ikifuatiwa na namba halisi. Namba ya kaya iliyochaguliwa itakuwa na tarakimu 4 na inatokana na namna kaya zilivyoorodheshwa wakati wa zoezi la kuorodhesha kaya katika kila kijiji kilichochaguliwa pamoja na maeneo ya mjini yaliyochaguliwa.

Ukiangalia upande wa kulia wa sehemu ya utambulisho wa kaya, utaona kisanduku chenye maneno; andika  $\rightarrow$  katika chumba na idadi ya fomu hapo chini iwapo utatumia fomu zaidi ya hii kuandika taarifa za kaya hakikisha unaandika vivyo hivyo kwenye fomu zote zitakazotumika kwa kaya hii.

Fomu ya \_\_\_\_\_ Kat i ya Jumla ya fomu \_\_\_\_\_

Iwapo umetumia fomu zaidi ya moja, unatakiwa kuandika  $\rightarrow$ X $\rightarrow$ ndani ya kisanduku kidogo kilicho kulia mwa ukurasa huu wa utambulisho. Pia utatakiwa kuandika ni fomu ya ngapi kati ya jumla ya fomu zote ulizotumia. Mfano: kama umetumia jumla ya fomu 4, fomu ya kwanza utaandika [FOMU YA 1 kati ya fomu 4 kwa ujumla] n.k.

**KIPENGELE 7:** Andika jina la mkuu wa kaya ambaye anategemewa kuwa ni mwanakaya namba moja katika orodha ya wanakaya, kama mkuu wa kaya ni yuleyule aliyehojoja kipindi kilichopita swali la 9 litakuwa sawa na hili. Kama kuna mabadiliko andika mkuu wa kaya mpya.

**KIPENGELE 7.1:** Katika awamu hii ya NPS, kutakuwa na kaya mpya ambazo hazikuwapo katika awamu iliyopita ya NPS (2012/2013). Ikiwa kaya ilihojiwa katika NPS 2012/2013, weka geresho 1. Ikiwa kaya ni mpya na haikuhojiwa katika NPS 2012/2013, weka gersho 2 na nenda swali la 13.

**KIPENGELE 8:** Andika jina halisi la mkuu wa kaya pindi kaya ilipotembelewa mwaka 2012/2013 hata kama mtu huyu si mwanakaya tena. Taarifa hizi zitapatikana kwenye karatasi ya ḥrosterø ya kaya utakayopewa ambayo utaendanayo kwenye kaya.

**KIPENGELE 9:** Nakili tarakimu 7 za utambulisho wa kaya kutoka kwenye karatasi ya ḥrosterø ya kaya uliyopewa. Namba hizi ziwe sawa na ulizopewa kwenye karatasi hata kama kaya imehamia sehemu nyinyine. Ni muhimu sana kunakili namba hizi kwa usahihi kwani itasaidia kuoanisha takwimu za miaka tofauti tofauti ya utafiti.

**KIPENGELE 10:** Kama kaya hii ni kaya ile ile iliyotembelewa utafiti uliopita, andika 1, kama ni kaya iliyogawanyika kutoka katika kaya ya awali andika 2.

**KIPENGELE 11:** Kama kaya bado makazi yake ni nyumba ile ile ya awali ilipotembelewa awamu iliyopita ya utafiti, andika 1, na uende kipengele la 14. Kama kaya imehamia sehemu nyininge ambapo ni umbali ulio chini ya saa moja ndani ya eneo hilohilo kaya hiyo itakuwa ni ya kufatilia ndani ya eneo hilohilo, andika 2. Kama kaya imehamia sehemu nyininge umbali unaozidi saa moja, kaya hii itakuwa ni ya kufatilia nje ya eneo la awali ḥ-distance tracking andika 3.

**KIPENGELE 12:** Kama kaya imehama kwenye eneo la awali, andika jina la anayefuatihi katika kaya. Kama kaya ni ileile ya awali anayefuatihi atakuwa mkuu wa kaya. Kama kaya imegawanyika wanaofuatihi wataaandikwa kwenye fomu ya T-2 (fomu ya ufutiliaji) itakayowezesha kufatilia kaya.

**KIPENGELE 13:** Andika namba ya chini(ndogo) ya Roster ID kutoka Sehemu ya B, Swali 6. Swali hili litajazwa baada ya kumaliza mahojiano katika dodoso la kaya. **Mfano:** Kama Sehemu B, Swali 6 lina Roster ID 02 na 05, hivyo 02 ndiyo itakuwa namba ya chini (ndogo) itakayojazwa katika swali hili.

Kama mwanakaya alikuwepo mwaka wa 1 wa utafiti na hakupatikana mwaka wa 2, atakuwa na Roster ID yenye tarakimu 3 kwenye T-0. **Mfano:** Mtu alikuwa na Roster ID 02 mwaka wa 1 na hakupatikana mwaka wa mwisho wa utafiti, Mwaka huu (2014/15) kwenye Roster ID atakuwa na geresho 102 kwenye T-0. Kama mwanakaya atakutwa na wanakaya wote wapya, kwamba kaya yake iligawanyika,namba 102 itarekodiwa katika swali la 14 kama namba ya chini (ndogo) kutoka Sehemu B, Swali 6.

Vivyo hivyo,kaya zote zenye wanakaya wote walio wapya,watakuwa na geresho 99 kwenye T-0 katika Swali la 6, Sehemu B. **Kwa hiyo kwa kaya zote mpya, katika swali la 14 jaza ‘001’, geresho 99 lisitokee hapa.**

**KIPENGELE 14:** Utaandika namba ya nyumba kama ipo, kama hakuna andika maelezo ya mahali kaya inapoishi andika vidokezo muhimu vya nyumba kama vile: jina la mkuu wa kaya ya jirani na anuani ya kudumu, namba ya simu kama ipo kama jina maarufu la jirani, shule, kituo cha polisi, kanisa, msikiti, jina la mtaa/kitongoji. Maelezo hayo yatosheleze kuelekeza jinsi ya kuifikia kaya husika kwa mtu ambaye hajui kaya ilipo, taarifa hizi zitatumika mara kwa mara wakati wa utafiti.

# **Sehemu A-2: Taarifa za Mdadisi na Msimamizi**

---

**KIPENGELE 15:** Andika jina lako kamili (Jina kamili la mdadisi).

**KIPENGELE 16:** Jaza namba yako, kila mdadisi atapewa namba, na anatakiwa kuitambua namba yake bila kuikosea na kujaza namba hii katika madodoso atakayoyatumia kama ilivyoelekezwa.

**KIPENGELE 17:** Andika muda ambao umeanza mahojiano na mwanakaya. Muda huo uandikwe kwa lugha ya kiswahili. Pia ukumbuke kuandika muda mara tu utakapomaliza mahojiano katika kisanduku kilicho mwishoni mwa dodoso.

**KIPENGELE 18:** Unatakiwa kuandika tarehe husika uliyofanya mahojiano na mwanakaya, ukianzia na siku, mwezi na mwaka.

**KIPENGELE 19, 20 na 21:** Kipengele hiki kinamhusu msimamizi tu. Anatakiwa kuandika jina lake kwa ufasaha, namba yake atakayokuwa amepewa na tarehe ya ukaguzi wa dodoso.

**KIPENGELE 22, 23 na 24:** Kipengele hiki kinamhusu mwingizaji wa taarifa aliye kwenye EA. Anatakiwa kujaza jina lake kwa ufasaha, namba yake ya utambulisho na tarehe ya kuingiza taarifa hizi.

**KIPENGELE 25 na 26:** Kipengele hiki kinamhusu mwingizaji wa taarifa makao makuu. Anatakiwa kujaza namba yake ya utambulisho na tarehe ya kuingiza taarifa hizi.

## **MAONI YA MDADISI JUU YA MAHOJIANO**

Ukiangalia kulia mwa ukurasa huu uitaona kisanduku kikubwa, katika kisanduku hicho kinakukumbusha kuandika maoni juu ya mahojiano, andika vidokezo muhimu kuhusu mahojiano yalivyokwenda. Pia andika taarifa muhimu zitakazomsaidia msimamizi pamoja na mchambuzi wa dodoso. Ikumbukwe kuwa sehemu hii inajazwa baada ya mahojiano kukamilika.

## **KUJITAMBULISHA KWENYE KAYAITAKAYOHOJIWA**

Mdadisi msomee mhojiwa ujumbe huu kwa ufasaha na kwa kujiamini. Mpe nafasi ya kuuliza swali kabla ya kuendelea na maswali yanayofuata. Baada ya mhojiwa kuuliza maswali kama yatakuwepo. Mwelezee kwa ufupi baadhi ya yaliyomo katika dodoso hili, kama vile: elimu, afya, ajira n.k, kuna aina tofauti ya kujitambulisha na unatakiwa kuchukua moja wapo ambayo itafaa kwa kaya utakayoihoji. Ikiwa kaya ni mpya na haikuwepo katika awamu iliyopita ya NPS, inatakiwa kuitwa òKaya Mpyao. Kama kaya ilihojiwa awamu iliyopita ya utafiti na hajigawanyika itatambulika inaitwa òKaya ya NPSö na kama kaya imegawanyika itaitwa òKaya Iliyogawanyikaö na utasoma sehemu ya ujumbe ya kaya zilizogawanyika. Kwa hiyo kaya zote zisikie sehemu zote za kipengele hiki kabla ya kuanza mahojiano.

# **Sehemu B: Taarifa za Wanakaya**

---

Unatakiwa kujaza swali la 1-6 kwa wanakaya wote kabla ya kuendelea na maswali mengine. Na pia jaza kikaratasi kilichokunjwa (Flap).

**Safuwima 1 (Swali la 1):** Orodhesha watu wote katika kaya ambao kwa kawaishi kwenye kaya hii ukianza na mkuu wa kaya, akifuatiwa na mwenzi wake (kama yupo), watoto, wazazi, bila kuwasahau watoto wachanga, ndugu na watumishi wa nyumbani. Unatakiwa kuorodhesha majina ya watu wanaoishi, kuchangia pato na kula pamoja kila siku katika kaya. Msomee majina mhojiwa ili kuhakikisha kuwa watu wote waemeorodhesha.

**Safuwima 2 (Swali la 2):** Geresho la jinsia ni aidha 1 kwa Mwanaume au 2 kwa Mwanamke. Swali hili ni muhimu kama yalivyo mengine kwa wanakaya wote walioorodheshwa. Hakikisha unaulizia jinsia ya mwanakaya. Usijaribu kubuni jinsia ya mwanakaya kwa kuangalia jina, kwani majina mengine yanatumika kwa jinsia zote mbili. Mfano Tumaini, Bahati, Happy anaweza kuwa mwanamke au mwanaume. Pia kwa watoto wadogo ni vyema kuulizia hata kama unamuona; ni vigumu kujua kama ni msichana au mvulana kwani hata nguo anaweza kuvalishwa zozote. Mdadisi unatakiwa kuainisha kwa ufasaha jinsi ya jina husika na epuka kukosea kwani kwa kufanya hivyo utapotosha mahojiano yanayoendelea.

**Safuwima 3 (swali 3):** Je, ni mwaka na mwezi gani [JINA] alizaliwa? Unatakiwa kujaza kwa ufasaha mwaka na mwezi aliozaliwa jina, na ikumbukwe kuwa mwaka huo uwe na tarakimu nne. Kwa mfano; Mwakanjenje alizaliwa mwaka 1950. Kama atakuwa hakumbuki/hajui mwezi utajaza -99ø katika safuwima ya mwezi.

Inawezekana mwanakaya hajui mwaka wa kuzaliwa. Hivyo mdadisi ajaribu kutumia matukio yaliyoorodheshwa hapa chini ili kumsaidia mhojiwa kukadiria umri wake.

Tukio	Mwaka
Kuanza vita kuu ya 1 ya dunia	1914
Mwisho wa vita kuu ya 1 ya dunia	1918
Kuanza kwa utawala wa Waingereza Tanganyika	1919
Kuanza kwa vita kuu ya 2 ya dunia	1938
Mwisho wa vita kuu ya pili ya dunia	1945
Kuzaliwa kwa TANU	1954
Uhuru wa Tanganyika	1961
Mapinduzi ya Zanzibar	1964
Azimio la Arusha	1967
Kuzaliwa kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM)	1977
Vita vya Kagera	1978
Kustaafu raisi wa kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania	1985

**Safuwima 4 (swali 4):** (JINA) ana umri gani? Ingiza umri wa wanakaya wote kwa kutumia tarakimu mbili. Ikiwa umri ni chini ya mwaka 1 andika '00' na ikiwa ni ana miaka 98 na zaidi andika -98ø Lazima uonyeshe kwamba kuna uwiano kati ya mwaka ulioorodhesha na swali lililopita. Linganisha taarifa na orodha ya kaya iliyochapishwa, kama kuna tofauti dodoso zaidi upate taarifa za uakika za wanakaya. Na weka maoni kama taarifa zilizochapishwa ni sahihi.

**Safuwima 5 (Swali la 5):** Ni nini uhusiano wa [JINA] na Mkuu wa Kaya? Ingiza geresho linalohusika la uhusiano wa mwanakaya na mkuu wa kaya. Ingiza geresho kama ilivyoonyeshwa kwenye dodoso, ni geresho lenye tarakimu moja kwa mfano (11 .10) kwenye sehemu inayohusika. Angalia kuwa watumishi wa nyumbani watakaojumuishwa hapa ni wale amba wanakula katika makazi ya kaya hiyo na wanamkulali mkuu wa kaya hiyo kama mkuu wao wa kaya. Tumia mageresho kama ilivyoonyeshwa kwenye dodoso. Pia linganisha taarifa na orodha ya kaya iliyochapishwa, kama kuna tofauti dodoso zaidi upate taarifa za uhakika za wanakaya. Na weka maoni kama taarifa zilizochapishwa ni sahihi.

**Safuwima 6 (Swali la 6):** Katika swali hili mdadisi anatakiwa kuandika namba ya mwanakaya kama alikuwepo katika utafiti uliopita (NPS3) vinginevyo jaza -99ø Ikiwa kaya ni mpya, jaza 99 kwa watu wote ndani ya kaya kwasababu hakuna mtu ye yote ndani ya kaya aliyekuwepo katika awamu liliyopita ya NPS.

**Angalizo:** Endapo mwanakaya alikuwepo kwenye utafiti uliopita, na akahamia(kuolewa) kwenye kaya nyingine iliyokuwepo kwenye utafiti uliopita, namba yake ya utambulisho itaanzia 501 na kuendelea. Mfano John ID 04 alimuoa Hilda ID 06 kutoka kwenye kaya nyingine iliyokuwepo katika utafiti uliopita, kwahiyo Hilda kwenye swali hili atatumia ID 506.

**Safuwima 7 (Swali la 7):** Je, [JINA] alikula mlo wowote kwenye kaya hii siku 7 zilizopita? Swali hili linahitaji kujua kama (JINA) alikula mlo wowote kwenye kaya hiyo katika siku saba zilizopita. Jaza geresho la  $\frac{1}{2}$  iwapo atajibu  $\frac{1}{2}$  ndiyo $\ddot{o}$  na  $\frac{1}{2}$  iwapo atajibu  $\frac{1}{2}$  hapana $\ddot{o}$

**Safuwima 8 (Swali la 8):** Ni kwa siku ngapi katika mwezi uliopita [JINA] alikuwepo kwenye kaya? Swali hili mdadisi anatakiwa kudodosa ni siku ngapi katika mwezi uliopita [JINA] alikuwepo kwenye kaya. Andika idadi ya siku kulingana na mwezi.

**Safuwima 9 (Swali la 9):** Je, katika miezi 12 iliyopita, [JINA] ameishi kwenye kaya hii kwa miezi 3 au zaidi? Jaza geresho la  $\frac{1}{2}$  iwapo jibu ni  $\frac{1}{2}$  ndiyo $\ddot{o}$  na  $\frac{1}{2}$  iwapo ni  $\frac{1}{2}$  hapana $\ddot{o}$ .

**Safuwima 10 (Swali la 10):** Katika miezi 12 iliyopita [MWEZI/MWAKA], ni miezi mingapi kwa ujumla [JINA] ameishi nje ya kaya hii? Andika miezi kamili ambayo mwanakaya ameishi nje ya kaya husika kwa kuzingatia kipindi cha miezi 12 iliyopita.

**Safuwima 11 (Swali la 11):** Nini shughuli kuu ya [JINA] kwa miezi 12 iliyopita?. Unatakiwa kunakili mageresho ya shughuli ya kila mwanakaya. Kwa mfano: Kilimo/Ufugaji...1, Uvuvi.....2 Madini.....3, Utalii.....4, n.k Jaza shughuli ambayo mhojiwa anaitegemea zaidi katika kipato. Tumia geresho 17, mdogo sana kwa watoto chini ya miaka 5 tu ambao hawako shule. Ikiwa mtoto ni chini ya miaka 6 na anasoma shule, tumia geresho la 16 öhana kaziö.

**Safuwima 12 (Swali la 12):** Ni wapi alipo baba mzazi wa [JINA]? Muulize mhojiwa ni wapi alipo baba mzazi wa [JINA]. Kama ni mwanakaya nakili namba yake na uende swali la 15. Andika geresho kulingana na jibu la mwanakaya, kwa mfano; anaishi nje ya kaya, geresho ni  $\frac{1}{2}$  na uende swali la 14. Ikiwa amefariki, weka geresho 98. Ikiwa Mhojiwa hajui, tumia geresho 99 na nenda swali la 14.

**Safuwima 13 (Swali la 13):** Umri wa [JINA] wakati baba yake alipofariki. Mhojiwa/mwanakaya akutajie umri wa [JINA] wakati baba yake alipofariki. Unatakiwa kuandika ni umri gani aliokuwa nao mtoto wakati baba yake alipofariki.

**Safuwima 14 (Swali la 14):** Kiwango cha elimu cha baba wa [JINA]? Swali hili linataka kujua kiwango cha elimu cha baba mzazi wa [JINA]. Unatakiwa kudadisi kiwango cha juu cha elimu alichofikia baba yake. Jaza mageresho husika yaliyoorodheshwa kwenye dodoso.

**Safuwima 15 (Swali la 15):** Ni wapi alipo mama mzazi wa [JINA]? Kama ni mwanakaya nakili namba yake na nenda swali la swali la 18, Ikiwa anaishi nje ya kaya jaza 97 na nenda swali la 17. Ikiwa amekufa, jaza geresho 98. Ikiwa Mhojiwa hajui, jaza geresho 99 na nenda swali la 17.

**Safuwima 16 (Swali la 16):** Umri wa (JINA) wakati mama yake alipofariki. Andika umri aliokuwanao (JINA) wakati mama yake alipofariki, sio umri wa mama wakati alipofariki.

**Safuwima 17 (Swali la 17):** Kiwango cha elimu cha mama wa [JINA]? Utajaza kiwango cha elimu cha mama wa (JINA). Jaza geresho linalohusika juu ya kiwango cha elimu alichofikia mama wa (JINA). Tumia mageresho yaliyoorodheshwa kwenye dodoso.

**Safuwima 18 (Swali la 18):** (JINA) ANA UMRI WA MIAKA 12 AU ZAIDI? Swali hili Mhojiwa hapaswi kuulizwa. Mdadisi angalia swali la 4 kama [JINA] ana umri wa miaka 12 au zaidi. Kama ni ndiyo utaandika geresho la 1, hapana geresho la 2 (Kama ni hapana na ni mwanakaya wa mwisho nenda sehemu inayofuata).

**Safuwima 19 (Swali la 19):** Hali ya ndoa ya [JINA]. Ainisha ni aina gani ya ndoa aliyonayo. Andika geresho linalohusika kama: Mke mmoja geresho ni  $\frac{1}{2}$  wake wengi  $\frac{1}{2}$  wanaishi pamoja  $\frac{1}{2}$  na uende swali la 22. Kwa wale waliotengana geresho ni  $\frac{1}{2}$  ambao hawajawahi kuo/kuolewa  $\frac{1}{2}$  waliofiwa na wenza  $\frac{1}{2}$  na uende swali la 26.

**Safuwima namba 20 (Swali la 20):** Hali ya ndoa ya (JINA) kabla ya hii ya sasa: Kama ndoa yake ya sasa ni ya kwanza, jaza  $\frac{1}{4}$  Kama mwanakaya alipewa talaka/talikiwa kabla ya ndoa ya sasa, jaza  $\frac{2}{4}$  Kama mwanakaya alikuwa mjane kabla ya ndoa yake ya sasa, jaza  $\frac{3}{4}$  Kama mwanakaya alishakuwa na ndoa zaidi ya moja kabla ya ndoa yake ya sasa, jaza  $\frac{4}{4}$  Kwa wanaume wenyewe wake wengi, jaza  $\frac{5}{4}$

**Safuwima 21 (swali 21):** Aina ya ndoa ya (JINA). Unatakiwa kuingiza geresho linalohusika kwa hali ya ndoa kama ilivyoonyeshwa kwenye dodoso. Kwa ajili ya utafiti huu neno öndoao lina maana kwamba watu wawili mwanaume na mwanamke, waliooana kimila, kiserikali, au kidini. Pia tafsiri hii itawahusu wale ambao wameamua kuishi pamoja kama mke na mume. Wale wanaofanya mapenzi ya kupita tu wasiingizwe katika tafsiri hii.

**Hakikisha mhojiwa anabainisha kwa ufasaha aina ya ndoa aliyonayo. Unatakiwa kuandika geresho husika iwapo kiserikali weka geresho '1', kidini geresho '2', na kimila weka geresho '3'.**

**Safuwima 22 (swali 22):** Mke/Mume wa [JINA] anaishi kwenye kaya hii? Unatakiwa kupata taarifa sahihi iwapo mke/mme anaishi ndani ya kaya husika au la. Kama jibu ni ndiyo andika geresho la  $\frac{1}{4}$  na hapana geresho  $\frac{2}{4}$  na nenda swalia la 24.

**Safuwima 23 (swali 23):** Safuwima hii kimsingi ni maelekezo ya kwako mdadisi na si kumsomea mhojiwa. Sehemu hii inahitaji uandike namba ya/za mume/wake zake kutoka orodha ya wanakaya. Iwapo mume ana mke zaidi ya mmoja andika namba zao zote, endapo atakuwa na wake zaidi ya 4 utajaza hadi yule wa nne tu.

**Safuwima 24 (swali 24):** [JINA] ana mke/mume anayeishi nje ya kaya hii? Unatakiwa kupata taarifa iwapo mke/mume anaishi nje ya kaya husika au la. Na kama ni ndio geresho ni  $\frac{1}{4}$  na kama ni hapana weka geresho  $\frac{2}{4}$  na nenda swali la 26.

**Safuwima 25 (swali 25):** Ni wake wangapi wa [JINA] ambao wanaishi nje ya kaya hii? Swali hili liulizwe kwa wanaume tu. Andika idadi kamili ya wake ambao wanaishi nje ya kaya husika.

**Safuwima 26 (swali 26):** Kwa miaka mingapi [JINA] ameishi kwenye jamii hii? Jaza jumla ya idadi ya miaka aliyoishi kwenye jamii hiyo. Pia andika  $\frac{99}{100}$  kama ameishi toka kuzaliwa, nenda sehemu inayofuata.

**Safuwima 27 (swali 27):** Kutoka wilaya gani [JINA] alihamia hapa? Swali hili ni muhimu sana kwani linahitaji kujua ni jinsi gani watu wanaondoka/kuhamia katika jamii hiyo. Unachotakiwa kufanya utajaza jina la nchi kama ametoka nchi nyingine, mkoaa kama ametoka mkoaa tofauti na ule alipo sasa na jina la wilaya endapo ametokea wilaya nyingine mkoaa ule ule, kama amehamia ndani ya wilaya hiyo hiyo, jaza wilaya aliyopo kwa kutumia mageresho yaliyopo nyuma ya dodoso. Kama ameishi nje ya Tanzania andika jina la nchi aliyatoka. Kama ameitaja nchi utaandika jina la nchi na kwenye geresho utaacha wazi.

**Safuwima 28 (swali 28):** Sababu za [JINA] kuhamia hapa. Ainisha sababu kuu iliyopelekea mwanakaya kuhamia katika jamii hiyo. Tumia mageresho kama yalivyoorodheshwa kwenye dodoso.

**Safuwima 29 (swali 29):** Ni wilaya ipi ambayo [JINA] amezaliwa? Zingatia kuuliza jina la nchi/wilaya aliyozaliwa mwanakaya. Hakikisha unapata jina kamili na kwa usahihi. Kama amezaliwa nje ya nchi kumbuka kuandika nchi aliyatoka. Kumbuka kutumia mageresho nyuma ya dodoso hili. Ikiwa nchi imetajwa, andika jina la nchi, na usiweke geresho.

## Sehemu C: Elimu

---

### Sehemu hii waulizwe wanakaya wa kuanzia umri wa miaka 5 na zaidi

**Safuwima 1 (Swali la 1):** Swali hili ni la mdadisi, mhojiwa hapaswi kuulizwa. Swali hili linakutaka uainishe wanakaya ambao wana umri wa miaka 5 na zaidi. Jaza mageresho yanayohusika. Ikiwa mwanakaya ana miaka 5 na zaidi weka geresho  $\frac{1}{4}$  kama hapana geresho ni  $\frac{2}{4}$  nenda sehemu inayofuata. Uliza kwa wanakaya wote.

**Swali la 2:** Je, [JINA] anaweza kusoma na kuandika? Unatakiwa kumtambua mwanakaya anayejua kusoma na kuandika katika lugha ya Kiswahili, Kiingereza, au lugha nyingine yoyote, bila kujali kwamba wamehudhuria shule au la. Wanakaya wote wenye umri wa miaka 5 na zaidi wanapaswa kuulizwa swali hili. Geresho namba ۱۰ ni kwa ajili ya Kiswahili tu, ۲۰ kwa Kiingereza tu, ۳۰ kwa Kiswahili na Kiingereza, na ۴۰ kwa lugha nyingine yoyote. Geresho ۵۰ ni kwa ajili ya wahojiwa wasiojua kusoma au kuandika katika lugha yoyote ile, halafu nenda swali la 3.

**Safu wima 3 (Swali la 3):** Je, [JINA] amewahi kusoma shule? Unatakiwa kuainisha wanakaya amba wana elimu na amba hawana elimu bila kujali ni kiwango gani cha elimu alichofikia mwanakaya. Swali hili litaalizwa kwa wanakaya wote. Jaza geresho ۱۰ kama ndiyo, na geresho ۲۰ kama hapana. Ikiwa jibu ni hapana nenda swali la 29.

**Safuwima 4 (swali 4):** Je, [JINA] alianza shule akiwa na miaka mingapi? Hakikisha unadadisi kwa ufasaha umri amba mwanakaya alianza elimu yake ya awali umri huo ndio utakaoandikwa kwenye swali hili.

**Safuwima 5 (swali 5):** Je, [JINA] anasoma shule sasa? Unatakiwa kupata taarifa kama mwanakaya husika anasoma kwa sasa au la. Iwapo jibu ni ndiyo weka geresho ۱۰ halafu nenda swali la 9, kama ni hapana weka geresho ۲۰(utaendelea na maswali yanayofuata).

**Safuwima 6 (swali 6):** Je, [JINA] alisoma shule mwaka jana? Swali hili linakutaka wewe mdadisi kutafiti iwapo mwanakaya alisoma shule mwaka jana(mwaka uliopita). Kama jibu ni ndiyo jaza geresho la ۱۰ kisha nenda swali la 10, kama ni hapana utajaza geresho la ۲۰ na uendelee na maswali yanayofuata.

**Safuwima 7 (swali 7):** Je, [JINA] amefikia kiwango gani cha elimu? Unatakiwa kuandika geresho la kiwango cha juu cha elimu alichofikia (JINA). Angalia mageresho hapo chini. Kumbuka geresho ۱۰ ni shule ya awali haijumuishi chekechea. Zingatia ya kuwa geresho ۱۹۶۰ ni la ōpre-form oneö(OSC), yaani mafunzo kabla ya elimu ya sekondari. Geresho hili linahusika tu kwa wanafunzi amba bado wako wanasona au wale amba wamesomea Zanzibar (Unguja au Pemba). Wahojiwa amba walosomea Tanzania Bara hawapaswi kutumia geresho hili.

#### Mageresho ya swali la 7, 9 na 10

Vidudu .....	01	Watu Wazima .....	02
<b>MSINGI</b>		<b>SEKONDARI</b>	
D1.....	11	F1 .....	21
D2.....	12	F2 .....	22
D3.....	13	F3 .....	23
D4.....	14	F4 .....	24
D5.....	15	'O'+KOZI.....	25
D6.....	16	F5 .....	31
D7.....	17	F6 .....	32
D8.....	18	'A'+KOZI.....	33
PRE-FORM 1 .....	19	DIPLOMA.....	34
MS+KOZI.....	20		
<b>CHUO KIKUU</b>			
U1.....	41	U2.....	42
U3.....	43	U4.....	44
		U5&+.	45

**Safuwima 8 (swali 8):** Je, ni mwaka gani [JINA] aliondoka shule kwa mara ya mwisho? Andika mwaka amba mhojiwa aliondoka shulenii mara ya mwisho. Kama waliondoka shule kwa ajili ya likizo fupi mwaka 1995 (kwa mfano kufanya kazi), na akarudi shule mwaka 1997, na baadae akamaliza shule mwaka 2000, andika mwaka 2000 kama mwaka amba aliondoka shule kwa mara ya mwisho. Halafu endelea na swali la 22 kwa wahojiwa wote.

**Safuwima 9 (swali 9):** Je, [JINA] anasoma kiwango gani cha elimu sasa? Unatakiwa kuuliza kama (JINA) ana kiwango gani cha juu cha elimu kwa wakati mahojiano yalipofanyika. Kwa mfano jina yupo darasa la saba jaza geresho la darasa la saba, D7fí 17 n.k.

**Safuwima 10 (swali 10):** Je, [JINA] alikuwa akisoma kiwango gani cha elimu mwaka jana? Unatakiwa kudadisi kama mwanakaya alikuwa akisoma kwa mwaka uliopita na akutajie kiwango cha elimu alichokuwa anasoma. Andika geresho husika kutokana na taarifa za mwanakaya. Kama hajaanza shule kabisa, geresho 90, kama hakuhudhuria 91.

**Safuwima 11 (swali 11):** Swali hili ni maelekezo yako wewe mdadisi Mhojiwa hapaswi kuulizwa. Angalia jibu la swali ka  $\frac{5}{5}$  na ainisha kama mwanakaya anasoma shule kwa sasa au la. Mhojiwa atakubaliwa kwamba anasoma shule kwa sasa ikiwa atajibu swali la  $\frac{5}{5}$ . Kama mhojiwa kwa sasa hahudhuri shule nenda swali la 22.

**Safuwima 12 (swali 12):** Nani anamiliki shule anayosoma [JINA]? Jaza mageresho kama ilivyoonyeshwa kwenye dodoso.

**Swali la 13:** Hii shule ni ya bweni? Ulizia kama shule anayosoma mhojiwa ni ya bweni. Kama ndiyo, tumia geresho  $\frac{1}{1}$  na nenda swali la 16. Kama hapana, tumia geresho  $\frac{2}{2}$  na endelea na swali linalofuatia.

**Swali la 14:** Kwa kawaida [JINA] huendaje shule? Ulizia njia ya kawaida ya usafiri amba mhojiwa anatumia kwenda shule. Tumia mageresho yaliyoonyeshwa kwenye dodoso.

**Swali la 15:** Je, inachukua muda gani [JINA] kufika shule kwa kutumia njia hii? Ulizia muda unaotumika kwenda shule (KWENDA SHULE TU) kwa kutumia njia ya usafiri kama zinavyoonekana katika swali la 14. Andika jibu lako katika dakika.

#### **ANGALIZO: Ni muda anaotumia kwenda tu au kurudi tu, usijumuushe kwenda na kurudi.**

**Safuwima 16 (Swali 16):** Je, [JINA] anapata mlo shulenii anakosoma? Zingatia kuwa mlo anaopata jina shulenii hatozwi gharama yeoyote. Jaza geresho 1 ikiwa hapati mlo shulenii anakosoma, au kama analipia mlo jaza geresho 2.

**Safuwima 17 (swali 17):** Je, [JINA] amekosa kuhudhuria shule katika wiki mbili zilizopita? Kama jibu ni ndiyo, andika geresho  $\frac{1}{1}$  na kama hapana,  $\frac{2}{2}$  na nenda swali la 19.

**Safuwima 18 (swali 18):** Kwa sababu gani [JINA] hakuhudhuria shulenii? Dadisi sababu iliyopelekea mwanakaya mwanafunzi kutoweza kuhudhuria shule. Tumia mageresho kama ilivyoonyeshwa kwenye dodoso.

**Swali la 19:** Ni nini hali ya vitabu vya kiada [JINA] anavyotumia shulenii? Ulizia kama mwanakaya anatumia vitabu vya kiada, kama wanaazima vitabu kutoka shulenii, au kama wanamiliki wenywewi, na kama wanaazima vitabu toka shulenii je wanaweza kwenda navyo nyumbani. Tumia mageresho kama yanavyoonekana katika dodoso.

**Swali la 20:** Katika wiki iliyopita, kwa makadirio, [JINA] alitumia saa ngapi kujisomea au kufanya mazoezi ya shule nyumbani (homework)? Ulizia ni muda gani mwanakaya anatumia kufanya kazi za shulenii nyumbani au nje ya shule. Andika jumla ya muda huo katika saa na dakika.

**Swali la 21:** Je, [JINA] alipata matatizo yoyote shulenii? Ulizia kama mwanakaya alikuwa na suala lolote au tatizo shulenii. Toa majibu mpaka mawili (2) na uyaandike kwa kufuata umuhimu wake kwa kutumia orodha ya mageresho kwenye dodoso.

**Swali 22:** Je, [JINA] alifanya mtihani wa kumaliza elimu ya msingi [PSLE]? Andika geresho  $\frac{1}{1}$ ; kama jibu ni ndiyo na uende swali linalofuatia. Tumia geresho la  $\frac{2}{2}$  kama jibu ni hapana na uende swali la 24.

**Angalizo; Kuwa makini katika swali hili na swali la 24 kwa wahojiwa amba o bado wako shule.**

**Swali la 23:** Je, [JINA] alipata matokeo gani katika mtihani wa darasa la saba? Onyesha kama mwanakaya alifaulu au alifeli mtihani wa kumaliza shule ya msingi, au hajui kama lifaulu au alifeli. Tumia geresho  $\frac{1}{10}$  kama alifaulu, geresho  $\frac{2}{10}$  kama alifeli, na geresho  $\frac{3}{10}$  kama hajui. Geresho la  $\frac{1}{10}$  zaidi ni kwa ajili ya wahojiwa wanaojibu kwa niaba ya wanakaya wengine wenye umri mkubwa na litumike tu kwa mara chache sana.

**Swali la 24:** Je, [JINA] alifanya mtihani wa kumaliza kidato cha 4 au cha 6? Ulizia kama mwanakaya alifanya mtihani wa kidato cha nne au cha sita. Tumia geresho  $\frac{1}{10}$  kwa waliofanya mtihani wa kidato cha 4, na geresho la  $\frac{2}{10}$  kama walifanya mtihani wa kidato cha 6, na geresho  $\frac{3}{10}$  kama hawakufanya mtihani wa kidato cha nne au cha 6 na uende katika swali la 28.

**Swali la 25:** Ni mwaka gani [JINA] alifanya mtihani? Onyesha mwaka ambao mhojiwa alifanya mtihani wa kumaliza kidato cha 4 au cha 6 kama ilivyoonyeshwa katika swali lililopita.

**Swali la 26:** Je, unaweza kunionyesha cheti cha matokeo? Omba kuona vyeti vya shulen, vya kidato cha 4 au cha 6. Onyesha kama mhojiwa alikubali au alikataa kukuonyesha cheti kwa kutumia mageresho katika dodoso.

**Swali la 27:** Je, [JINA] alipata matokeo gani? Uliza swali hili kwa kila mwanakaya aliyefanya mtihani wa kumaliza kidato cha 4 au cha 6 na ambao wana cheti cha shule. Andika jibu ukitumia mageresho yaliyo katika dodoso.

**Swali la 28:** Je, kaya yako ilitumia kiasi gani cha fedha kwa ajili ya elimu ya [JINA] katika kipindi cha meizi 12 iliyopita? Swali la 28 linaulizia gharama mbali mbali ambazo [JINA] anaweza kuwa alilipa kwa ajili ya elimu/shule katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Kadiria gharama katika shilingi (TSH), ukijumuisha na gharama ya malipo ya vitu. Kama hakuna gharama katika kifungu kimojawapo, andika  $\frac{1}{10}$  Katika Safu wima ya mwisho mdadisi anapaswa kuweka jumla ya gharama zote zilizo katika safu wima zilizotangulia. Zingatia kuwa viatu vinachukuliwa kama sehemu ya sare za shule (uniform).

**Swali la 29:** Je, [JINA] amewahi kuhudhuria darasa la elimu ya watu wazima? Ni darasa gani? Andika kama mwanakaya amehudhuria elimu ya watu wazima, kwa kutumia mageresho yaliyo kwenye dodoso. Kama mhojiwa hakuhudhuria elimu yoyote ya watu wazima, andika  $\frac{1}{10}$  na uende sehemu inayofuatia. MUKEJA ni mpango wa kuwawezesha wale waliookosa elimu ya msingi kwa sababu yoyote ile katika umri mdogo kuweza kupata elimu hiyo. KCM (*Kisomo Cha Manufaa*) ni kwa ajili ya wale wanaotaka tu kujua kusoma na kuandika. KCK (*Kisomo Cha Kujiendeleza*) ni mpango kwa wale wanaohitaji kufikia lengo fulani katika mfumo rasmi wa elimu mfano kumaliza elimu ya msingi ili kwenda elimu ya sekondari.

**Swali la 30:** Je, [JINA] alihudhuria elimu ya watu wazima kwa miezi mingapi? Andika jibu katika miezi.

## Sehemu D: Afya

Sehemu hii inahusu afya za wanakaya wote bila kujali umri. Kwa wanakaya wenye umri wa miaka 12 au zaidi wajibu maswali haya wenyewe. Tumia/jaza geresho linalostahili kama yanavyooneshwa katika dodoso.

**Safuwima 1 (swali 1):** Haya ni maelekezo kwa mdadisi, hutakiwi kumuuliza mhojiwa. Andika geresho la  $\frac{1}{10}$ endapo mhojiwa anajibu maswali mwenyewe na geresho la  $\frac{2}{10}$  iwapo hajibu mwenyewe.

**Safuwima 2 (swali 2):** Je, [JINA] alikwenda kupata huduma yoyote ya afya katika wiki 4 zilizopita? Swali hili anaulizwa kila mwanakaya bila kujali kama aliuga au hakuugua katika kipindi cha wiki 4 zilizopita. Hii ni kwa sababu ya ukweli kwamba baadhi ya watu huwa na kawaida ya kwenda sehemu ya kutolea huduma za afya, kupata ushauri au kufanya vipimo kuona kama afya zao ni njema hata bila ya kujisikia kuumwa. Kama jibu ni  $\frac{1}{10}$ ndiyoö weka geresho  $\frac{1}{10}$  na endelea na swali linalofuatia. Kama jibu ni  $\frac{2}{10}$ Hapanaö weka geresho  $\frac{2}{10}$ ; ikiwa hakwenda sehemu yeyote kupata huduma ya afya/ushauri katika kipindi cha wiki 4 zilizopita, nenda swali la 7.

**Safuwima 3 (Swali la 3):** Je, katika kipindi cha wiki 4 zilizopita, [JINA] alikwenda wapi kupata huduma yoyote ya afya? Swali hili linauliza kwa wale wanakaya waliokwenda kupata ushauri/huduma yoyote ya kiafya, ni sehemu gani walipopata ushauri/huduma hiyo. Katika swali hili, jibu linaweza kuwa ni zahanati, kituo cha afya, hospitali, daktari binafsi, mganga wa jadi au daktari wa meno. Kumbuka kwamba zahanati wagonjwa hawalazwi, wanapatiwa matibabu na kurudi nyumbani. Kituo cha afya wagonjwa wanalazwa na kina Mganga Msaidizi (Medical Assistant) au/na Mganga (Medical Officer). Kama atakutajia sehemu aliyopata huduma/ushauri na haipo kwenye orodha tumia geresho namba 17 na uandike sehemu hiyo.

Hospitali ni sehemu ambayo wagonjwa na majeruhi wanalazwa na kupatiwa matibabu (ya kisasa) na kwa kawaida ni kubwa na ina uwezo wa kuhudumia wagonjwa wengi na wa aina nyingi za magonjwa kwa wakati mmoja ikilinganishwa na kituo cha afya/zahanati.

**Safuwima 4 (swali 4):** Je, matibabu ya [JINA] yaligharamiwa vipi? Hospitali karibu zote hutoza pesa kama kuchangia huduma ya afya unapokwenda kupata huduma hiyo. Muulize mhojiwa ni njia gani aliyotumia kugharamia matibabu. Unatakiwa kujaza njia kuu hadi 2 alizotumia. Tumia mageresho yaliyoorodheshwa hapa. Kama njia aliyotumia kugharamia matibabu si mojawapo ya zilizoorodheshwa tumia geresho namba 9 na iandike njia hiyo.

**Swali la 5:** Ni kiasi gani cha pesa ultumia ulipokwenda [SEHEMU YA KUTOA HUDUMA YA AFYA]? Andika kiasi cha fedha kilichotumika wakati mwanakaya alipokwenda kupata huduma ya afya katika swali la 4. Kama mwanakaya anatoa aina 2 za watoa huduma, ulizia gharama zinazoambatana na kila mtoe huduma tofauti, na andika kiasi kilichotumika kwa kila mmoja.

**Swali la 6:** Je, [JINA] alipata matatizo yoyote wakati alipokwenda kupata ushauri au huduma ya afya? Ulizia kama mwanakaya alikuwa na masuala yoyote wakati alipomuona mtoe huduma. Andika mpaka majibu mawili (2) kwa kutumia mageresho yaliyo kwenye dodoso.

Maswali 7 ó 9 yanahu su gharama za matibabu. Unatakiwa kujumlisha thamani ya malipo kwa njia ya vitu, pesa zilizotolewa na kaya au Bima ya afya. Andika kiasi katika shilingi.

**Safuwima 7 (swali 7):** Je, kaya iligharamia kiasi gani kwa ujumla kwa ajili ya matibabu mfano ya majeraha, vipimo, kumuona daktari, kulazwa, kununua dawa zilizoandikwa na daktari kwa (JINA) n.k. kama zilikuwepo katika kipindi cha wiki 4 zilizopita? Andika jumla ya gharama zilizotumika katika wiki 4 zilizopita kumtibu (JINA) magonjwa kama vile majeraha, vipimo, kumwona daktari, kulazwa, n.k. Badilisha malipo yoyote aliyolipia ambayo si ya namna ya pesa kwenda katika shilingi. Usijumuisha gharama za matibabu yasiyoandikwa na daktari, maana gharama zake zitaonekana katika swali namba 9. Jumuisha gharama zinazoonekana katika swali la 5.

**Safuwina 8 (swali 8):** Je, kaya iligharamia kiasi gani kwa ujumla kwa ajili ya huduma za kinga kwa (JINA) kama kupima, uzazi wa mpango, katika kipindi cha wiki 4 zilizopita, kama zilikuwepo? Andika jumla ya gharama zilizotumika katika wiki 4 zilizopita kwa ajili ya huduma ambazo hazihusiani na kutunza afya kama vile kinga, kliniki ya uzazi, kupima afya. Kumbuka kujumuisha thamani kwa njia ya vitu na pesa taslimu. Jumuisha thamani iliyotajwa swali la 5.

**Safuwima 9 (swali 9):** Je, mlitumia Kiasi gani kwa jumla katika wiki 4 zilizopita kwa (JINA) kwa ajili ya kununulia dawa zisizoandikwa na daktari kama vile Panadol, Fansidar, dawa ya kikohozi, n.k.? Andika jumla ya gharama zilizotumika katika wiki 4 zilizopita kwa ajili ya kununulia dawa zisizoandikwa na daktari kama vile panado, fansidar, dawa ya kikohozi, n.k. Kumbuka kujumuisha thamani kwa njia ya vitu na pesa taslimu. Jumuisha thamani iliyotajwa swali la 5.

**Swali la 10:** Je, kipindi cha miezi 12 iliyopita [JINA], alilazwa au kupumzishwa kwenye sehemu ya kutolea huduma ya afya? Ulizia kama mwanakaya alilala angalau usiku mmoja katika kituo cha kutoa huduma za afya. Jibu òNdiyoö au òHapanaö. Kama ni Ndiyo, weka geresho 4. Kama hapana, geresho ni 2 na uende swali la 14.

**Swali la 11:** Je, [JINA] alikaa mara ngapi na alilazwa kwa siku ngapi? Kama mwanakaya alijibu òndiyoo katika swali la 10, andika idadi alikaa kwa siku (usiku) ngapi hospitali au sehemu ingine ya kutolea huduma za afya. Idadi ya siku za kukaa itakuwa ni mara ambazo mtu alikwenda hospitali na kukaa kwa angalau

usiku mmoja, bila kujali jumla ya siku za kukaa sehemu ya kutolea huduma za afya. Kwa mfano, kama mwanakaya alilazwa hospitali katika wiki ya kwanza ya mwezi kwa usiku 3, halafu wiki ya tatu akakaa kwa usiku mmoja, na mwisho katika wiki ya nne akakaa kwa usiku 4, idadi ya siku mpya za kukaa ni 3, na idadi ya siku za kulazwa itakuwa 8.

**Swali la 12:** Ni ugonjwa au majeraha gani yalisababisha [JINA] kulazwa? Andika jina la ugonjwa au jeraha kwa kutumia mageresho yaliyo katika dodoso. Orodhesha mpaka majibu 2. kama ugonjwa haukuorodheshwa kwenye dodoso, tumia geresho la ðMengineö na andika jina hilo.

**Swali la 13:** Je, huduma za kulazwa au kupumzishwa [JINA] ziligharimu kiasi gani kwa ujumla? Andika jumla ya gharama zote zilizotumika wakati [JINA] alipolazwa sehemu ya kutolea huduma ya afya katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Kumbuka kujumlisha thamani kwa njia ya vitu na pesa taslimu.

**Swali la 14:** Katika kipindi cha miezi 12 iliyopita [JINA] aliwahi kupumzishwa kwa usiku angalau mmoja kwa mganga wa jadi au mtoe huduma za kiroho/ kiimani? Unatakiwa kutambua kama mwanakaya alilazwa/kupumzishwa katika sehemu ya kutoa huduma za kiimani/kiroho au kwa mganga wa jadi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita Kama jibu ni ndio andika geresho -1øna kama ni hapana andika geresho -2øna uende swali la 16. Swali hili halitahusisha huduma za kiafya hususani hospitalini au katika zahanati.

**Swali la 15:** Katika kipindi cha miezi 12 iliyopita ni kiasi gani cha gharama kwa ujumla kilitumika kwa ajili ya [JINA] kupumzishwa kwa mganga wa jadi au mtoe huduma za kiroho/kiimani? Andika jumla ya gharama zote zilizotumika wakati [JINA] alipolazwa kwenye sehemu ya kutolea huduma za kiroho au kwa mganga wa jadi kwa miezi 12 iliyopita. Kumbuka kujumlisha thamani kwa njia ya vitu na pesa taslimu. Kama malipo yalifanywa zaidi ya mara moja katika miezi 12 iliyopita, malipo yote yanapaswa kujumlishwa na idadi yake iandikwe hapa.

**Swali la 16:** Swali hili ni kwa mdadisi mwenyewe kwa ajili ya kutambua wanakaya wenye umri wa miaka chini ya 5. Kama mwanakaya ni mtoto mwenye umri chini ya miaka 5, nenda swali la 31. Maswali ya ulemavu ni kwa ajili tu ya watu wazima na watoto wa miaka zaidi ya mitano.

*Maswali ya 17-30 yanaulizia juu ya ulemavu wa mwanakaya. Baadhi ya watu hawatasema kuwa wao ni walemvu, ingawa hawawezi kufanya baadhi ya vitu/kazi. Maswali haya yametengenezwa kutoa tafsiri pana ya ulemavu zaidi ya ule unaoonekana kimwili, kifkira n.k.*

*Zingatia kwamba maelekezo ya kuruka yanaweza kuwa magumu kuyafuutilia katika sehemu hii. Kama wahojiva watasema hawana ugumu wowote katika kufanya kitu chochote, weka geresho '1', na uruke swali linalofuatia juu ya umri tatizo lilipoanza. Kama mhojiva atasema ana matatizo katika kufanya kitu fulani kilichooodheshwa, dadisi kupata ukubwa wa tatizo hilo na tumia mageresho yaliyooodheshwa katika swali la 17. Swali linalofuatia juu ya umri tatizo lilipoanza liulizwe kwa wanakaya ambao wamejibowi geresho '2', '3', au '4' katika swali lililotangulia.*

**Maswali ya 17 na 18:** Yanaulizia kama mwanakaya ana matatizo ya kuona, hata kama amevaa miwani? Kama jibu ni hapana, andika geresho la -1øna uende swali la 19. Kama jibu ni ndiyo, dadisi kujua ukubwa wa tatizo na uende swali la 18 uandike umri wa mwanakaya wakati alipoanza tatizo hilo.

**Maswali ya 19 na 20:** Yanaulizia matatizo ya kusikia, hata kama utamuona mwanakaya amevaa vifaa vya kumsaidia kusikia. Kama jibu ni hapana, andika geresho la -1øna uende swali la 21. Kama jibu ni ndiyo, dadisi kujua ukubwa wa tatizo na uende swali la 20 uandike umri wa mwanakaya wakati alipoanza tatizo hilo.

**Mswali ya 21 na 22:** Yanaulizia kama mwanakaya ana matatizo ya kutembea au kupanda ngazi. Kama jibu ni hapana, andika geresho la -1øna uende swali la 23. Kama jibu ni ndiyo, dadisi kujua ukubwa wa tatizo na uende swali la 22 uandike umri wa mwanakaya wakati alipoanza tatizo hilo.

**Maswali ya 23 na 24:** Yanaulizia kama kuna mwanakaya mwenye matatizo ya kukumbuka au kufikiri kwa makini. Kama jibu ni hapana, andika geresho la  $\frac{1}{10}$  na uende swali la 25. Kama jibu ni ndiyo, dadisi kujuwa ukubwa wa tatizo na uende swali la 24 uandike umri wa mwanakaya wakati alipoanza tatizo hilo.

**Maswali ya 25 na 26:** Yanaulizia juu ya kama kuna mwanakaya mwenye matatizo ya kujihudumia kama vile kufua, kuvaa nguo, kwenda chooni. Kama jibu ni hapana, andika geresho la  $\frac{1}{10}$  na uende swali la 27. Kama jibu ni ndiyo, dadisi kujuwa ukubwa wa tatizo na uende swali la 26 uandike umri wa mwanakaya wakati alipoanza tatizo hilo.

**Maswali ya 27 na 28:** Yanaulizia kama kuna mwanakaya mwenye matatizo ya mawasiliano; kwa mfano kuelewa au kueleweka kwa kutumia lugha yake ya kawaida. Kama jibu ni hapana, andika geresho la  $\frac{1}{10}$  na uende swali la 29. Kama jibu ni ndiyo, dadisi kujuwa ukubwa wa tatizo na uende swali la 28 uandike umri wa mwanakaya wakati alipoanza tatizo hilo.

**Swali la 29:** Je, matatizo haya yanapunguza kiasi cha kazi [JINA] anachowenza kufanya nyumbani, kazini au shuleni? Sasa angalia majibu ya maswali ya mwanzo (17, 19, 21, 23, 25, 27). Kama mwanakaya amejibu ndiyo katika swali lolote kati ya maswali ya namba witiri, kwamba jibu ni 2, 3, au 4 ulizia swali la 30. Ulizia kama matatizo ya mwanakaya yanamfanya apunguze kiasi cha kazi anachofanya kazini/nyumbani na shuleni, na ni kwa kiasi gani kazi hiyo inapungua. Kama jibu halihusiani, kwa mfano mwanakaya hasomi, tumia geresho la  $\frac{1}{10}$  (geresho 4). Kama mhojiwa amejibu  $\frac{1}{10}$  katika maswali yote ya awali (17, 19, 21, 23, 25, 27), nenda swali la 31.

**Swali la 30:** Katika miezi 12 iliyopita, ni hatua gani zimechukuliwa kutatua matatizo ya [JINA]? Kama mwanakaya alijibu swali la 29, ulizia kama kuna hatua zimechukuliwa kutatua matatizo yake. Andika jibu kwa kutumia mageresho yaliyopo kwenye dodoso.

**Safuwima 31 (swali 31):** Je, [JINA] alilala ndani ya chandarua jana? Kama ndiyo, cha aina gani? Muulize mhojiwa iwapo [JINA] alitumia chandarua kujikinga na ugonjwa hatari wa malaria walipolala usiku wa jana. Tumia magersho yaliyo kwenye dodoso kuonyesha kama walilala ndani ya chandarua, na dadisi kujuwa kama kiliwekwa dawa au hapana. Kama hawakutumia andika  $\frac{1}{10}$  na uende swali la 34 kama hawajui andiika 5 na uendelee na swali linalofuata.

**Safuwima 32 (swali 32):** Je, kaya ilikipataje hiki chandarua? (Hati punguzo, kununua, kupewa, n.k.). Swali hili linahitaji kujuwa njia gani au ni namna gani chandarua kilipatikana alichotumia [JINA]. Tumia mageresho yaliyo katika dodoso. Kama chandarua kilipatikana bure, jibu geresho  $\frac{1}{10}$  nenda swali la 34.

**Safuwima 33 (swali 33):** Je, kaya ililipa kiasi gani kwa ajili ya hiki chandarua? Hakikisha anakutajia ni shilling ngapi alitumia kwa ajili ya kukipata hicho chandarua. Iwapo alitoa kitu tofauti na pesa, atathmini kama ingekuwa ni pesa ingekuwa ni kiasi gani. **KUMBUKA KAMA WANASHIRIKIANA CHANDARUA JAZA KIASI KWA MWANAKAYA MMOJA TU KATI YA WANAOSHIRIKIANA.** Mfano: baba na mama (chandarua 1). Kama chandarua kinatumika na zaidi ya mwanakaya mmoja kwa mfano-baba na mama, andika gharama za chandarua hiko mara moja tu.

**Swali la 34:** Je, [JINA] ana cheti cha kuzaliwa? Ulizia kama mwanakaya ana cheti cha kuzaliwa. Kama hapana, dadisi kujuwa kama uzazi wa mwanakaya huyo umeandikishwa katika mamlaka husika. Tumia mageresho kama yalivyo katika dodoso.

**Swali la 35:** Katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, [JINA] alipata msamaha wa matibabu katika kituo cha kutolea huduma za afya cha umma? Andika  $\frac{1}{10}$  au hajui kwa kutumia mageresho kama yalivyo katika dodoso.

**Safuwima ya maswali ya 36-41 waulizwe wanawake wenye umri wa miaka 12-49 tu.**

**Safuwima 36 (swali 36):** Swali hili ni maelekezo ya mdadisi, asiulizwe mhojiwa. Ainisha iwapo [JINA] ni mwanamke wa umri kati ya miaka 12 - 49, kama jibu ni ndiyo andika geresho la  $\frac{1}{10}$  kama hapana andika geresho la  $\frac{1}{20}$  uende swali la 42.

**Safuwima 37 (Swali 37):** Je, katika miezi 24 iliyopita [JINA] alizaa mtoto, hata kama hakuwa hai? Kama ndiyo andika geresho la 1, hapana andika geresho la 2 na nenda sehemu inayofuata. Kuwa mwangalifu katika kuuliza swali hili kwani linaweza kuleta hisia fulani.

**Safuwima 38 (swali 38):** Je, [JINA] alikuwa akihuduria kliniki ya wajawazito mara kwa mara alipokuwa na ujauzito wa mtoto wake wa mwisho aliyemzaa katika miezi 24 iliyopita?

Ni muhimu kwa kila mwanamke kujua maendeleo ya kiafya kila mara zaidi pindi anapokuwa mjamzito. Muulize (JINA) iwapo alikuwa akihuduria kliniki na kwa muda muafaka alipokuwa na ujauzito wa mtoto wake wa mwisho aliyemzaa katika miezi 24 iliyopita. Utajaza geresho husika, kama ndiyo geresho -1Ø na kama hapana geresho -2Ø

**Safuwima 39 (swali 39):** Je, ni wapi [JINA] alijifungulia mtoto wake wa mwisho aliyemzaa katika miezi 24 iliyopita? Tumia mageresho yaliyoorodheshwa katika swali hili. Endapo mhojiwa atakutajia jina la sehemu ambayo si mojawapo ya zilizoorodheshwa, tumia geresho namba 4 na andika sehemu hiyo kwa maneno.

**Safuwima 40 (swali 40):** Je, ni nani alimhudumia [JINA] wakati wa kujifungua? Wakati wa kujifungua mtoto (JINA) alisaidiwa na nani bila kujali alijifungulia kwenye huduma ya afya au la. Tumia mageresho yaliyoorodheshwa hapa. Iwapo (JINA) atakutajia mtu ambaye hakuorodheshwa kwenye mageresho, tumia geresho namba 7 na mwandike mtu huyo kwa maneno.

**Safuwima 41 (swali 41):** Je, uzazi huu uliandikishwa kwenye mamlaka husika? Ni muhimu kwa Taifa kujua takwimu za vizazi na vifo. Unatakiwa kudadisi iwapo uzazi uliopatikana katika miezi 24 uliandikishwa. Kama ndiyo uliandikishwa, andika geresho la -1Ø kama hapana geresho la -2Ø

**Maswali 42-49 yaulizwe kwa wanakaya amba ni watoto wenyenye umri chini ya miezi 60 (chini ya miaka 5).**

**Safuwima 42:** Maelekezo haya yanakuhusu wewe mdadisi, ainisha iwapo mwanakaya ni mtoto mwenye umri wa miezi chini ya 60 (chini ya miaka 5) kwa kutumia orodha ya wanakaya. Kama ndiyo utaandika geresho la 1 na kuendelea, na kama ni hapana geresho la 2 na nenda sehemu inayofuata.

**Safuwima 43 (swali 43):** Je, [JINA] amewahi kuharisha katika kipindi cha wiki mbili zilizopita? Kuharisha kunatokana na mtazamo wa mama au mlezi, au kwa kwenda choo laini au cha maji maji, au cha damu mara tatu au nne kwa siku. Kama ndiyo andika geresho -1Ø na kama hapana andika geresho -2Ø na uende sehemu inayofuata.

**Swali la 44:** Sasa ningependa kujua kiasi cha kinywaji alichopewa [JINA] wakati alipokuwa anaharisha. Je, alipewa kiasi cha kinywaji pungufu ya kwaida, kiasi cha kawaida au kiasi zaidi ya kwaida? Je, alipewa kinywaji kiasi kidogo zaidi ya kawaida, kiasi kama kile kile, au zaidi ya kawaida? Kama ni pungufu, dadisi kupata taarifa zaidi juu ya kiasi gani pungufu? Tumia mageresho yaliyo katika dodoso.

**Swali la 45:** Wakati [JINA] alipokuwa anaharisha, alipewa chakula kiasi kidogo ya kawaida, karibu kiasi kile kile, au zaidi ya kawaida, au hakupewa chakula chochote? Kama ni pungufu, dadisi kupata taarifa zaidi juu ya kiasi gani pungufu? Tumia mageresho yaliyo katika dodoso.

**Maswali ya 46 & 47:** Muulize mhojiwa kama wakati mtoto anaharisha alipewa kinywaji cha maji maalumu ya chumvichumvi na sukari kwenye paketi (ORS) au kinywaji cha kutengeneza nyumbani kilichoshauriwa na mtaalamu wa afya. Kama ndiyo utaandika geresho la -1Ø na kama hapana geresho la 2.

**Swali la 48:** Je, ultafuta ushauri au matibabu ya kuharisha? Kama jibu ni ndiyo utaandika geresho la -1Ø na kama hapana geresho la 2 na uende sehemu inayofuata.

**Swali la 49:** Je, ni wapi ultafuta ushauri au matibabu? Swali hii utajaza sehemu hadi 3 za huduma za afya alizoenda mhojiwa kwa ajili ya kupata ushauri au matibabu. Dadisi kupata sehemu zaidi ya moja alizoenda mhojiwa. Tumia mageresho yaliyoorodheshwa katika swali la 3 la sehemu hii, na jaza mpaka majibu matatu kwa kufuata umuhimu wake.

# Sehemu E: Maswali ya Ajira na Kazi

---

Sehemu hii inahusu shughuli mbalimbali ambazo wanakaya wanazifanya ili waweze kumudu maisha yao. Maswali haya yanapaswa waulizwe wanakaya wenyewe umri wa miaka 5 na zaidi, kama inawezekana, kila mwanakaya ajibu maswali yake mwenyewe. Fuata maelekezo na weka mageresho sahihi.

## MAANA YA KAZI/SHUGHULI

Kazi ni shughuli yoyote halali ambayo mtu anafanya kwa lengo la kujipatia riziki/kipato cha kujikimu/kujitegemea kimaisha, inahusisha kuajiri au kuajiriwa inaweza kuwa kwa shughuli za kilimo (kama kusafisha shamba, kulima, n.k) au zisizo za kilimo (kama biashara, ujenzi, n.k).

**Siku 7 zilizopita:** ni kipimo cha kimataifa katika kumbukumbu kuhusu kazi, na hii imekuwa ikitumika kwa miaka mingi. Katika maswali haya, siku 7 zilizopita imetumika kumaanisha siku 7 kabla ya siku ya utafiti. Kipindi hiki ni muhimu sana katika kutambua shughuli zinazoendelea.

**Miezi 12 iliyopita:** Kwa maswali haya, miezi 12 iliyopita ni kuanzia mwezi wa kalenda uliopita kurudi nyuma miezi 12 (miezi 12 iliyopita kabla ya utafiti). Ikiwa mahojiano yalifanywa tarehe ye yote ndani ya mwezi machi 2014, hivyo miezi 12 iliyopita itaanzia mwisho wa mwezi Februari 2014.

**Mafunzo kwa vitendo:** Hii inaeleza ambapo mtu anafanya kazi kwa kiasi fulani cha wakati kwa mwajiri kwa ajili ya kupatiwa mafunzo (mtu anayejifunza kazi) kama; sanaa, biashara au taaluma. Kazi inaweza kuwa ya malipo au bila malipo.

**Shughuli za kaya zisizokuwa za kilimo:** Shughuli zisizokuwa za kilimo zinazoipatia kaya kipato ni pamoja na zile zinazosalisha bidhaa au kutoa huduma, pamoja na kumiliki maduka au kufanya biashara, bila kujali ukubwa wake. Shughuli hii itajumuisha, Kwa mfano kutengeneza mikeka, matofali au mkaa, fundi ujenzi, selemala, kuuza kuni, n.k.

## Maelekezo ya Karatasi ya Kukunja (Flap) ya Orodha ya Wanakaya kwa ajili ya Sehemu ya Ajira

Katika sehemu hii ya Ajira, kuna baadhi ya maswali yanahitaji mdadisi arudi nyuma kwenye maswali ya 4ab-4e na 8ab-8e mwanzoni mwa sehemu ya Ajira. Kwa kuzuia makosa yatokanayo na mdadisi kuwa anafungua kurasa za nyuma na kurasa za mbele wakati wa kuhoji, kuna safu wima nne kwenye sehemu ya Ajira –sehemu EØ upande wa kulia wa karatasi ya kukunja ya orodha ya wanakaya ili kumsaidia mdadisi kutofungua kurasa za nyuma. Hizi safu wima tatu zinatakiwa kujazwa kwa wanakaya wote wenyewe umri zaidi ya miaka 5 baada ya swali la 9.

**Safuwima 1.** Usiulize swali hili kwa mhojiwa. Angalia kama jibu la swali 4AB au 8AB ni ñNDIYOØkwa mwanakaya. Kama jibu ni ñNDIOØ kwa angalau swali moja kati ya haya, weka alama ya ñXØ katika safu wima hii kwa mwanakaya. Kama jibu ni ñHAPANAØkwa maswali yote 4AB na 8AB, acha wazi safu wima hiyo. Ikiwa jibu la 4AB na 8AB ni ñNDIOØ weka alama ya ñXØna zungushia duara katika safuwima hiyo.

**Safuwima 2.** Usiulize swali hili kwa mhojiwa. Angalia jibu la swali 4E au 8E. Kama jibu ni ñNDIYOØ kwa mwanakaya. Ikiwa jibu ni ñNDIOØ kwa angalau swali moja kati ya 4E au 8E, weka alama ya ñXØ katika safu wima hii kwa mwanakaya. Ikiwa jibu ni ñHAPANAØ acha wazi safu wima hiyo.

**Safuwima 3.** Usiulize swali hili kwa mhojiwa. Angalia kama jibu la swali la 8CD ni ñNDIYOØ kwa mwanakaya. Kama jibu ni ñNDIYOØ, weka alama ya ñXØ katika safu wima hii kwa mwanakaya. Kama jibu ni ñHAPANAØkwa maswali yote 4CD na 8CD, acha wazi safu wima hiyo.

## MASWALI HAYA YA AJIRA NA KAZI WAULIZWE WANAKAYA WENYE UMRI WA MIAKA MITANO NA KUENDELEA.

**Swali la 1:** Swali hili linakutaka wewe mdadisi kuthibitisha kama mwanakaya ana umri wa miaka 5 au zaidi. Kama ndio weka geresho 1Ø na kuendelea swali linalofuata, kama hapana weka geresho 2Ø na endelea kuhoji mwanakaya mwingine.

**Maswali ya 4ab-4e yanauiliza kuhusu aina ya kazi ambayo mwanakaya alishiriki katika kipindi cha miezi 12 iliyopita.**

**Swali la 4ab:** Uliza kama mwanakaya alitumia muda wake katika kipindi cha miezi 12 iliyopita kufanya kazi kama mwanafunzi anayejifunza kazi kwa vitendo bila malipo au alifanya kazi yoyote kwa ajili ya malipo ya fedha taslimu, mshahara, posho, au aina yoyote ya malipo yasiyo ya fedha taslimu; ikijumuisha kufanya kazi za kujifunza kwa vitendo kwa malipo, au kufanya kazi za nyumbani za kulipwa, au kazi za shambani za kulipwa hata kama kwa saa moja. Kama jibu ndiyo jaza geresho la 1Ø kama hapana jaza geresho la 2Ø

**Swali la 4cd:** Muulize mhojiwa kama alimiliki au kufanya biashara isiyokuwa ya kilimo yenyenye ukubwa wowote iliyoendeshwa na kaya au yeze mwenyewe, au kama alisaidia bila malipo kufanya biashara ya kaya isiyohusiana na kilimo hata kama ni kwa saa moja kwa kipindi cha miezi 12 iliyopita. Ikiwa jibu ni ndiyo jaza geresho 1Ø kama hapana jaza geresho 2Ø

**Swali la 4e:** Muulize mhojiwa kama katika kipindi cha miezi 12 iliyopita [JINA] alifanya kazi katika shughuli za kaya za kilimo (ukijumuisha kutunza mifugo au uvuvi iwe kwa ajili ya kuuza au kwa matumizi ya chakula nyumbani), hata kama ni kwa saa moja. Ikiwa jibu ni ndiyo jaza geresho 1Ø kama hapana jaza geresho 2Ø

**Swali la 5:** Usiulize swali hili kwa mhojiwa. Ikiwa mhojiwa kajibu ndiyoØkwa swali lolote kati 4ab-4e, jaza geresho 1Ø Kama maswali yote ya 4ab-4e yana jibu la ØhapanaØ unatakiwa kujaza geresho 2Ø na kwenda swali la 8ab.

**Swali la 6:** Je, ni katika shughuli gani ya kiuchumi ambapo umetumia muda wako mwingi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita? Muulize mhojiwa ni ipi kati hizi shughuli mbali mbali alitumia muda wake mwingi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Kama mhojiwa anafanya shughuli mbali mbali, andika ile anayofanya muda wake mwingi. Kumbuka, Mama wa nyumba anachukuliwa kama mwanafamilia asiyelipwa (si kilimo) au mwanafamilia asiyelipwa (kilimo) inategemea na kama amefanya kazi yoyote ya shamba katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Tumia mageresho yaliyomo kwenye dodoso, andika shughuli ambayo mhojiwa alitumia muda wake mwingi kuifanya katika kipindi cha miezi 12 iliyopita kwenye safu wima ya kazi kuu. Andika shughuli ambayo mhojiwa alitumia muda wake wa ziada kuifanya katika miezi 12 iliyopita kwenye safu wima ya kazi ya ziada.

**Maswali ya 8ab-10b ni sawa na maswali ya 4a-6 lakini haya ni ya kipindi cha siku 7 zilizopita badala ya miezi 12 iliyopita.**

**Swali la 8ab:** Uliza kama mwanakaya alitumia muda wake katika kipindi cha siku 7 zilizopita kufanya kazi kama mwanafunzi anayejifunza kazi kwa vitendo bila malipo au alifanya kazi yoyote kwa ajili ya malipo ya fedha taslimu, mshahara, posho, au aina yoyote ya malipo yasiyo ya fedha taslimu; ikijumuisha kufanya kazi za kujifunza kwa vitendo kwa malipo, au kufanya kazi za nyumbani za kulipwa, au kazi za shambani za kulipwa hata kama kwa saa moja. Kama jibu ndiyo jaza geresho la 1, kama hapana jaza geresho la 2.

**Swali la 8cd:** Muulize mhojiwa kama alimiliki au kufanya biashara isiyokua ya kilimo yenyenye ukubwa wowote iliyoendeshwa na kaya au yeze mwenyewe, au kama alisaidia bila malipo kufanya biashara ya kaya isiyohusiana na kilimo hata kama ni kwa saa moja kwa kipindi cha siku 7 zilizopita. Kama jibu ndiyo jaza geresho la 1, kama hapana jaza geresho la 2.

**Swali la 8e:** Muulize mhojiwa kama katika kipindi cha siku 7 zilizopita [JINA] alifanya kazi katika shughuli za kaya za kilimo (ukijumuisha kutunza mifugo au uvuvi iwe kwa ajili ya kuuza au kwa matumizi ya chakula nyumbani), hata kama ni kwa saa moja. Kama jibu ndiyo jaza geresho la 1, kama hapana jaza geresho la 2.

**Swali la 9:** Usiulize swali hili kwa mhojiwa. Kama mhojiwa kajibu ndiyo kwa swali lolote kati 8ab-8e, jaza geresho 1. Kama maswali yote ya 8ab-8e yana jibu la hapana, unatakiwa kujaza geresho la 2 na kwenda swali la 12.

**Swali la 10:** Je, ni katika shughuli gani ya kiuchumi ambapo umetumia muda wako mwangi katika kipindi cha siku 7 iliyopita? Muulize mhojiwa ni ipi kati hizi shughuli mbali mbali alitumia muda wake mwangi katika kipindi cha siku 7 zilizopita. Kama mhojiwa anafanya shughuli mbali mbali, andika ile anayofanya muda wake mwangi. Kumbuka, Mama wa nyumba anachukuliwa kama mwanafamilia asiyelipwa (si kilimo) au mwanafamilia asiyelipwa (kilimo) inategemea na kama amefanya kazi yoyote ya shamba katika kipindi cha siku 7 zilizopita. Tumia mageresho yaliyomo kwenye dodoso, andika shughuli ambayo mhojiwa alitumia muda wake mwangi kuifanya katika kipindi cha siku 7 zilizopita kwenye safu wima ya kazi kuu. Andika shughuli ambayo mhojiwa alitumia muda wake wa ziada kuifanya katika siku 7 zilizopita kwenye safu wima ya kazi ya ziada. Ikiwa mhojiwa atajibu kwamba ni mwajiriwa au anafanya kazi kwa vitendo bila malipo, nenda swali la 17.

**Swali la 10a:** Kwa kawaida ni aina gani ya kazi mhojiwa anayofanya katika shughuli hii? Swali hili linaluza kuhusu kazi ambayo kwa kawaida mhojiwa anafanya. Andika maelezo sahihi ya kazi ya mhojiwa na kisha weka geresho la TASCO ambalo zinafanana kwa usahihi sana na maelezo ya kazi. Ikiwa mhojiwa anafanya shughuli zaidi ya moja, Shughuli yake kuu aliyojiriwa kwa kazi ni ile anayofanya yeye binafsi au anayotumia muda mwangi kuifanya. Kwa wale wenyewe shughuli mbili na muda wa kuzifanya unalingana shughuli kuu itakayochukuliwa ni ile inayomwingizia kipato kikubwa zaidi. Kama muda wa kazi na kipato vinalingana itachukuliwa shughuli ile mhojiwa anaona ndiyo shughuli yake kuu. Shughuli inamaanisha ni aina ya kazi mtu anayofanya au aliyofanya, wakati alipokuwa anafanya kazi kwa mara ya kwanza. Swali hili linahitaji kujua kwa ukaribu asili ya kazi mtu anayofanya kwa muda mwangi.

**Swali la 10b:** Je, mwajiri wa [JINA] anajihusisha na biashara au shughuli za aina gani?

Katika swali hili tunahitaji kujua sekta ya kiuchumi anayofanya kazi mhojiwa. Andika maelezo ya kampuni pale mhojiwa anakofanya kazi na nakili geresho la sekta husika ambalo linaelezea kwa usahihi kabisa biashara hiyo kwa kutumia ISIC. Fahamu kwamba tunahitaji kujua biashara au shughuli kampuni inayofanya au huduma/bidhaa kampuni inayotoa/inayozalisha, na wala sio kila mtu anachokifanya. Kampuni inafahamika kutokana na aina ya biashara au shughuli inayofanya.

- USIANDIKE jina kamili la kampuni au taasisi, isipokuwa kwa wale wanaofanya kazi katika wizara za serikali, au mashirika ya umma yanayotambulika.
- USIANDIKE maelezo ya ujumla kama ōkarakanaō, ōwiwandaō, ōkiwandaō, n.k. kwani hii haitatoa maelekezo yanayojitosheleza kwa shughuli inayofanya.

Ikiwa anapofanya kazi mhojiwa kuna shughuli zaidi ya mmoja (kama kiwanda kinazalisha bidhaa mbili tofauti) andika ile bidhaa kuu/ya msingi inayozalishwa. Kwa mfano: Mhojiwa anaweza kuwa ni karani wa uhasibu na amejiriwa na mwajiri wa shamba la kufugia ngombe wa maziwa, kazi yake ni ūkarani wa uhasibu ūlakini sekta anayojishughulisha nayo ni ūzalishaji wa maziwa

**Mifano zaidi:**

**Maelezo kamili**

Kiwanda cha nguo

Wizara ya kilimo

Madini ya Makaa ya mawe

**Maelezo hafifu**

Kiwanda

Serikalini

Madini

**Maswali ya 12-16 yanawahu su watu ambao wamekosa ajira kwa maana nyingine hawana ajira yoyote kwa muda wa siku 7 zilizopita.**

**Swali la 12:** Je [JINA] alikua tayari kufanya kazi siku 7 zilizopita? Uliza iwapo katika siku 7 zilizopita [JINA] alikuwa tayari kufanya kazi. Utayari maana yake ni kuwa tayari na kutaka kufanya kazi, isipokua ugonjwa au majukumu mengine yatakayomzuia mhojiwa asiwe na uwezo wakufanya kazi, hata kama hana kazi. Utaandika geresho la -1Ø kwa jibu la ndiyo na uende swali la 14, hapana andika geresho la -2Ø

**Swali la 13:** Ni kwa sababu gani [JINA] hakuwa tayari kufanya kazi siku 7 zilizopita? Muulize (JINA) ni sababu gani hakuwa tayari kufanya kazi katika siku 7 zilizopita. Andika geresho la sababu husika. Kumbuka kuwa kwa jibu lolote nenda swali la 17.

**Swali 14** Ingawa [JINA] hakufanya kazi yoyote katika kipindi cha siku 7 zilizopita, je, [JINA] ana kazi au ana shamba au biashara/kampuni ambapo atarejea kuifanya? Swali hili linahusu shamba/kazi za biashara/shughuli ambazo mtu anategemea kurudia tena kuzifanya hata kama hakufanya kwa siku 7 zilizopita. Mfano mzuri wa mwalimu aliye likizo kwa sababu shule imefungwa. Mifano mingine ni kama mtu yupo kwenye sikukuu, likizo ya kujifungua au ana kazi za msimu. Kama jibu ni NDIYO geresho ni -1Ø na kwenda swali la 17, na kama jibu ni HAPANA geresho ni -2Ø

**swali la 15:** Je, umefanya jitihada yoyote ya kutafuta kazi katika kipindi cha majuma 4 yaliyopita? Swali linahitaji kujua endapo [JINA] amefanya jitihada yoyote ya kutafuta kazi katika kipindi cha wiki 4 zilizopita. Hatua za kutafuta kazi ni pamoja na kusambaza CV au kwenda sehemu mbalimbali kuulizia nafasi za kazi. Andika geresho 1 kwa jibu la -ndiyoØ na geresho 2 kwa jibu la -hapanaØna nenda swali la 17.

**Swali la 16:** Je, umechukua hatua gani? Swali hili linauliza kuhusu hatua ambazo (JINA) amechukua kujaribu kupata kazi katika kipindi cha wiki 4 zilizopita. Andika hadi hatua mbili ambazo zimefanywa mara nyingi na mhojiwa. Tumia mageresho kwenye dodoso kuonyesha hatua ambazo mhojiwa alichukua. Kama hatua aliyochukua mhojiwa haipo kwenye orodha, weka geresho la 5 na andika hatua iliyochochukuliwa kwa maneno.

**Maswali kuanzia 17-35 yanauliza wanakaya waliofanya kazi za ujira au kazi za kujifunza kwa vitendo za ujira.**

**Swali la 17:** Usiulize swali hili kwa mhojiwa, badala yake angalia safuwima ya pili katika sehemu E kwenye karatasi ya kukunja ya kaya kuona jinsi mhojiwa alivyojibu swali la 4AB na 8AB. Kama kuna alama -XØ katika safuwima ya kwanza kwa mhojiwa, jaza geresho la 1 kisha nenda swali la 19. Kama kuna ØXØ iliyozungushiwa duara, katika safuwima ya kwanza kwa mhojiwa andika geresho 2. Kama safuwima iko wazi, jaza geresho la 3 na nenda swali la 62a.

**Swali la 18:** Kwa kuwa mhojiwa amesema ana kazi ya malipo katika kipindi cha miezi 12 iliyopita na siku saba zilizopita, ni muhimu kujua ikiwa mhojiwa alifanya kazi ya aina moja ya malipo katika kipindi cha siku saba zilizopita na miezi 12 iliyopita. Ikiwa mhojiwa alifanya kazi tofauti katika vipindi hivi, uliza taarifa zinazohusu kazi aliyoofanya katika kipindi cha siku saba zilizopita. Hii inamaana kuwa swali la 19-35 yaulizwe kuhusu kazi ya malipo ambayo mhojiwa alifanya katika siku saba zilizopita.

**Swali la 19:** Je, mwajiri wa [JINA] nií ? Kama ilivyo tafsiri ya mwajiri ni mtu aliyemkubali mtu mwingine afanye kazi kutokana na mkataba uliowekwa kwa makubalino maalumu ya kumlipa malipo fulani kwa kipindi cha muda maalumu. Jaza geresho husika, kutoka katika mageresho yaliyoorodheshwa katika swali hili.

**Swali la 20:** Kwa kawaida ni aina gani ya kazi mhojiwa anayofanya katika shughuli hii?

Katika swali hili linauliza kuhusu kazi ambayo kwa kawaida mhojiwa anafanya. Andika maelezo sahihi ya kazi ya mhojiwa na kisha weka geresho za TASCO ambazo zinafanana kwa usahihi sana na maelezo ya kazi. Shughuli kuu katika kipindi cha miezi 12 iliyopita kwa mhojiwa anafanya mwenyewe au mhojiwa anatumia muda mwingi kuifanya, ikiwa mhojiwa ana shughuli zaidi ya moja andika ile ambayo anatumia muda mwingi. Kwa wale wenye shughuli mbili na muda wa kuzifanya unalingana shughuli itakayochukuliwa ni ile

inayomwingizia kipato kikubwa zaidi. Kama muda wa kazi na kipato vinalingana itachukuliwa shughuli ile mhojiwa anaona ndiyo shughuli yake kuu. Shughuli inamaanisha ni aina ya kazi mtu anayofanya au aliyofanya, wakati alipokuwa anafanya kazi kwa mara ya kwanza. Swali hili linahitaji kujua kwa ukaribu asili ya kazi mtu anayofanya kwa muda mwinci.

**Swali la 21:** Je, mwajiri wa [JINA] anajihusisha na biashara au shughuli za aina gani?

Katika swali hili tunahitaji kujua sekta ya kiuchumi anayofanya kazi mhojiwa. Andika maelezo ya kampuni pale mhojiwa anakofanya kazi na nakili geresho la sekta husika ambalo linaelezea kwa usahihi kabisa biashara hiyo kwa kutumia ISIC. Fahamu kwamba tunahitaji kujua biashara au shughuli kampuni inayofanya au huduma/bidhaa kampuni inayotoa/inayozalisha, na wala sio kila mtu anachokifanya. Kampuni inafahamika kutokana na aina ya biashara au shughuli inayofanya.

**Swali la 22:** Kuna jumla ya watu wangapi wanaofanya kazi mahali [JINA] anapofanya kazi? Swali linataka kufahamu jumla ya idadi ya watu pale mhojiwa/mwanakaya anapofanya kazi na jaza jumla hiyo. Unatakiwa kudadisi zaidi unapopewa majibu ya ujumla mfano wachache, wengi n.k. ili upate idadi.

**Swali la 24:** Je, [JINA] anapokea ujira, mshahara au malipo mengine ya pesa taslimu au vitu kutoka kwa mwajiri wake anakofanya kazi? Kama atajibu ndiyo jaza geresho la 1Ø na uende swali la 26, kama hapana jaza geresho la 2Øna endelea na maswali yanayofuata.

**Swali la 25:** Kwa nini [JINA] halipwi kwa kazi anayoifanya? Ni sababu gani iliyosababisha mwanakaya/mhojiwa kutolipwa kwa kazi anayofanya. Kama mafunzo bila malipo weka geresho 1Ø analipa deni, geresho 2Ø nyingine (elezea), weka geresho 3Ø na ukumbuke kuiandika maelezo. Kwa jibu lolote utakalopata katи ya matatu ya hapo juu, nenda swali la 29.

**Swali la 26:** Mara ya mwisho [JINA] alilipwa kiasi gani cha fedha? Mara nyingi majibu ya swali hili yanatoka kwenye mshahara uliopokelewa mwezi uliopita. Iwapo mhojiwa hajawahi kulipwa, muulize: anategemea kulipwa kiasi gani? malipo hayo yanahusisha kipindi gani? Andika kiasi cha pesa pamoja na kipindi anacholipwa angalia mageresho husika kutokana na jibu utakalopewa na mhojiwa/mwanakaya; saa, geresho 1Ø siku, geresho 2Ø wiki, geresho 3Ø wiki 2, geresho 4Ø mwezi, geresho 5Ø Robo mwaka, geresho 6Ø nusu mwaka, geresho 7Ø na mwaka mzima, geresho 8Ø Mfano, kama mhojiwa alipokea shilingi za kitanzania 5000 kwa saa, andika 5000 katika safuwima ya kwanza na andika 1 katika safuwima ya pili. Kama mhojiwa alipokea shilingi 2,000,000 kwa mwezi, andika 2,000,000 katika safuwima ya kwanza na andika 5 katika safuwima ya pili.

**Swali la 27:** Je, unapokea malipo aina nyingine yoyote kwa kazi hii? Swali hili linataka kujua kama mhojiwa analipwa bidhaa au malipo katika mfumo mwincine wowote, mbali na mshahara kwa kazi anayoifanya. Kama Ndiyo geresho ni 1 na kama Hapana geresho ni 2 na nenda swali la 29.

**Swali la 28:** Malipo hayo yana thamani gani? Muulize mhojiwa kukadiria thamani ya aina ya malipo na andika thamani hiyo katika shilingi ya kitanzania. Pia onyesha ni kwa kipindi gani malipo yanafanya, tumia mageresho husika. Mfano, kama mhojiwa anapokea jozi ya viatu thamani yake inakadiliwa ni shilingi za kitanzania 50,000 kila baada ya miezi 6 kutoka anakofanya kazi, kwa hiyo andika 50,000 katika safuwima ya kwanza na andika 7 katika safuwima ya pili.

**Swali la 29:** Katika miezi 12 iliyopita, ni kwa miezi mingapi mhojiwa alifanya kazi katika shughuli hii? Andika idadi ya miezi aliyofanya kazi mhojiwa jumuisha pamoja na likizo ya malipo na miezi aliokuwa mgongjwa. Idadi ya juu ni miezi 12 kwasababu kipindi tunachorejea ni miezi 12.

**Swali 30:** Katika miezi 12 iliyopita, kwa kawaida ni wiki ngapi kwa mwezi mhojiwa alifanya kazi katika shughuli hii? Kutokana na miezi aliyofanya kazi mhojiwa, andika wastani wa idadi ya wiki ambazo kwa kawaida amefanya kazi. Idadi ya juu inayoweza kuandikwa ni 5 kwa sababu haiwezekani kuwa na wiki zaidi ya 5 katika mwezi.

**Swali la 31:** Katika miezi 12 iliyopita, kwa kawaida ni masaa mangapi kwa wiki mhojiwa alifanya kazi? Kwa wiki alizofanya kazi mhojiwa, andika wastani wa idadi ya masaa ambayo kwa kawaida amefanya kazi. Idadi ya juu inayoweza kuandikwa ni 168 kwasababu kuna saa 168 tu katika wiki.

**Swali la 32:** Je, ulitumia masaa mangapi kufanya kazi katika siku 7 zilizopita? Andika pia na likizo ya malipo na masaa aliyokuwa mgonjwa. Kama mwanakaya akijibu alifanya kazi kwa siku mbili, muulize afafanue kwa masaa. Idadi ya juu inayoweza kuandikwa ni 168 kwa sababu kuna saa 168 tu katika siku 7.

**Swali la 34:** Je, una mkataba wa kazi hii? Andika geresho 1 kama ndiyo, na geresho 2 kama hapana, na uende swali la 35.

**Swali la 34a:** Je, ni aina gani ya mkataba unao? Andika aina ya mkataba wa kazi mhojiwa alionao. Ikiwa mhojiwa na mkataba wa kudumu, weka geresho 1. Kama ana mkataba wa muda, chagua aina ya mkataba wa muda alionao katika mageresho yaliyopo kwenye dodoso.

**Swali la 35:** Katika swali hili, safuwima ya kwanza inauliza kama kazi ya mhojiwa ina likizo ya uzazi kwa baba au kwa mama. Safuwima ya pili inauliza kama kazi ya mhojiwa inatoa kodi kutoka kwenye mshahara. Safuwima ya tatu inauliza kama kazi ya mhojiwa inatoa bima ya afya. Kwa kila safuwima weka geresho 1 kwa ndiyo, na geresho 2 kwa hapana.

**Maswali kuanzia 36-52a yanahu kazi za ziada zaujira au malipo ya mafunzo kwa vitendo, ikiwa mwanakaya ana aina zaidi ya moja ya kazi zaujira au malipo ya mafunzo kwa vitendo.**

**Swali la 36:** Mbali na kazi ulizotaja, je, [JINA] aliquwa na ajira nyingine ya malipo au kujifunza kwa vitendo kwa malipo? Muulize mhojiwa mbali na kazi alizotaja awali aliquwa na ajira nyingine katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, hii ni zaidi ya ile ya awali katika maswali ya 19-35. Kama mwanakaya alifanya kazi tofauti kwa wakati mmoja katika mwaka huo na hafanyi kazi hiyo kwa sasa, pia itajumuishwa hapa. Kama jibu ni NDIYO geresho ni 1 na kama ni HAPANA geresho ni 2 kisha nenda swali namba 62a.

**Maswali ya 37-52a** Maswali haya kwa kazi za malipo ya ziada ya ni sawa kama ilivyokuwa kwenye shughuli kuu(kazi zaujira) katika maswali 19 - 35. Rejea katika sehemu ya ökazi zaujiraö kwenye mwongozo huu hapo juu kwa ufanuzi zaidi juu ya maswali haya.

**Swali la 62a:** Je, wewe ni mwanachama wa vyama vya wafanyakazi? Swali hili linauliza kama mhojiwa ni mwanachama wa vyama vya wafanyakazi. Ikiwa jibu ni ndiyo, weka geresho 1. Kama jibu ni hapana, weka geresho 2.

**maswali ya 63-68a yanauliza aina nyingine za kazi ambazo mhojiwa anaweza kuwa amezifanya.** Maswali haya ni muhimu sana katika utafiti huu, na yanapaswa kuulizwa kwa kila mwanakaya mwenye umri wa zaidi ya miaka 5. Ni muhimu kujua muda(masaa) aliyotumia kufanya kazi, ili isaidie kuangalia wale wote wanaofanya kazi chini ya masaa 40 kwa wiki. Hii inaweza kuainisha watu wanaofanya kazi kulingana na viwango vya kimataifa vya kazi. Haya ni muhimu sana katika kupima ukuaji wa uchumi, na pia serikali inahitaji kujua ukweli huu kwa jili ya kuandaa masuala ya sera kwa wafanyakazi.

**Swali la 63:** Swali hili mhojiwa hapaswi kuulizwa. Badala yake, angalia safuwima ya tatu katika sehemu E, kwenye flap ya kaya kuona kama mhijiwa alijibu ndio katika 8cd. Ikiwa kuna alama ya -Xøkwa mwanakaya katika safuwima ya tatu, hapo weka geresho 1. Ikiwa safuwima ya kwanza ipo wazi kwa mwanakaya, hapo weka geresho 2 na nenda swali la 65.

**Swali la 64:** Je, katika siku 7 zilizopita [JINA] ametumia masaa mangapi kufanya kazi za familia zisizo na malipo na zisizo za shamba? Katika siku 7 zilizopita, muulize mhojiwa ni kwa saa ngapi alisaidia kufanya kazi katika biashara yoyote isiyohusisha kilimo inayoendeshwa na kaya hii bila malipo. Iwapo mwanakaya/mhojiwa atajibu kwamba alifanya kazi kwa siku mbili, muombe ataje saa alizofanya kazi. Idadi ya juu ya saa isizidi 168 kwa sababu muda wa wiki moja una jumla ya saa 168 tu. Kama hakuna jaza 0.

**Swali la 65:** Swali hili hatakiwi kuulizwa mhojiwa. Badala yake, angalia safuwima ya tatu sehemu E ya karatasi ya kukunja ya orodha ya wanakaya (flap) kuona kama mhojiwa amejibu ndiyo katika mojawapo ya swali la 4E au 8E. Kama kuna alama ya X katika safuwima ya tatu, andika geresho 1. Kama safuwima ya kwanza iko wazi kwa mwanakaya, andika geresho 2, kisha nenda sehemu inayofuata.

**Swali la 66:** Je, katika kipindi cha siku 7 zilizopita [JINA] amefanya kazi kwa masaa mangapi kwenye shamba la kaya (ukijumuisha kutunza mifugo au uvuvi iwe kwa ajili ya kuuza au kwa matumizi ya chakula nyumbani)? muulize mhojiwa ni kwa masaa mangapi alifanya kazi katika shughuli za kaya ukijumuisha kutunza mifugo au uvuvi iwe kwa ajili ya kuuza au kwa matumizi ya chakula nyumbani. Kwa siku alizofanya kazi mhojiwa, andika wastani wa idadi ya masaa ambayo kwa kawaida amefanya kazi. Idadi ya juu inayoweza kuandikwa ni 168 kwasababu kuna saa 168 tu katika wiki.

**Swali la 66a:** Muulize mhojiwa kama alikuwa tayari kufanya kazi kwa masaa zaidi katika siku 7 zilizopita. Swali hili linajaribu kucheki kama mhojiwa alikuwa tayari kufanya kazi kwa masaa zaidi na alihitaji kufanya kazi kwa masaa zaidi, lakini hakuwa na nafasi ya kufanya kazi masaa zaidi.

**Swali la 70:** Je, [JINA] alitumia masaa mangapi jana kutafuta kuni au malighafi ingine kwa ajili ya nishati? Mhojaji anatakiwa kuandika kiasi cha muda, kwa masaa aliyotumia mhojiwa jana kwa ajili ya kutafuta kuni au malighafi nyingine kwa ajili ya nishati. Jaza  $\text{--}1$  kama hakuna.

**Swali la 71:** Je, [JINA] alitumia masaa mangapi jana kuchota maji na kuyaleta nyumbani? Mhojaji anatakiwa kuandika kiasi cha muda, kwa masaa aliyotumia mhojiwa jana kwa ajili ya kuchota maji. Unatakiwa kujumuisha muda wa kwenda, kusubiri na kurudi nyumbani. Jaza  $\text{--}1$  kama hakuna.

## Sehemu F: Matumizi ya Chakula Nje ya Kaya

---

**Usijumuisehawadizilizotolewa. Ingiza zawadi zilizopelewa na kuliwa. Uliza thamani yake ya soko. Maswali yote katika sehemu hii yanahusu kipindi cha siku 7 zilizopita.**

**Safuwima 1:** Je, kuna mwanakaya aliye kula chakula/kinywaji nje ya kaya katika siku 7 zilizopita? Swali hili waulizwe wanakaya wote iwapo kuna mwanakaya alikula chakula/kinywaji nje ya kaya katika siku 7 zilizopita, jaza geresho  $\text{--}1$  kama  $\text{--}1$  nondo na kama hapana jaza geresho 2, nenda sehemu inayofuata.

**Safuwima 2 na 3:** Muulize (JINA) kama alikula mlo kamili (asubuhi, mchana au usiku) nje ya kayakatika siku saba zilizopita. Kama swali la 2 geresho ni  $\text{--}1$  unatakiwa kujaza thamani ya chakula hicho katika swali 3, na kama swali la 2 geresho ni  $\text{--}2$  nenda swali la 4.

**Safuwima 4 na 5:** Muulize (JINA) kama alikula nyama za kuchoma, viazi vya kukaanga, ndizi za kuchoma au asusa nyingine nje ya kaya. Ikiwa swali la 4 geresho ni  $\text{--}1$  unatakiwa kujaza thamani ya chakula hicho katika swali 5, na kama swali la 4 geresho ni  $\text{--}2$  nenda swali la 6.

**Safuwima 6 na 7:** Muulize (JINA) kama alikunywa kibuku au pombe ya kienyeji nje ya kaya. Ikiwa swali la 6 geresho ni  $\text{--}1$  unatakiwa kujaza thamani ya kinywaji hicho katika swali 7, na kama swali la 6 geresho ni  $\text{--}2$  nenda swali la 8.

**Safuwima 8 na 9:** Muulize (JINA) kama alikunywa mvinyo, bia au vinywaji vikali nje ya kaya. Ikiwa swali la 8 geresho ni  $\text{--}1$  unatakiwa kujaza thamani ya kinywaji hicho katika swali 9, na kama swali la 8 geresho ni  $\text{--}2$  nenda swali la 10.

**Safuwima 10 na 11:** Muulize (JINA) kama alikunywa soda au vinywaji baridi nje ya kaya. Ikiwa swali la 10 geresho ni  $\text{--}1$  unatakiwa kujaza thamani ya kinywaji hicho katika swali 11, na kama swali la 10 geresho ni  $\text{--}2$  nenda swali la 12.

**Safuwima 12 & 13:** Muulize (JINA) kama alikula pipi, ice-cream au viburudisho nje ya kaya. Ikiwa swali la 12 geresho ni 1 unatakiwa kujaza thamani ya viburudisho hivyo katika swali 13, na kama swali la 12 geresho ni 2 nenda swali la 14.

**Safuwima 14 & 15:** Muulize (JINA) kama alikunywa chai, kahawa, sambusa, keki, na vitafunwa vingine vya hotelini nje ya kaya. Ikiwa swali la 14 geresho ni -1Ø unatakiwa kujaza thamani ya viburudisho hivyo katika swali 15, na kama swali la 14 geresho ni -2Ø nenda mwanakaya mwngine.

## Sehemu G: Mwonekano wa Ustawi wa Maisha na Uhalifu

### Sehemu hii inawahuisha wanakaya wenyenye umri usiopungua miaka 15.

**Swali la 1:** Hii ni kwa anayehoji, asiulizwe mhojiwa, kwa sababu swali la ustawi wa jamii, linamuuliza mhojiwa maoni yake binafsi kuhusu ustawi wa jamii, hayawezi kujibiwa na mwanakaya mwngine. Jaza geresho -1Ø kama mhojiwa anajibu mwenyewe, na -2Ø kama hajibu. Nenda kwa mwanakaya mwngine.

**Swali la 2:** Hii ni kwa anayehoji, asiulizwe mhojiwa. Swali hili ni la mchujo wa umri wa mhojiwa, swali la ustawi wa jamii liulizwe kwa wenye umri wa miaka 15 na zaidi.

**Swali la 3:** Swali hili, linamuuliza mhojiwa anaridhika vipi na hali ya maisha katika vigegele mbalimbali, uliza kila kipengele na tumia geresho lililopo kwenye maswali. Kama kipengele hakihusiki kwa mhojiwa jaza geresho 8, mfano kama mhojiwa ni mwanafunzi na hafanyi kazi, kipengele D - kazi, hahusiki.

**Swali la 4:** Swali hili linamhitaji mhojiwa aelezee hali yake ya kifedha kwa sasa.

**Swali la 5:** Swali hili linauliza ukifikilia hali yako uliyokuwa ukiishi katika miaka kama 2 iliyopita, utaielezeaje hali yako kifedha kwa kipindi hiko. Ikiwa mwanakaya alikuwa akiishi kwenye kaya tofauti miaka 2 iliyopita, ajibu hali ya kaya aliyokuwa akiishi kwa miaka 2 iliyopita, na siyo kwa kaya anayoishi kwa sasa ikiwa miaka 2 iliyopita alikuwa haishi hapo. Tumia mageresho kwenye dodoso.

### Swali la 6-10 linauliza kuhusu Uhalifu ikiwa mhojiwa amewahi kuwa muathiriwa wa uhalifu katika miezi 12 iliyopita.

**Swali la 6:** Swali hili ni swali linalochuja mhojiwa kulingana na umri. Maswali ya uhalifu yanatakiwa waulizwe wahojiwa wenye umri wa miaka 12 na zaidi.

**Swali la 7:** Swali hili linauliza ikiwa mhojiwa alikuwa muathirika wa uhalifu kwa kipindi cha miezi 12 iliyopita. Ikiwa mhojiwa alikuwa muathirika wa uhalifu, weka geresho -1Ø na endelea na swali linalofuata. Ikiwa hapana weka geresho -2Ø na nenda kwa mwanakaya anayefuata.

**Swali la 8:** Swali hili linauliza aina ya uhalifu uliofanyika kwa mwanakaya. Ikiwa mhojiwa amekuwa muathirika zaidi ya uhalifu mmoja katika miezi 12 iliyopita, uliza kuhusu uhalifu wa karibuni uliotokea.

Wizi wa kitu cha mtu unachukuliwa kama wizi wa mali za mtu kama vile simu ya mkononi, pochi, saa, vito (vitu vya thamani), pesa taslimu, computa mpakato na mavazi. Wizi wa majumbani ni pale mtu anapoingia kwenye nyumba ya mtu bila ruhusa na kuiba vitu (kwa mfano samani, luninga). Tukio hili linaweza kutokea iwapo mhusika anakuwepo au anakuwa hayupo nyumbani wakati wa tukio linapotokea. Shambulio ni pale muathirika anapovamiwa au kuumizwa. Silaha zinaweza kutumika, lakini hakuna kinachoibowi.

**Swali la 9:** Swali hili linauliza kama taarifa ya uhalifu ilitolewa polisi. Ikiwa taarifa ya uhalifu ilitolewa polisi, weka geresho 1 na nenda kwa mwanakaya anayefuata. Ikiwa taarifa haikutolewa, weka geresho 2.

**Swali la 10:** Swali hili linauliza sababu iliyosababisha kutokutoa taarifa polisi juu ya uhalifu.

# Sehemu H : Uhakika wa Chakula

---

**Sehemu hii inapaswa kuulizwa kwa ambao wana jukumu kubwa la kuandaa chakula cha kaya.**

Mwanzoni mwa sehemu hii, ni muhimu kumkumbushia mhojiwa juu ya madhumuni ya utafiti huu. Wahojiwa wanaweza kufikiria kuwa kutoa taarifa fulani (zisizo sahihi) zitawawezesha kupata huduma/bidhaa fulani zitakazowawezesha kupata mabadiliko chanya kwenye viwango vyao veya maisha.

**Swali la 1:** Katika siku 7 zilizopita, uliwahi kuwa na wasi wasi kuwa kaya yako haitakuwa na chakula cha kutosha? Swali hili linataka kujua kama kaya ina wasi wasi na kiasi cha chakula walichokula siku saba zilizopita.

**Swali la 2:** Ikiwa jibu la swali hili ni  $\frac{1}{2}$  (Ndiyo) au  $\frac{2}{2}$  (hapana), vipengele A-H bado vinapaswa kuulizwa. Inawezekana kuwa mhojiwa anasema hawakuwa na wasi wasi wowote katika siku 7 zilizopita juu ya kuwa na chakula cha kutosha ( $\frac{1}{2}$  hapana  $\frac{1}{2}$  katika swali la 1), lakini kaya bado ilichukua hatua mbali mbali zilizoorodheshwa katika swali la 2.

**Swali la 3:** Je, ni milo mingapi ukijumuisha na mlo wa asubuhi (kifungua kinywa) kaya yako inapata kwa siku? Swali hili linaulizia kama kaya imekuwa ikipata baadhi ya milo kila siku. Swali hili zaidi linataka kujua kama watoto chini ya miaka 5 wanakula idadi ya milo sawa na walio na umri zaidi ya miaka 5. Ikiwa hivyo, kama wanakaya wote wanakula idadi sawa ya milo, safu wima zote mbili zitakuwa na majibu sawa, kinyume chake ni sahihi, kama wanakaya wana idadi tofauti ya milo kwa siku.

**Swali la 4:** Ni, chakula gani watoto wako wa chini ya miaka 5 (miaka 0- 4) walikula katika mlo wa asubuhi jana? Swali hili linataka kufahamu chakula cha asubuhi walichokula watoto walio na umri chini ya miaka 5 siku hiyo hiyo kabla ya mahojiano. Tumia mageresho kujaza swali hili kuhusiana na chakula cha asubuhi. Kama hakuna watoto wa umri chini ya miaka 5 katika kaya, andika  $\frac{1}{2}$  000.ö

**Swali la 5:** Ni, chakula gani watoto wako wenyе umri wa miaka kati ya 5 na 13 walikula katika mlo wa asubuhi jana? Swali hili linataka kujua chakula walichokula kama mlo wa asubuhi watoto wenyе umri wa miaka 5-13 siku hiyo, kabla ya mahojiano. Kama hakuna watoto wenyе umri huo wa miaka 5-13 katika kaya, andika  $\frac{1}{2}$  000.ö

**Swali la 6:** Je, wanakaya wote hula chakula cha aina moja? Uliza kama wanakaya wote kwa makadirio wanakula chakula/mlo wa aina moja. Kama mwanakaya mmoja hapendi kula ndizi, na badala yake anakula wali, hiyo kwa makadirio ihesabike kuwa wote wanakula chakula cha aina moja. Na jibu lake linapaswa kuwa  $\frac{1}{2}$  ndiyo  $\frac{1}{2}$  Kama mmojawapo wa wanakaya, ana matatizo ya tumbo kiasi kwamba hawesi kula samaki na badala yake anakula kuku, hiyo bado ielewewe kama chakula cha aina moja na jibu lake linapaswa kuwa  $\frac{1}{2}$  ndiyo  $\frac{1}{2}$  Kama ni ndiyo, weka geresho  $\frac{1}{2}$  na nenda swali la 8. Kama ni hapana, weka geresho  $\frac{2}{2}$  na uende swali linalofuatia.

**Swali la 7:** Ni nani katika kaya kawaida hula mlo wa vyakula vya aina nyingi au mlo wa vyakula vya aina chache? Andika mwanakaya ambaye hula vyakula vya aina nyingi na vya aina chache katika kaya. Chakula cha aina nyingi, kitatushisha vyakula vingi kutoka kwenye aina nyingi za vyakula kama wanga, protini, mboga za majani, vitu vitamu. Andika kama wanaume, wanawake na watoto (wa miezi 6-59) wanakula vyakula vya aina nyingi au aina chache. Kama hakuna wanakaya wa kundi lolote kati ya makundi hayo (kama vile hakuna wanawake katika kaya), andika  $\frac{1}{2}$  000 ö kwa kundi hilo.

**Swali la 8:** Katika miezi 12 iliyopita, uliwahi kuwa katika hali ya kukosa chakula cha kutosha kulisha kaya yako? Ulizia kama kaya imepata matatizo ambapo hawakuwa na chakula cha kutosha kulisha kaya katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Kama ndiyo, weka geresho  $\frac{1}{2}$  ö Kama hapana, andika geresho  $\frac{2}{2}$  na nenda sehemu inayofuatia.

**Swali la 9:** Hali hii ilitokea lini? Hapa unapaswa kuandika miezi ambayo kaya haikuwa na chakula cha kutosha kulisha wanakaya wote. Ulizia tu katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, hivyo kama unafanya mahojiano mwezi wa Oktoba 2014, anza kuulizia hali hiyo kwa kuanzia mwezi Oktoba 2013. Kama unafanya mahojiano mwezi wa tatu (Machi ) 2015, anza kwa kuulizia hali hiyo kwa kuanzia mwezi Machi 2014.

**Swali la 10:** Nini ilikuwa sababu ya hali hii? Elezea sababu ya kukosa chakula kwa ajili ya kaya katika miezi iliyopita. Tumia mageresho yaliyo chini ya ukurasa wa dodoso. Chagua mpaka sababu 3 kwa kufuata umuhimu wake.

## Sehemu I: Makazi, Maji na Usafi

---

Sehemu hii inahusu huduma ambazo kaya inatumia katika makazi yao. Sehemu hii inapaswa kuulizwa kwa mwanakaya ambaye ana ufahamu mkubwa kuhusiana na masuala ya huduma hizi.

**Swali la 1:** Je, nani anayemiliki makazi ambamo kaya hii inaishi? Swali hili linahitaji kujua umilikaji wa jengo linalokaliwa na kaya. Jengo linaweza kuwa ni mali ya kaya, la kupangishwa (jengo zima au sehemu yake), la kupangiwa na mwajiri, n.k. kama ilivyoonyeshwa katika dodoso. Jaza mageresho kutokana na jibu toka kwa mhojiwa. Kumbuka kuwa linapojoitokeza geresho la 2 & 4 utaacha swali la pili na kujibu swali la tatu. Kumbuka kama jibu ni 3 au 5 utakwenda swali la 4, na kama ni 6 utaenda swali la 5.

**Swali 2:** Je, kaya ina hati au umiliki wa aina gani wa nyumba inamoishi? Muulize mhojiwa kuhusu hati miliki ya nyumba yake. Kama nyumba ni ya kupangisha, muulize mhojiwa kuhusiana na mkataba wa kupangisha na kumbuka geresho ni 9. Kama ni aina ya mkataba ambao haukueleze hapa kwenye orodha, weka geresho namba 8 na uandike aina ya mkataba huo kwa maneno. Kama kaya haina umiliki wa aina yejote , andika geresho la 10. Kwa jibu lolote nenda swali la 4.

**Swali 3:** Je, kaya hii inalipa kodi kiasi gani kwa mwezi? Swali hili linaulizia kiasi cha kodi inayolipwa kwa ajili ya pango, au ni kiasi gani kaya inalipa kwa mwezi kwa jengo lote inalolitumia. Kama kodi inalipwa na mwajiri, andika kiasi cha fedha kinacholipwa kwa nyumba hiyo.

**Swali 4:** Kadiria gharama ya kodi kwa mwezi ambayo ungepokea ikiwa ungekuwa umekodisha makazi haya? Swali hili linalenga kufahamu kuwa kaya ingeweza kupata kiasi gani kwa mwezi ikiwa ingekodisha makazi hayo.

**Swali 5:** Katika mwaka uliopita, uligharamia kiasi gani kufanya marekebisho ya makazi yako? Swali hili linalenga kufahamu gharama zilizotumika kufanya marekebisho ya makazi katika mwaka uliopita.

**Swali 6:** Katika mwaka uliopita uligharamia kiasi gani kuboresha nyumba yako (ukiondoa gharama nyingine zozote ulizozitaja kwenye maswali yaliyotangulia)? Swali hili linalenga kufahamu gharama zilizotumika kuboresha makazi kwa mwaka uliopita bila kuhusisha gharama za maswali yaliyopita.

**Swali 7:** Kuna vyumba vingapi nya kuishi vilivyopo katika kila nyumba inayotumiwa na kaya hii? Hapa kinachohitajika ni idadi ya vyumba vinavyotumiwa na kaya. Kumbuka idadi hii ya vyumba haitatushisha stoo, choo, bafu, kumbi na baraza. Jumuisha tu vyumba vinavyotumiwa na kaya kama sebule, chumba cha kulia na jiko. Kama kuna nyumba kuu na nyumba nyingine, tofautisha jumla ya idadi ya vyumba kama inavyoonyeshwa katika swali hili. Kama kuna nyumba nyingine zaidi ya 1, jumlisha idadi ya vyumba vinavyopatikana katika nyumba hizo na weka jumla yake katika nyumba kuu.

**Swali 8:** Je, ni vifaa gani vilivyotumika kujengea kuta za nyumba kuu? Vifaa nya ujenzi wa ukuta ni pamoja na miti, mbao, udongo, udongo na miti, matofali ya udongo/saruji, n.k. kama ilivyoonyeshwa katika dodoso. Jaza geresho husika kama ilivyoonyeshwa hapo chini. Kama mhojiwa atataja kifaa ambacho hakipo katika orodha, jaza nyingine (geresho 7) kisha itaje. Katika awamu iliyopita, kulikuwa na majibu yaonyingine mengi kwa swali hili, ambayo kiuhalisi yalitakiwa kujumuishwa katika mojawapo ya mageresho yaliyotajwa

hana. Hii inachukua muda mrefu kurudia na kuweka mageresho upya. Hivyo mdadisi anatakiwa kufanya juhudhi za kutumia mageresho yaliyopo, atatumia geresho la önyingineö endapo tu geresho lililotajwa halipo kwenye orodha.

**Swali 9:** Ni vifaa gani vilivyotumika kuezekea nyumba kuu? Swali hili linalenga kufahamu vifaa vilivyotumika kuezekea, inahusisha :nyasi, mianzi, tiles kama ambavyo mageresho yalivyo kwenye maswali, mhojiwa akitaja kitu ambacho hakipo kwenye geresho jaza -7øna utaje.

**Swali 10:** Ni vifaa gani vilivyotumika kusakafia nyumba kuu? Hapa vinahitajika vifaa vilivyotumika kusakafia nyumba /jengo kuu linalotumiwa na kaya. Vifaa hivyo ni pamoja na udongo, zege, saruji na vifaa vinginevyo kama vile vipande vya mbao, n.k. Angalia geresho la vifaa hivyo hapo kwenye dodoso. Kama mhojiwa atataja kifaa ambacho hakipo katika orodha jaza önyingineö (geresho 3) na andika kifaa hicho kwa maneno.

**Swali 11:** Je, katika kaya hii, taka taka zinatupwaje? Swali hili linahusu mazingira, linalenga kufahamu ni jinsi gani kaya inahifadhi/tupa taka zake, kama kaya inatumia njia ambazo hazipo kwenye mageresho jaza geresho -6øna taja njia hiyo.

**Swali 12:** Je, ni nini aina kuu ya choo kinachotumiwa na kaya hii kwa kawaida? Swali hili linaulizia aina ya choo kinachotumiwa na kaya. ØHakuna chooø inahusisha matumizi ya vichaka, sehemu zenye majani na maeneo mengine ya wazi kama vyoo. Kwa mageresho ya pili, tatu, nne yanaelezea vyoo ambavyo vimechimbwa na kinyesi kinaenda moja kwa moja kwenye shimo, vyoo hivyo ni kama; Choo cha wazi kisicho na mfuniko, choo cha shimo chenye mfuniko (kisichosafishika), Choo cha shimo chenye mfuniko (kinachosafishika)Ø Kwa ØChoo cha kuvutaø ni aina ya choo ambacho kina sifa kwamba kinyesi cha binadamu kinaondolewa kwa kumwagiwa maji kwa mfumo maalumu. ØChoo cha kumwaga majiøkinafanana na choo cha kuvuta, ila hapa maji humwagwa kwa kutumia vyombo kama ndoo n.k. ili kuondoa kinyesi ØChoo cha shimo cha kisasaø ni kile kilichojengengewa bomba la kutoa harufu ambacho kinatafsiriwa choo cha namna ya kutupa kinyesi katika hali ya usafi, cha gharama ndogo na kinachokubalika. Sura za kimsingi za choo cha VIP ni kwamba kina jengo lililojengengwa kikamilifu (ukuta na paa) na kipenyo cha 110mm hivi, bomba la PVC la kutolea hewa chafu lililosimamishwa kuelekea nje ili kutoa hewa kupitia kwemue paa kwenda nje. Mara nyingi vyoo hivi vimejengwa kwa mfuniko wa zege wenyre shimo. ØEcosan (choo cha ekologia)Ø ni aina ya choo ambacho hutofautisha kinyesi cha binadamu kilicho kigumu na kile kilaini, ambapo hutumiwa kwa kunyeshea na mbolea kwa mimea. -Choo cha shimo cha kawaida (kilicho na sakafu isiyosafishika)Ø ni choo cha shimo kilichojengengwa bila kufuata kanuni zinazoambatana na usafi. Sakafu ya choo imetengenezwa kwa udongo au aina nyingine ya sakafu ambayo haiwezi kusafishika kwa urahisi. ØChoo cha shimo cha kawaida (kilicho na sakafu inayosafishika) ni choo ambacho kimesakafiwa na zege au aina sakafu ya aina nyingine inayofanana na zege. Angalia pitcha kwenye viambatanisho kwa maelezo zaidi yanayohusiana na aina ya vyoo.

**Swali 13:** Je, kaya yako huchangia choo na kaya nyingine? Uliza kama kaya inashirikiana choo na kaya nyingine. Jaza -1økama ndiyo na -2økama hapana nenda swali la 15.

**Swali 14:** Je, ni kaya ngapi zingine zinatumia choo hiki? Jaza idadi ya kaya zinazotumia choo (zinazoshirikiana choo).

**Swali 15:** Je, mara ya mwisho mtoto mdogo kabisa wa kaya hii alipojisaidia, nini kilifanywa ili kutupa kinyesi hicho? Ni jinsi gani choo/kinyesi cha watoto kinahifadhiwa,tumia mageresho yaliyopo kwenye swali, kama kaya haina watoto, jaza -8ø

**Swali 16:** Je, ni nini nishati kuu ya kupikia? Swali hili linahitaji kufahamu kaya inatumia nishati gani kwa kupikia, kama kaya inatumia nishati ambayo haipo kwenye orodha jaza geresho -8øna andika aina hiyo kwa maneno.

**Swali 17:** Je, ni nini aina kuu ya nishati kwa ajili ya kuangazia? Swali hili linahitaji kufahamu kaya inatumia nishati gani kwa kuangazia ndani ya nyumba. Tumia mageresho yaliyoorodheshwa katika dodoso hili. Kama kaya inatumia nishati ambayo haikuorodheshwa hapa jaza geresho 9 na iandike kwa maneno.

**Swali 18:** Ni nini chanzo kikuu cha umeme wa kaya yako? Swali hili linahitaji kujua chanzo cha umeme unaotumika katika kaya hii. Tumia mageresho yaliyoorodheshwa hapa. Kama kaya inatumia chanzo cha umeme ambacho hakikuorodheshwa hapa jaza 7 na andika chanzo hicho kwa maneno.

**Swali 19:** Je, nini chanzo kikuu cha maji ya kunywa katika msimu wa masika? Swali hili linaulizia chanzo kikuu cha maji ya kunywa yanayotumiwa na kaya katika kipindi cha masika. Tumia mageresho yaliyopo chini kwenye ukurasa huu. Ukijaza geresho 012ö hakikisha umeandika chanzo hicho kwa maneno. Kama kuna vyanzo zaidi ya viwili, taja kile kinachotumika mara kwa mara. Ukijaza geresho 08ö nenda swali la 25.

**Swali 20:** Swali hili linauliza chanzo kikuu cha maji kinapopatikana katika msimu wa masika. Ikiwa chanzo cha maji ni cha jumuiya, weka geresho 4. Na hii itatokea iwapo chanzo cha maji kitakuwa kwenye ziwa, dimbwi, mito au mifereji.

**Swali 21:** Andika utambulisho wa mwanakaya kutoka katika roster ambase huwa anaenda kuchota maji katiika msimu wa masika. Jina la mwanakaya huyu litumike pia katika kujibu swali la 22 na 23. Ikiwa hakuna mwanakaya nayekwenda kuchota maji, andika 099ö. Kwa mfano, Kama kaya ina bomba la maji ndani ya nyumba, hakuna mwanakaya anayechota maji ya kunywa. Kwa mantiki hii, utaandika 099ö kwa swali hili.

**Swali 22:** Je, inachukua muda gani kwenda na kurudi, kuchota maji ya kunywa ya nyumbani katika msimu wa masika? Swali hili linaulizia muda unaotumiwa na kaya kwenda na kurudi kuchota maji katika kipindi cha masika (kama ilivyoelezewa kwenye swali lililopita). Hapa utajumuisha muda wa kwenda, muda wa kusubiri na muda wa kurudi. Kwa mfano kama kaya inatumia saa 1 na dakika 35, andika dakika 95 kwenye chumba cha dakika. Usiandike dakika 135.

**Swali 23:** Kati ya dakika hizi (MSOME DAKIKA), unachukua muda gani kusubiri hadi unapata maji? Msomee mhojiwa dakika zilizotajwa katika swali la 20, muulize kati ya dakika hizo, ni dakika ngapi anatumia kusubiri kuchota maji. Mhojiwa akijibu katika masaa badilisha katika dakika.

**Swali 24:** Je, kaya hii inachukua hatua zipi ili kuhakikisha usalama wa maji ya kunywa ambayo kaya inatumia? Swali hili linauliza ni njia gani inayotumiwa na kaya kuhakikisha usalama wa maji. Kama hakuna hatua zozote wanazochukua kuhakikisha usalama wa maji, tumia geresho 07ö. Jaza mpaka majibu 2 kwa swali hili. Picha zinazoonyesha njia tofauti za kuhakikisha usalama wa maji zimeonyeshwa kwenye kiambatanishi katika mwongozo huu.

**Swali 25:** Nini chanzo kikuu cha maji kinachotumiwa na kaya yako kwa matumizi mengine kama, kupikia na kunawa mikono? Andika chanzo kikuu cha maji kinachotumika kwa matumizi mengine kama kupikia na kufulia kinachotumiwa na kaya kwa kipindi cha masika.

**Swali la 26:** Swali hili linauliza ni kiasi gani cha fedha kwa wastani kaya inatumia katika matumizi yote ya maji kwa wiki wakati wa msimu wa masika. Ikiwa kaya ina bomba la maji, uliza ni kiasi gani cha fedha wanalipa katika mamlaka husika (mfano, DAWASCO). Mdodose mhojiwa ajumuhihe gharama za usafirishaji kwa wale wanaoletewa maji. Ikiwa kaya haikutumia chochote kwa ajili ya maji, weka 0ö. Muulize akadirie gharama zisizokuwa za fedha alizotumia kwa ajili ya maji.

**Swali la 27:** Swali hili linauliza ikiwa kaya imetumia chanzo kilekile cha maji ya kunywa wakati wa msimu wa kiangazi kama ilivyokuwa msimu wa masika. Ikiwa chanzo ni kilekile, weka gersho 1 na nenda sehemu inayofuata (Sehemu J). Ikiwa chanzo ni tofauti, weka geresho 2öna endelea na swali la 28.

**Swali la 28:** Swali hili linauliza sababu kuu ya kaya kutumia chanzo tofauti cha maji ya kunywa wakati wa msimu wa kiangazi.

**Swali la 29:** Swali hili linaulizia chanzo kikuu cha maji ya kunywa yanayotumiwa na kaya katika kipindi cha kiangazi. Angalia swali la 19 kwa ajili ya ufanuzi zaidi wa swali hili.

**Swali la 30:** Swali hili linauliza chanzo kikuu cha maji kinapopatikana katika msimu wa kiangazi. Angalia swali la 20 kwa ajili ya ufanuzi zaidi wa swali hili.

**Swali la 31:** Swali hili linaulizia nani huwa anaenda kuchota maji katika msimu wa kiangazi. Andika utambulisho wa mwanakaya kutoka kwenye roster ambaye huwa anaenda kuchota maji. Angalia swali la 21 kwa ajili ya ufanuzi zaidi wa swali hili.

**Swali la 32:** Swali hili linaulizia muda unaotumika kwenda na kurudi kuchota maji kutoka kwenye chanzo hadi kwenye makazi katika kipindi cha kiangazi. Angalia swali la 22 kwa ajili ya ufanuzi zaidi wa swali hili.

**Swali la 33:** Swali hil linauliza muda unaotumika wakati wa kusubiri na kuchota maji katika kipindi cha kiangazi. Angalia swali la 23 kwa ajili ya ufanuzi zaidi wa swali hili.

**Swali la 34:** Je, kaya hii inachukua hatua zipi ili kuhakikisha usalama wa maji ya kunywa ambayo kaya inatumia wakati wa kipindi cha kiangazi. Angalia swali la 24 kwa ajili ya ufanuzi zaidi wa swali hili.

**Swali la 35:** Nini chanzo kikuu cha maji kinachotumiwa na kaya yako kwa matumizi mengine kama, kupikia na kunawa mikono? Andika chanzo kikuu cha maji kinachotumika kwa matumizi mengine kama kupikia na kufulia kinachotumiwa na kaya kwa kipindi cha kiangazi.

**Swali la 36:** Swali hili linauliza ni kiasi gani cha fedha kwa wastani kaya inatumia katika matumizi yote ya maji kwa wiki wakati wa msimu wa kiangazi. Angalia swali la 26 kwa ajili ya ufanuzi zaidi wa swali hili.

## Sehemu J: Matumizi ya Chakula kwa Wiki Moja Iliyopita

---

Sehemu hii tutaangalia matumizi ya chakula kwa kaya ambayo ni bidhaa za nafaka, vyakula vya wanga wa mizizi, sukari na bidhaa za sukari, mazao jamii ya kunde, nazi na mbegu, mbogamboga, matunda, nyama/kitoweo, maziwa na bidhaa za mazao yatokanayo na maziwa, mafuta ya kula na samli, viungo, mahitaji ya vinywaji vya chai na vinywaji baridi, chai na kahawa. Maswali haya yanahitaji kujua kama kaya imetumia mazao/bidhaa mojawapo kati ya hizi kwa kipindi cha siku 7 zilizopita.

**KUMBUKA:** sehemu hii inapima kile kaya imetumia. Maswali haya yanaulizia kile ambacho kaya imetumia (imepika na kula), na sio ambacho kaya imenunua au kuzalisha. Kwa mfano kaya imenunua kilo 50 za mchele kwa mwezi huu kwa Tsh 35,000/= na wanatumia kilo 1.5 kwa siku. Katika siku 7 za wiki hakuna manunuzi, itakuwa wametumia  $7 * 1.5\text{kg} = 10.5\text{kg}$  za mchele. Kinachotakiwa ni kilo 10.5kg ambazo kaya imetumia. Unatakiwa kujua kiasi cha pesa kaya ilitumia kutoka katika kilo 10.5 (Tshs 35,000/50kg= Tsh 700. kwahiyo kwa kilo 10.5 kiasi cha pesa ni Tsh  $700 * 10.5 = \text{Tsh } 13,500 =$ )

**MAELEZO KUHUSU VIPIMO VYA KIENYEJI:** Wahojiwa wanaweza kutoa majibu katika vipimo vya kienyeji. Kama hawataweza kubadilisha vipimo hivi kwenda vipimo vya kawaida (vilivyoordheshwa kwenye dodoso), unapaswa kuandika majibu katika vipimo vya kienyeji. Wewe na msimamizi wako mnapaswa kupima vipimo hivi vya kienyeji (kama mafungu, vibaba, pawa, n.k) na kujua uzito halisi kama vile kilogram, gram, n.k. kabla ya kuondoka eneo la kazi.

Pia kuwa mwangalifu na geresho la 5 (idadi) katika swali la vipimo. Hili litumike tu kwa bidhaa ambazo zina ukubwa unaokaribiana na ambavyo havitofautiani kutoka eneo moja/kijiji kimoja na eneo lingine/kijiji kingine. Bidhaa zifuatavyo zinaweza kuwa katika vipimo vya kienyeji pale inapobidi. Vitu vingine vyote

vinapaswa kubadilishwa viwe katika vipimo vya kawaida (grams, kilograms, lita, mililita) kabla ya kuondoka eneo la kazi au kijiji cha kazi.

0807	Mayai
------	-------

**MAELEZO KWA WASIMAMIZI:** Angalia matumizi ya majibu ya vitu/bidhaa<sup>katika</sup> sehemu  $\frac{1}{2}$  mara tu baada ya mahojiano kukamilika na hakikisha kuwa wewe au mdadisi unapima vitu katika kaya au sokoni na kubadilisha katika vipimo vya kawaida (kilo, grams n.k.).

**Kwa mfano:**

Kaya inaweza kusema kuwa walikula mikate mitano waliyonunua sokoni. Nenda sokoni na upime mkate mmoja. Kama mkate una gram 150, jumla ya matumizi kwa kaya itakuwa  $5 \times 150$  grams = 750 grams.

Kaya inaweza kusema kuwa ilitumia vitunguu vitatu (3) na nyanya sita (6). Kama kaya bado ina vitunguu na nyanya kutoka kwenye bustani yake ambavo/ambazo zinafanana na vile vilivyotumika, unatakiwa uvipime. Kama kila kitunguu kina uzito wa gramu 200 na kila nyanya ina uzito wa gramu 125, basi jumla ya matumizi kwa bidhaa ya 0601 katika sehemu K ni  $(3 \times 200 \text{ grams}) + (6 \times 125 \text{ grams}) = 1,350 \text{ grams}$  au 1.35 kg.

**Safuwima 1:** Katika siku 7 zilizopita, wanakaya wenu walitumia mazao/bidhaa zifuatazo kwa ajili ya chakula ndani ya kaya?

Unachotakiwa kufanya wewe mdadisi ni kuandika geresho  $\frac{1}{4}$  endapo kaya ilitumia mazao/bidhaa husika na geresho  $\frac{2}{3}$  endapo kaya haikutumia mazao/bidhaa husika. Jaza vyakula vilivyoliwa ndani ya kaya tu na usijaze vilivyoliwa nje ya kaya. Uliza swali hili kwa vyakula vyote kuanzia geresho 101-1108 kabla ya kuuliza safuwima 2.

**ZINGATIA:** ÕSiku saba zilizopitaö ina maana ya siku saba kuishia jana. Kama mahojiano yanafanyika Jumanne, siku saba zilizopita zitaanza Jumanne iliyopita mpaka Jumatatu, siku moja kabla ya siku ya mahojiano, NA SIO juma/siku saba za kalenda zilizopita.

**Safuwima 2:** Je, kaya yenu ilitumia kiasi gani kwa jumla katika kipindi cha siku 7 zilizopita?

Uliza kwa lile lenye jibu la ndio kwenye safuwima 1, Jaza ni kiasi gani kwa jumla kaya ilitumia kwa siku 7 zilizopita. Ukijumuisha kile ambacho kaya imenunua, imezalisha, na zawadi. Hakikisha unakuwa mwangalifu katika vipimo, inawezekana kaya kutumia gram 300 kwa wiki na si kilo 300 kwa wiki.

**Safuwima 3:** Je, ni mlinunua kiasi gani katika siku 7 zilizopita?

Utajaza jumla ya kiasi ambacho kaya imenunua katika siku 7 zilizopita. Kuwa mwangalifu na vipimo.

**Safuwima 4:** Andika jumla ya kiasi cha fedha kaya ilitumia kununua chakula/bidhaa katika siku 7 zilizopita.

**Safuwima 4\_1:** Andika mahali bidhaa iliponunuliwa. Ikiwa bidhaa ililinunuliwa zaidi ya sehemu moja, andika mahali ambapo kiasi kikubwa cha bidhaa kiliponunuliwa. Swalii hili ni kwa ajili ya bidhaa nne tu: unga wa mahindi, unga wa ngano, mafuta ya kupikia na chumvi. Kwa bidhaa nyingine zote, nenda sehemu nyingine.

**Safuwima 5:** Je, ni kiasi gani mlichotumia kilitokana na uzalishaji wa kaya?

Hapa unatakiwa kujaza kiasi kile tu ambacho kaya ilitumia siku saba zilizopita lakini kilitokana na uzalishaji wa kaya. Zingatia kuwa õuzalishaji wa kayaö inahusisha bidhaa zote zilizokusanywa kutoka msituni au kutoka ardhi ya umma, kama vile nazi, dawa za mitishamba, n.k.

**Safuwima 6:** Ni kiasi gani mlichotumia kilitokana na zawadi na vyanzo vingine?

Muulize mhojiwa endapo katika siku 7 zilizopita kama kaya ilipokea zawadi yoyote ya mazao/bidhaa husika. Kama atajibu ndiyo kaya ilipokea, muulize ni kiasi gani kimetumika kati ya kile kilichopokelewa.

**Kumbuka:** Hakikisha kuwa jumla ya uzito ni sahihi Swali la 2 = Swali la 3 + Swali la 5 + Swali la 6. Kama kuna tofauti kubwa, unatakiwa kumuuliza mhojiwa upate uafanuzi.

KAMA mhojiwa amejibu öndiyoö kwa swali la 1, hakikisha unajibu katika safuwima husika kwa kila chakula. Kwa mfano kaya imejibu öndiyoö imetumia mahindi mabichi, ingawa mahindi mabichi yametoka shambani (safuwima 5) hakikisha unaweka öø katika safuwima 3 na 6. Hutakiwi kuweka kipimo kama kiasi ni öø Hautakiwi kuweka kiasi cha pesa (safuwima 4) kama bidhaa hajjanunuliwa.

Angalia mfano ukurasa unaofuatia:

SEHEMU J1: MATUMIZI YA CHAKULA KWA WIKI MOJA ILIYOPITA		SWALI 3, 5, 6: TUMIA GERESHO TOKA SW.2									
G E R E S H O		1 Katika siku 7 zilizopita, wanakaya wenu walitumla mazao bidhaa zifutazo kwa ajili ya chakula ndani ya kaya?  <b>JAZA VYAKULA VILIVYOLIWA NDANI YA KAYA TU NA UBIJAZE VILIVYOLIWA NJE YA</b>  ULIZA SWALI HILI KWA VYAKULA VYOTE KABLA YA KUULIZA MASWALI MENGINE KWA VYAKULA VYENYE JIBU LA NDIO	2 Je, kaya yenu litumua kiasi ganjil kwa jumla katika kipindi cha siku 7 zilizopita?  <b>KIPIMO KILO.....1 GRAM.....2 LITA.....3 MILILITA..4 IDADI.....5</b>  NDIYO..1 HAPANA..2 (WING'INE)	3 Je, ni milinunua kiasi ganjil katika siku 7 zilizopita?  <b>KAMA HAKUNA, JAZA '0' KATIKA KIASI NA ACHA WAZI KATIKA KIPIMO ► 8w. 6</b>	4 Je, ni kiasi gani mligharamia?  <b>SWALI HILI LINAHUSU KIASI KILICHOONYE&amp;HWA KATIKA SWALI 3</b>	5 Je, ni kiasi ganjil milchotumia kilitokana na uzalishaji wa kaya?  <b>KAMA HAKUNA, JAZA '0' KATIKA KIASI NA ACHA WAZI KATIKA KIPIMO</b>	6 Ni kiasi ganjil milchotumia kilitokana na zawadi na vyanzo vingline?  <b>ONDOA VYAKULA VILIVYOLIWA NJE YA KAYA</b>  <b>KAMA HAKUNA, JAZA '0' KATIKA KIASI NA ACHA WAZI KATIKA KIPIMO</b>				
<b>Bidhaa za Nafaka</b>											
101	Mpunga	1	1	2.5	1	1	800	1	0.5		0
102	Mchele	2									
103	Mahindi mabichi	1	2	400	0			2	400		0

**Swali la 7:** Swali hili linapima kiwango cha madini joto kwa chumvi za kaya. Omba kijiko kidogo cha chumvi kaya inachokitumia kwenye chakula. Tumia kipimo cha kupimia kiwango cha madini joto kulingana na maelekezo yaliyotolewa kwenye kifaa husika. Hii inajumuhisha kuongeza matone ya iodine katika sampuli ya chumvi, na kulinganisha rangi iliyotokea na ile inayoonekana katika mchoro. Andika ppm ya iodine katika hiyo chumvi baada ya kulinganisha na rangi ya chumvi katika mchoro.

**Swali 8:** Katika siku 7 zilizopita, ni siku ngapi wewe au mwanakaya mwingine mlitumia chochote kati ya [...]?

Swali hili linalenga kufahamu idadi ya siku ambazo kaya ilitumia chakula cha aina hiyo. Kama kaya ilikula maembe kila siku katika siku saba, kwahiyo 7 itaandikwa F-matunda, kama kaya ilikula wali siku 3 na mahindi siku 3, andika 6 kwenye safu mlalo A-Nafaka, mbegu na bidhaa zitokanazo na nafaka.

**Swali 9:** Katika siku 7 zilizopita, kuna watu wowote wasio wanakaya ambao walikula mlo wowote hapa kwenye kaya yenu?

Katika swali hili unatakiwa kumuuliza mhojiwa kama kuna mtu yeyote ambaye si mwanakaya alikula pamoja na wanakaya hata kama ni mlo mmoja kati ya milo inayopatikana kwenye kaya ndani ya siku 7 zilizopita. Kama atajibu ndiyo, utaandika geresho öøna kama hapana öøna nenda sehemu inayofuata.

**Swali 10:** Je, ni [...] wangapi walikula chakula kwa pamoja katika siku 7 zilizopita?

Mhojiwa akutajie jumla ya watu waliokula nao (WASIO WANAKAYA). Zingatia kuandika kwa kuwatenganisha watu hao katika makundi ya miaka kama ilivyoainishwa katika kipengele A, B, C & D.

**Swali la 11:** Ni milo mingapi kwa ujumla mlikula na [WASIO WANAKAYA] katika siku 7 zilizopita? Pia dadisi idadi ya milo waliyokula na hawa (WASIO WANAKAYA). Jaza kama ulivyojaza swali 10.

# **Sehemu K : Matumizi Yasiyo ya Chakula – Wiki Moja na Mwezi Mmoja**

---

## **Kumbukumbu ya Wiki Moja**

**Swali 1 & 2:** Kwa vitu vilivyoorodheshwa hapo chini, msomee mwanakaya/mhojiwa kitu kimoja baada ya kingine (yaani geresho 101-103), umuulize kama alitumia katika siku 7 zilizopita. Kama atakujibu alitumia kwenye kitu husika utajaza geresho la -1Ø na utajaza kiasi cha jumla ya shilingi alizotumia kwa ajili ya kununua/kulipia kitu hicho katika swali la 2, kama hapana andika geresho la -2Ø

**ZINGATIA:** õSiku saba zilizopitaö ina maana ya siku saba kuishia jana. Kama mahojiano yanafanyika Jumanne, siku saba zilizopita zitaanzia Jumanne iliyopita mpaka Jumatatu, siku moja kabla ya siku ya mahojiano, NA SIO juma/siku saba za kalenda zilizopita.

## **Kumbukumbu ya Mwezi Mmoja**

**Swali 1 na 2:** Pia swali hili utauliza mwanakaya/mhojiwa kama alinunua vitu vilivyoorodheshwa hapo chini katika kipindi cha mwezi mmoja uliopita. Msomee mhojiwa kitu kimoja baada ya kingine kuanzia geresho la 201-223, akijibu ndiyo alinunua kwenye kitu husika utaandika geresho la 1 na utajaza kiasi cha shilingi kilichotimika kwa jumla kukipata kitu hicho, kama ni hapana utajaza geresho la 2. Hakikisha umemsomea vitu vyote bila kusahau hata kimoja.

**ZINGATIA:** õSiku 30 zilizopitaö katika sehemu ya K ina maana ya siku 30 kuishia jana. Kama mahojiano yanafanyika Aprili 16, siku 30 zilizopita zitaanzia Machi 16 mpaka Aprili 15, siku moja kabla ya siku ya mahojiano, NA SIO mwezi wa kikalenda uliopita.

# **Sehemu L : Matumizi Yasiyo ya Chakula Miezi 12 Iliyopita**

---

**Swali 1 & 2:** Kwa vitu vilivyoorodheshwa hapo chini, msomee mwanakaya/mhojiwa kitu kimoja baada ya kingine (yaani kuanzia geresho la 301-326), umuulize kama alitumia katika miezi 12 iliyopita. Kama atakujibu alitumia kwenye kitu hicho utaandika geresho la 1 na kujaza kiasi alichotumia kununua kitu hicho. Kama hapana andika geresho la 2, nenda kitu kingine.

Vitu visivyo chakula vinavyoweza kupatikana bila kununua.

**Swali 1:** Katika miezi 12 iliyopita, mlkusanya, mlinunua au mlilipia vitu vifuatavyo? Muulize mwanakaya/mhojiwa kama alikusanya, alinunua au alilipia vitu vivyoorodheshwa hapo katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Kwa kila kitu atakachosema ndiyo utaandika geresho la 1, hapana utaandika geresho la 2.

**Swali 2 & 3:** Katika safuwima ya 2 & 3 inategemea majibu ya swali lililopita.

Kama jibu ni ndiyo (geresho la -1Ø), safuwima 2 utaandika makadirio ya thamani ya kitu alichotumia. Kwa mfano; mhojiwa anakujibu kuwa alitumia lundo moja la mianzi, itakubidi umuulize kwa kukadiria thamani ya mianzi hiyo inaweza kugharimu shilingi ngapi. Hicho kiasi atakachokutaja ndicho kitakachoandikwa katika safuwima ya 2. Pia muulize kama angepeleka sokoni mianzi hiyo angeiuza kwa shilingi ngapi.

Unapojibu maswali haya, kumbuka utaratibu ufuatao:

Swali la 2 linahusu bidhaa zote zilizotumika, ikiwa zimenunuliwa au kutoka kwenye uzalishaji wa kaya.

Jibu la swali la 2 mara zote litakuwa kubwa au sawa na jibu la swali la 3.

Kwa mfano, kama mtu amenunua kilo 50 za kuni kwa shilingi 3,000 na kukusanya mwenyewe kilo zingine 50, utajaza shilingi 6,000 kwenye swali la 2 (thamani ya kilo 100) na shilingi 3,000 kwenye swali la3 kwa kuni ambazo zilinunuliwa.

## Sehemu M : Rasilimali za Kaya

---

Maswali haya yanahusu umilikaji wa rasilimali na vitu vya thamani na vya kudumu kama ilivyooneshwa katika dodoso. Kuna wakati mhojiwa anaweza kuwa na wasiwasi juu ya maswali haya, hivyo basi jitahidi kutumia lugha nzuri kumtoa wasiwasi na kuhakikishia kuwa taarifa hizi ni za siri na zitatumika kwa malengo yaliyokusudiwa na si vinginevyo. Kumbuka maswali haya yanagusa vifaa/rasilimali muhimu ambazo mhojiwa asingependelea kujadili na mtu ambaye hana mazoea naye kabisa.

### Safuwima 1 (geresho 401-453)

Je, kaya hii inamiliki idadi gani ya [KITU]? Unatakiwa kumuuliza kama mhojiwa/wanakaya iwapo kaya inamiliki orodha ya vitu vilivyoordheshwa hapo, msomee kitu kimoja baada ya kingine naye unatakiwa kujibu jumla ya idadi (namba) ya kitu ambacho kaya husika inamiliki na idadi hiyo utaandika katika chumba cha idadi. Kama hakuna utajaza Øø katika idadinenda kitu kinachofuata.

Zingatia: 408 ó jaza idadi ya viti kimoja kimoja na sio idadi ya Øsetiö.

**Swali la 2:** Je, [BIDHAA] ina miaka mingapi? Andika umri wa bidhaa inayomilikiwa na kaya. Kama kaya inamiliki kifaa zaidi ya kimoja andika wastani wake. Mfano kaya inamiliki simu za mkononi moja ina miaka 5, nyingine 2 na nyingine mwaka 1, wastani wa umri itakuwa 2.7, jaza kwenye swali la 2  $(5 + 2 + 1)/3 = 2.667$ .

**Swali la 3:** Je, ulinunua [BIDHAA] hii kwa bei gani? Andika bei ya bidhaa iliyonunuliwa. Kama kayainamiliki zaidi ya kitu kimoja, andika wastani wa bei ya vitu vyote. Mfano kaya ilinunua kiti kwa sh. 90,000 na kingine kwa sh. 75,000 kwahiyio utaandika sh. 82,000 kama wastani wa viti vyote.  $(90,000 + 75,000)/2 = 82,000$ .

**Swali la 4:** Kama ungetaka kuuza [BIDHAA] leo ungepata kiasi gani? Andika kiasi cha bei ambayo kaya ingetaka kuuza bidhaa hiyo kwa sasa / ingeuza kwa bei gani. Usiandike kiasi walicholipia kwa bidhaa hiyo kwani itakuwa tayari imeshaandikwa kwenye swali la 3. Kama kaya ina zaidi ya bidhaa moja andika wastani wa bei ya bidhaa, mfano: mhojiwa amekadiria angeuza kiti kwa sh. 50,000 na kingine kwa sh. 35,000, kwahiyio utaandika sh. 42,500 kwenye swali la 4 kama wastani wa bei  $(50,000 + 35,000)/2 = 42,500$ .

## Sehemu N: Shughuli za Kibashara za Familia / Kaya Zisizo za Kilimo

---

### Maana

Shughuli au b Bashara za kaya ni zile shughuli ambazo zinamilikiwa na kaya au mwanakaya kwa ajili ya kuongeza kipato katika kaya. Zinaweza kuwa si rasmi na hizajiri wafanyakazi au sio zilizosajiliwa rasmi. Kwa mfano shughuli ambazo si za kilimo ambazo mwanakaya anazifanya peke yake na anatoa huduma zitahesabika katika sehemu hii.

Katika sehemu hii tunakusanya taarifa za umiliki na kipato kinachozalishwa tokana na shughuli husika katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Kigezo cha shughuli kuweza kuorodheshwa ni lazima iwe imefanyika hata mwezi mmoja na zaidi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, pamoja na zile zimefanyika katika miezi 12 iliyopita lakini kwa sasa zimefungwa kwa muda au moja kwa moja katika siku ya mahojiano, na zile

hazijamaliza hata mwezi mmoja katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Kimsingi katika sehemu hii lengo ni kupata zile shughuli zinazo fanywa kwa msimu ina maana hazijafanyika miezi 12 yote.

Kaya ambazo zinafanya shughuli ambazo si za kilimo ni pamoja zile zinazotoa huduma au kuzalisha bidhaa, pamoja kumiliki maduka bila kujali ukubwa wa duka. Shughuli hizi zinajumuisha, Kwa mfano kutengeneza mikeka, matofali au mkaa, fundi ujenzi, selemala, kuuza kuni, kazi za vyuma; fundi cherehani, kazi ya kukarabati, watengeneza chakula, biashara ya samaki, wauza vitu vidogovidogo, n.k. mfano wa kaya hizi katika sehemu hii ni kama ifuatavyo:

- Fundi cherehani anashona nguo na kuuza viatu sokoni.
- Mfanya biashara wa kike anayeenda China kununua nguo za biashara na kuuza Dar es Salaam.
- Mfanyabishara anayenunua mahindi vijiji na kusafirisha Dar es salaam.
- Fundi muashi anayefanya kazi katika sehemu tofauti.
- Muuza mkaa anayeuya njiani.
- Mtu binafsi anayemiliki bodaboda/taxi/bajaji.
- Mtu anayechora ramani za nyumba na kutoa ushauri wa kiufundi katika kampuni tofauti na wakati mwengine serikalini kwa miradi mbali mbali.

**Swali la 1a:** Katika kipindi cha miezi 12 iliyopita kuna mwanakaya yoyote aliyejihusisha na shughuli ye yote ya kuingiza kipato isiyokuwa ya kilimo, ufugaji au uvuvi? Swali hili linataka kujua kama katika kipindi cha miezi 12 iliyopita kaya imejihusisha na shughuli yoyote ya kuingiza kipato isiyokuwa ya kilimo. Kama jibu ni ndio jaza geresho namba 1 kisha nenda swali la 2. Kama jibu hapana, jaza geresho namba 2.

**Swali la 1b:** Swali hili haulizwi mhojiwa. Mdadisi angalia swali la 4C na 4D katika sehemu E (ajira) kama kuna mwanakaya aliyejibu ndio swali la 4C au 4D. Kama kuna mwanakaya yoyote kajibu ndio swali la 4C au 4D, jaza geresho namba 1. Kama wanakaya wote wamejibu hapana kwa maswali yote ya 4C na 4D, jaza geresho namba 2 na uende sehemu inayofuata.

**Swali la 2:** Tafadhali naomba unipatie maelezo ya kina kuhusiana na bidhaa au huduma kuu ya kila [SHUGHULI/BISHARA] ambayo kaya yako iliendesha katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Orodhesha taarifa ya shughuli isiyokuwa ya kilimo iliyofanywa na kaya katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Andika maelezo ya bidhaa na huduma kuu isiyokuwa ya kilimo inayotolewa na kaya katika safuwima ya kushoto, na nakili geresho la sekta ISIC katika safuwima ya kulia. Jumuisha shughuli ambazo sasa zimefungwa moja kwa moja au kwa muda lakini zilifanyika miezi 12 iliyopita. Orodhesha hadi shughuli 5 zisizokuwa za kilimo.

**Swali la 3:** Ni wanakaya wapi walijishughulisha na [BIASHARA] hii? Orodhesha namba za wanakaya waliojishughulisha kwa kipindi chochote kile katika miezi 12 iliyopita na shughuli za kaya zisizokuwa za kilimo hata kama walikuwa wakilipwa au hawakulipwa. Orodhesha hadi wanakaya 6. Kama kuna wanakaya zaidi ya 6 waliofanya shughuli hiyo ya kaya isiyokua ya kilimo, orodhesha 6 tu waliotumia muda wao mwangi katika shughuli hiyo.

**Swali la 4:** Ni nani mwendeshaji mkuu wa biashara hii au mwenye ufahamu mkubwa wa biashara hii? Orodhesha namba za wanakaya wanoendesha au wenye ufahamu mkubwa wa biashara hiyo. Orodhesha namba za wanakaya kutoka orodha ya wanakaya, mpaka wawili. Kama wapo zaidi ya wawili, orodhesha wawili wanaotoa maamuzi makubwa kuhusiana na biashara.

**Swali la 5:** Ni nani katika kaya anayemiliki shughuli hii? Orodhesha wanakaya wanaomiliki shughuli hiyo. Jaza namba za wanakaya kutoka kwenye orodha ya wanakaya. Jaza mpaka namba 2 za wanakaya kama biashara inamilikiwa na zaidi ya mtu mmoja katika kaya.

**Swali la 6:** Je, shughuli/biashara hii inafanyikia wapi? Tumia mageresho yaliyoorodheshwa kwenye swali kujua sehemu ilipo. Kama shughuli imehama kwa muda, andika pale kwa kawaida wanapofanya. Kama shughuli haina sehemu maalum, jaza geresho namba 12. Kwa mfano, muuza matunda ambaye anatembeza matunda yake mjini hana sehemu maalum, hii inawekwa geresho namba 12.

**Swali la 7:** Shughuli/biashara hii imedumu kwa muda gani? Andika idadi ya miaka na miezi tangu ameanza kufanya shughuli hii. Sio mwaka alioanza. Kama shughuli hii ilisimama kuendeshwa na ikaanza tena, tarehe inayotakiwa kuitaja ni ya wakati shughuli ilianza uendeshaji (kufanyika) kwa mara ya kwanza.

**Swali la 8:** Je, nini chanzo cha mtaji wa kuanzisha shughuli hii ya kujiongezea kipato? Orodhesha chanzo cha mtaji wa kuanzisha shughuli hii. Tumia mageresho yaliyopo kwenye swali. Kama mhojiwa ametaja chanzo cha mtaji ambacho hakipo kwenye orodha ya mageresho, tumia geresho namba 12 na andika chanzo cha mtaji kwa maneno. Hadi vyanzo 3 muhimu vya mtaji vinaweza kuorodheshwa. Angalizo ḥMkopoḥ unahitaji kulipwa wakati ḥzawadiḥ haitaji kulipwa. ḥAliuza mali zakeḥ ina maana mmiliki aliuza baadhi ya mali zake ili apate fedha zinazohitajika kuanzisha biashara aliyojihusisha nayo. Kama hakukuwa na gharama za kuanzisha shughuli hiyo, andika geresho namba 13.

**Swali la 9:** Je, una muuzia nani bidhaa/huduma zako? Jaza anaowauzia hadi 2, kwakutumia mageresho yaliyoorodheshwa kwenye swali. Mtumiaji wa mwisho jaza geresho namba 1, hii inaonyesha biashara hiyo ni ya rejareja. Hii ina maana kwamba mtu anayenunua bidhaa anakwenda kuitumia, na si anayekwenda kuiiza tena. Taasisi inajumuisha mashule, hospitali, magereza n.k. ḥWazalishajiḥ hii ina maana kwamba biashara hii inatoa bidhaa zisizokamilika au malighafi kwenye biashara nyingine, ambao matumizi yao kama sehemu ya mchakato wa kuunda bidhaa ya mwisho kwa ajili ya soko.

**Maswali ya 10-12, kuwa mwangalifu. Mtaji inajumuisha rasilimali zinazotumika kuzalisha bidhaa nyingine, matumizi ambayo hayazui kutumia kwaajili ya baadae. Pembejeo au malighafi ni bidhaa zinazotumika kuzalisha bidhaa nyingine, lakini zinapungua kutokana na matumizi. Bidhaa ni zile mali zilizo tayari kwa mauzo.**

#### **Mifano:**

1. Fundi cherehani: Mtaji wake ni cherehani, sindano, mikasi(swali 10). Pia malighafi ni vitambaa na uzi(swali 11) na mali iliyopo tayari kwa mauzo ni magauni, mashati, n.k. (swali 12).
2. Muuza maji: Katika mfano huu biashara haina mtaji (swali 10) au malighafi (swali 11). Lakini ana mali iliyopo tayari kwa mauzo maji (swali la 12).
3. Msagishaji: Msagishaji mtaji ni mashine ya kusaga (swali la 10). Maligafi ni mafuta ya kuendesha mshine na mahindi (swali la 11). Mali iliyopo tayari kwa mauzo ni unga wa mahindi (swali la 12).
4. Duka la vifaa vya ofisini: Mtaji wake ni kompyuta,printers, na mashine za kudurufu (photocopy machines), na vifaa vidogo vinavyotumiwa na duka la vifaa vya ofisini kama staplers (swali la 10). Malighafi ni karatasi na wino au toner (swali la 11). Mali iliyopo tayari kwa mauzo ni madaftari, vitabu, peni, folders au vifaa vingine vinavyouzwa na duka la vifaa vya ofisini kwa matumizi ya wateja (swali la 12).
5. Huduma ya kukodisha Baskeli: Mtaji wa kukodisha baskeli ni baskeli zenyewe na vifaa vingine vyovyote ambavyo wanakaya wanatumia kutengenezea baskeli (swali 10). Huduma ya kukodisha baskeli haina malighafi (swali 11). Kama kwenye huduma ya kukodisha baskeli pia kunauzwa matairini na mipira ya ndani, hizo ndio zinakua bidhaa za kuuza (swali 12). Kama huduma ni kukodisha baskeli tu, kwa iyo biashara inakua haina bidhaa ya kuuza (swali 12).
6. Uuzaji wa Mayai: Ikiwa mwanakaya anasema wanauzu mayai kutoka kwenye shamba lao kama biasahara. TAARIFA HII ISIINGIZWE HAPA. Shughuli hii inapaswa kuingizwa katika dodoso la kilimo kuepuka kuandika taarifa ya aina moja mara mbili.

**Swali la 10:** Nini jumla ya thamani ya rasilimali iliyopo kwa ajili ya [BIASHARA] hii kama vile vifaa, majengo, ardhi, magari n.k.? Unahitaji kuwa makini unapouliza swali hili. Unatakiwa kujumlisha thamani ya mali aliyonayo, hata zilizokua stoo, shambani, vifaa vya shambani, majengo, ardhi, magari n.k. Jaza jumla ya thamani kwenye swali hili. Ni muhimu kuweka maelezo pembedi ya ukurasa kurahisisha mahesabu.

**Swali ka 11:** Nini jumla ya thamani ya malighafi iliyopo sasa? Pia hapa unatakiwa kupata thamani ya malighafi au vitendea kazi ambavyo vitakuwepo kwa wakati huo tu. Hii inajumuisha mali zote ambazo zipo mkononi kwa ajili ya kutengeneza au kuzalisha bidhaa.

**Swali la 12.** Je, nini thamani ya mali iliyo tayari kwa mauzo? Orodhesha thamani ya mali iliyo tayari kwa mauzo.

<p>2. Tafadhali naomba unipatie maelezo ya kina kuhusiana na bidhaa au huduma kuu ya kila [SHUGHULI/BISHARA] ambayo kaya yako iliendesa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita.</p> <p>I D ANDIKA MAELEZO YA KUHUSIANA NA · BIDHAA /HUDUMA KUU YA KILA SHUGHULI AU BIASHARA AMBAYO KAYA ILIENDESHA Y KATIKA KIPINDI CHA MIEZI 12 ILIYOPITA, A KABLA YA KWENDA SWALI LA 3. B TAFADHALI JUMUISHA BIASHARA AMBAZO I ZIMEFUNGWA MOJA KWA MOJA AU KWA A MUDA KATIKA KIPINDI CHA MIEZI 12 S ILIYOPITA.</p> <p>H A R A</p>	<p>10. Nini jumla ya thamani ya rasilimali iliyopo kwa ajili ya [BIASHARA] hii kama vile vifaa, majengo, ardhi, magari n.k.?</p>	<p>11. Nini jumla ya thamani ya malighafi iliyopo sasa?</p>	<p>12. Je, nini thamani ya mali iliyo tayari kwa mauzo?</p>
ITAJE	ISIC GERESHO	SHILINGI	SHILINGI
1 Ushonaji	80,000	10,000	25,000
2 Kuuza maji	0	0	7000
3 Usagishaji wa nafaka	300,000	12,000	8,000
4 Duka la stationary	225,000	20,000	40,000
5 Ukodishaji wa baiskeli	150,000	0	15,000

*Maswali ya 13 na 14, uwe mwangalifu kutofautisha kati ya MAUZO na FAIDA. Mauzo ni pale kabla hujatoa gharama za biashara na kodi zinazo husika. Faida ni baada ya kutoa gharama zote za biashara na kodi. Pia, uwe mwangalifu kama swali la 13 taarifa zake zimetolewa kwa wiki. Swali la 16, 17 na 18 taarifa zake zinatolewa kwa mwezi kwa hiyo unatakiwa kubadili tarakimu zake kwa kugawanya na 4 ili kupata kiasi kwa wiki.*

**Maswali ya 16-18: Yanafafanua zaidi matumizi mbali mbali ya biashara. Utakapomaliza sehemu hii hakikisha kwamba:**

$$\boxed{Q14 = Q13 - Q16 - Q17 - Q18 \text{ (FAIDA KWA MWEZI)}}$$

$$\boxed{Q14 = Q13 - (Q16/4) - (Q17/4) - (Q18/4) \text{ (FAIDA KWA WIKI)}}$$

**Mifano:**

1. Fundi cherehani: Ili kujua jumla ya mapato /Mauzo jumla (swali 13), unahitaji kujua mauzo ya magauni (Tsh 15,000) na mangapi yaliuzwa mwezi uliopita (yaliuzwa 8); Mapato ya mashati (Tsh 10,000 ) na mangapi yaliuzwa mwezi uliopita (yaliuzwa 3). Angalia kwamba  $Q14 = Q13 - Q16 - Q17 - Q18$ . Bei zote zinapaswa kuwa katika vipimo vinavyofanana.
2. Muuza maji: Kwa mfanyakishara kama huyu, jumuisha fedha iliyotumika kwenye bidhaa na gharama za malighafi (swali 17). Kwakuwa swali la 18 taarifa zake zinatolewa kwa mwezi, gwawanya kwa nne kupata wastani wa kiasi kwa wiki.  $Q14 = Q13 - (Q17/4)$ .
3. Msagishaji: Jumla ya mapato/mauzo (swali la 13) ni fedha zote za malipo ya huduma ya usagishaji. Faida (swali la 14) hii ni baada kulipia mafuta au bili ya umeme (swali la 18).
4. Duka la vifaa vya ofisini: Mapato kabla ya makato (Swali la 13) inajumuisha fedha zote za mauzo ya bidhaa au uchapishaji. Kwa hiyo, Mapato (Swali la 13) yatatolewa kwa wiki isipokuwa swali la 16, 17 na 18 yatatolewa kwa mwezi.  $Q14 = Q13 - (Q16/4) - (Q17/4)$ .
5. Ukodishaji Baiskeli: Mapato kabla ya makato (swali la 13) inajumuisha fedha zote za ukodishaji baiskeli zilizopokelewa. Faida (swali 14) inapatikana baada ya kutoa jumla ya fedha kwa wiki zilizotumika kutengeneza baskeli (swali la 18).  $Q14 = Q13 - (Q18/4)$ .

**Swali la 13:** Ulipata kiasi gani cha fedha kabla ya makato kutokana na biashara yako/zako katika kipindi cha wiki iliyopita/mwezi? Tafuta mapato kwa wiki/mwezi kabla ya kodi na gharama zingine za uendeshaji wakati shughuli ikifanyika. Kwa mapato ya wiki moja jaza geresho la 1, kwa mwezi utaandika geresho la 2 kwenye safu wima ya kipindi na utajaza fedha zilizotajwa.

**Swali la 14:** Ulipata kiasi gani cha mapato (faida) baada ya makato kutokana na [BIASHARA] katika kipindi cha wiki/mwezi uliopita? Swali hili linahitaji kujua mapato (Faida) kwa wiki/mwezi baada ya kodi na gharama zingine za uendeshaji shughuli ikifanyika. Kwa mapato ya wiki moja jaza geresho la 1, kwa mwezi utaandika geresho la 2 kwenye safu wima ya kipindi na utajaza fedha zilizotajwa. Gharama kwenye swali hili zitakua ndogo kuliko swali la 13, kwasababu linatoa gharama zilizotumika kwenye biashara.

**Swali la 15:** Je, ni wafanyakazi wangapi ambao si wanakaya walijishughulisha katika shughuli hii kipindi cha mwezi mmoja uliopita? Muulize mhojiwa kuna wafanyakazi wangapi ambao si wanakaya walijishughulisha katika shughuli hii kipindi cha mwezi mmoja uliopita. Andika idadi. Kama hakuna andika 0.

**Swali la 16:** Je ni kiasi gani cha fedha kilichotumika katika kulipa mishahara mwezi uliopita? Andika kiasi kinachotumika kulipa mishahara kwa mwezi. Kama kiasi ni sifuri, andika 0.

**Swali la 17:** Je, kiasi gani cha fedha kilichotumika kununua malighafi ya uzalishaji mwezi uliopita? Andika kiasi kilichotumika kununua malighafi na vifaa vya uzalishaji. Andika kiasi kwa shilingi. Kama kiasi ni sifuri, andika 0.

**Swali la 18:** Je, ni kiasi gani cha fedha kinachotumika kwa ajili ya kugharamia mahitaji mengine kama vile nishati, mafuta, umeme, n.k? Andika gharama iliyotumika kwa mwezi kulipia hizo huduma nyinginezo. Jaza gharama hizo katika shilingi.

**Swali la 19:** Ni kwa miezi mingapi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita uliendesha shughuli/biashara hii?

I D Y A B I A S H A R A	2. Tafadhali naomba unipatie maelezo ya kina kuhusiana na bidhaa au huduma kuu ya kila [SHUGHULI/BISHARA] ambayo kaya yako iliendesa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita.  ANDIKA MAELEZO YA KUHUSIANA NA BIDHAA · IHUDUMA KUU YA KILA SHUGHULI AU BIASHARA AMBAYO KAYA ILIENDESHA KATIKA KIPINDI CHA MIEZI 12 ILIYOPITA, KABLA YA KWENDA SWALI LA 3. TAFADHALI JUMUISHA BIASHARA AMBAZO ZIMEFUNGWA MOJA KWA MOJA AU KWA MUDA KATIKA KIPINDI CHA MIEZI 12 ILIYOPITA.	13. Ulipata kiasi gani cha fedha kabla ya makato kutokana na [BIASHARA] katika kipindi cha wiki/mwezi uliopita? (Mauzo jumla)	14. Ulipata kiasi gani cha mapato (faida) baada ya makato kutokana na [BIASHARA] katika kipindi cha wiki/mwezi uliopita?  [KUMBUKA FEDHA KABLA YA MAKATO (Sw. 13) NI KUBWA AU SAWA NA FEDHA BAADA YA MAKATO (Sw. 14)]	15. Je, ni wafanyakazi wangapi ambao si wanakaya walijishughulisha katika shughuli hii kipindi cha mwezi mmoja uliopita?  WAFANYAKAZI WASIO WANAKAYA	16. Je, ni kiasi gani cha fedha kilichotumika katika kulipa mishahara kununua mwezi uliopita?  KAMA HAKUNA ANDIKA '0'	17. Je, ni kiasi gani cha fedha kilichotumika kununua malighafi ya uzalishaji mwezi uliopita?  KAMA HAKUNA ANDIKA '0'	18. Je, ni kiasi gani cha fedha alichotumia [JINA] mwezi uliopita kwa ajili ya kugharamia mahitaji mengine kama vile nishati ya mafuta na umeme?
ITAJE	ISIC GERESHO	KIPINDI	SHILINGI	KIPINDI	SHILINGI	SHILINGI	SHILINGI
1	<b>Ushonaji</b>	2	150,000	2	100,000	0	0
2	<b>Kuuza maji</b>	1	15,000	1	13,500	0	0
3	<b>Usagishaji wa nafaka</b>	2	240,000	2	100,000	0	0
4	<b>Duka la stationary</b>	1	60,000	1	42,500	1	60,000
5	<b>Ukodishaji wa baiskeli</b>	1	25,000	1	23,750	0	0

Andika ni kwa miezi mingapi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita biashara hii iliendeshwa. Kama biashara iliendeshwa kwa kipindi chote cha mwaka uliopita, andika 12.

**Swali la 20:** Nini WASTANI wa mapato halisi (faida) kwa mwezi katika miezi ambayo ulifanya biashara hii miezi 12 iliyopita? Andika wastani wa faida kwa miezi ambayo biashara hii ilifanyika. Hii ni sawa na kuchukua jumla ya kiasi cha fedha toa gharama zingine za uendeshaji wa biashara.

**Swali la 21:** Je, shughuli/kampuni hii imesajiliwa rasmi na í ? Andika shughuli/kampuni hiyo imesajiliwa rasmi na mamlaka husika. Kama jibu ndiyo, andika geresho la -1ø Kama jibu hapana, andika øø.

# Sehemu O: Misaada na Vikundi Kusaidiana

Katika sehemu hii, uliza maswali kwa safuwima 1 ó 5 kwa safu mlalo → Aøkabla kuendelea safuwima ya →Bø

**Safuwima ya 1:** Je, katika miezi 12 iliyopita, wewe au mwanakaya yejote amechukua [í .] kutoka serikalini au mashirika yasiyo ya kiserikali (kama vile ya kidini)? Swali hili linataka kujua kama mwanakaya/mhojiwa amepokea zawadi (pesa au kitu) kutoka serikalini au mashirika yasiyo ya kiserikali (kama vile ya kidini) kama ilivyoorodheshwa katika safumlalo A-F, usijumuushe vikundi vya SACCOS na makundi ya kusaidiana (UPATU). Kama amepokea utajaza geresho la ndiyo ambalo ni 1 katika safumlalo husika, hapana utaandika geresho la 2, nenda sehemu inayofuata.

**Safuwima ya 2:** Ni taasisi/mpango gani ulihusika katika kutoa huo msaada? Swali hili linategemea vipengele vyenye geresho la 1 kutoka katika safuwima 1. Mhojiwa akutajie ni taasisi/mpango gani ulihusika katika kutoa huo msaada, utauliza misaada yote yenye geresho la 1.

**Safuwima ya 3:** Je, mmepewa kiasi gani cha pesa taslimu kutoka [CHANZO] katika miezi 12 iliyopita? Hapa tutajibu iwapo chanzo kilitoa msaada wa pesa taslimu. Mwanakaya/mhojiwa akutajie kiasi cha pesa taslimu alichopokea kutoka (CHANZO) katika miezi 12 iliyopita. Vyanzo tunavyozungumzia hapa ni vile vilivyopo katika safuwima 2.

**Safuwima ya 4:** Thamani ya chakula mllichopokea kutoka [CHANZO] kama zawadi katika miezi 12 iliyopita ni kiasi gani? Muulize mhojiwa iwapo (CHANZO) kilitoa msaada wa chakula kama zawadi. Mhojiwa akutajie thamani ya chakula walichopokea kutoka chanzo katika safuwima 2 katika miezi 12 iliyopita.

**Safuwima ya 5:** Thamani ya vitu vingine mlivyopokea kutoka [CHANZO] kama zawadi katika miezi 12 iliyopita ni kiasi gani? Swali hili linahitaji kujua thamani ya vitu vingine ni shilingi ngapi alivyopokea mwanakaya/mhojiwa kutoka (CHANZO) kama zawadi katika miezi 12 iliyopita. Vitu vingine ni vile vilivyotajwa katika safuwima ya 1.

**Swali la 6:** Ni wanakaya gani walishiriki katika mpango huu? Jaza utambulisho →roster IDø wa wanakaya mpaka watatu walioshiriki katika mpango huu.

**Swali la 7:** Nani katika kaya anayetoea maamuzi ya matumizi ya misaada inayopatikana katika mpango huu? Jaza utambulisho →roster IDø wa wanakaya mpaka wawili ambao walitoa maamuzi ya matumizi ya msaada uliopatikana kwenye vikundi.

**Safuwima ya 8:** Je, kuna mwanakaya yejote ambaye ni mwanachama wa chama cha kuweka na kukopa (SACCOS)? Muulize mhojiwa kama kuna mwanakaya yejote ambaye ni mwanachama wa chama cha kuweka na kukopa (SACCOS ni mfano mzuri). Akijibu ndiyo utajaza geresho la 1, hapana utajaza geresho la 2 na nenda sehemu inayofuata kwani maswali haya hayatamhusu.

Muulize mhojiwa majina/jina la wanakaya/mwanakaya yejote ambaye ni mwanachama wa chama cha kuweka na kukopa katika safuwima husika na orodhesha majina hayo na namba zao katika vipengele A-D kutoka kwenye orodha ya wanakaya. Katika sehemu hii utauliza swali la 9 hadi 18 kwa kila mtu aliyeorodheshwa.

**Safuwima ya 9:** Tafadhali taja wanakaya ambao ni wanachama. Swali hili linahitaji kujua mhojiwa ana akiba/salio kiasi gani katika kikundi. Chukua tahadhari unapouliza swali hili, hususani kama kuna watu karibu. Mhojiwa anaweza asikwambie kiasi gani cha fedha alichonacho kama watu wanamsikia.

**Safuwima ya 10:** Je, [JINA] ana salio/akiba ya kiasi gani katika kikundi?. Muulize mwanachama wa kikundi cha SACCOS ni kiasi gani anachochangia katika kikundi. Andika kiwango hicho kwa shilingi za Kitanzania.

**Safuwima ya 11:** Je, ni Mara ngapi [JINA] anachangia katika kikundi? Swali hili linahitaji kujuu ni Mara ngapi na kwa kipindi gani mwanakaya anachangia/anaweka akiba yake katika SACCOS. Utaandika kama alivyokwambia. Kama ni Mara mbili kwa mwezi, utaandika ö2ö kwenye safu wima iliyoandikwa öMARAö na ö3ö kwenye safuwima iliyoandikwa öKIPINDIö.

**Safuwima ya 12:** Je (JINA) anachangia kiasi gani kila Mara? Ingiza kiasi cha fedha anachochangia mwanakaya kwenye swali hili.

**Safuwima ya 13:** Uliza ni lini Mara ya mwisho mhojiwa alichukua mkopo kutoka kwenye kikundi. Ulizia ni mwezi na mwaka gani. Andika mwaka kwa tarakimu 4. Kama hawajawahi kuchukua mkopo kwenye kikundi, andika ööö, nenda safumlalo inayofuata.

**Safuwima ya 14:** Je, Ni kiasi gani [JINA] alichukua? Ingiza kiasi cha fedha (MKOPO) alichochukua mwanakaya kwenye swali hili.

**Safuwima ya 15:** Je, (JINA) alikuwa na salio/akiba la kiasi gani kabla hajachukua? Mwanakaya/mhojiwa ambaye ni mwanachama ataulizwa, alikuwa na salio/akiba ya kiasi gani kabla ya kuchukua mkopo huo.

**Safuwima ya 16:** Je, ni sababu gani kuu ilimfanya (JINA) achukue mkopo Mara ya mwisho? Muulize mhojiwa sababu kuu iliyomfanya achukue mkopo kwa Mara ya mwisho. Utajaza geresho la sababu, tumia mageresho yaliyoko katika ukurasa huu.

**Swali la 17 & 18:** Katika swali hili muulize mwanakaya mkopo aliochukua atalipa kwa kipindi gani. Andika geresho husika katika safuwima ya kipindi na jumla ya kiasi cha shilingi anacholipa/anachorudisha kwa kila kipindi husika katika swali la 17. Mfano; analipa shilingi 20,000/= kwa wiki, utaandika 20,000/= katika safuwima ya shilingi na geresho la -2ø katika safuwima ya kipindi. Swali la 18 mwanakaya atakutajia muda atakaotumia kurudisha/kulipa mkopo aliochukua.

## Sehemu P: Mikopo

---

Sehemu hii aulizwe mkuu wa kaya au mwanakaya anayehusika na mikopo iliyoordheshwa, na inahusisha mikopo ambayo haitoki katika SACCOS.

**Swali la 1:** Je, ulichukua mkopo/mwanakaya ye yote alichukua mkopo nje ya kaya au katika kampuni/shirika katika mfumo wa pesa, vitu au huduma katika kipindi cha miezi 12 iliyopita? Muulize mhojiwa kama kuna mwanakaya ye yote aliye kopa pesa, vitu au huduma kutoka nje ya kaya katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Kwa jibu la ndiyo utajaza geresho la -1ø hapana utajaza geresho la -2ø na nenda sehemu Q. Kumbuka kudadisi zaidi mikopo yote ikiwa kwa ajili ya shughuli za kilimo au mikopo iliyo chukuliwa kwa njia ya vitu au huduma na kuvithaminisha vitu hivyo katika pesa.

**Swali la 2:** Taja majina ya watu au taasisi ambapo mwanakaya wenu alichukua mkopo katika kipindi cha miezi 12 iliyopita? Mwanakaya akutajie majina ya watu/taasisi ambapo mwanakaya wamekopa katika miezi 12 iliyopita. Hakikisha unaorodhesha watu au taasisi zote kabla ya kwenda swali linalofuata.

**Safuwima ya 3:** Kimsingi hili sio swali kwa mwanakaya/mhojiwa. Ni maelekezo yako wewe kama mdadisi, unatakiwa kuweka mageresho ya chanzo cha mkopo. Tumia mageresho yaliyoko chini mwa ukurasa huu.

**Safuwima ya 4:** Mwanakaya gani alichukua mkopo huo? Katika swali hili, utajaza namba ya mwanakaya aliye husika na mkopo katika taasisi husika zile ulizoorodhesha katika safuwima 2.

**Safuwima ya 5:** Mkopo ulikuwa wa fedha au vitu? Muulize mhojiwa iwapo mkopo aliochukua ulikuwa wa fedha au vitu. Kama ni fedha utajaza geresho la  $\frac{1}{4}$  vitu utajaza geresho la  $\frac{2}{3}$

**Safuwima ya 6:** Thamani ya mkopo. Utajaza thamani ya mkopo ilikuwa shilingi ngapi (Kumbuka kama alikopa vitu ni lazima vipewe thamani ya shilingi na utajaza thamani hiyo).

**Safuwima ya 7:** Je, Mkopo umeshalipwa wote? Mhojiwa akujibu endapo mkopo uliochukuliwa meshalipwa wote, kwa jibu la ndiyo utajaza geresho la  $\frac{1}{10}$ na uende swali la 9 na jibu la hapana geresho la  $\frac{2}{3}$

**Safuwima ya 8:** Mnatarajia mtamaliza kulipa mkopo lini? Pia mhoji mwankaya ni lini anakisia atakuwa amemaliza kulipa mkopo aliochukua. Utajaza mwaka na mwezi unaotarajiwa. Kumbuka kujaza mwaka katika tarakimu 4.

**Safuwima ya 9:** Jumla ya malipo ya mkopo pamoja na riba. Muulize mhojiwa jumla ya malipo ya mkopo pamoja na riba. Ufuatao ni mfano wa jibu linalokusudiwa; Eli alikopa benki kiasi cha sh.100, 000 ikiwa na riba ya 25%, utajaza jumla ya Tsh. 125,000.

**Safuwima ya 10:** Matumizi makuu matatu ya mkopo (kama yapo). Inategemewa kuwa mtu anapohitaji mkopo anakuwa na matumizi maalumu ya kutatua lile alilokusudia, muulize mhojiwa/mwanakaya matumizi hadi 3 kufuatana na umuhimu wake. Utaandika geresho husika, kama atakutajia matumizi ambayo hayapo hapo kwenye mageresho, utajaza geresho la  $\frac{1}{10}$ na andika matumizi hayo.

## Sehemu Q: Fedha

---

Sehemu hii inakusudia kuulizia masuala ya matumizi ya huduma za kibenki za kimtandao wa ajili ya kuhamishia pesa, misaada ya kipesa na akaunti za benki. Ulizia hii sehemu kwa mkuu wa kaya au mwankaya mwingine yejote ambaye ana ufahamu mkubwa juu ya fedha za kaya.

**Swali la 1:** Je, wewe au mwankaya yejote amewahi kutumia njia yoyote kati ya hizi zilizotajwa kusafirisha/kuhamisha pesa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita? Ulizia kama mmojawapo wa wanakaya ametumia huduma za kuhamishia/kusafirisha pesa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Tofautisha majibu M-PESA, EZY PESA, AIRTEL MONEY, na TIGO PESA. Kama jibu ni ndiyo, weka geresho,  $\frac{1}{4}$  kama hapana,  $\frac{2}{3}$  Kama ni hapana kwa njia zote nne, nenda swali la 5.

**Swali la 2:** Ni mara ngapi kaya yako inatumia huduma hii? Andika ni mara ngapi kaya hutumia njia hizi. Kama wanakaya tofauti hutumia njia hizi, au kaya hutumia njia tofauti, andika jumla itokanayo na wanakaya wote na huduma zote 4. Tumia mageresho yaliyopo kwenye dodoso.

**Swali la 3:** Ulitumia/mlitumia huduma hii? dadisi ni kwa madhumuni gani kaya ilitumia huduma hiyo,. Kwa kila huduma, A-H, tumia geresho  $\frac{1}{4}$  kama kaya ilitumia huduma hiyo na geresho,  $\frac{2}{3}$  kama hawakutumia huduma hiyo.

**Swali la 4:** Ni lipi kati ya haya (3A - H) ilikuwa matumizi makuu muhimu ya huduma hii? Angalia matumizi yote yaliyowekewa geresho la öndiyoö,  $\frac{1}{4}$  katika swali la 3. Ulizia katika matumizi hayo A-H, ni yapi yalikuwa muhimu sana katika kutumia njia ya kuhamishia pesa.

**Swali la 5:** Je, chanzo kikuu cha mapato ya kifedha cha kaya hii ni nini? Andika chanzo kikuu cha mapato ya kifedha ya kaya, tumia mageresho yaliyopo upande wa kulia wa ukurasa. Ikiwa mhojiwa atasema chanzo ambacho hakipo kwenye mageresho jaza geresho  $\frac{1}{10}$ na andika aina hiyo.

**Swali la 6:** Je, ni kiasi gani kaya yako imepata kwa kukodisha vitu kama (ardhi / nyumba / duka / stoo) katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, ukiondoa ardhi ya kilimo? Andika kiasi cha shilingi/pesa zinazopatikana kwa mwaka kutokana na hivyo vitu wanavyovimiliki, ardhi ya kilimo isijumuishwe kwani

taarifa zake zitajazwa kwenye dodoso la kilimo. Kama kaya inakodisha zaidi ya kitu kimoja , jumlisha thamani ya mwaka pembeni mwa ukurasa, halafu ujaze jumla hiyo kibox.sanduku.

**Swali la 7:** Ni kiasi gani cha pesa kaya yako imepata kama malipo ya uezini katika kipindi cha miezi 12 iliyopita? Swali linalenga kufahamu ni kiasi gani kaya inapata kama malipo ya uezini, yawezekana kutoka serikalini ama secta binafsi, kama ni mwanakaya zaidi ya mmoja wanapata malipo ya uezini jumlisha kiasi kinachopatikana kwa mwaka na ujaze kwenye kisanduku.

**Swali la 8:** Je, ni kipato cha kiasi gani kaya yako imeweza kupata kwa njia yoyote ya kuingiza mapato mengine katika kipindi cha miezi 12 iliyopita? Swali linalenga kufahamu mapato mengine ya kaya katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Mapato hayayasijumuishe malipo ya uezini wala mapato yatokanayo na kukodisha vitu vya kaya ambayo yameshaandikwa kwenye maswali yaliyopita. Kama hakuna mapato kaya imepata kwa kipindi cha miezi 12 iliyopita jaza  $\frac{1}{2}$  na nenda swali la 10.

**Swali la 9:** Ni aina gani ingine ya kipato kaya yako ilipata katika kipindi cha miezi 12 iliyopita? Swali hili linalenga kufahamu aina nyngine ya kipato cha kaya katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, tumia mageresho yaliyowekwa, ikiwa kipato hicho hakipo kwenye mageresho, jaza geresho  $\frac{1}{2}$  na andika kwa maneno, orodhesha hadi aina tatu ya mapato.

**Swali la 10:** Je, kuna mwanakaya yeyote katika kaya yako mwenye Akaunti ya akiba ya fedha benki, iwe benki ya kibiashara, chama cha kuweka na kukopa au taasisi nyngine zinazofanana? Uliza kama kuna mwanakaya yeyote mwenye akaunti ya akiba katika benki ya biashara, chama cha akiba na kukopa, au taasisi nyngine ya kifedha. Kama jibu ni ndiyo, andika geresho  $\frac{1}{2}$  Kama hapana, andika geresho la  $\frac{1}{2}$  na nenda swali la 13. Usijumuishe akaunti za mitandao ya mkononi kama M-PESA, EAZY PESA, AIRTEL MONEY, TIGO PESA.

**Swali la 11:** Tafadhali orodhesha mpaka taasisi 3 ambapo wewe au mwanakaya mwingine ana akaunti ya akiba ya fedha. Andika jina la taasisi ambayo mwanakaya ana akaunti ya akiba. Andika jina kamili la taasisi.

**Swali la 12:** Ni mwaka gani ulifunguaakaunti yako ya kwanza ya akiba? Andika mwaka amba mwanakaya alifungua akaunti hiyo kwa mara ya kwanza. Toa jibu la mwaka katika tarakimu 4; usiandike idadi ya miaka ambayo mwanakaya amekuwa na akaunti hiyo. Halafu nenda swali la 14.

**Swali la 13:** Kwanini huna akaunti ya akiba ya fedha? Kama hakuna mwanakaya mwenye akaunti ya akiba katika kaya, andika sababu ya kutokuwa na akaunti hiyo. Orodhesha mpaka sababu 3, ukitumia mageresho yaliyotolewa kwenye dodoso.

**Swali la 14:** Je, wewe au mwanakaya yeyote amewahi kupata msaada wa kitu chochote au msaada wa kifedha katika kipindi cha miezi 12 iliyopita? Ulizia kama kuna mwanakaya yeyote aliyepokea misaada katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Jumuisha vyote pesa na vitu. Zinaweza kuwa pesa au vitu vilivytumwa na mwanakaya, rafiki kwa ajili ya matumizi mbalimbali kama ada ya shule, kununua nyumba au gari. Kama ndiyo jaza  $\frac{1}{2}$  kama hapana  $\frac{1}{2}$  na nenda sehemu inayofuata.

**Swali la 15:** Je, mtoaji wa msaada huo anaitwa nani? Andika jina la mtu ambaye ametuma misaada kwenye kaya. Orodhesha hadi watu wanne.

**Swali la 16:** Nini uhusiano wa [MTOAJI] na mkuu wa kaya? Andika uhusiano kati ya mkuu wa kaya na mtu ambaye ameleta msaada huo. Tumia mageresho yaliyo kwenye dodoso chini.

**Swali la 17:** Je, [MTOAJI] ana umri gani ? Andika umri wa mtu aliyetuma misaada. Kama mhojiwa hajui umri wa huyo mtu andika 99.

**Swali la 18:** Ni nini jinsi ya [MTOAJI]? Andika jinsia ya mtu aliyetuma misaada.

**Swali la 19:** Ni kiwango gani cha juu cha elimu [MTOAJI] alichohitimu? Andika kiwango cha juu cha elimu alichohitimu huyu mtu aliyetuma misaada.

**Swali la 20:** Je, [MTOAJI] alituma misaada hiyo kutokea wapi? Andika nchi au mkoa ambako misaada ya fedha ilitoka. Tumia mageresho yaliyopo upande wa chini wa ukurasa.

**Swali la 21:** Kwa muda gani [MTOAJI] ameishi huko aliko sasa? Uliza kwa muda gani huyo anayetoa misaada amekuwa akiishi hapo anapoishi sasa , andika kipindi na idadi. Mfano: mtoaji ameishi nje ya nchi kwa miaka 15, andika 2 kwenye safuwima ya kipindi na 15 safuwima ya idadi.

**Swali la 22:** Njia ipi [MTOAJI] aliitumia kutuma misaada? Andika namna ambavyo kaya imepokea misaada. Hii ni njia ambayo mtumaji pesa ametumia kutuma pesa ili kaya izipokee. Tumia mageresho yaliyo chini ya ukurasa wa maswali haya. Unaweza kuorodheshampaka njia tatu za kutumia pesa.

**Swali la 23:** Je, ni kiasi gani cha pesa taslimu ulipata kutoka kwa [MTOAJI] katika kipindi cha miezi 12 iliyopita? Andika thamani ya pesa zilizopokelewa na kaya katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, andika kwa T-shilingi hata kama pesa hiyo ilipokelewa kwa thamani ya pesa ya nchi nyingine, kama kaya haikupokea pesa ye yote andika 0 na nenda swali la 26.

**Swali la 24:** Je, pesa kutoka kwa [MTOAJI] ilitumika kwa matumizi yapi kwenye kaya katika kipindi cha miezi 12 iliyopita? Andika kaya ilitumiaje pesa iliyopokea, andika hadi matumizi matatu kwa kutumia mageresho yaliyopo chini ya ukurasa.

**Swali la 25:** Nani katika kaya alifanya maamuzi ya matumizi ya pesa zilizotumwa na [MTOAJI] katika kipindi cha miezi 12 iliyopita? Andika namba ya mwanakaya anayetoa maamuzi ya nini kifanyike kwa pesa iliyopokea kutoka kwa mtoaji. Andika hadi watu wawili katika kaya.

**Swali la 26:** Ni nini jumla ya thamani ya vitu vyote mlivyopokea katika kipindi cha miezi 12 iliyopita? Andika jumla ya thamani ya msaada kwa njia ya vitu waliyopokea katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Kama kiasi halisi hakifahamiki, muulize mhojiwa kufanya makadirio katika shilingi za kitanzania. Kama kaya haikupokea misaada ya vitu andika 0 na nenda chanzo kingine.

**Swali la 27:** Nani katika kaya aliyefanya maamuzi ya vitu vilivyotumwa na [MTOAJI] katika kipindi cha miezi 12 iliyopita? Andika namba ya mwanakaya anayetoa maamuzi ya nini kifanyike kwa vitu ilivyopokea kaya kutoka kwa mtoaji. Andika hadi watu wawili katika kaya.

## Sehemu R: Mishtuko/Maafa ya Karibuni kwa Ustawi wa Kaya

---

Sehemu hii muulize mkuu wa kaya au mwanakaya anayefahamu kikamilifu masuala ya kaya.

**Safuwima ya 1:** Je, katika miaka 2 iliyopita, kaya yenu iliwahi kuathiriwa vibaya na moja ya mishtuko/maafa yafuatayo? Swali hili linahitaji kujua kama wanakaya wamepatwana maafa/matukio mojawapo kati ya haya yaliyoorodheshwa katika safuwima hii kwa kipindi cha miaka 2 iliyopita. Unatakiwa kumsomea mwanakaya/mhojiwa mishtuko/maafa yote kama yaliyoorodheshwa hapo kwenye safuwima. Unachotakiwa kufanya wewe mdadisi ni kuandika geresho 1 endapo kaya ilipatwa mishtuko/maafa husika na geresho 2 endapo kaya haikupatwa na mishtuko/maafa husika. Uliza swali hili kwa mishtuko/maafa yote (kipengele cha 101 mpaka 119) kabla ya kuuliza maswali mengine kwenye safuwima ya 2. Iwapo ni 119, elezea mshutuko huo kwa maneno.

**Safuwima ya 2:** Taja matukio/mishtuko mikuu matatu iliyokuathiri. Kabla ya kujibu swali la 2, soma orodha ya mishtuko iliyopata kaya katika miaka miwili iliyopita. Muulize mhojiwa ni mishtuko ipi kati ya aliyo taja iliyoonesa kumwathiri zaidi katika ustawi wa kaya yake, ndipo ujaze 1 kwenye safuwima ya 2 kwa

mshutuko huo. Muulize mwanakaya ni mshtuko gani wa pili kiukubwa na ujaze 2 kwenye safuwima ya 2 kwa mshutuko huo vilevile, andika geresho 3 kwa mshtuko wa 3. Kama kaya imeonesha kuwa imepatwa na mishtuko 2 katika miaka mitano iliyopita, hapatakuwa na geresho 3 kwenye hii safuwima. Safuwima ya 2 isiwe na namba za kujirudia rudia 1, 2 au 3. Kama mhojiwa atasema matukio yote yanafanana, dadisi zaidi kujua mshituko upi ulionekana kuwaathiri zaidi.

**Safuwima 3:** Maswali yaliyopo katika safuwima hizi, yaulizwe tu kuhusu maafa makuu matatu yaliyopo katika swali la 2. Utaacha wazi mistari ambayo iliyopo katika safuwima ya 2. Katika swali la 3 mhojiwa atajibu iwapo maafa hayo yalisababisha kupungua kwa kipato cha kaya.

**Swali la 4:** Ni kitu gani kaya yako ilifanya ili kukabiliana na [MAAFA] na kurudisha hali yako ya maisha ya kabla? Orodhesha angalau mawili kwa kutumia mageresho yaliyopo upande wa kulia wa ukurasa.

## Sehemu S: Vifo katika Kaya

---

Maswali haya yanataka kujua juu ya vifo vyovyyote vilivyotokea katika kaya ndani ya miaka miwili iliyopita.

**Swali ya 1:** Je, katika miaka 2 iliyopita, kuna wanakaya wowote waliofariki wakiwemo watoto wachanga na wale waliorodheshwa kwenye FOMU YA UFUATILIAJI kuwa "wamefariki"? Muulize mhojiwa iwapo kuna wanakaya wowote waliofariki wakiwemo watoto na watoto wachanga katika miaka miwili iliyopita. Kama jibu ni ndiyo utaandika geresho 1, kama jibu ni hapana utaandika geresho la 2 na kwenda sehemu inayofuata.

**Safuwima za 2, 3, 4, 5, 6 & 7:** Swali la 2 utaandika jina la marehemu ambalo mhojiwa atakutajia, swali la 3 utaandika geresho la uhusiano wa marehemu na mkuu wa kaya kwa kuangalia mageresho husika hapo chini ya ukurasa huu.

Katika swali la 4 unatakiwa kuandika geresho kama marehemu alikuwepo kwenye kaya mwaka 2013/14), swali hili linafanana na swali la 6 sehemu B. Tumia geresho la orodha ya watu lililochapishwa (fomu ya ufuatiliaji), na tumia geresho -99 kama mwanakaya hakuwepo 2013/14. Ikiwa kaya ni mpya, andika 99 kwa wanakaya. Katika swali la 5 andika jinsia ya marehemu. Swali la 6 linauliza kama kifo kilisajiliwa, andika geresho -10 kama ndiyo na -20 kama hapana. Swali la 7 linauliza umri wa marehemu alipofariki, kama marehemu alikuwa chini ya miaka 5, tafadhalu andika umri katika miaka pamoja na miezi, kama chini ya miaka 12 nenda swali la 9.

**Safuwima ya 8:** Je, ni shughuli gani kuu aliyofanya [MAREHEMU] kwa sehemu kubwa ya uhai wake? Swali hili linataka kujua shughuli kuu ya marehemu wakati wa uhai wake. Tumia mageresho yalipo chini ya ukurasa kama yalivyo kwenye dodoso.

**Safuwima ya 9:** Je, [MAREHEMU] alifariki kutokana na umri mkubwa, ugonjwa au sababu nyingine? Swali hili linauliza sababu ya kifo. Jaza jibu kwa kuangalia geresho lilorodheshwa kwenye swali. Kama sababu ilikuwa ni umri mkubwa (uzee) geresho lake ni 1, nenda swali la 13. Kama sababu ilikuwa ni ugonjwa geresho ni 2, nenda swali la 11, kama kulikuwa na sababu nyingine geresho ni 3. Nenda swali jingine.

**Safuwima ya 10:** Sababu isiyo ya ugonjwa iliosababisha kifo cha [MAREHEMU]? Kwa swali la 10, kama marehemu alikufa kwa sababu nyingine tofauti na ugonjwa, kwa jibu lolote litakalotolewa, weka geresho lake na nenda swali la 14.

**Safuwima ya 11:** Je, ni ugonjwa gani uliosababisha kifo cha [MAREHEMU]? Swali la 11 linauliza sababu ya kifo, tumia mageresho yaliyoko chini, ukitumia geresho 34, kumbuka kuandika sababu. Kama mhojiwa akitaja sababu zaidi ya mbili, chagua sababu kuu mbili.

**Safuwima ya 12:** Marehemu [JINA] aliugua muda gani kabla ya kifo chake? Katika safuwima ya kipimo kama alichukua siku kadhaa andika geresho la -10 wiki andika geresho -20 miezi andika geresho -30 na

miaka andika geresho 4. Katika safuwima ya kipimo unatakiwa kujaza kipimo cha muda. Mfano marehemu aliugua miezi 4 kabla ya kifo chake, utaandika 4 katika safuwima ya kiasi/muda na geresho la  $\frac{3}{8}$  katika safuwima ya kipimo.

**Safuwima ya 13:** Je, sababu ya kifo ilichunguzwa au ni maoni yako tu? Swali hili linahitaji kujua sababu ya kifo; je, kifo hiki kilichunguzwa na mtaalamu wa afya (tabibu) au ni maoni ya mhojiwa tu. Tumia mageresho yaliyopo katika dodoso.

**Safu wima ya 14 & 15:** Marehemu alipokufa walipoteza ardhi au mali kutokana na mila. Kama ndiyo andika geresho la  $\frac{1}{4}$ , hapana andika geresho la  $\frac{2}{8}$  na nenda kwa marehemu mwingine endapo mhojiwa alikutajia marehemu zaidi ya mmoja. Safuwima 15 utajaza thamani ya fedha ya ardhi iliyopotea au rasilimali nyingine.

## Sehemu U-1: Taarifa za Kuifutilia Kaya

---

Sehemu hii ni muhimu kwa ajili ya kuandika taarifa za kutembelea kaya iwapo kaya hii itahamia sehemu nyingine.

Kabla ya kuanza kudadisi namba za simu, unatakiwa kuchukua vipimo vya GPS kwa kila kaya, itakayofanyiwa mahojiano mdadisi anatakiwa kuchukua vipimo vya mahali ilipo kaya kutoka kwenye kona ya kaskazini (Northings) na mashariki (Eastings).

**Swali la 1:** Jaza namba ya simu ya mkuu wa kaya. Kama hana simu jaza  $\frac{9}{8}$

**Swali la 2:** Jaza namba za simu za wanakaya wengine. Utajaza hadi wanakaya 3 kama zipo. Utajaza majina pamoja na namba zao simu.

**Swali la 3: MTU WA KARIBU KATIKA JAMII ANAYOISHI.** Sehemu hii inajumuisha ndugu, jamaa, rafiki, n.k anayeishi ndani ya mji/kijiji/mtaa/kitongoji ambacho mkuu wa kaya anaishi. Utajaza jina lake, uhusiano na mkuu wa kaya, kazi yake, eneo anapoishi, maelezo ya ziada na simu yake.

**Swali la 4: MTU WA KARIBU (NJE YA JAMII UA KIJIJI KINGINE).** Sehemu hii inajumuisha ndugu, jamaa, rafiki, n.k ambaye anaishi nje ya mji au kijiji husika. Utajaza jina lake, uhusiano na mkuu wa kaya, kazi yake, eneo anapoishi, maelezo ya ziada na simu yake.

**ANGALIZO:** Katika swali la tatu na la nne, hakikisha unaandika jina kamili, uhusiano sahihi na mkuu wa kaya, kazi yake kuu, eneo anapoishi, namba yake sahihi ya simu. Katika sehemu ya maelezo ya ziada, andika maelezo yatakayoweza kumtambulisha mhusika kama vile cheo, jina maarufu n.k. Mdadisi ukimaliza mahojiano ya sehemu ya A-3, iombe kaya kutoa taarifa ya mahali kaya itakapohamia kwenye ofisi ya mtendaji pindi ikibidi wahame.

## Sehemu U-2: Maswali ya Mchujo wa Sehemu ya Kilimo na Ufugaji & Uvuvi

---

**Swali la 1:** Je, kuna mwanakaya yejote anaelima shamba lolote? Swali linataka kujua kama kuna mwanakaya yejote analima shamba lolote au mazao yoyote. Ikiwa jibu ni, jaza geresho 1 kama jibu ni hapana jaza geresho 2.

**Swali la 2:** Je, kuna mwanakaya yejote anamiliki shamba la kulima lakini shamba hilo halilimwi? Pia muulize mhojiwa kama kuna mwanakaya yejote anamiliki shamba la kulima lakini shamba hilo halilimwi. Yawezekana shamba hilo likalawa limekoidishwa kwa watu wengine, au limepumzishwa. Kama jibu ni ndiyo utajaza geresho la  $\frac{1}{4}$  na kama hapana geresho la  $\frac{2}{8}$

**Swali la 3:** Je, kuna mwanakaya yeyote alimiliki au alilima shamba katika msimu masika wa mwaka 2012? Muulize mhojiwa kama kuna mwanakaya yeyote aliyelima au kulima mazao yoyote katika msimu wa masika wa mwaka 2012. Kwa jibu la ndiyo utaandika geresho la -1Ø na hapana utajaza geresho la 2.

**Swali la 4:** Je, kuna mwanakaya yeyote alimiliki au alilima shamba katika msimu wa vuli uliopita? Uliza endapo kuna mwanakaya yeyote alimiliki au alilima shamba katika msimu wa vuli. Akijibu ndiyo utajaza geresho la -1Ø na akijibu hapana utajaza geresho la -2Ø

**Swali la 5:** Swali hili asiulizwe mhojiwa. Onyesha kama mwanakaya anauwezo wa kujihusisha na shughuli za kilimo. Kama mwanakaya amejibu ḥndiyoØ kwa swali lolote lililoorozeshwa 1-4, huyu anahusika na weka geresho -1Ø wanakaya wote wenye geresho -1Ø wataulizwa maswali ya kilimo. Kama maswali yote 1-4 ni ḥhapanaØ hawahusiki na jaza geresho -2Ø

**Swali la 6:** Je, kuna mwanakaya yeyote aliyejishughulisha na ufugaji (mfano ng'ombe, mbuzi, kuku n.k) katika kipindi cha miezi 12 iliyopita? Uliza endapo kuna mwanakaya yeyote alimiliki mifugo katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Utajaza geresho la -1Ø kwa jibu la ndiyo na geresho la -2Ø kwa jibu la hapana.

**Swali la 7:** Kuna mwanakaya yeyote aliyejihuisha na uvuvi au shamba la samaki katika kipindi cha miezi 12 iliyopita? Muulize mwanakaya/mhojiwa kama kuna mwanakaya yeyote anajishughulisha na uvuvi au kuwa na shamba la uvuvi katika miezi 12 iliyopita. Utajaza geresho la -1Ø kwa jibu la ndiyo na geresho la -2Ø kwa jibu la hapana.

**Swali la 8:** Kuna mwanakaya yeyote aliyejihuisha na uuza ji wa samaki katika kipindi cha miezi 12 iliyopita? Uliza kama kuna mwanakaya alijihuisha na biashara ya samaki katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Biashara ya samaki ni uuza ji wa samaki (kwa rejareja au jumla) amba o hawajatayarishwa au aliotayarishwa na wavuvi wengine, uuza ji wa samaki waliovuliwa na mwanakaya hii haihesabiki kamani biashara ya samaki. Kama jibu ndiyo geresho 1, kama jibu hapana geresho 2.

**Swali la 9:** Swali hili asiulizwe mhojiwa. Onyesha kama kaya itahusika na sehemu ya mifugo/uvuvi. Kama mhojiwa amejibu ḥndiyoØ kwa swali la 6-8, hivyo anastahili na andika geresho 1, wale wote wenye geresho 1 watahusika na dodoso la mifugo/ uvuvi , kama jibu ni ḥhapanaØ hawastaili, jaza geresho 2.

## Zawadi kwa Mhojiwa

---

Katika kipengele hiki unatakiwa kumweleza mhojiwa kwamba ungependa kuwapa zawadi kwa ajili ya kuwashukuru kwa ushirikiano wao katika utafiti. Kumbuka zawadi hii zinategemeana na eneo, kama ni maeneo ya mjini watapatiwa chandarua na vijijini watapatiwa majembe.

**Swali la 10:** Kama kaya imepokea jembe utajaza geresho -1Ø chandarua utajaza geresho la -2Ø

**Swali la 11:** Katika kipengele hiki unatakiwa kuandika jina la mtu aliyepokea zawadi, namba ya utambulisho ambayo utaipata kwenye orodha ya wanakaya na pia kumbuka kumwambia aweke sahihi yake.

## Sehemu V: Vipimo vyta Uzito na Urefu

---

Vipimo vyta uzito na urefu vinachukuliwa kwa wanakaya wote chini ya umri wa miaka 15 (wakijumuishwa watoto wachanga) na wanawake kati ya umri wa miaka 15-49.

Pima uzito na urefu wa kila mwanakaya: watoto na watu wazima. Kama mwanakaya hayupo nyumbani wakati wa mahojiano, inakupasa kuweka miadi na urudi nyumbani kwa ajili kuchukua vipimo.

Inatakiwa kuwa na watu wawili wakati wa kuwapima wanakaya, mmoja anasoma uzito katika mashine na mwininge anaandika katika dodoso.

Kwa watoto walio chini ya miezi 24 wanatakiwa kupimwa tofauti. Urefu wa mtoto ukiwa chini ya sentimenta 45 unatakiwa kupimwa wakiwa wamelala sio kusimama. Uzito wanatakiwa kupimwa wakiwa na mama zao (au mwanakaya yoyote), kwanza mpime mama uzito na kisha futa katika sehemu ya kioo, alafu mpe mama amshike mtoto mikononi mashine itatoa uzito wa mtoto na andika katika dodoso.

Angalia majibu hakikisha yanaleta maana. Kwa mtoto aliye chini ya mwaka mmoja uzito wake hauwezi kufika kilo 20. Mtoto wa miaka 6 urefu wake hauwezi kuwa mita 1.7. Epuka makosa kama hayo.

**Maswali ya 1 na 2:** Maswali haya yanatakiwa kujazwa na mdadisi kwa kutumia taarifa zilizo katika orodha ya wanakaya. Maswali haya yataonyesha kama vipimo vitatakiwa kuchukuliwa kwa mwanakaya husika. Kwa swali la 1 tumia taarifa ya orodha ya wanakaya kujua kama mwanakaya ni mwanamke mwenye umri wa miaka 15-49. Ikiwa jibu ni ndiyo, weka geresho 1 na endelea na swali la 3. Ikiwa jibu ni hapana, weka geresho 2 na endelea na swali la 2.

Kwa swali la 2, tumia orodha ya wanakaya kujua kama mwanakaya ana umri zaidi ya miaka 15. Ikiwa mwanakaya ana umri zaidi ya miaka 15, weka geresho 1 na nenda kwa mwanakaya mwininge. Ikiwa hana miaka zaidi ya 15, weka geresho 2 na endelea na swali la 3.


**Maswali ya 3 na 4:** Maswali haya yasiulizwe kwa wahojowi. Swali la 2 linauliza kama mwanakaya alichukuliwa vipimo. Weka geresho 1 ikiwa ndio, na geresho 2 ikiwa hapana. Ikiwa hapana utatakiwa kuonyesha sababu kwanini vipimo havikuchukuliwa. Ikiwa sababu hajaorodheshwa katika dodoso, weka geresho 4 na andika sababu kwa maneno.

**Swali la 5:** Uzito utajazwa kwa kilogramu, ukianzia na sifuri. Kwa mfano kilo 3.2 itaandkwa 03.20. Hakikisha kipimo kipo sawasawa kipo kwenye kizio cha sifuri kabla hujaanza kupima, kama mtoto ni mdogo sana hawezi kusimama mwenyewe kwenye kipimo, pima uzito wa mama na mtoto kwa pamoja, kisha mpime mama peke yake, halafu toa uzito wa mama na mtoto na wa mama peke yake upate tofauti (tofauti ndio itakuwa uzito wa mtoto), kwa vipimo vyote angalia kama majibu yanafaa kabla ya kujaza kwenye dodoso. Kwa mfano ikiwa uzito wa mtoto unaonekana ni kilo 100, inaonyesha kwamba vipimo havijafanyika vizuri. Na hata baada ya kutoa, uzito wa mtoto ukionekana ni kilo 2, inaonyesha kuna kosa limefanyika. Program ya kuingiza data itaangalia mtiririko wa vipimo vya uferu, uzito, umri ambao hautakuwa sawasawa, Ikiwa vipimo havijanakiliwa kwa usahihi, itatakiwa kurudi tena kwenye kaya.

**Swali la 6:** Urefu kwa wanakaya utajazwa kwa kutumia sentimeta, utaanzia na sifuri. Mfano sentimeta 97, ziandikwe 097. Zifuatazo ni hatua za kuchukua vipimo sahihi kwa watoto wadogo wanaopimwa kwa kulazwa chini na watoto/watu wazima waopimwa kwa kusimama. Kwa kawaida watoto walio warefu zaidi ya sentimeta 45 au wenyе umri zaidi ya miezi 24 wapimwe wakiwa wamesimama.

#### Kupima urefu wa mtoto akiwa amelala:

1. Weka kifaa cha kupimia kwenye sehemu ngumu iliyonyooka (chini, sakafuni)
2. Msaidizi apige magoti na miguu yote miwili, nyuma ya ubao.



Source: How to Weigh and Measure Children: Assessing the Nutritional Status of Young Children, UNICEF/MICN, 1996.

3. Piga magoti upande wa kulia wa mtoto, ili uweze kushikilia miguu ya chini kwa mkono wako wa kulia.

4. Kwa msaada wa mama, mlaze mtoto kwenye ubao kwa kumshikilia nyuma kwenye kichwa kwa mkono mmoja na mwili kwa mkono mwingine, taratibu mlaze mtoto kwenye ubao. Muombe mama au mlezi apige magoti karibu na ubao amuangularie mpimaji, hii itasaidia kuleta utulivu kwa mtoto.

5. Msaidizi anapaswa kumuweka sawa mtoto kwa kutumia mikono yake iliyo juu ya masikio ya mtoto (kama vile anamziba masikio). Mikono ikiwa imenyooka na kutulia, msaidizi aweke alaze kichwa cha mtoto kwenye ubao ili mtoto awe anaangalia juu moja kwa moja. Anakoangalia mtoto kunapaswa kuwa nyuzi 90 (perpendicular) na ardhi. Kichwa cha msaidizi kiwe moja kwa moja kinaangaliana na cha mtoto, akiangalia moja kwa moja machoni mwa mtoto.

6. Hakikisha kwamba mtoto amenyooka kwenye ubao. Weka mkono wako wa kushoto kwenye muundi wa mtoto (juu ya ya ankle) au kwenye miguu. Ikandamize taratibu sambamba na ubao, kwa kutumia mkono wako wa kulia kandamiza mguu wake taratibu na visigino vyake.

7. Mtoto anapokuwa amekaa vizuri, soma na nakili vipimo katika miguu yake ya chini (visigino) karibia sentimita 0.1.

### Kupima Urefu wa Mtu mzima au mtoto Anaesimama

1. Weka ubao wa kupimia katika sehemu ilitonyooka na ngumu sambamba na ukuta, meza, mti n.k hakikisha ubao hauchezichezi.

2. Muombe mama ama mlezi amvue mtoto viatu na asimbane nywele za aina ye yeyote ambazo zinaweza kuathiri upimaji wa urefu, mwambie amuweke mtoto kwenye ubao na akae mbele yake ili mtoto asiwe na wasi wasi.


3. Hakikisha miguu ya mtoto imenyooka na imekaa kwa pamoja katikati ya ubao na awe amesimama vizuri sambamba na nguzo ya ubao wa kupimia. Msaidizi aweke mkono wake wa kulia juu ya enka kwenye muundi. Taratibu weka mkono wako usimfumbe mdomo au masikio. Hakikisha mabega yamelingana, mikono imenyooka na kichwa, mgongo na makalio viko sambamba na ubao wa kupimia. Kwa kutumia mkono wako wa kulia shusha kibao ulichoshikilia juu ya kichwa cha mtoto, hakikisha unashusha kibao usawa wa nywele.

4. Mtoto akishasimama vizuri, soma na nakili vipimo juu ya kichwa sentimita 0.1 ya karibu.

**Swali la 7:** Wanakaya wenge urefu zaidi ya sentimita 45 na wenge uwezo wa kusimama wachukuliwe vipimo wakiwa wamesimama. Watoto wenge urefu chini ya sentimenta 45 au wale ambao si rahisi kusimama sawasawa (na hasa wale wenge umri chini ya miezi 24) inabidi kuchukua vipomo vyao wakiwa wamelala. Onyesha kama alikuwa amesimama au amelala chini wakati wa kuchukuliwa vipimo. Hii itatumika kwa wanakaya wote siyo watoto pekee yao.

**Swali la 8:** Swali hili ni kwa ajili ya kupima mzingo/mzunguko wa mkono (kipisi cha juu). Hii itakuwa kwa watoto wenge umri chini ya miezi 60 tu, watakaojibu swali la 9.

**Swali la 9:** Swali hili linakutaka utumie utepe (tape) ya kupimia mkono. Kupima unene wa mkono wa mtoto, zungusha utepe wa kupimia kuzunguka mkono juu ya kiwiko lakini chini ya bega, jaza kipimo sentimita moja ya karibu.



# BAADA YA KUMALIZA MAHOJIANO

---

Tafadhalii kumbuka kuandika muda chini kulia mwa ukurasa huu mara unapomaliza mahojiano kwenye kisanduku.

Washukuru wahojiwa wote walioshiriki kikamilifu katika kukamilisha zoezi la utafiti. Wafahamishe ya kwamba taarifa zao zilizochukuliwa zitahifadhiwa kwa siri. Pia, waambie ya kwamba utafiti huu ni wa kila baada ya mwaka mmoja na mawasiliano yatafanyika kwa kaya husika, na kuzitafuta tena kaya hizo ni muhimu. Kaya zinazotarajia kuhama kutoka katika jamii inayoishi zitoe taarifa kwenye ofisi ya Mtendaji wa Kijiji (VEO).

## **II. Dodoso la Kilimo**

---

# Utangulizi

---

## Muhtasari wa Majukumu ya Mdadisi wa Dodoso la Kilimo:

1. Unatakiwa kusaidia na kushiriki katika kutoa taarifa za awali au kutangaza eneo lako la kazi kuhusu kufanyika kwa utafiti huu. Hii ni pamoja na kuwataarifu Wenyeviti wa mitaa/vijiji makusudi ya utafiti utakaofanyika na kuelewana nao mapema kutasaidia kurahisisha kazi.
2. Unatakiwa kuzielewa na kuziona kaya zilizochaguliwa katika sampuli ya eneo lako. Pamoja na kupima mashamba.
3. Unatakiwa kumwona mkuu wa kaya au mkazi yoyote mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea, wa kila kaya uliyopangiwa na kumweleza madhumuni ya shughuli yako na kupanga muda wa mahojiano.
4. Panga muda mzuri wa kwenda kudadisi wakazi wa kaya zilizochaguliwa.
5. Unapokuwa umemaliza kujaza dodoso liangalie kwa makini ili kuhakikisha kuwa hakuna makosa kabla ya kuondoka kwenye kaya. Hakikisha unapima mashamba kwa kaya zote. Mashamba yote yatakayo pimwa yatakuwa katika umbali wa saa mmoja toka kwenye kaya (kwa miguu, baiskeli, piki piki n.k.), kama unadhani shamba lipo mbali ni lazima upate ruhusa toka kwa msimamizi wako.
6. Unatakiwa kuwa na mawasiliano ya mara kwa mara na msimamizi wako ili aweze kukusaidia na pia kukagua kazi yako.
7. Utalazimika wakati wowote au ikitibidi kujibu hoja zozote toka kwa msimamizi wako au viongozi toka makao makuu. Hii ni katika kuhakikisha ufanisi wa kazi yako.
8. Unatakiwa kumkabidhi kazi msimamizi wako mara baada ya kumaliza.

## Sehemu A – 1: Utambulisho

---

Utapata orodha ya mageresho ya Mkoa, Wilaya, Kata\Shehia, Kijiji\eneo la kuhesabia toka kwa msimamizi wako. Andika utambulisho wa kaya kama ulivyoandika katika dodoso la kaya, *“**kuhakikisha utambulisho katika dodoso la kaya na utambulisho katika dodoso la kilimo hazitofautiani**” kisha jaza jina lako, namba yako na muda wa kuanza mahojiano katika ukurasa wa 2. Pia kuna sehemu maalum ya kuweka maoni.*

## Sehemu 1: Taarifa za Wanakaya

---

Nakili taarifa zote husika kutoka dodoso la Kaya, Ni MUHIMU SANA kuhakikisha kuwa kila mwanakaya ana utambulisho unaofanana kwa madodoso yote mawili.

**Swali la 4:** Weka alama ya  $\rightarrow X \phi$  kwa mwanakaya anayejibu dodoso la kilimo. Kama kuna wanakaya wawili au zaidi wanajibu maswali wawekee alama ya  $\rightarrow X \phi$

## Sehemu 2: Orodha ya Mashamba

---

**MAANA YA SHAMBA:** Mara nyingi kipande cha ardhi kilichoungana kinajulikana kama shamba. Hata hivyo, iwapo mwenye shamba anakichukulia kama mashamba tofauti kutokana na kuwa na umiliki tofauti, hapana budi kwa mdadisi kukichukulia hivyo.

*Mfano 1: Iwapo kaya inamiliki eka nne za shamba kupitia mume, na eka moja iliyoungana inayolimwa na kumilikiwa na mke, ni vyema ardhi hii ichukuliwe kama mashamba tofauti.*

Mfano 2: Iwapo mkulima ana eka mbili zenyenye hati na eka mbili nyingine zilizoungana zisizo na hati, ni vyema ardhi hii ihesabiwe kama mashamba tofauti.

Mfano 3: Kwa upande mwininge, iwapo mkulima ana eka kumi za ardhi lakini analima kwenye eka mbili tu kati ya hizo kumi, ni vyema hili lihesabike kama shamba moja la eka 10.

**Ukubwa wa shamba:** Katika maeneo ya vijijini maana ya shamba inaeleweka vizuri. Kwenye kaya nyingi huwa wanapanda chochote (mimea) kuzunguka nyumba (*shamba la nyumbani*), hilo litahesabika kama shamba. Kwa maeneo ya mjini, kaya inaweza kuwa na miti michache au mimea kuzunguka nyumba. Tumia kanuni zifuatazo kuamua endapo eneo hili litahesabika kama shamba.

Mti/mmea	Kiasi cha ukubwa wa shamba
Mwembe, mparachichi, mpesheni, mpera, mchungwa, mfenesi, mndimu/mlimau, jack fruit	Mti 1
Mgomba, mpapai	Miti 4
Nyanya, karoti, kabeji, spinachi, n.k.	Mita za mraba 4

#### **Swali la 1: Je, kuna mwanakaya yejote aliyelema au aliyemiliki shamba lolote katika masika 2014?**

Uliza kwa mashamba yote yanayolimwa na kaya iwe yanamiliikiwa au hayamiliiki na kaya (yalikodiwa au kulimwa bure). Ikiwa jibu ni NDIYO endelea na Jedwali A na iwapo jibu ni HAPANA nenda swali la 11 kuulizia msimu wa vuli.

**Jedwali A:** Orodhesha mashamba yote ambayo yalimiliikiwa au kulimwa na mwanakaya yejote katika msimu wa masika 2014. Orodhesha mashamba yaliyolimwa na kaya ikiwa yanamiliikiwa au kukodishwa. Hakikisha kwamba mashamba yote yaliorodheshwa na kulimwa na kaya yanaonekana sehemu hii.

#### **Swali la 2: Jina la Shamba**

Kama mashamba yaliyoorodheshwa kipindi cha 2012/2013, yanatakiwa kuorodheshwa hapa kwa kutumia majina yaleyale, hata kama ukubwa wake umebadilika. Mashamba yote mapya yapewe utambulisho ambao yatatambulika. Kwahiyo kwa kutumia utambulisho mhojiwa atayatambua mashamba na kupata taarifa zinazotakiwa. Majina ya mashamba ni lazima yawe wazi. Tunahitaji kuweza kuyafuatilia mashamba kwa kipindi kirefu. Hivyo basi, kwa kutumia majina sahihi ya kilitambua shamba, wahojiwa wataweza kutambua ni mashamba gani tunayohitaji kufuatilia taarifa zake kwa muda huo. Inawezekana asiwe mhojiwa yuleyule atakayetoa taarifa za mashamba kwa mwaka unaofuata, lakini inabidi mwanakaya yejote atakayehusika aweze kutambua mashamba hayo.

**Mfano:** Jina kama ōShamba la mahindiō halitoshelezi kwa kuwa shamba hilo linaweza lisiwe na mahindi katika miaka inayofuata. Andika jina la shamba, kama vile ōshamba la Kiswagaō ōshamba la nyumbaniō, n.k.

**Swali la 3: Maelezo/mahali lilipo shamba.**

Ni muhimu kutoa maelezo yanayojitosheleza kutambua mahali shamba lilipo ili liweze kutambulika baadae. Unatakiwa kutumia taarifa za mwaka 2012/2013 kupata mashamba yaleyale.

**Mfano:** Shamba lipo eneo la mahameni, nyumbani, mbugani n.k.

**Swali la 4: Eneo (EKA) makadirio**

Uliza ukubwa wa shamba katika kipimo cha ekari. Eneo la ekari liwe na tarakimu tatu na nafasi moja ya desimali, mfano 002.5, 034.2, n.k. Baadae utapima shamba kwa kutumia GPS, ila swali hili litaulizwa kwanza.

**Swali la 5: Namba ya shamba katika mwaka 2012/2013 wa NPS.**

Nakili namba ya Shamba kutoka orodha iliyochapishwa. Kama shamba halikuorodheshwa mwaka 2012/2013 andika -99q kama ulivyofanya kwenye dodoso la kaya kwa wanakaya wapya. Ikiwa kaya ni kaya mpya ambayo haikuwepo katika awamu zilizopita za NPS, hapo jaza 99 kwa mashamba yote. Mashamba yote ambayo aliyoorodheshwa na bado yanalinwa ni lazima yaonekane/aandikwe kwenye orodha.

**Angalizo:** Kuwa mwangalifu. Kuwa makini kulinganisha mashamba na maelezo/mahali lilipo shamba na majina kama yapo sahihi.

**Swali la 6: VIPIMO VYA GPS (GPS LOCATION)**

Sehemu hii tuna andika vipimo vya GPS vya kwenye kona ulipoanza kuzunguka shamba wakati wa kupima eneo. õSö SOUTH katika mstari wajuu na õEö EAST katika mstari wa pili. Kuchukua vipimo baada ya kuhoji dodoso la kilimo. Hii isiangiliane na mahojiano ya dodoso. Maelezo zaidi yanapatikana katika maelezo ya kupima mashamba.

**Swali la 7: SHAMBA LIMEPIMWA?**

Usipime shamba mpaka uwe umepewa ruhusa toka kwa msimamizi wako. Unatakiwa kupima mashamba yote ya kaya isipokuwa kwa yale ambayo umepewa ruhusa ya kutopima na msimamizi wako. Kanuni za upimaji shamba, unatakiwa kupima shamba umbali wa saa mmoja toka katika kaya kwa kutembea au kwa njia yoyote ya usafiri, hii inajumuisha kutumia pipipiki, au balskeli, n.k kufika shambani. Wakati mwingine mhojiwa anaweza kukataa kupima shamba kwasababu ni mbali sana au amechoka. Unatakiwa mweleza umuhimu na pengine kubadilisha muda wa kwenda au kwenda na mwanakaya mwingine anayefahamu vizuri shamba.

**Swali la 8: KWANINI SHAMBA HALIKUPIMWA?**

katika swali hili unatakiwa kutoa sababu kwanini shamba halikupimwa. **Angalizo: unatakiwa kupata ruhusa ya kutopima shamba toka kwa msimamizi wako.** Inawezekana shamba likawa mbali sana -geresho ni 1ø inawezekana mhojiwa amekataa -geresho ni 2ø . ni mara chache sana kupata sababu nyingine geresho 3, kama ikiwepo unatakiwa kuielezea. Kama nafasi haitoshi tumia ukurasa 2.

**Swali la 9: EKARI (VIPIMO VYA GPS)**

Andika vipimo vilivypatikana toka katika GPS (**vipimo vya GPS**). Andika katika EKARI na nafasi mbili za decimali. Kwa maelezo zaidi jinsi ya kuandika vipimo angalia nyuma ya mwongozo huu.

**Swali la 10: HALI YA HEWA WAKATI WA KUPIMA SHAMBA**

Swali ili ni kwa mdadisi, usimuulize mhojiwa. Linakutaka kuandika hali ya hewa wakati unapima shamba, hii ni kwasababu nyakati fulani za hali ya hewa zinaweza kuathiri usomaji wa GPS. Tumia jedwali hapo chini.

Picha	Hali ya hewa	Geresho	Maelezo
	Kweupe/jua kali/Kiangazi	1	Anga yote hakuna mawingu.
	Anga linaonekana vizuri (kweupe)/ Kiangazi zaidi/ jua kali	2	1/8 <sup>th</sup> to 2/8 <sup>th</sup> ya Anga imetandwa/limefunikwa na mawingu
	Sehemu ndogo ya anga ni mawingu na jua (mawingu kidogo/jua kidogo)	3	3/8 <sup>th</sup> to 4/8 <sup>th</sup> ya anga imetandwa/imefunikwa na mawingu
	Sehemu kubwa ya anga ni mawingu (mawingu zaidi/mawingu ya kuridhisha)	4	5/8 <sup>th</sup> to 7/8 <sup>th</sup> ya anga imefunikwa na mawingu.
	Mawingu kabisa (mawingu mazito)	5	Anga limetandwa na mawingu
	Mvua	6	Anga limetandwa na mawingu pamoja na ukungu

### Swali la 11: Msimu wa vuli uliopita ni wa mwaka gani?

Uliza msimu wa vuli uliopita ni wa mwaka gani, aidha vuli 2013 au 2014 kwa kujaza geresho 1 au 2. *Kumbuka kwamba msimu wa vuli unaanza mwezi Septemba hadi Desemba kila mwaka kwenye sehemu ambazo zinapata mvua ya misimu miwili kwa mwaka (vuli na masika).*

### Swali la 12: Zaidi ya mashamba hapo juu (jedwali A), je, Kuna mwanakaya ye yeyote alilima au alimiliki shamba lolote katika msimu wa vuli uliopita?

Muulize mhojiwa iwapo kuna mwanakaya anayelima au anayemiliki shamba lolote katika msimu wa vuli wa mwaka husika tumia mwaka katika swali la 11. *Iwapo jibu ni hapana nenda swali la 22.*

**Jedwali B:** Licha ya mashamba yaliyoordheshwa hapo juu tafadhali orodhesha mashamba yaliyolimwa au kumilikiwa na kaya katika msimu wa vuli [í ..] (angalia jedwali A). Uliza tu kwa mashamba ya ziada ambayo hayakuordheshwa katika Jedwali A. Hii inamaanisha kuwa mara nyingi Jedwali B litakuwa tupu bila taarifa yoyote.

### Maswali ya 13–21: Maelezo ya maswali haya ni sawa na yale yaliyoko katika jedwali A (SW.2 ó 10 )

**Sehemu ya Ramani:** Tafadhali chora ramani ya mahali lilipo shamba kuanzia kwenye nyumba. Katika mchoro wa shamba, hakikisha unaonyesha upande lililopo kutoka makazi na mashamba mengine ya kaya kwa kutumia dira (Kaskazini, Mashariki, Kusini na Magharibi). Pia kadiria umbali

na muda kutoka nyumbani hadi lilipo shamba (kwa kutembea/baiskeli, n.k) au masafa kutegemea na uwezo wa mhojiwa.

## Maelezo ya Sehemu ya 2 – 7

---

### HAKIKISHA SEHEMU 2-7 ZINASHABIHIANA.

#### **Mashamba yaliyoorodheshwa katika sehemu ya 2 ikifuatiwa kwa juu na 3 (na ikiwezekana 4 na 6).**

- Mashamba yote yaliyoorodheshwa kwenye sehemu ya 2A lazima yaonekane kwenye sehemu ya 3A.
- Mashamba yote yaliyoorodheshwa kwenye 2A na 2B lazima yaonekane kwenye sehemu ya 3B.
- Mashamba yote yaliyoorodheshwa kwenye 2A lazima yaonekane kwenye sehemu ya 4A au 6A. Kwa kuongeza, shamba lolote lililoorodheshwa kwenye sehemu ya 3B ambalo jibu la 3B swali la 40 lilikuwa ḍöndiyoö lazima lioneckane kwenye 4B au 6B.
- Zao lolote lililoorodheshwa kwenye sehemu ya 4A ambalo jibu la 4A swali la 31 ni ḍöndiyoö lazima lioneckane sehemu ya 5A.
- Mazao yote yaliorodheshwa kwenye sehemu ya 4B lazima yaonekane kwenye sehemu ya 5B kama jibu kwenye sehemu ya 4B swali la 31 ni ḍöndiyoö.

Ikiwa ulivuna mahindi kutoka shamba lolote, unatakiwa angalau utuambie katika sehemu ya 5 kwamba uliuza/haukuuza mahindi yoyote. Unaweza kuruka maswali ya mavuno yanayofuata (Sehemu ya 5) ikiwa Mhojiwa atasema hawakuvuna zao lolote katika sehemu ya 4, swali la 31. (Lakini hakikisha wanasema ḍöhapanaö katika swali la 31 kwa mashamba yote yenye zao).

- Matunda/mazao yote yaliyoorodheshwa katika sehemu 6a yanapaswa kutokea katika sehemu ya 7A. Matunda/mazao yote yaliyoorodheshwa katika sehemu 6b yanapaswa kutokea katika sehemu ya 7B.
- Mashamba yote yaliyoorodheshwa katika sehemu ya 2B yanapaswa kutokea katika sehemu ya 4B au 6B ikiwa jibu katika sehemu ya 3B swali la 1b lilikuwa ḍöndiyoö. Kwa kuongeza shamba lolote lililoorodheshwa katika sehemu ya 3B ambalo jibu katika sehemu ya 3B swali la 40 lilikuwa ḍöndiyoö linapaswa pia kutokea katika sehemu ya 4B na 6B. Hivyo hivyo kwa sehemu ya 2A, lakini haiwezi kufanya kazi kinyume na hapo. Ikiwa ulikuwa na shamba katika msimu wa vuli na ulilima, unapaswa kueleza zao hapo shambani. Lakini kulima shamba katika msimu wa vuli haimaanishi inapaswa kuorodheshwa katika 2B, haya ni mashamba ambayo yalilimwa msimu wa vuli tu.

#### **Usiongeze mashamba mapya baada ya sehemu ya 2. Usiongeze mazao mapya katika sehemu ya 5 au sehemu ya 7.**

- Sehemu ya 2 inapaswa kuorodheshwa mashamba yote yaliyotajwa sehemu yoyote katika dodoso. Usiongeze mashamba mapya katika sehemu ya 3, sehemu ya 4 au sehemu ya 6.
- Sehemu ya 4 inapaswa kuorodheshwa mazao yote ya msimu / mwaka. Usiongeze mazao mapya katika sehemu ya 5 ambayo hayapo katika sehemu ya 4.
- Sehemu ya 6 inapaswa kuorodheshwa miti yote ya matunda na mazao ya kudumu. Usiongeze mazao mapya katika sehemu ya 7 ambayo hayakuwa yameorodheshwa katika sehemu ya 6.

#### **Epuka kuhesabu mara mbili**

- Shamba husika halipaswi kurudiwa katika 3A au katika 3B.
- Mazao mchanganyiko husika katika shamba hayapaswi kurudiwa katika 4A au 4B.
- Zao husika halipaswi kurudiwa katika sehemu 5A au katika 5B au katika 7A au 7B.
- Mashamba yote yaliyoorodheshwa katika 2A yanapaswa kutokea katika 4A au 6A ikiwa jibu la 3A swali la 30 lilikuwa ḍöndiyoö. (Angalizo: mashamba yanaweza kurudiwa katika 4A na

6A. Mazao mchanganyiko hayapaswi kurudiwa). Sehemu ya 2A ni orodha ya mashamba anayomiliki au anayolima. Ikiwa atatueleza katika sehemu ya 3 kwamba alilima shamba, anapaswa kutuambia kama ni mazao ya mwaka (Sehemu ya 4) au ni ya kudumu (Sehemu ya 6) katika shamba hilo.

**Mfano:**

Kama kaya ina mashamba yalivyoonyeshwa katika picha hapa chini. Mazao yanayolimwa katika kila shamba yameonyeshwa katika msimu wa masika na vuli. Mashamba yaliyopumzishwa yameonyeshwa na rangi ya kijivu. Mazao ambayo yalipandwa lakini hayakutoa mavuno yametolewa.

Ukurasa ufuatao unaonyesha jinsi dodoso litakavyojazwa kwa ajili ya haya mashamba. Mchoro katika ukurasa unaofuata unaonyesha mwanzo wa kila sehemu, kuonyesha ni mashamba yapi na mazao gani yanapaswa kuorodheshwa. Kumbuka yafuatayo:

- Mashamba ya waziri na bondeni yameorodheshwa katika 2A kwa sababu yalilimwa kipindi cha masika.
- Shamba la Mtembeni limeorodheshwa katika 2B kwa sababu halikumilikiwa au kulimwa masika ó ila vuli tu.
- Mashamba yote ya 2A yameorodheshwa 3A. Na yote yameorodheshwa katika sehemu ya 3B.
- Shamba la Waziri lilorodheshwa mara mbili katika sehemu ya 4A na 4B, kwa sababu kulikuwa na mazao mchanganyiko ya mwaka (mahindi na maharage) yaliyolimwa katika shamba hili katika msimu wa masika na vuli.
- Mahindi yanalinwa katika mashamba mawili katika sehemu 4A, lakini yameorodheshwa mara moja tu katika sehemu ya 5A. Kwa kila zao, unganisha mashamba yote katika mstari mmoja kwenye sehemu ya 5.
- Katika msimu wa vuli, Maharage yalitolewa katika sehemu 4B kwa sababu hakuna kilichovunwa.
- Miti ya matunda (kama mwembe) na mazao ya kudumu (kama muhogo) yameorodheshwa katika sehemu ya 6.
- Muhogo ultolewa katika sehemu 6B kwa sababu hakuna kilichovunwa.

## Masika

Waziri

mahindi  
maharage  
mwembe  
~~mihogo~~

Mlimani

mahindi

## Vuli

Waziri

mahindi  
~~maharage~~  
mwembe  
~~mihogo~~

Mlimani

lilipumzishwa

Mtembeni

mahindi



# Watoa Huduma

---

ØWatoa hudumaö (*network roster*) ni orodha ya watu wote (ambao si wanakaya), makampuni au mashirika ambapo mhojiwa hufanya biashara nao. Orodha ya watoa huduma inajengwa na mdadisi wakati wa mahojiano, kadiri mhojiwa anavyo jibu maswali ndivyo wale anaoshirikiana nao wanafahamika.

## **Jaribu kukamilisha orodha ya watoa huduma wakati wa mahojiano.**

Katika dodoso lote la kilimo, kila wakati swali linauliza ḋnaniø litakutaka wewe kunakili geresho la watoa huduma husika. Kwa mfano øNani mnashirikiana kumiliki shamba hili?ø, øUlienda wapi kununua mbeguø na øUliuza kwa nani mazao yako?ø

Wakati mhojiwa anaorodhesha orodha ya mfanyabiashara wa mara ya kwanza ameshirikiana nao, unatakiwa kujumuisha majina hayo katika orodha ya øwatoa hudumaö. Tumia namba mpya za utambulisho {N1, N2, n.k} kwa kujaza kama jibu la swali husika. Pia ujaze taarifa zake katika sehemu ya watoa huduma.

Kwa mara nyingine mhojiwa atamtaja mtu yuleyule au kampuni ileile tumia utambulisho ule wa awali. Tenganisha mtu binafsi na taasisi.

Usiandike mtu mmoja au taasisi moja zaidi ya mara moja katika orodha ya watoa hudumu kwa utambulisho mmoja. Kwa mfano N1 ó jirani, N1 ó Oxfam hii si sahihi.

Ikiwa mhojiwa hawezi kukumbuka majina ya watoa huduma, mdadisi lazima atambue kuwa utambulisho utakuwepo hata kama mhojiwa hakumbuki jina, ina maana N1 itakuwepo ila jina halitakuwepo kwahiyø yaandikwe maelezo mafupi kumtambulisha. Kila mara mtoa huduma anapohusika katika matukio tofauti utambulisho mmoja utumike.

Orodha ya watoa huduma ipo katika ukurasa wa mwisho wa dodoso.

## **SWALI LA 1: JINA**

Jaza jina husika, kampuni au shirika linalozungumziwa. Usiandike ḋnduguø ḋjiraniø au mageresho mengine yoyote kutoka kwenye boksi hapo kulia.Hii inahitaji umakini wa hali ya juu. Tuchukulie,labda mhojiwa alikodi shamba kutoka kwa ḋFrank Mhandoøau aliuza mazao yake katika ḋsoko la Korogweø au alipokea vitendea kazi toka kwa ḋushirika wa wakulima wa pamba Tangaø

## **SWALI LA 2: MAGERESHO**

Chagua geresho moja kutoka kwenye boksi hapo kulia, palipoandikwa ømageresho ya swali la 2ø Haya mageresho yatagawa wahusika mmojammoja na mashirika katika mgawanyiko wa watoa huduma. Zingatia kuwa swali hili linakuwa katika herufi kubwa [GERESHO]. Hakuna haja ya kumsomea mhojiwa kama itakuwa inaeleweka toka kwenye swali kama lilivyo, sema ndugu au jirani.

## **SWALI LA 3: MAHALI/ENEKO**

Chagua geresho moja kutoka kwenye boksi hapo chini katika ukurasa ulioandikwa ømagaresho ya swali la 3ø. Haya mageresho yanaelekeza kwa urahisi mahali walipo washauri husika au mashirika. Ili kujua mahali tutazingatia wakati malipo yalipofanyikia. Kama mkulima wa kijiji cha mkoa wa Tanga atasema aliuza pamba kwa mnunuzi fulani ambaye ofisi yake ipo Tanga mjini, lakini huwa anakuja kwa usafiri wake kijijini kwa ajili ya kukusanya pamba, utaandika mahali 1, øNDANI YA KIJIIJØ.

## MFANO:

Chukulima mkulima amepata mbolea zote (samadi) na mbegu kwa ajili ya mahindi yake tok kwa jirani yake Frank Mhando. Kwa maelezo haya, utakapoingia swali la 46 katika Sehemu ya 3 utajumuisha jina la Frank katika orodha ya watoa huduma katika mstari mwagine unaofuata (N2) halafu weka geresho kama kutokana na jibu la swali la 46. utakapoingia swali la 13 katika Sehemu ya 4, utaweka GERESHO HILO HILO kwa sababu nilinunua mbegu kutoka kwa mtu huyo huyo.

42. Ni wapi minunuakupewa sehemu kubwa ya samadi?	<b>4A. MSIMU WA MASIKA 2008</b> <table border="1" style="width: 100%; border-collapse: collapse;"> <tr> <td style="width: 33.33%; padding: 5px;">S H A M B A</td> <td style="width: 33.33%; padding: 5px;">Z A O</td> <td style="width: 33.33%; padding: 5px;">21. Ni wapi minunuakupewa sehemu kubwa ya mbegu?</td> </tr> <tr> <td style="padding: 5px;">GERES HO</td> <td style="padding: 5px;">GERES HO</td> <td style="padding: 5px;">ORODESHA WATOAHUDUMA HADI WAWILI</td> </tr> <tr> <td style="padding: 5px; text-align: center;">1</td> <td style="padding: 5px; text-align: center;">2</td> <td style="padding: 5px; text-align: center;">1</td> </tr> <tr> <td colspan="3" style="text-align: center; background-color: #e0e0e0;"><b>N2</b></td> </tr> <tr> <td colspan="3" style="height: 100px;"></td> </tr> </table>		S H A M B A	Z A O	21. Ni wapi minunuakupewa sehemu kubwa ya mbegu?	GERES HO	GERES HO	ORODESHA WATOAHUDUMA HADI WAWILI	1	2	1	<b>N2</b>					
S H A M B A	Z A O	21. Ni wapi minunuakupewa sehemu kubwa ya mbegu?															
GERES HO	GERES HO	ORODESHA WATOAHUDUMA HADI WAWILI															
1	2	1															
<b>N2</b>																	
ORODESHA WATOAHUDUMA HADI WAWILI																	

**NETWORK ROSTER CARD**

ID	1. JINA	2. GERESHO	3. MAHALI	
			M1	N1
N1	Soko ya Korogwe	3	3	
N2	Frank Mhando	2	1	
N3	Tanga Sisal Coop	5	4	

## Sehemu 3: Taarifa za Mashamba

Jaza majina ya mashamba kwenye **Flap** kabla hujaanza sehemu hii. Tumia **Flap** hii kuhakikisha taarifa za shamba husika ziko katika mstari sahihi.

**Sehemu 3A** – maswali katika sehemu hii yanahusu msimu wa masika na mashamba yote yaliyoorodheshwa kwenye Jedwali A katika Sehemu 2.

**Sehemu 3B** ó maswali katika sehemu hii yanahusu vuli kwa mashamba yote yaliyoorodheshwa kwenye Majedwali A na B katika Sehemu 2. maswali katika sehemu 3A na 3B yanafanana ila ni maswali yanayouliza katika vipindi tofauti yaani 3A ni msimu wa masika 2014 na 3B ni msimu wa vuli uliopita.

## **HAYA NI MAELEKEZO KWA MDADISI.**

**Swali la 1: ORODHESHA MASHAMBA YOTE YALIYOLIMWA AU KUMILIKIWA NA KAYA KATIKA MSIMU WA KILIMO WA MASIKA 2014, TUMIA TAARIFA TOKA SEHEMU YA 2A.**

**Swali la 2: Umbali toka shambani hadi?**

Muulize mhojiwa umbali kwa kilometa (km) toka shambani hadi nyumbani, barabarani na sokoni. Muombe akadirie kama hana uhakika. Kama mhojiwa atakupa umbali kwa dakika au masaa, chukua kwa makadirio kutembea kilometa moja (1) iwe sawa na dakika 15. Kwa hiyo kwa dakika 22 na sekunde 30, mtu atakua ametembea kilometa 1.5.

**Swali la 3: Je, shamba hili lilitumikaje msimu wa kilimo uliopita?**

Lengo la swali hili ni kujua jinsi shamba lilivytumika katika msimu masika wa kilimo uliopita. Mfano shamba limwa, likodishwa, ligawiva bure, lipumzishwa n.k. Angalia mageresho husika katika dodoso. Kama jibu ni ōliligaiwaö ina maana mmiliki wa shamba hili hakupokea mazao kama malipo au malipo kwa njia ya pesa au malipo kwa njia yeyote ile kutoka kwa mtu aliyelelima shamba hili. Kama malipo yalifanyika kwa njia ya pesa au kwa njia yeyote ile isiyo ya pesa kutoka kwa mtu aliyelelima shamba utatakiwa kutumia geresho ōlililokodishwaö.

**Swali la 4: Je, ni kiasi gani cha kodi mllichopata katika miezi 12 iliyopita kwa kukodisha shamba hili?**  
Muulize mhojiwa kiasi cha fedha ya kodi alichopata kutokana na kukodisha shamba hilo. [PAMOJA MALIPO YASIYO YA FEDHA, MALIPO YA MAZAO NA MALIPO MENGINE YALIYOLIPWA AU YATAYOLIPWA KATIKA MIEZI 12 ILIYOPITA]

**Swali la 7: Je, ni zao gani kuu lilipandwa katika shamba hili msimu wa masika wa 2014?**

Muulize mhojiwa ni zao gani kuu lililo pandwa katika msimu wa masika wa 2014. Zao kuu ni lile lilipandwa sehemu kubwa la shamba au mhojiwa analichukulia kama lina umuhimu mkubwa kwake. Mageresho ya mazao yapo katika ukurasa wa mwisho wa dodoso. Kuwa mwangalifu unapo tumia geresho laø nyingineø mara nyingi vitu vimekua vikiandikwa kama nyingine na hali vinakuwa ni vilevile ila kwa majina mengine.

**Swali la 8: Nani alitoa maamuzi katika aina ya zao lilipandwa katika msimu wa masika wa 2014?**

Uliza nani aliyetoea maamuzi katika zao lilipandwa katika msimu wa kilimo wa masika 2014. Andika hadi namba tatu za wanakaya kutoka katika orodha ya wanakaya na watoa huduma. Andika sifuri kama haihusiki. Mfano: Mkuu wa kaya na mwenza wake ndio waliota maamuzi ya aina ya zao lilipandwa kwa msimu wa masika uliopita, andika namba zao za kaya kutoka sehemu -lø (inaweza ikawa ō01ø au ō02ø). Kama mkulima mkubwa ame ahidi kununua kilo 100 za mananasi toka shambani, utumie orodha ya watoa huduma.

**Swali la 9: Nani alitoa maamuzi ya utumiaji wa pembejeo za kilimo kwenye shamba hili katika msimu wa masika wa 2014?**

Muulize ni nani aliyetoea maamuzi ya utumiaji wa pembejeo kama: pembejeo gani, kiasi gani, itumiwaje kwenye shamba. Mfano; Kama mkuu wa kaya aliamua pembejeo gani itumike, na mwenziwake alitoa maamuzi ya kiasi gani kitumike kwa kila shamba, kwahiyoo namba zao za kaya itabidi ziandikwe kutoka kwenye orodha ya kaya, orodhesha mpaka watatu na mmoja ambaye si mwakaya kutoka kwenye orodha ya watoa huduma.

**Swali la 10: Aina gani ya udongo katika shamba?**

Aina ya udongo hutumika sana kujua shamba linazalisha mazao kwa kiasi gani. Udongo wa mchanga ni ōmwepesiö, na udongo wa mfinyanzi ni ōmzitoö. Udongo wa mfinyanzi ni mzuri kwa kutengeneza matofali. Udongo wa kichanga si mzuri kwa kutengeneza matofali. Udongo wa mchanganyiko upo katikati ya udongo wa kichanga na mfinyanzi.

**Swali la 11: Ni ubora gani wa udongo katika shamba?**

Muulize mhojiwa kutoa maoni yake juu ya ubora wa udongo katika shamba na andika geresho husika ubora wa udongo una maana ya rutuba ya udongo. Udongo mzuri una rutuba na unaweza kupanda na kuvuna

mavuno mengi. Udongo mbaya hauwezi kutoa mavuno mengi. Udongo wa wastani upo katikati ya udongo mzuri na mbaya.

#### **Swali la 12: Je, umetambuaje ubora wa udongo?**

Muulize mhojiwa jinsi anavyotambua ubora wa udongo. Mara nyingi kujua ubora wa udongo unategemeana na uzoefu wa mtu mwenyewe labda afisa ugani awe ameshawahi kuwatembelea wakulima na kupima ardhi yao na kujua aina ya udongo. Andika geresho linalostahili.

#### **Swali la 13: Je, kulikuwa na tatizo la mmomonyoko wa udongo katika shamba hili msimu wa masika wa 2014?**

Mmomonyoko wa udongo ni kuenguliwa/kutolewa kwa sehemu ya juu ya udongo kwa mvua, upepo, wanyama na binadamu. Jaza geresho la ndiyo kama baadhi au mashamba yote yamepata tatizo la mmomonyoko katika msimu wa masika uliopita, na hapana kama hakuna tatizo hilo na nenda swali la 15.

#### **Swali la 14: Je, nini sababu ya mmomonyoko huo?**

Tumia/mageresho yaliyoorodheshwa katika dodoso hili. Kumbuka kuwa ōkilimo ambacho hakiendani/hakizingattii utunzaji wa udongoō kitatusika kusababisha mmomonyoko wa udongo.

#### **Swali la 15: Je, kulikuwa na mbinu yoyote ya kudhibiti mmomonyoko/kuvuna maji katika shamba hili msimu wa masika uliopita?**

Muulize mhojiwa kama alitumia njia yoyote katika kudhibiti mmomonyoko/kuvuna maji katika shamba msimu wa kilimo wa masika 2014. Orodha ya njia zitumikazo zimetolewa katika swali la 16 kama mhojiwa haelewi unamaanisha nini kwa ōkudhibiti mmomonyoko/kuvuna maji.

#### **Swali la 16: Je, njia/mbinu gani mnayotumia kudhibiti mmomonyoko/kuvuna maji katika shamba hili? [ORODHESHA NJIA MBILI KUU ZA KUDHIBITI MMOMONYOKO WA KUFUATA UMUHIMU WAKE]**

Maana ya njia hizo zimeorodheshwa hapa chini na pia kuna picha katika kiambatanisho.

- *Matuta*: Matuta yanafanana na ngazi zilizokatisha katika pande za shamba lenye mwinuko kufanya shamba liwe tambarare.
- *Matuta ya kuzuia mmomonyoko*: Matuta haya hutengenezwa na wakulima, mara nyingi hutengenezwa kwa mawe au udongo kuzuia mmomonyoko kwenye mwinuko mkali.
- *Mifuko ya mchanga*: Gabions kwa kawaida inatengenezwa na waya wenye matundu (wire mesh), ambao umejazwa na udongo na/au mawe kutengeneza kuta kwenye miinuko. Mifuko ya mchanga pia hutumika kuzuia maji au udongo kuondoka kwenye shamba.
- *Majani ya vetiva*: Majani ya vetiva yanaweza kuwekwa kama kizuizi cha majani katika kitako cha tuta ili kupunguza kasi ya maji kutiririka. Pia yanazuia mabaki ya mazao na vitu vingine vya asili (organic matters), ambavyo vinaongeza kuongezeka kwa majani yanayozuia mmomonyoko pamoja na kuzuia kuhribia kwa matuta.
- *Ukanda wa miti*: Ukanda wa miti ni mstari wa miti uliooteshwa labda kwa lengo la kuzuia upepo au kuimarisha maeneo yaliyo katika hatari ya kupatwa na mmomonyoko.
- *Makinga maji*: Vifaa vya kukingia maji ya mavua vinatengenezwa kwa kutumia udongo au mawe kuelekeza maji katika maeneo ya kukusanya maji.
- *Mitaro*: Mitaro imetengenezwa kukusanya maji. Mara nyingi hupatikana katika kingo za barabara.
- *Bwawa*: Bwawa linasimamisha au kupunguza kasi ya mto au mkondo wa maji kuachia maji kukusanya kwenye ziwa au dimbwi.

#### **Swali la 17: Shamba lako lina mwinuko wa aina gani?**

Muulize mhojiwa shamba lake lina mwinuko wa aina gani na andika geresho sahihi kulingana na jibu utakalopewa na mhojiwa. Kama maji hayatiririki kwenye shamba, shamba hilo ni tambarare. Lenye mwinuko mkali au kiasi litakuwa gumu kulimika kwa sababu ya mwinuko huo.

**Swali la 18: Je, shamba hili lilimwagiliwa maji msimu wa masika wa 2014 ?**

Uliza iwapo shamba husika lilimwagiliwa maji msimu wa kilimo wa masika wa mwaka 2014. Hii inajumuisha kilimo cha kisasa na kile cha kunyeshea kwa kawaida. Iwapo jibu ni ndiyo endelea na swali la 19, iwapo jibu ni hapana nenda swali la 22.

**Swali la 19: Je, mlitumia aina gani ya umwagiliaji?**

Muulize mhojiwa ni aina gani ya umwagiliaji anaotumia kumwagilia maji shamba. Andika geresho husika. Umwagiliaji wa kunyunuzia unafanana na mvua ya kawaida. Aina hii inaweza kutumika kwenye mazao tofauti tofauti, udongo na katika hali yoyote ya hewa. Umwagiliaji wa matone unahusisha teknologia mbali mbali, ambapo maji hutumiwa kwa sehemu tu ya shamba. Njia hii inaweza kusaidia kupunguza matumizi ya maji na uzalishaji. Gharama ya kununua, kuendesha na kutunza kifaa hiki ni kubwa. Ndoo (Watering can) ni njia rahisi ya umwagiliaji na hutumiwa sana na wakulima wadogo wadogo. Ni nzuri kwa mashamba madogo ya mboga yaliyopo karibu na vyanzo vya maji.

**Swali la 20: Njia ipi uliyoitumia kupata maji?**

Muulize mhojiwa njia inayotumia kupata maji ya kumwagilia shamba na uandike geresho husika. Yanayotiririka ni jibu sahihi kwa njia yoyote ya kupata maji ambayo inafanana na ile ya maji yanayotiririka kwenye mfereji au mwinuko, inaweza kuwa ya kawaida au ya kutengenezwa. Pampu za umeme au mafuta (motorized pumps) ni vifaa vinavyotumika kupandisha maji kwa kutumia dizeli, petroli au umeme. Mfano wa pampu ya umeme (motor pump) ni ōradial flow pumpö mara nyingi hujulikana kama ōcentrifugal pumpö.

**Swali la 21: Maji mliyotumia kumwagilia yalipatikana toka chanzo gani?**

Uliza chanzo cha maji ya kumwagiliaji. Andika geresho linalostahili.

**Swali la 22: Je, ni mwaka gani wa karibuni shamba limewahi kupumzishwa kulimwa ?**

Kulipumzisha shamba ni kuacha shamba wazi bila kulilima kwa kipindi fulani, kwa lengo la kuengeza ubora wa udongo. Uliza mwaka wa karibuni shamba lilipumzishwa kulima (mwaka uandikwe katika tarakimu 4, mfano 2007, 2008, n.k). Kama hapana andika 0 nenda swali la 24, kama hajui andika 98 nenda swali la 24

**Swali la 23: Kwa miaka mingapi mfululizo shamba hili lilipumzishwa kwa mara ya mwisho?**

Andika idadi ya miaka mfululizo ambayo shamba lilipumzishwa.

**Mfano:** Shamba lilipumzishwa kwa miaka ō2ö, mwaka ō2012ö na ō2013ö. Na lililimwa ō2012ö na ō2014ö. Kwa hiyo jibu la swali la 22 litakuwa ō2013ö na jibu la swali la 23 litakuwa ō1ö.

**Swali la 24: Iwapo shamba hili lingezuwa leo, unadhani lina thamani gani?**

Muulize mhojiwa thamani ya shamba iwapo lingezuwa leo. Katika Swali hili thamani ya shamba isihusishe mazao ya muda yaliyopandwa humo. Hata hivyo, thamani miti ya matunda na mazao ya kudumu ijuishwe. Hakikisha kuwa wahojiva wote wanapewa ufanuzi huu wanapotakiwa kutaja thamani ya shamba. Mweleze mhojiwa kwa umakini kuwa taarifa hizi zitatumika kwa lengo la uafiti tu na si vinginevyo.

**ANGALIZO:** Swali hili la umiliki wa ardhi ni muhimu sana kwa utafiti. Hapa tunahitaji kujua ni kiasi gani cha ardhi kinamilikiwa na kilipatikanaje. Swali hili ni muhimu lakini ni nyeti, kaya inaweza kudhani serikali inapanga kunyanganya ardhi yao au kufidia kwa kaya zenye mashamba machache/ madogo.

**Swali la 25: Shamba hili lilipatikanaje?**

Chagua geresho husika linaloelezea jinsi kaya ilivyolipata shamba. Ikiwa kaya inamili ki shamba, dodosi zaidi kama lilikuwa la kurithishwa, zawadi au lilinunuliwa na kaya. Ni shamba ambalo ō linatumwiwa bureö au ō limetolewa na kijijiö linaweza kurudishwa kwa mmiliki wake au viongozi wa kijiji katika muda fulani hapo baadae.

**Swali la 26: Mmeshirikiana na nani kumiliki shamba hili?**

Uliza iwapo kaya inashirikiana katika kumiliki shamba hili. Kumbuka kuwa swali hili linawahu wale waliosema kuwa ni shamba linalomilikiwa kwa kushirikiana. Kama hakuna mtu anayeshirikiana nae kumiliki andika N99.

Andika utambulisho wa mtu/kaya wanaoshirikiana kumiliki shamba. Mfano: Kama ninashirikiana kumiliki shamba na kaka yangu ninatakiwa nitafute jina lake au (nijumuushe jina lake) katika utambulisho wa watoa huduma na kuandika utambulisho wake (mfano: N1, N2 n.k).

**Swali la 27: Mnagawana mazao kwa uwiano gani?**

Iwapo shamba linamiliikiwa kwa kushirikiana, ni dhahiri kwamba kuna kugawana sehemu ya mazao au yote. Uliza iwapo kaya inagawana mazao kwa uwiano gani na jaza geresho stahiki.

**Swali la 28a: Ni aina gani ya hati ya umiliki halali kaya yako iliyonayo kwa shamba hili?**

Chagua aina ya hati kaya iliyonayo kuhakikisha umiliki wa shamba lao Ikiwa kaya haina hati ya umiliki wa kimila au hati ya kupewa ardhi/kiwanja, hapo weka geresho 3. Nenda swali la 28d ikiwa geresho ni 1au 2.

**Swali la 28b: Je, ungependa kuwa na hati ya kimila/ rasmi?**

Dodosa kama Kaya ingependa kuwa na hati iliyo rasmi au halali kisheria kudhibitisha umiliki wa shamba.

**Swali la 28c: Je, ungekuwa tayari kulipia hati milliki?**

Uliza kaya kama wangkuwa tayari kulipa ili wawe na hati iliyo rasmi/kisheria kwa shamba.

**Swali la 28d: Ni aina gani nyingine ya umiliki au hati za kisheria ambayo kaya hii inayo kwa ajili ya shamba hili?**

Uliza kama kaya ina aina nyingine za hati kwa shamba. Ikiwa kaya haina nyaraka au hati za shamba, weka geresho 8.

**Swali la 29: Ni nani katika kaya anamiliiki shamba hili?**

Orodhesha hadi wamiliki 2 kwa umuhimu wao ukitumia namba zao kutoka katika orodha ya wanakaya.

**Swali la 30: Je, mmiliki/kaya ina haki ya kuuza au kutumia shamba hili kama dhamana/rehani ya mkopo?**

Kaya inamiliiki shamba kama ina haki ya kulilima bila kulipa kodi kwa mtu yejote na hashirikiani kulimiliki na mtu mwingine yejote. Pia viongozi wa kijiji wanaweza kuzuia shamba lisiuzwe hata kama linamiliiki na mtu.

Kutumia shamba kama dhamana/rehani ni kutumia shamba kama mbadala wa mkopo uliokopwa, mpaka mkopo huo utakapolipwa na akishindwa kulipa shamba hilo litachukuliwa hata kama analimiliki. Jaza -1Ø kama jibu ni ndiyo na -2Økama hapana, utaenda swali la 38.

**Swali la 31: Nani katika kaya anayeweza kutoa maamuzi ya kuuza shamaba au kutumia kama dhamana?**

Uliza nani ana uwezo wa kufanya maamuzi ya kuuza ama kutumia ardhi kama dhamana. Andika namba ya mwanakaya, orodhesha hadi wawili. Jibu lolote utakalopewa hapa, nenda swali la 38.

**Swali la 31a: Kama unataka kuuza shamba hili, je utahitaji ruhusa toka mtu yoyote/mamlaka yoyote?**

Uliza kama kaya inahitaji ruhusa/kibali kutoka kwa mtu yoyote kabla ya kuuza shamba. Kaya bado inaweza kuhitaji ruhusa kutoka sehemu nyingine hata kama walisema -NDIOØkatika swali la 30. Kwa mfano, mkuu wa kaya anamiliiki shamba lakini bado anahitaji kibali kutoka kwa viongozi wa kijiji kabla ya kuuza shamba.

**Swali la 32: Unashirikiana na nani katika kukodi?**

Andika kwenye orodha ya watoa huduma jina la mmiliki mwenza. Kukodisha shamba ina maana kulipa pesa au malipo kwa mfumo mwingine wowote kwa mmiliki wa shamba kwa kupata haki ya kulilima. Swali la 32 lina maana ya mtu/kaya kukodi shamba kwa kushirikiana na mtu/kaya nyingine. Mfano mimi na kaka yangu tumelipa kodi kwa mmiliki wa shamba na tukalilima shamba pamoja, kwa hiyo mimi nimeshirikiana na kaka yangu kukodisha shamba.

**Swali la 33: Ni kiasi gani mlimlipa mmiliki wa shamba kwa kulitumia msimu wa masika wa 2014?**

Jumuisha thamani ya malipo yasiyo ya fedha, malipo kwa njia ya mavuno na malipo mengine ya kabla au baada katika msimu wa masika 2014.

**Swali la 34: Je, malipo hayo yalikuwa kwa kipindi gani?**

Swali la 33,imeonyesha kiwango cha pesa kilichotumika kulipa kodi ya shamba. Swali la 34 linauliza kama malipo hayo yalikuwa ni kwa mwaka mzima, kwa kipindi fulani katika mwaka, kwa miaka kadhaa n.k.

Mfano: Kaya ililipa sh. 40,000 mwaka 2010 kwa ajili ya kutumia shamba msimu wa masika 2010, 2011, na 2012, kwa hiyo sh. 40,000 zijazwe swali la 33 na katika swali la 34, safuwima ya kwanza ijazwe idadi na safuwima ya pili ijazwe kipimo.

**Swali la 35: Ni gawio kiasi gani cha mavuno alipewa mmiliki wa shamba kwa kulitumia msimu wa masika wa 2014?**

Kama mhojiwa analima shamba linalomilikiwa na mtu mwingine, anaweza kumpa mmiliki kiasi Fulani cha mavuno, swali hili linauliza ni kiasi gani kilitolewa/alipewa. Mdadisi achague geresho linalofaa kwa kiasi alichotoa mhojiwa. Mfano; Kama alivuna kilo 30 na kilo 10 alipewa mmiliki hiyo ni sawa na asilimia 33 au 10/30, weka geresho 3, au kama thani ya mazao ilikuwa 125,000 na sh. 35,000/= alipewa mmiliki, ni sawa na asilimia 72 au 90,000/125,000, jaza geresho 5.

**Swali la 36: Nani anamiliki shamba hili?**

Taja orodha ya watoa huduma.

**Swali la 37: Nani katika kaya ana haki ya kutumia shamba hili?**

Uliza nani katika kaya ana haki ya kutumia ardhi, huyu ni mtu anaewasiliana na mmiliki wa shamba. Mfano: Kama mmiliki wa shamba anahusika/wasiliana na mkuu wa kaya,utajaza namba ya mkuu wa kaya kutoka kwenye orodha ya kaya, kwa jibu lolote utaenda swali la 39.

**Swali la 38: Ni mwaka gani shamba lilipatikana?**

Uliza mwaka gani shamba lilipatikana, andika mwaka katika tarakimu 4. Kama shamba lilikuwa ni mali ya kaya toka/kabla mhojiwa hajazaliwa andika 1900.

**Swali la 38a Je kulikwa na mgogoro au kutolewana na mtu yoyote kuhusu shamba hili katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Uliza kama kaya imewahi kutolewana na watu wengine juu ya ardhi ambapo shamba lipo. Kutolewana kunaweza kutokana na; nani anamiliki ardhi, ukumbwa wa shamba, au mipaka ya kuzunguka shamba lilipo.

**Swali la 39 : Je, mnaweza kuliacha shamba hili bila kulilima kwa miezi kadhaa na msiwe na wasiwasi wa kulipoteza?**

Muulize mwanakaya kama wanaweza kuliacha shamba hilo bila kulima kwa miezi kadhaa na wasiwe na wasiwasi wa kulipoteza. Mara nyininge viongozi wa kijiji wanaweza kumpatia shamba mtu muhitaji zaidi. Kama shamba halitalimwa kwa kipindi fulani, uongozi wa kijiji unaweza kumpatia mtu mwingine. Pia mtu mwingine anaweza kulichukua na kusema ni miliki yake, kama litakaa kwa muda bila kulimwa.

**Swali la 40: JE KAYA HII ILILIMA SHAMBA HILI KATKA MSIMU WA MASIKI 2014?**

Haya ni maelekezo kwa Mdadisi. Kama ḋndiyoጀgeresho ḋløkama hapana geresho ḋøna nenda swali la 75.

## Matumizi ya Samadi

**Swali 41-46** yanahu su matumizi ya mbole aina ya samadi, samadi ni mbolea itokanayo na kinyesi cha wanyama. Maswali haya yaulizwe mara moja kwa kila shamba. Mara nyininge inawezekana kuna aina zaidi ya moja ya mazao yaliyolimwa katika shamba moja. Kwa hali hii toa jumla ya kiwango cha mbolea iliyoumika kwa mazao yote yaliyopo katika shamba. (Utaratibu huu utatumika pia kwa mbolea za viwandani,dawa za kuulia wadudu, dawa za kuulia majani n.k).

**Swali la 41: Je, mlitumia samadi [SHAMBA] katika msimu wa kilimo wa masika wa 2014?**

Muulize mhojiwa kama alitumia samadi katika [SHAMBA] katika msimu wa kilimo wa masika wa 2014 uliopita. Kama jibu ni ndiyo andika  $\frac{1}{4}$  kama ni hapana andika  $\frac{2}{3}$  kisha nenda Swali la 47.

**Swali la 42: Mlitumia kiasi gani cha samadi?**

Muulize mhojiwa kiasi cha samadi walichotumia. Andika katika uzito wa kilogramu.

**Swali la 43: Kuna kiasi chochote cha samadi mllichonunua?**

Inawezekana mkulima kutumia mbolea toka kwenye zizi lake, au toka kwa jirani pasipo kulipa chochote. Katika swali muulize mhojiwa kama alinunua mbolea andika  $\frac{1}{4}$  kisha endelea na swali linalofuata, vinginevyo andika  $\frac{2}{3}$  kisha nenda sw 47.

**Swali la 44: Kiasi gani cha samadi mlinunua?**

Muulize mhojiwa kiasi cha samadi walichonunua. Hakikisha unakibadilisha kipimo kuwa katika kilogramu.

**Swali la 45: Samadi mliyonunua ina thamani gani?**

Muulize thamani ya samadi hiyo aliyoinunua na uandike thamani katika shilingi. Kama malipo yalifanyika kwa kulipa kitu  $\frac{1}{4}$ - $\frac{1}{2}$  muombe mhojiwa athaminishe vitu hivyo katika pesa (shilingi).

**Swali la 46: wapi mlinunua/kupewa sehemu kubwa ya samadi?**

Uliza ni wapi walilinunua sehemu kubwa ya samadi, andika namba ya mtu au kampuni inayouza samadi kutoka kwenye orodha ya watoa huduma.

## Matumizi ya Mbolea ya Viwandani

Maswali ya 47 ó 53 yanahusu matumizi ya mbolea ya kiwandani, kama vile DAP, mbolea ya chumvi chumvi n.k. Swali la 54 ó 59 yanajirudia kwa aina nyingine ya mbolea ya kiwandani iliyotumika.

**Swali la 47/54: Je, mlitumia mbolea ya kiwandani katika shamba katika msimu wa kilimo wa masika 2014?**

Muulize mhojiwa kama walitumia mbolea ye yeyote ya viwandani katika [SHAMBA] katika msimu wa kilimo wa masika 2014. Katika swali la 54 uliza kama walitumia aina ya nyingine ya mbolea ya kiwandani zaidi ya ile iliyoorodheshwa swali la 47-53. Kama jibu ni ndiyo andika  $\frac{1}{4}$  kama ni hapana andika  $\frac{2}{3}$  kisha nenda Swali la 60.

**Swali la 48/55: Mbolea ya kwanza ya kiwandani kutumia katika shamba hili ilikuwa mbolea gani?**

Muulize mhojiwa ni aina gani ya mbolea ya kiwandani aliyoitumia katika shamba lake. Tumia mageresho katika dodoso hili. Kwa swali la 55 utauliza aina ya pili ya mbolea iliyotumika.

**Swali la 49/56: Mlitumia kiasi gani cha (MBOLEA)?**

Muulize mhojiwa kiasi gani cha mbolea kilichotumika. Andika kiasi katika kilogramu, **Angalizo:** badilisha vipimo vya kienyeji kwenda katika kilogramu.

**Swali la 50/57: Je, ulipokea vocha/cheti/hati kwa ajili ya aina yoyote ya (MBOLEA)?**

Serikali imeanzisha mpango maalumu kwa baadhi ya maeneo nchini kusaidia watu kulipia mbolea kwa vocha. Vocha hizi zaweza kuwa zinasambazwa na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika(MAFC) na zinaweza kukombolewa kutoka kwa mawakala waliopewa kibali. Swali hili lina lengo la kupima ni asilimia ngapi ya wakulima wanashiriki katika mpango huu.

**Swali la 51/58: Nini thamani ya mbolea ya kiwandani iliyonunuliwa?**

Muulize thamani ya mbolea ya kiwandani iliyonunuliwa. Kama mhojiwa alitumia vocha, jaza thamani ile aliyoitumia tu, sio thamani ya mbolea yote aliyopokea.

**Swali la 52: Kwanini uliamua kutumia aina hii ya mbolea?**

Mhojiwa akupe sababu ya kuchagua kutumia aina hiyo ya mbolea. Geresho  $\frac{1}{4}$  ni Ushauri wa kitaalamu kama vile ushauri alioupara kutoka kwa maafisa ugani, na kwa kupitia mpango maalumu kutoka kwa asasi zisizo za kiserikali au mpango mwingine wowote kama huu. Geresho  $\frac{2}{3}$  ni mhojiwa akijibu alichagua

kununua kwasababu alipokea vocha ya aina hiyo, geresho 3 kama alinunua kwa mazoea. Geresho 40 mhojiwa aliongea na jirani, rafiki au mkulima yoyote kwenye jamii yao. Kama aliamua kutumia kwa sababu ambayo haikuorodheshwa hapa tumia geresho 50 na andika sababu hiyo kwa maneno.

#### **Swali la 53/59: Ni wapi mulinunua/kupewa sehemu kubwa ya mbolea ya viwandani?**

Katika Maswali haya unatakiwa kuuliza ni wapi kaya imenunua mbolea orodhesha wapi amenunua kiasi kikubwa, tumia orodha ya watoa huduma kupata majibu.

#### **Swali la 59a: Je, mlitumia mbolea nyingine ya kiwandani zaidi ya hii?**

Swali hili linataka tu kufahamu kama kaya ilitumia aina zaidi ya mbili ya mbolea ya viwandani.

## **Madawa ya Wadudu/Magugu**

Swali 60 ó 65e yanahuus matumizi ya dawa za kuulia wadudu/magugu.

#### **Swali la 60: Je, ulitumia dawa ya kuulia magugu katika shamba katika msimu wa masika 2014?**

Muulize mhojiwa kama walitumia dawa ya magugu katika [SHAMBA] katika msimu wa kilimo wa masika 2014. Haya ni madawa ambayo yanatumika kuua wadudu au wanyama wadogo wadogo wanaoharibu mazao au mavuno. Na kuna dawa ambazio zinatumika kuua mimea mingine inayo haribu mazao. Iwapo jibu ni ndiyo jaza 1 kisha endelea swali linalifuata, kama ni hapana jaza 2 kisha nenda swali la 66.

#### **Swali la 62: Ni kiasi gani cha dawa kilichotumika?**

Muulize mhojiwa ni kiasi gani cha dawa kilichotumika. Kama mhojiwa ametumia dawa hiyo zaidi ya mara moja andika kiasi chote cha dawa aliyyotumia. Onyesha kiasi katika vipomo vilivyo onyeshwa katika dodoso.

#### **Swali la 63: Je, dawa za magugu mlizonunua zina thamani gani?**

Muulize mhojiwa akupe jumla ya thamani ya dawa ya magugu alizonunua. Ikiwa mhojiwa amenunua dawa zaidi ya mbili.

**Mfano:** Mkulima amenunua kilo 50 kwa Tsh 100,000 na ametumia kilo 10 msimu huu kwa shamba M1, na kilo 20 kwa shamba M2, andika Kilo 10 na kilo 20 katika swali la 62, ila andika bei ya 100,000 katika safumlalo ya shamba la M1 na 0 katika shamba la M2 kwa Swali la 63. Onyesha katika sanduku la maoni kwamba bei ya 100,000 ni gharama iliyyotumika kununulia dawa za magugu kwa shamba la M1 na M2.

#### **Swali la 64: Kwanini uliamua kutumia aina hii ya dawa?**

Andika geresho la sababu zilizopelekeea mhojiwa kutumia aina ya dawa kama alivyotaja. Angalia na jaza geresho husika kama ni USHAURI WA KITAALAMU, ALIPATA VOCHA, MAZOEA, USHAURI WA JIRANI N.K.

#### **Swali la 65: Mlinunua wapi/kupewa na nani sehemu kubwa ya dawa za magugu?**

Katika swali hili andika sehemu ambazo kaya imenunua dawa za kuua magugu. Tumia orodha ya watoa huduma kujibu swali hili.

#### **Swali la 65a-65e yanauliza kuhusu utumiaji wa dawa za wadudu katika mashamba ya kaya. Uhojaji wake unafanana kama maswali yaliyyotangulia yanayohusu utumiaji wa dawa za magugu.**

## **Pembejeo za Mkopo**

Maswali ya 66 ó 71 yanahuus pembejeo ambazo kaya zimepata kwa mkopo, sehemu hii inalenga kutaka kujua kuhusu upatikanaji wa mikopo kwa shughuli za kilimo. Mkopo unaweza kuwa ni wa fedha taslimu au vitu (kwa mfano mbegu, mbolea ya viwandani, samadi, madawa ya kuua wadudu au kitu chochote) kwa madhumuni ya uzalishaji. Mkopo unaweza kulipwa kwa fedha taslimu au kitokana na mazao yatakayovunwa.

**Chunguza:** Mhojiwa anaweza asifikiri kama pembejeo zinaweza kutolewa kwa mkopo. Kama amepokea pembejeo bila kulipa malipo yote, na anatarajia kumalizia malipo baada ya kuuza mazao, huu unaitwa mkopo wa pembejeo.

**Swali la 66: Umewahi kupokea mbegu, mbolea, madawa ya kuua wadudu ya (MASHAMBA) kwa mkopo, kwa ajili ya kulipa baadae katika msimu wa kilimo cha Masika cha 2014?**

Ni muhimu kumdadisi mhojiwa katika swali hili. Mhojiwa anaweza asifkilie pembejeo zinaweza kutolewa kwa mkopo. Hata hivyo kama amepokea pembejeo bila kulipa pesa kamaili lakini anatarajia kulipa baadae au kumuuzia mazao mtu aliye mpa pembejeo, hii ni inatambulika kama mkopo.

**Swali la 67: Ulipokea aina gani ya pembejeo kwa mkopo?**

Orodhesha aina ya pembejeo alizopokea kwa mkopo, dodosi zaidi mara baada ya kukutajia ile ya kwanza na aendelee kukutajia hadi ya nne. Aina ya pembejeo katika swali hili ni MBEGU, MBOLEA YA VIWANDANI, SAMADI na DAWA ZA KUUA WADUDU

**Swali la 68: Ulitanguliza kiasi gani cha malipo kwa ajili ya pembejeo hizo?**

Muulize mhojiwa alitanguliza kiasi gani cha malipo kwa ajili ya pembejeo. Jumuisha pembejeo zote katika swali la 67.

**Swali la 69: Ni kiasi gani cha fedha tasilimu ulimalizia/utamalizia kwa ajili ya pembejeo hizo?**

Muulize mhojiwa ni kiasi gani cha fedha tasilimu alimalizia kulipa kwa ajili ya pembejeo hizo alizozitaja katika swali namba 67. Asijumuushe malipo yasiyo ya pesa na vitu kwani yataulizwa katika swali linalofuata.

**Swali la 70: Ni malipo gani yasiyo pesa tasilimu uliyolipa baadaye kwa ajili ya pembejeo hizo?**

Muulize mhojiwa ni malipo gani yasiyo pesa tasilimu aliyolipa baadaye kwa ajili ya pembejeo hizo. Muulize idadi ya alicholipa na jaza geresho, kama mazao geresho ni 1, kama nguvu kazi geresho ni 2, shilingi 3, mengineyo 4.

**Swali la 71: Ulipata pembejeo hizo kwa mkopo kutoka kwa nani?**

Muulize mhojiwa ni nani aliymkopessa pembejeo hizo. Tumia Orodha ya watoa huduma kupata jibu la swali hili.

## Zana za Kilimo

**Swali la 71a: Je, ulitumia mashine (trekta, Power tiller, n.k.) yoyote katika shamba hili wakati wa msimu wa masika 2014?**

Muulize mhojiwa kama walitumia aina yoyote ya mashine za kulimia (trekta, power tiller) katika shamba. Weka geresho ḥōikiwa jibu ni ndio na geresho ḥōikiwa jibu ni hapana.

**Swali la 71b: Je umetumia wanyama kazi katika shamba hili kipindi cha masika 2014?**

Muulize mhojiwa ikiwa kaya ilitumia wanyama kazi kufanya kazi kwenye shamba. Mfano unaweza kuwa kutumia ngōmbe kwa ajili ya kulima ardhini au kupanda mbegu. Weka geresho ḥōikiwa jibu ni ndio na geresho ḥōikiwa jibu ni hapana.

## Ajira Na Kazi

Katika Sehemu hii jumuisha ajira na kazi katika mashamba. Utatumia namba za wanakaya ili kuainisha namba ya mwanakaya unaetoa taarifa zake

**Swali la 72: Katika msimu wa kilimo wa masika 2014, ni kwa siku ngapi [JINA] alifanya kazi zifuatazo katika shamba hili?**

Muulize mhojiwa katika msimu wa kilimo wa masika 2014, ni siku ngapi [JINA] alifanya kazi kama vile ūkusafisha shamba na kupandaō, ūkulalilia, kuweka matuta, kuweka mbolea, shughuli zisizo za mavuno na shughuli zisizo za kupandaō ūkuvuna na kukafua/kupukuchuaō. Andika namba yake kama ilivyo katika

dodoso la kaya katika safuwima husika, na onyesha ni kwa siku ngapi ametumia kwa kila shughuli iliyotolewa kwa kila shamba la kaya lililoorodheshwa. Kisha uliza kwa kawaida hutumia saa ngapi kwa siku kufanya kazi kwenye shamba husika.

**Mfano:** Kaya ya Mzee Juma mwanakaya namba 01 na mkewe Asha mwanakaya namba 02. Katika shamba lao la 1 (M1), Mzee Juma alifanya kazi wa siku 10 kusafisha shamba na siku 4 kupanda, siku 13 kupalilia, na siku 2 kuweka mbolea shambani. Mkewe Asha alifanya kazi siku 7 kusafisha shamba, siku 5 kupanda, siku 4 kupalilia, pia mjukuu wake Ali (ambaye anaishi nyumba nyingine) aliwasaidia kusafisha shamba kwa siku 14 na kupanda kwa siku 4, na siku 10 kwa kupalilia. Katika shamba lao la pili (M2), mkewe alitumia siku 5 kwa kusafisha shamba, siku 2 kwa kupanda na siku 3 kwa kupalilia. Ali alimsaidia bibi yake kupalilia, alifanya naye kazi ya kupalilia kwa siku 3.

**Angalizo:** mtu asiye mwanakaya alishughulika bila malipo kwenye shamba la kaya, (kwa mfano Ali anayeishi sehemu nyingine anasaidia Babu yake katika kazi za shamba), hali hii iijazwe katika swal la 74 kama ajira ya malipo. Iwapo kaya haikulipia ajira hii, jaza 40 kwenye safuwima za jumla ya gharama.

**Swali la 73: Je, uliajiri mtu ye yeyote kufanya kazi katika shamba hili katika msimu wa kilimo wa masika wa 2014?**

Muulize mhojiwa kama kaya iliajiri mtu ye yeyote kufanya kazi katika shamba kwa malipo katika msimu wa kilimo wa masika wa 2014. Taarifa hizi zitajumuisha mtu ye yeyote aliefanya kazi shambani ambaye si mwanakaya, hata kama hakulipwa.

**Swali la 74: Katika msimu wa masika wa 2014 ni kwa siku ngapi kaya iliajiri mtu katika shamba kwa ajili ya [.....]?**

Muulize mhojiwa katika msimu wa kilimo wa masika 2014, ni kwa siku ngapi kaya iliajiri mtu kufanya kazi katika shamba kwa shughuli tatu zilizoorodheshwa ökusafisha shamba na kupandaö, ökupalilia, kuweka matuta, kuweka mbolea, shughuli zisizo za mavuno na shughuli zisizo za kupandaö ökvuna na kukafua/kupukuchuaö. Taarifa hizi zimegawanyika katika vipengele, kama siku kwa mwanaume, siku kwa mwanamkwe, siku kwa mtoto, na jumla ya malipo yanayolipwa.

**Angalizo:**

*Mtu asiye mwanakaya aliyefanya kazi katika shamba la kaya bila malipo utajaza '0' kwenye safuwima za jumla ya gharama.*

*"Siku za mtu kufanya kazi" ni sawa na jumla ya watu waliofanya kazi zidisha siku walizofanya kazi.*

*Kwa mfano kwenye shamba langu la kwanza (M1) niliajiri watu 5 kwa ajili ya kusafisha shamba na kupalilia na kumlipa kila mmoja wao Sh 2000 kila siku. Kama niliajiri wanaume 2, wanawake 2 na mtoto 1 na Mwanaume A alifanya kazi kwa siku 3, Mwanaume B alifanya kazi kwa siku 2, Mwanamke C na mtoto wake wakafanya kazi kwa siku 7, na mwanamke D alifanya kwa siku 1. Hivyo taarifa zifuatazo zitatakiwa kujazwa. Mtoto hakulipwa. Katika shamba langu la pili watoto wa shangazi yangu walisafisha shamba na kupalilia. Watoto hao 6 ambao walifanya kazi kwa siku 4 kila mmoja kwa ajili ya kusafisha shamba, siku 4 kila mmoja kwa ajili ya kupanda, na siku 5 kwa ajili ya kupalilia. Hivyo hao ni watoto wa shangazi yangu, sintowalipa kwa kuwa wamesaidia katika shughuli za shamba.*

72

Katika msimu wa kilimo wa masika 2014, ni kwa siku ngapi [JINA] al

G E R E S H O	L A			Kupalilia, Matuta, kuweka mbolea,shughuli nyingine zisizo za kuvuna au kupanda		
S H A M B A	ID: <b>01</b>	ID: <b>02</b>	Idadi kamili ya masaa kwa siku miliyofanya kazi kwenye shamba hili.	ID: <b>01</b>	ID: <b>02</b>	Idadi kamili ya masaa kwa siku miliyofanya kazi kwenye shamba hili.
M1	<b>14</b>	<b>12</b>	<b>4</b>	<b>13</b>	<b>6</b>	<b>1.5</b>
M2	<b>0</b>	<b>7</b>	<b>4</b>	<b>0</b>	<b>3</b>	<b>2</b>

G E R E S H O	72. Katika msimu wa kilimo wa masika 2010, ni kwa siku ngapi kaya iliajiri mtu katika shamba kwa ajili ya [...]?							
	JUMUISHA PIA MALIPO KWA NJIA YA VITU				Kusafisha shamba na kupanda?			
Kupalilia								
	W/WAKE SIKU KAZI	W/MUME SIKU KAZI	WATOTO SIKU KAZI	JUMLA YA MALIPO (TSH)	W/WAKE SIKU KAZI	W/MUME SIKU KAZI	WATOTO SIKU KAZI	JUMLA YA MALIPO (TSH)
M1	5	8	7	26,000	0	0	0	0
M2	0	0	48	0	0	0	30	0

## Msimu wa Vuli (Sehemu 3A)

Maswali 75 hadi 84 sehemu 3A yapo tofauti na maswali ya sehemu 3B (swali 75 ó 78).

### Swali la 75: Je, MSIMU WA VULI ULIOPITA NI WA MWAKA GANI?

Swali hili ni maelekezo kwa mdadisi, kumbuka maandishi yenye herufi kubwa ni maelekezo kwa mdadisi. Tumia taarifa za swali la 11 sehemu ya 2.

### Swali la 76: Je, ulilima shamba hili katika msimu wa kilimo wa vuli 2013?

Muulize mhojiwa kama alilima shamba katika msimu wa kilimo wa vuli 2013. Fuata maswali ya mchujo kama yalivyo kwenye dodoso.

### Swali la 77: Zao gani kuu lililolimwa katika shamba hili katika msimu wa kilimo wa vuli 2013?

Swali hili linalenga kutaka kujua zao gani kuu lililolimwa katika shamba katika msimu wa kilimo wa vuli 2013. Inawezekana mkulima amelima mazao tofauti katika shamba, sasa unatakiwa kumuuliza ni zao gani lilichukua sehemu kubwa katika shamba. Kwa jibu lolote katika swali hili unatakiwa kwenda shamba lingine.

### Swali la 78: Je, ulilima shamba hili katika msimu wa vuli 2013?

Swali hili linataka kujua kama kaya ilimiliki shamba hili katika msimu wa vuli 2013. au walikuwa na ruhusa ya kulitumia tu.

### Swali la 79: Ulipataje shamba hili katika msimu wa masika 2014?

Swali hili limelenga kujua upatikanaji wa shamba hili katika msimu wa 2014. Zingatia mageresho kama yanavyoonekana kwenye dodoso. Kwa jibu lolote nenda shamba lingine.

### Swali la 80: Je, ultumiaje shamba hili katika msimu wa kilimo wa vuli 2013?

Muulize mhojiwa matumizi ya shamba lake katika msimu wa vuli 2013, kwa jibu lolote nenda shamba lingine.

### Swali la 81: Je, ulilima shamba hili katika msimu wa vuli 2014?

Hii inajumuisha miti ya matunda na mazao mengine ya kudumu, ambayo kaya inaweza kuwa ilivuna katika kipindi cha vuli.

**Swali la 82: Zao gani kuu lililolimwa katika shamba hili katika msimu wa vuli 2014?**

Katika swali hili uliza zao kuu lililolimwa na kaya katika shamba wakati wa msimu wa vuli 2014. Kama kuna mazao mengi katika shamba, muulize mhojiwa zao lilo muhimu au lililopandwa sehemu kubwa zaidi. Andika geresho la zao/mazao husika kama utakavyojibwa namhojiwa na kwa jibu lolote nenda shamba linalofuata.

**Swali la 83: Je, ulimiliki shamba hili katika msimu wa vuli wa 2014?**

Muulize mhojiwa kama shamba hili **alilimiliki** katika msimu wa vuli 2014, si lazima kaya iwe inamiliki shamba, labda inaruhusa kulitumia katika kipindi husika.

**Swali la 84: Kwanini hukumiliki au kulima shamba hili katika msimu wa vuli 2014?**

Andika geresho linalostahili halafu nenda mstari mwagine uliza shamba lingine.

## **Msimu wa Vuli (Sehemu 3B)**

Anza kwa kujaza ḋkijisehemuø cha mashamba (flap). Sehemu 3B inapaswa kuhusisha mashamba YOTE yaliyomilikiwa au yaliyolimwa na kaya, katika misimu yote ya vuli na masika. Sehemu kubwa ya sehemu ya 3B inafanana na sehemu ya 3A, hata hivyo mwanzo na mwisho unatofautiana.

**Swali la 1b: MDADISI: UMESHAORODHESHA SHAMBA HILI KATIKA SEHEMU YA 3A?** Kumbuka, UTARUDIA mashamba ya sehemu ya 3A hapa kwenye sehemu ya 3B. Unapaswa kujibu ḋndiyoø kama shamba tayari lilishaorodheshwa katika sehemu ya 3A. Katika mazingira haya, utaruka nusu ya sehemu hii ya 3B, hadi swali la 40. Kama hapana endelea maswali yanayofuata.

**ANGALIZO:** **Maswali ya 2-39** katika sehemu 3B yanahusiana na mashamba kwa ujumla. Hata hivyo, **maswali ya 39-74** yanahusiana na msimu wa vuli. Inawezekana, kwa mfano, kwamba kaya imetumia mbolea za viwandani katika shamba kwenye msimu wa masika lakini si katika msimu wa vuli. Hivyo, maswali haya yanajirudia katika msimu wa masika na vuli kwa mashamba kwa mashamba yaleyale.

**Swali la 75: MDADISI: UMESHAORODHESHA SHAMBA HILI KATIKA SEHEMU YA 3A SWALI LA 1?**

Swali hili linarudia swali la 1b. Utajibu ḋNdiyoø kama shamba tayari lilishaorodheshwa katika sehemu ya 3A. Katika mazingira haya, utaenda shamba linalofuatia. Kama hapana emdelea na maswali yanayofuata.

**Swali la 76: MSIMU WA VULI ULIOPITA ULIKUWA MWAKA GANI?**

Rejea taarifa zinazotoka kwenye swali la 11 katika Sehemu ya 2.

**Swali la 77: Kwanini hukumiliki au kulima shamba hili katika msimu wa masika 2014?**

Mhojiwa ataulizwa swali hili pale ambapo shamba lilimilikiwa au kulimwa katika msimu wa vuli wa 2013 lakini HALIKUMILIKIWA/KULIMWA katika msimu wa masika wa 2014. Hii inapaswa kutokea mara chache. Andika maelezo ya hali hii, kwa kutumia majibu yaliyoorodheshwa. Labda shamba liliuzwa baada ya msimu wa vuli wa 2013 kwa hiyo halikumilikiwa wakati wa msimu wa masika wa 2014, n.k.

**Swali la 78: Je, ulipataje shamba hili katika msimu wa vuli 2014?**

Mhojiwa ataulizwa swali hili kama shamba lilimilikiwa au kulimwa katika msimu wa vuli wa 2014, lakini HALIKUMILIKIWA AU KULIMWA katika msimu wa masika wa 2014. Hii pia itatokea mara chache sana. Waulize ni namna gani walilipata shamba kwa kilimo cha msimu wa vuli wakati hawakuwa nalo katika msimu wa masika.

# Sehemu 4. Mazao Katika Shamba

Katika sehemu ya 3, mstari mmoja uliwakilisha shamba moja. Sehemu ya 4 mstari mmoja utawakilisha zao husika katika shamba husika. Ikiwa kaya imepanda mazao mchanganyiko katika shamba hilohilo, wanapaswa waorodheshe mazao yote. (kwa mfano, mahindi na maharage katika shamba moja yatakuwa katika mistari tofauti). Ikiwa kaya imepanda zao la aina moja katika mashamba tofauti (kwa mfano, mihogo katika mashamba mawili) haya yanapaswa kuwa katika mistari tofauti.

**KUMBUKA:** Sehemu 4 inahusu mazao ya mwaka. Usiorodheshe: matunda, miti, mihogo, au zao lolote la kudumu.

**Anza kujaza katika kijishemu maalumu kilicho kushoto “Flap”.** Tumia ōflapö kuhakikisha unazingatia mchanganyiko wa zao shambani kwa kila mstari.

**Sehemu ya 4a, orodhesha mazao yote yaliyolimwa katika msimu wa masika 2014.** Hii inajumuisha mazao yote yaliyoorodheshwa katika sehemu 2A na/au 3A. Kwa kila shamba, orodhesha mazao yote yaliyolimwa katika msimu wa masika katika mstari tofauti.


**Sehemu ya 4a, orodhesha mazao yote yaliyolimwa katika msimu husika wa vuli.** Hii inajumuisha mazao yote yaliyoorodheshwa katika sehemu 2B na mazao yote uliyosema ōndioö kwenye swalii la 40 katika sehemu 3B. Kwa kila shamba, orodhesha mazao yote yaliyoorodheshwa katika vuli kwenye mstari tofauti.

**Jaza karatasi ya kukunja (Flap)** kwa usahihi ili kuhakikisha unajaza taarifa sahihi kwa shamba sahihi.

**Safuwima ya 1:** Orodhesha mashamba yote na mageresho yake yanayohusika, angalia sehemu ya jedwali A na B.


**Safuwima ya 2:** Orodhesha mazao yote yaliyolimwa wakati wa msimu wa mwisho wa vuli/masika.

**Shamba la 1**



Pure Stand Crop Planted Half Maize and Half Beans

**Shamba la 2**



Intercropped Maize and Beans

## Swali la 1: Je, zao hili lilipandwa katika eneo lote la shamba?

Katika swali hili muulize mhojiwa kama zao lilipandwa katika eneo lote la shamba, au ni sehemu tu ya shamba. Angalia mfano hapo juu, shamba 1 mahindi na maharage halijapandwa eneo lote la shamba, mahindi sehemu yake na maharage sehemu yake. Shamba 2 yote mahindi na maharage yamepandwa shamba zima. Ikiwa jibu ni NDIYO geresho -10kisha nenda swali la 4. kama HAPANA geresho ni -20%

## Swali la 2: Ni sehemu gani ya shamba iliyopandwa [ZAO]?

Uliza ni sehemu gani ya shamba iliyopandwa (zao). Kwenye mfano hapo juu shamba la kwanza, mahindi yangepandwa 50% na maharage 50%.

### **Swali la 3: Nini sababu ya kutopanda eneo lote la shamba?**

Kuna sababu nyingi kwanini kaya haikupanda eneo lote la shamba. Katika mfano hapo juu sababu inaweza kuwa geresho  $\frac{1}{10}$  diligawanywa $\varnothing$  shamba liligawanya katika sehemu ya maharage na mahindi, sababu nyingine inaweza kuwa ukame, upungufu wa zana n.k. Chagua sababu iliyosahihi na andika geresho husika.

### **Swali la 4: Je, Mlilima mazao mchanganyiko katika shamba?**

Mazao mchanganyiko, inamaanisha kulima aina tofauti ya mazao katika eneo moja. Mfano hapo juu shamba la kwanza haikuchanganywa mazao, shamba la pili lilichanganywa. Kama jibu ni ndiyo andika  $\frac{1}{10}$  na kama jibu ni Hapana andika  $\frac{2}{10}$  nenda swali la 6.

### **Swali la 5 Je, nini sababu ya kuchanganya mazao?**

Wanakaya wanasababu tofauti za kuchanganya mazao. Tumia mageresho kwenye swali kujaza sababu sahihi.

## **Mbegu**

### **Swali la 6: Ni mbegu ya aina gani ya [ZAO] lililolimwa kwenye shamaba hili?**

Muulize mhojiwa kuhusu aina kuu za mbegu zilizopandwa shambani. Mbegu kuu ni ile ambayo kaya ilipandwa kwa kiasi kikubwa shambani. Kama kaya imechanganya mbegu mbalimbali, mbegu kuu itakuwa ni ile iliyokuwa nyingi kwenye mchanganyiko huo (wakati wa kuchanganya).

### **Swali la 8: Je, mbegu hizi:?**

Hapa nia ni kufahamu kama mbegu hizi ni ziliboreshw, za asili, ziliboreshw zikatumika tena au kama kuna aina nyingine yeyote itaje.

### **Swali la 10: Ni mbegu kiasi gani zilitumika?**

Andika kiasi cha mbegu kilichotumika katika safu wima ya kwanza na ya pili jaza idadi. Tazama mageresho kama yanavyolekeza, kama aina atakayotaja haipo kwenye mageresho, jaza geresho 5 na uiandike kwa maneno. Na kwakuwa ujazo wa vikapu unatofautiana jaribu kuhoji zaidi ili uweze kukadiria katika kilogram.

### **Swali la 10a: Ni kiasi gani cha mbegu kilichotumika kilitunzwa toka msimu uliopita?**

Andika jumla ya kiasi cha mbegu kilichotumika shambani ambacho kilitunzwa kutoka msimu uliopita. Andika kiasi katika safuwima ya kwanza na kipimo katika safuwima ya pili. Kwa kipimo, kikombe kidogo kinatakiwa kuwa na ujazo kati ya ml 250 na kikombe kikubwa kuwa na ujazo wa ml 500. Kama kipimo hakipo katika orodha ya mageresho, weka 5 na andika aina ya kipimo kwa maneno. Kwa sababu ukubwa wa bidhaa unatofautiana sana, kama muhojiwa atataja bidhaa kama kipimo, dadisi zaidi kujaribu kupata makadirio ya muhojiwa katika kilogramu. Kama mwanakaya hakutumia mbegu zilizotunzwa kutoka msimu uliopita andika 0 kisha nenda 10C.

### **Swali la 10b: Ni aina gani ya mbegu za zilitumika msimu uliopita?**

Kama kaya ilitumia mbegu zilizotunzwa toka msimu uliopita, hapo dadisi ni aina gani ya mbegu iliyotumika.

### **Swali la 10c: Ni kiasi gani cha mbegu kilichonunuliwa (au kupewa)?**

Andika jumla ya kiasi cha mbegu kilichonunuliwa ambacho kaya ilitumia. Andika kiasi katika safuwima ya kwanza na kipimo katika safuwima ya pili. Kwa kipimo, kikombe kidogo kinatakiwa kuwa kati ya ujazo wa ml 250 na kikombe kikubwa kati ya ujazo wa ml 500. Kama kipimo hakipo katika orodha ya mageresho andika 5 na andika kipimo kwa maneno. Kwa kuwa ukubwa wa bidhaa unatofautiana sana, kama muhojiwa atataja bidhaa kama kipimo, dadisi Zaidi kujaribu kupata makadirio ya muhojiwa katika kilogramu. Kama mwanakaya hakununua mbegu andika  $\frac{1}{10}$

### **Swali la 12: Kiasi gani kililipwa kwa ajili ya mbegu?**

Kama mhojiwa alitumia vocha andika kiasi alicholipia tu na sio gharama ya mbegu kwa ujumla. Hapa tunahitaji gharama yote kwa ujumla aliyotumia kwa ajili ya mbegu.

### **Swali la 13: Mmenunua wapi sehemu kubwa ya mbegu?**

Mhojiwa ataje watoa hoduma ambao walimuuzia/kumpa mbegu, tumia orodha ya watoa huduma/(network roster ID), kama mbegu zilinunuliwa sehemu moja na mbolea hakikisha network rosta/orodha ya watoa huduma inafanana na ile ya sehemu ya 3 kwenye maswali ya mbolea.

### **Swali la 13a: Je, ulipokea vocha/hati kwa ajili ya aina yoyote ya (mbegu)?**

Serikali inaendesha mfumo wa malipo kwa vocha katika baadhi ya maeneo nchini ili kusaidia watu kulipia mbegu za mahindi na mpunga. Vocha hizi zitasambazwa na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na mawakala wengine wa kilimo watakaopewa kibali. Swali hili linalenga kupima asilimia ya watu wanaotumia mfumo huu.

## **Upotevu kabla ya Mavuno / Hasara**

### **Swali la 17: Je, kuna upotevu wowote wa mazao yakiwa bado shambani?**

Upotevu inamaanisha mazao yoyote yaliyoharibiwa na magonjwa, wanyama n.k. kabla ya kuvunwa.

### **Swali la 18: Ni aina gani ya upotevu?**

Muulize Mhojiwa sababu hasa za upotevu huo ni nini. Mara nyingi waweza kutokana na Wadudu, Wanyama n.k, hivyo mhojiwa ataje mwenyewe.

## **Mavuno**

### **Swali la 19: Je, [ZAO] lolote liliunwa?**

Swali hili linauliza kama kuna zao lolote liliunwa katika kipindi cha masika 2014, andika ndiyo hata kama zao liliharibiwa baada ya kuvunwa.

### **Swali la 20: Kwanini [ZAO] halikuvunwa?**

Swali hili linauliza kwa nini kaya haikuvuna zao shambani.

-halikuwa languø itakuwa ni sababu nzuri ,kama zao liliopandwa halimilikiwi na kaya na hivyo haliwezi kuvunwa na wanakaya. -Bado lipo shambaniø hili pia ni jibu ikiwa zao bado lipo shambani halijawa tayari kwa kuvunwa. Kwa jibu lolote nenda zao linalofuata.

### **Swali la 21: Eneo lipi liliuvunwa msimu wa masika 2014**

Uliza eneo (ekari) la shamba liliuvunwa msimu wa masika 2014. Angalia eneo hili lisiwe kubwa kuliko jumla ya eneo la shamba lilioorodheshwa katika sehemu ya 2.

### **Swali la 22: Je, eneo liliuvunwa ni dogo kuliko liliopandwa?**

Kama kaya imepata upotevu wa mazao shambani, eneo itakalovunwa litakuwa dogo kulinganishwa na eneo liliopandwa.

### **Swali la 23: Sababu za eneo liliuvunwa kuwa dogo kuliko liliopandwa?**

Nini sababu ya eneo liliuvunwa kuwa dogo kuliko liliopandwa? Tumia geresho husika kujaza sababu sahihi.

### **Swali la 24: Taja miezi ya kuanza na kumaliza kipindi cha kuvuna.**

Andika mwezi wa kuanza na kumaliza kuvuna, iwapo hajamaliza kuvuna andika 0 kwenye sehemu ya kumaliza. **Kumbuka:** hii haimaanishi kuanza na kumalizika kwa msimu [kupanda mpaka kuvuna]. Inamaanisha tu wakati kaya ilianza kuvuna na wakati ilimaliza kuvuna.

**Swali la 25 : Mmemaliza kuvuna?**

Hata kama mwanakaya yuko katika harakati za kuvuna, haitahesabika kuwa amemaliza, hadi mazao yote katika shamba yamalizwe kuvunwa, kumbuka hii imetenganishwa na mazao na shamba, kama shamba la mahindi limemalizwa kuvunwa itahesabika shamba hilo limeisha kuvunwa, na sehemu nyingine bado.

**Swali la 26 : Zimebaki siku ngapi mkamilishe kuvuna?**

Swali hili liulizwe kwa zao mojamoja na shamba mojamoja. Mfano, zimebaki siku ngapi mmalize kuvuna shamba la mahindi la nyumbani?

**Swali la 27 : Sehemu gani ya mazao imebaki kuvunwa?**

Muulize mhojiwa kujua ni asilimia ngapi iliyobaki, na onyesha asilimia hii kwa tarakimu mbili.

**Swali la 28 : Kiasi gani kimeshavunwa?**

Swali hili linauliza ni kiasi gani kilichovunwa kwa kila zao katika shamba husika, ni vema kama kipimo kitakuwa katika kilogram. Hii inamaanisha kwamba ni lazima ubadili vipimo vya kienyeji katika kilogram.

**Swali la 29: Thamani ya mavuno?**

Muulize mhojiwa bei ya mazao sokoni wakati wa kipindi cha mavuno. Wanapaswa kujibu swali hili hata kama hawakuuza zao lolote. Waulize wakadilie bei ya zao katika muda wa mavuno.

**Swali la 30: Nani kwenye kaya hufanya maamuzi ya matumizi ya mazao yaliyovunwa?**

Orodhesha utambulisho wa mwanakaya kutoka katika roaster ambaye huwa anafanya maamuzi ya matumizi ya mazao yalivunwa katika shamba. Orozesha hadi wanakaya wawili waliota maamuzi.

## Sehemu 5: Jumla ya Mauzo na Hifadhi ya Mazao katika Kaya

Sehemu ya 5A inahu mazao yaliyolimwa msimu wa masika na sehemu ya 5B inahu mazao yaliyolimwa msimu wa vuli. Mazao yote yaliyoorodheshwa katika sehemu nyingine zilizopita yanatakiwa kuonekana katika sehemu hii. Mazao ambayo hayataonekana au kuorodheshwa katika sehemu zilizotangulia hayataonekana katika sehemu hii. Hii itathibitishwa na program ya kuingiza data na marudio lazima yafanywe kwenye tukio ambako halikufanyika vizuri.

### MAUZO

**Swali la 1: Je, uliuza [ZAO] lililovunwa 2014?**

Je uliuza (ZAO) lolote lililozalishwa katika msimu wa mvua wa masika 2014? Onyesha ikiwa Mhojiwa aliuza (ZAO) lolote lililozalishwa katika msimu wa mvua wa masika 2014. Ikiwa jibu ni ndio, weka geresho 1 na endelea na swali linalofuata. Ikiwa hapana, weka geresho 2 na nenda Swali la 23.

**Swali la 2: Ni uzito gani uliuzwa?**

Andika kiasi cha [ZAO] kilichouzwa katika kipimo cha kilo. Ikiwa mhojiwa atakupa vipimo vya kienyeji, badili kipimo hicho kuwa katika kilo. Ibadilishwe kuwa kilogramu kabla ya kwenda EA nyingine. Uhakikishe kwamba kiasi kilichouzwa kwa kila zao hakizidi kiasi kilichovunwa kwenye mashamba yote. Hakikisha kwamba kiasi kilichouzwa hakizidi kiasi kilichovunwa .

**Swali la 3: Mauzo yote yalikuwa na thamani gani?**

Andika kiasi cha fedha kilichopatikana baada ya mauzo katika shilingi.

**Swali la 4: Je, ni mtu gani au Taasisi ipi uliuzia zaidi [MAZAO] yako?**

Muulize mhojiwa mahali alipouzia sehemu kubwa ya mazao, kwa kufuatana umuhimu wa zao. Andika wanunuzi au watoa huduma. Orodha ya watoa huduma inapatikana katika ukurasa wa mwisho wa dodoso. Kumbuka kwamba huyu sio lazima sikuzote awe mteja wa kujitegemea, isipokuwa inaweza kuwa sehemu, kama vile soko la kienyeji katika kipindi cha kuzalisha (kama vile nyanya, vitunguu, n.k).

**ANGALIZO:** *Angalia wanunuzi ambao wamenunua kiasi kukubwa zaidi, hata kama ni zaidi ya mnunuzi mmoja chagua wawili tu. Hii ni kwa swali la 4 na 11.*

**Maswali ya 5-10 yanauliza kuhusu mauzo kwa mnunuzi #1.**

**Swali la 5: Ni kiasi gani cha [ZAO] ulichouza kwa [MNUNUZI #1]?**

Muulize mhojiwa ni kiasi gani cha mazao alichouza kwa mnunuzi wa kwanza, na kisha andika mnunuzi mwingine anayefuata kwa kununua kiasi kikubwa. Andika kiasi hicho kwa kipimo cha kilo.

**Swali la 6: Mauzo yalikuwa na thamani gani?**

Andika jumla ya thamani ya mauzo hayo (bei iliyolipwa na mnunuzi #1) katika shilingi ya Tanzania.

**Swali la 7: Katika mwezi gani uliuza kiasi kikubwa cha (ZAO) kwa (MNUNUZI #1)?**

Muulize muhojiwa ni mwezi gani mauzo yalikuwa mengi zaidi . Hii inaweza kuwa rahisi (kama vile kwa zao ambalo linauzwa lote kwa mara moja), au kuwa ngumu (kama vile kwa nyanya ambazo zinauzwa mara nyingi katika mwaka mzima). Lazima udodose ili upate taarifa nzuri kutoka kwa mhojiwa.

**Swali la 8: Kwa kukadiria, ni mara ngapi mauzo yalifanyika wakati wa kuuza(ZAO) kwa (MNUNUZI #1)?**

Kwa kukadiria ni mara ngapi mauzo yalifanyika wakati wa kuuza (ZAO) kwa (MNUNUZI # 1)? Swali hili linauliza ni mara ngapi zao liliuzwa kwa mnunuzi. Ikiwa zao liliuzwa lote kwa mara moja, jaza 1. Ikiwa ni mara nyingi, unatakiwa ujitatihidi kutafuta makadilio mazuri ikiwezekana. Kwa mfano, ikiwa mavuno yalikuwa siku 40 zilizopita, na mhojiwa aliuza maharage sokoni kila siku toka siku hiyo katika wastani wa watu watatu kwa siku, makadirio mazuri yatakuwa ni 120.

**Swali la 9: Nani katika kaya mwenye jukumu la kujadili mauzo ya [ZAO] kwa [MNUNUZI #1]?**

Nani katika kaya yako alifanya maamuzi ya kujadili uuzaaji wa zao kwa mnunuzi. Swali hili linamuuliza mhojiwa ni nani katika kaya anafanya maamuzi yanayohusiana na mauzo ya zao. Unatakiwa kutumia mageresho yaliyoorodheshwa katika roster ya kaya. Andika wanakaya waliohusika zaidi na maamuzi ya mauzo.

**Swali la 10: Nani katika kaya yako aliamua matumizi ya mapato haya?**

Uliza ni nani katika kaya yako aliamua matumizi ya mapato yaliyopatikana baada ya kuuza mazao. Baadhi ya kaya maamuzi hufanywa kwa kushirikiana mume na mke kama ni hivyo jaza (01 na 02) na kaya zingine utakuta ni mkuu wa kaya tu 01, au mwenza 02 pekeyake ndo anafanya maamuzi. Andika namba za waliofanya maamuzi kwa kutumia orodha ya wanakaya, andika wanakaya hadi wawili waliofanya maamuzi.

**Swali la 11: Kwa mtu yupi au Taasisi ipi ulimuuzia/uliuzia [ZAO] la pili?**

Muulize muhojiwa akutajie wateja walionunua zao la pili, tumia orodha ya watoa huduma ñetwork rosterø Kumbuka kwamba huyu sio lazima siku zote awe mteja wa kujitegemea, isipokuwa inaweza kuwa sehemu, kama vile soko la kienyeji katika kipindi cha kuzalisha (kama vile nyanya, vitunguu, n.k). Kama kaya iliuza mazao yote kwa mtu mmoja, jaza 99 na nenda swali la 18.

**Maswali ya 12-17 yanafanana na maswali ya 5-10 lakini yanauliza kuhusu mnunuzi # 2. Rejea kwenye maalekezo ya swali 5-10 kwa maelezo zaidi jinsi ya kujaza maswali haya.**

## **USAIRI**

### **Swali la 18: Ulisafirisha [ZAO] kwa ajili ya kuuza?**

Muulize mhojiwa kama alisafirisha [ZAO] kwa madhumuni ya kuuza. Usafilishaji unaweza kuwa kwa kutembea, kwa baiskeli, n.k. Orodha kamili inapatikana Swali la 21.

### **Swali la 19: Ulisafirisha [ZAO] kwa wastani wa umbali gani kwa ajili ya kuuza?**

Muulize mhojiwa ni umbali gani alisafirisha mazao kwa ajili ya kuuza. Andika umbali katika kilometa. Ikiwa mhojiwa atakupa jina la sehemu, muulize akupe umbali wa sehemu hiyo katika kilometa.

### **Swali la 20: Ni mara ngapi umesafirisha (ZAO) kwa ajili ya kuuza msimu wa masika 2014?**

Muulize Mhojiwa ni mara ngapi alisafirisha mazao yake kwenda sokoni. Jibu hili linaweza kuwa sawa au kutofautiana na idadi ya mara ambazo mauzo yalifanyika kama inavyoonekana katika Swali la 8 na 15. Hali hii inaweza kutokea ikiwa mhojiwa alisafirisha mazao lakini hakuza kwa sababu yejote ile.

### **Swali la 21: Umesafirishaje [ZAO]?**

Muulize Mhojiwa namna alivyosafirisha mazao kwenda sokoni. Ikiwa wanatumia njia zaidi ya moja, dodosi ujue ni njia ipi ni muhimu zaidi. Tumia mageresho yaliyoorodheshwa katika dodoso. Ikiwa Mhojiwa atatoa njia ambayo haipo kwenye dodoso, weka 5 öNYINGINEö na andika hiyo njia kwa maneno.

### **Swali la 22: Ni kiasi gani ulilipa kusafirisha [ZAO] msimu wa masika 2014?**

Muulize mhojiwa kiasi cha fedha (Tshs) ambacho alitumia kwa kusafirisha mazao katika msimu wa masika 2012. Kama walisafirisha mazao zaidi ya mara moja, akutajie fedha iliyolipwa kwa safari zote.

## **UHIFADHI NA MAVUNO**

### **Swali la 23: Je, kuna mazao yoyote ya msimu wa masika 2014 ya shamba hili ghalani sasa?**

Muulize mhojiwa kama kuna mazao yoyote ghalani ama nyumbani au mahali pengine alipohifadhi. Kama jibu ni ndio jaza geresho1 kisha endelea na swali linalofuata, ikiwa jibu ni hapana andika geresho 2 kisha nenda swali la 29.

### **Swali la 24: Ni kiasi gani cha mavuno mmehifadhi?**

Muulize mhojiwa kiasi cha mavuno alichokihifadhi ghalani kwa muda huu. Andika uzito kwa kipimo cha kilo na siyo kipimo cha kienyeji. Kiasi hiki kisizidi kiasi kilichovunwa.

### **Swali la 25: Njia gani kuu unayotumia kwa kuhifadhi mazao?**

Muulize mhojiwa njia kuu anayotumia katika kuhifadhi mazao. Angalia mageresho yaliyoorodheshwa kwenye dodoso. Ikiwa imetumika njia zaidi ya moja ya kuhifadhi mazao, uliza ni njia ipi ilitumika zaidi kuliko nyingine. Ikiwa mhojiwa atakutajia njia ambayo haipo katika orodha ya mageresho, jaza geresho 8 öNYINGINEö kisha andika njia hiyo kwa maneno.

### **Swali la 26: Je, mlifanya chochote kulinda mavuno ghalani dhidi ya uharibifu?**

Swali hili linauliza kama mhojiwa alichukua hatua yoyote ya kuzuia mazao yasioze au kuliwa na wadudu.

**Swali la 27: Mlifanya nini?**

Andika njia ambayo mhojiwa alitumia katika kulinda mazao ili yasiliwe na wadudu. Tumia mageresho yaliyoorodheshwa kwenye dodoso. Ikiwa mhojiwa atakutajia njia ambayo haipo kwenye orodha ya mageresho, jaza geresho 3 -~~NYINGINE~~ kisha andika jina la njia hiyo kwa maneno.

**Swali la 28: Je, unapohifadhi [ZAO] nini makusudio ya uhifadhi huo?**

Muulize mhojiwa sababu kuu ya kuhifadhi zao lililoorodheshwa kwenye dodoso. Endapo mhojiwa atakutajia sababu ambayo haipo katika orodha ya mageresho, jaza geresho 4 -~~NYINGINE~~ kisha andika sababu hiyo kwa maneno.

## UPOTEVU/HASARA

**Swali la 29: Je, kuna mavuno yoyote yaliyopotea baada ya kuvuna kutokana na kuoza, wadudu, panya, n.k?**

Wakati mwingine sehemu fulani ya mazao inaweza kupotea baada ya mavuno na kabla ya kuuza mazao, kama vile kuoza, kuliwa na wadudu au panya au kuibwa. Swali hili halitajumuisha hasara iliyopatikana kabla ya kuvuna mazao. Kama vile, kuliwa na wadudu au ndege yakiwa bado shambani. Endapo mhojiwa atakuwa amepata hasara ya namna hii jaza geresho 1 kisha endelea na swali linalofuata.

**Swali la 30: Sababu kuu ya kupotea.**

Muulize mhojiwa sababu kuu ya kupotea kwa mavuno hayo. Endapo atakutajia sababu zaidi ya moja uliza zaidi ili upate sababu ambayo ni kuu au muhimu kuliko nyingine. Angalia geresho linalotakiwa kujazwa. Ikiwa muhojiwa atakutajia sababu ambayo haikuorodheshwa katika mageresho yaliyopo kwenye dodoso, jaza geresho 5 -~~NYINGINE~~ kisha andika sababu hiyo kwa maneno.

**Swali la 31: Ni sehemu gani ya kumi ya mavuno yaliyopotea?**

Sehemu hii ya kumi ya mavuno yaliyopotea itakuwa kati ya namba 1 na 10. Kwa mfano, kama mkulima amepoteza mahindi 5 kati ya 10 (au 50%) yaliyoliwa na ndege kabla ya kuuza, hivyo jibu litakuwa ni 5. ikiwa mkulima amepoteza mahindi 3 kati ya 10 (au 30%), jibu litakuwa ni 3. ikiwa mhojiwa atkupa asilimia ambayo siyo rahisi kuitambua/kuitafasiri, mfano 25%, ikaribishe namba hiyo kwa namba nzima iliyo karibu (ambayo ni 3) na kuandika jibu.

**Swali la 32: Mavuno yaliyopotea yana thamani gani?**

Uliza thamani ya mavuno yaliyopotea katika shilingi ya ki-tanzania. Mhojiwa anaweza kukadiria endapo hatakuwa na uhakika na thamani ya mavuno yaliyopotea.

**Maswali ya (32a-32e), ikiwa mhojiwa atatoa taarifa za kiasi kwa vipimo vya kienyeji kama ndoo au begi, muulize mhojiwa akadirie kiasi katika kilogramu.****Swali la 32a: Ni kiasi gani cha mavuno kimetumika kwenye kaya?**

Uliza kiasi cha mazao yaliyovunwa ambayo yalitumiwa na kaya. Andika kiasi katika kilogramu.

**Swali la 32b: Ni kiasi gani cha mavuno kimehifadhiwa kama mbegu wakati wa msimu ujao wa kupanda?**

Uliza kiasi cha mazao yaliyovunwa ambayo kaya ilihifadhi kama mbegu ili zije kutumika katika msimu ujao wa kupanda. Andika kiasi katika kilogramu. Ikiwa kulikuwa hakuna, weka geresho -0.Ø

**Swali la 32c: Ni kiasi gani cha mavuno kimetumika kama malipo kwa vibarua?**

Uliza kiasi cha mazao yaliyovunwa ambayo kaya ilitumia kama malipo kwa vitu kama kibarua au kodi. Andika kiasi katika kilogramu. Ikiwa hakuna mavuno yaliyotumika kama malipo, hapo weka 0.

**Swali la 32d: Ni kiasi gani cha mavuno umetoa kama zawadi?**

Uliza kiasi cha mazao yaliyovunwa ambayo kaya imetoa kama zawadi kwa watu walio nje ya kaya. Andika kiasi katika kilogramu. Ikiwa hakuna mavuno yaliyotolewa kama zawadi, hapo weka -0ø

**Swali la 32e: kiasi gani cha mavuno kimetumika kulishia mifugo?**

Uliza kiasi cha mazao yaliyovunwa ambayo kaya ilitumia kulishia mifugo ya kaya. Andika kiasi katika kilogramu. Ikiwa hakuna mavuno yaliyotumika kulishia mifugo, hapo andika -0ø Ikiwa kaya haimiliki mifugo,pia andika -0ø

**KUMBUKA:** Jumla ya kiasi kitakachoandikwa katika maswali haya matano (32a-32b) kamwe hayatazidi jumla ya kiasi cha mavuno kilichtolewa katika sehemu ya 4 ya mazao, swali la 28.

**MABAKI YA ZAO**

Mabaki ni yale masalia ya mazao yaliyobaki shambani baada ya kuvuna mazao haya ni kama mabua, maganda ya mbegu n.k.

**Swali la 33: Nini kilifanyika kwa makapi/mabaki yalitokana na zao hili?**

Swali hili linauliza nini kilifanyika kutokana na makapi/mabaki baada ya zao kuvunwa. Tumia mageresho yaliyopo kwenye dodoso, orodhesha hadi mawili. Kumbuka geresho la -4ø na -6ø yanatofautiana: geresho la -4ø chakula cha mifugo kwa kuchungia shambani, na geresho -6ø malisho ya mifugo yake kwa kutoa shambani na kuwalishia nyumbani au sehemu yejote ya malisho.

**Swali la 34: Ni kiasi gani kiliuzwa?**

Andika kiasi kilichouzwa katika kilogramu- badilisha kutoka vipimo vyta kienyeji ikiwa inawezekana.

**Swali la 35: Nini jumla ya mauzo?**

Andika thamani yake katika shilingi. Ikiwa kulikuwa na mauzo mengi, andika kiasi chake kwa jumla.

**Swali la 36: Ni nani, asasi au taasisi gani uliuzia makapi yaliyotokana na (ZAO) hili?**

Tumia orodha ya watoa huduma, orodhesha wanunuza wawili kufuatana na umuhimu.

**SEHEMU 5B MASWALI YANAJIRUDIA KWA YALIYOUЛИZWA SEHEMU 5A KWA MAZAO YALIYOLIMWA MSIMU WA VULI.**

## **Sehemu 6. Mazao ya Kudumu & Miti ya Matunda katika Shamba**

---

Sehemu ya 6 inafanana na sehemu ya 4. Mstari mmoja unawakilisha zao husika katika shamba husika. Ikiwa kaya inapanda mazao mchanganyiko ya kudumu katika shamba moja, yanapaswa kuorodheshwa peke yake. Ikiwa kaya inapanda mazao ya kudumu yanayofanana katika mashamba tofauti (kwa mfano, mihogo katika mashamba mawili) yanapaswa kuwa katika mistari tofauti.

Tafadhalii hakikisha kuwa unaweka kila zao katika sehemu yake husika: mazao ya mwaka katika sehemu ya 4-5, mazao ya kudumu katika sehemu ya 6-7. Chini ni orodha ya mazao ya kawaida ya mwaka na ya kudumu.

Mazao ya Mwaka: Sehemu ya 4- 5  
**Mahindi**

Mazao ya kudumu: Sehemu ya 6 -7  
**Mihogo**

## **6A. Miti ya Matunda**

Sehemu hii inahusu miti ya matunda iliyolimwa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita katika shamba husika. Kama kaya haina mazao ya miti katika shamba nenda sehemu 6B. Orodhesha miti yote ya matunda katika ardhi ya kaya. Mifano ya miti ya matunda inayojulikana ni mapesheni, ndizi, embe, papai, na machungwa. Orodha ya mageresho ya miti ya matunda imeorodheshwa ukurasa wa mwisho wa dodoso. Hakikisha unadodosa kwa undani zaidi kama muhojiwa atakupa jina la tunda ambalo halipo katika orodha. Yawezekana jina analotumia la tunda ni la kiasili ambalo kiukweli lipo katika orodha. Kama inawezekana, mwombe muhojiwa akuonyeshe tunda unapokwenda kuchukua vipimo vya GPS, au tafuta aina hiyo ya tunda katika soko linalopatikana eneo hilo, jaribu kulitambua jina.

**Safuwima ya 1.** Andika utambulisho wa shamba, mfano shamba la M1, M2, M3, n.k.

**Safuwima ya 2.** Andika geresho la zao lililopandwa katika shamba lililooodheshwa katika safuwima ya kwanza.

### **SWALI LA 1 ORODHESHA MASHAMBA YOTE YALIYOLIMWA KATIKA KIPINDI CHA MIEZI 12 ILIYOPITA. KWA KILA SHAMBA ORODHESHA MATUNDA YOTE YALIYOLIMWA.**

*Haya ni maelekezo kwa mdadisi usimsomee mhojiwa.*

Muombe muhojiwa akutajie orodha yote ya matunda yaliyopo katika shamba lake. Kumbuka, kiwango cha chini kwa miembe, miparachichi, mipesheni, mipera, michungwa, mindimu/milimao ni mti mmoja na namba ya chini kwa migomba na mipapai ni minne.

#### **Swali la 2: Idadi ya miti hiyo katika shamba hili?**

Andika idadi ya miti iliyopo ndani ya shamba ulilooodheshwa. Ulizia idadi ya miti/mazao yaliyopo LEO, na sio idadi ya miti/mazao yaliyopandwa mwanzoni.

#### **Swali la 3: Je, mwaka gani sehemu kubwa ya miti ya matunda ilipandwa?**

Andika mwaka (kwa Tarakimu 4) ambao sehemu ya miti ya matunda ilipandwa katika shamba. Ikiwa miti ilipandwa zaidi ya mara moja, andika mwaka ambao kwa kiasi kikubwa miti ilipandwa. Kama miti ilipandwa kabla ya mhojiwa ajazaliwa andika 1900.

#### **Swali la 4: Miti mingapi ya matunda ilipandwa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Uliza idadi ya miti ya matunda iliyopandwa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Hii ni miti mipya tu.

#### **Swali la 5: Je, ulipanda mazao mchanganyiko katika shamba hili katika miezi 12 iliyopita??**

Uliza kama kuna shamba ambalo lilipandwa mazao mchanganyiko katika shamba katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Kama lina mazao mchanganyiko jaza geresho 1ø kama shamba halikulimwa mazao mchanganyiko jaza geresho 2ø na nenda swali la 7. Hakikisha kwamba majibu yanalingana na kile kilichoandikwa kwenye dodoso. Kwa shamba lolote lenye zao zaidi ya moja lililooodheshwa. Kwa shamba lenye zao zaidi ya moja lililooodheshwa, jibu linapaswa kuwa ndio.

#### **Swali la 6: Je, ni nini sababu ya kuchanganya mazao?**

Andika geresho linalostahili kutoka kwenye dodoso.

#### **Swali la 7: Ni kipindi gani mara ya mwisho mlipovuna matunda ya [TUNDA]?**

Swali hili linauliza kuhusu msimu wa mavuno wa matunda. Onyesha mwezi na mwaka ambao msimu wa mwisho wa matunda ulianza(wakati matunda ya kwanza yalipopatikana) na mwaka na mwezi ambapo msimu uliisha. Kama msimu ni endelevu tumia miezi 12 iliyopita kuelezea msimu.Kama miti yote kwenye shamba imepandwa karibuni na bado ni midogo kutoa matunda, andika 99 kwenye safuwima zote.

**Swali la 8: Nani katika kaya alifanya maamuzi kuhusu matumizi ya [MATUNDA] yaliyovunwa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Uliza ili kufahamu nani mwenye maamuzi juu ya nini cha kufanya kuhusu matunda yaliyovunwa, andika namba ya utambulisho wa mwanakaya, orodhesha hadi wanakaya wawili.

**Swali la 9:-Mlivuna kiasi gani cha tunda?**

Andika kiasi cha matunda kilichovunwa katika kipimo cha kilogramu ó badili vipimo vya kiasili viende katika Kilo.

**Swali la 10: Je, kuna upotevu wowote wa [TUNDA] yakiwa bado shambani?**

Uliza kama kuna upotevu wowote wa matunda yakiwa bado shambani (kabla ya kuvunwa). Hii inajumuisha upotevu uliotokea matunda yakiwa bado mtini tu. Kama jibu ni ndiyo uliza swali linalofuata na kama jibu ni hapana uliza taarifa za tunda lingine.

**Swali la 11: Ni aina gani ya upotevu?**

Andika geresho linalostahili.

## 6B. Mazao ya Kudumu

Mazao ya kudumu ni mazao ambayo yakishapandwa huchukua miaka mingi shambani na hayahitaji kupandwa tena baada ya mavuno ya kila mwaka, zao la muhogo limechuliwa kama zao la kudumu kwa kuwa mihogo inavunwa kuanzia miezi 6 hadi miaka 2 kulingana na aina ya mbegu. Mara nyingi mazao ya kudumu huwa ni ya miti kwa mfano minazi, miwa, mikorosho n.k.

*Maswali yote ya sehemu ya 6B yanafanana na ya sehemu ya 6A.*

## Sehemu 7. Mauzo na Hifadhi ya Mazao ya Kudumu na Miti ya Matunda

### 7A & 7B MITI YA MATUNDA & MAZAO YA KUDUMU

**Angalizo:** Mazao/matunda ambayo yameorodheshwa katika sehemu ya 6 yanatakiwa yawepo katika sehemu hii ya 7. Mazao ya kudumu au matunda ambayo hayakuorodheshwa katika sehemu ya 6 hayata orodheshwa kwenye sehemu hii ya saba (7). **Hii itathibitishwa na programu ya kuingiza ya takwimu, kama kuna kosa lolote unatakiwa kurudi katika kaya kudodoso zaidi.**

#### 7A: Miti ya Matunda

**Swali la 1: ORODHESHA AINA YA MITI YOTE YA MATUNDA KAMA ILIVYO KATIKA SEHEMU YA 6A. ANDIKA JINA LA TUNDA.**

Haya ni maelekezo kwa mdadisi. Nakili orodha toka sehemu 6A. Hakuna zao ambalo halikuoneshwatika sehemu 6A litakaloonyweshwa kwenye sehemu ya 7A.

**Swali la 2: Mliuza sehemu yoyote ya [TUNDA] mliyovuna?**

Onesha kama mhojiwa aliiza sehemu yoyote ya matunda aliyovuna. Andika geresho 1 na endelea na maswali yanayofuata. Andika 2 kwa jibu la hapana nenda Swali la 8.

**Swali la 3: Mliuza kiasi gani cha [TUNDA] mlovuna?**

Muulize mhojiwa kiasi cha [tunda] walichovuna na kuuza. Andika kipimo katika kilogramu,kwa kipimo cha kienyeji badili kiwe katika kilo.

#### **Swali la 4: Je, [MATUNDA] yaliyouzwa yalikuwa na thamani gani?**

Andika thamani (TZ shilingi) ya tunda iliyouzwa baada ya mavuno. Anaweza kuwa ameuza mazao kidogo kidogo kwa muda mrefu. Katika hali hii anaweza akafanya kukadiria jumla ya kiasi cha mazao yaliyouzwa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita na katika shilingi ya Tanzania.

#### **Swali la 5: Nani katika kaya alikuwa na jukumu la kujadili mauzo ya [MATUNDA]?**

Uliza nani alikuwa na jukumu la kujadili mauzo ya matunda, hata kama yalipelekwa sehemu kama vile sokoni, aliyepeka kuuza sokoni ndo aorodheshwe, andika namba yake ya kaya kutoka kwenye orodha ya wanakaya, orodhesha hadi wanakaya wawili waliohusika na kujadili suala zima la mauzo.

#### **Swali la 6: Nani katika kaya alitoa maamuzi ya nini cha kufanya kwa kilichopatikana?**

Uliza nani katika kaya alitoa maamuzi ya namna ya kutumia mapato yaliyopatikana baada ya kuuza matunda. Baadhi ya kaya maamuzi hufanywa kwa kushirikiana, mkuu wa kaya na mwenzi (ikiwa ni hivyo utaandika wote 01 na 02), kaya nyine maamuzi hufanywa na mkuu wa kaya tu ₩10 na zingine hufanywa na mwenza tu ₩20 au na mwanakaya mwingine. Andika namba ya mwanakaya toka kwenye orodha ya wanakaya, orodhesha hadi wanakaya wawili.

#### **Swali la 7: Mliuza wapi sehemu kubwa ya matunda?**

Onyesha ni wapi mhojiwa alipouzia sehemu kubwa ya matunda waliyovuna. Orodhesha watoa huduma wasiozidi wawili kwa kujaza utambulisho wao kutoka ukurasa wa mwisho wa dodoso .

### **Uhifadhi wa Mavuno**

#### **Swali la 8: Je, kuna mazao yoyote ya shamba hili ghalani sasa?**

Muulize mhojiwa kama kuna mazao yoyote katika ghalani ambalo lipo nyumbani au mahali pengine. Kama jibu ni ndiyo jaza geresho ₩10 kama na endelea na Swali la linalofuata. Kama jibu ni hapana jaza geresho ₩20 na nenda swali la 13.

#### **Swali la 9: Mmehifadhi kiasi gani cha mavuno?**

Andika kiasi cha mavuno ambacho kimehifadhiwa ghalani kwa sasa. Kiasi hiki kiandikwe katika kipimo cha uzito wa kilogramu na sio kipimo cha kienyeji.

#### **Swali la 10: Mnatumia mbinu gani kuu kuhifadhi mazao?**

Muulize mhojiwa njia kuu inayotumika katika kuhifadhi mazao yake. Kama anahifadhi katika njia za kuhifadhi zaidi ya moja basi akutajie ile anayotumia zaidi. Kama atataja njia ambayo haijaorodheshwa, andika geresho 70 NYINGINE ö taja kwa maneno.

#### **Swali la 11: Je, mlifanya chochote kulinda mavuno ghalani dhidi ya uharibifu?**

Swali hili linalenga kujua kama mhojiwa alifanya chochote katika kulinda mavuno ghalani ili yasiharibike kwa kuoza na wadudu. Kama jibu ni ndiyo andika geresho ₩10 kisha endelea na Swali linalofuata na kama jibu ni hapana nenda swali la 13.

#### **Swali la 12: Mlifanya nini?**

Onyesha njia ya uhifadhi ambayo mhojiwa hutumia katika kulinda mazao. Mageresho yameorodheshwa kwenye dodoso. Kama atataja njia ambayo haijaorodheshwa, andika geresho 30 NYINGINE ö kisha andika jina la njia hiyo kwa maneno.

### **Upotevu / Hasara**

#### **Swali la 13: Je, kuna sehemu yoyote ya uzalishaji iliyopotea baada ya kuvuna kutokana na kuoza, wadudu, panya, n.k.**

Mavuno kupotea baada kuvuna kutokana na kuoza wadudu, panya, n.k. Inawezekana sehemu ya mavuno ya [TUNDA/ZAO] yaaliyopotea baada ya kuvunwa kabla ya kuuzwa kutokana na kuoza, kuliwa na wadudu, panya, au kwa kuibiwa n.k.

Swali halijumuishi upotevu kabla ya kuvunwa kwa kuharibiwa na wadudu au ndege wakati yakiwa bado juu ya miti. Kama mhojiwa atajibu ndiyo andika geresho -1økisha endelea maswali yanayofuata,, kama jibu ni hapana andika geresho -2økisha endelea tunda lingine.

**Swali la 14: Sababu kuu ya kupotea mavuno.**

Uliza sababu kubwa iliyosababisha kupotea mavuno ya [tunda/zao]. Kama kuna sababu zaidi ya moja, chunguza zaidi ili uweze kupata sababu iliyo kuu zaidi. Tumia mageresho yaliyoorodheshwa kwenye dodoso. Iwapo mhojiwa atataja sababu ambayo haipo kwenye dodoso, jaza 5 öNyingineö na andika sababu kwa maneno. Andika geresho linalostahili.

**Swali la 15: Ni sehemu gani ya kumi ya mavuno yaliyopotea?**

Muulize mhojiwa ni sehemu gani katika 10 ya mavuno yaliyopotea. Jibu litakuwa ni namba kati ya 0-10, mfano 2, 3, 4, n.k. Kwa mfano; Kama mkulima wa maembe atapoteza embe 5 kati ya embe 10 ni sawa na 50% yalioza kabla ya kuuzwa, hivyo jibu ni 5. Kama mkulima wa maembe atapoteza embe 3 kati ya kila embe 10 ni sawa na 30%, hivyo jibu ni 3. Kama mhojiwa atajibu kwa asilimia ambayo ni ngumu kubadili, 25% kwa mfano, kadiria katika namba nzima ya karibu kwa hali hii jibu ni 3.

**Swali la 16: Mavuno yaliyopotea yalikuwa na thamani gani?**

Andika thamani (shilingi) ya mazao yaliyopotea baada ya kuvuna. Mhojiwa anaweza kukadiria iwapo hana uhakika.

**Maswali ya (17-21), ikiwa mhojiwa atatoa taarifa za kiasi kwa vipimo vya kienyeji kama ndoo au begi, muulize mhojiwa akadirie kiasi katika kilogramu.**

**Swali la 17: Ni kiasi gani cha mavuno kimetumika kwenye kaya?**

Uliza kiasi cha mazao yaliyovunwa ambayo yalitumiwa na kaya. Andika kiasi katika kilogramu.

**Swali la 18: Ni kiasi gani cha mavuno kimehifadhiwa kama mbegu wakati wa msimu ujao wa kupanda?**

Uliza kiasi cha mazao yaliyovunwa ambayo kaya ilihifadhi kama mbegu ili zije kutumika katika msimu ujao wa kupanda. Andika kiasi katika kilogramu. Ikiwa kulikuwa hakuna, weka geresho -0.ø

**Swali la 19: Ni kiasi gani cha mavuno kimetumika kama malipo kwa vibarua?**

Uliza kiasi cha mazao yaliyovunwa ambayo kaya ilitumia kama malipo kwa vitu kama kibarua au kodi.

Andika kiasi katika kilogramu. Ikiwa hakuna mavuno yaliyotumika kama malipo, hapo weka 0.

**Swali la 20: Ni kiasi gani cha mavuno umetoa kama zawadi?**

Uliza kiasi cha mazao yaliyovunwa ambayo kaya imetoa kama zawadi kwa watu walio nje ya kaya. Andika kiasi katika kilogramu. Ikiwa hakuna mavuno yaliyotolewa kama zawadi, hapo weka -0ø

**Swali la 21: kiasi gani cha mavuno kimetumika kulishia mifugo?**

Uliza kiasi cha mazao yaliyovunwa ambayo kaya ilitumia kulishia mifugo ya kaya. Andika kiasi katika kilogramu. Ikiwa hakuna mavuno yaliyotumika kulishia mifugo, hapo andika -0ø Ikiwa kaya haimiliki mifugo,pia andika -0ø

**KUMBUKA:** Jumla ya kiasi kitakachoandikwa katika maswali haya matano (32a-32b) kamwe hayatazidi jumla ya kiasi cha mavuno kilichtolewa katika sehemu ya 4 ya mazao, swali la 28.

## **7B: Mazao ya Kudumu**

*Maswali yote ya sehemu ya 7B yanafanana na yale ya sehemu ya 7A.*

# Sehemu 10. Bidhaa na Mabaki ya Mazao

---

Sehemu hii inauliza bidhaa za kilimo zilizosindikwa na mabaki ya kilimo. Mageresho ya bidhaa hizi yameorodheshwa kwenye dodoso. Kumbuka kwamba baadhi ya bidhaa inaweza kuonekana mara mbili. Kwanza öBidhaa/zaoö na pili öMabaki ya zao/bidhaaö. Ikiwa bidhaa ilizalishwa kwa ajili ya kuuza au kutumiwa na kaya hii itakuwa ni bidhaa ya kilimo. Kwa mfano, ikiwa kaya imesaga mahindi yaliyolimwa kuwa unga na kuuza, hii itakuwa ni bidhaa ya kilimo. Iwapo bidhaa itazalishwa baada ya kusindika bidhaa nyingine, haya ni mabaki ya bidhaa. Mfano wa bidhaa ya mabaki ya bidhaa ni pumba inatokana na mahindi yaliyokobolewa na kuuzwa kama chakula cha mifugo.

Ni muhimu kwa bidhaa hizi kuzitofautisha kati ya bidhaa mbili. Kwa mfano, kukamua juice ya matunda ya apple kwa ajili ya kuuza kutokana na matunda ya apple yaliyolimwa katika shamba la mhojiwa hii itakuwa ni bidhaa ya kilimo. Ikiwa kaya imezalishwa vipande (slice) vikavu vya apple kwa ajili ya kuuza, lakini kabla ya kukausha vipande (slice) za apple ni lazima juisi ikamuliwe kwanza, na juisi hiyo hatimaye inakuwa tayari kwa ajili ya kuuza sokoni, haya yatakuwa ni mabaki ya bidhaa ya kilimo. Kitu cha muhimu katika kutofautisha ni lengo la msingi la uzalishaji.

## **Swali la 1: Je, kaya yenu ilisindika mazao yoyote mliyovuna miezi 12 iliyopita (dadisi unga, pumba)?**

Uliza zaidi ili kuhakikisha kwamba mhojiwa anaelewa bidhaa na mabaki yote ya kilimo yanayotalajiwu kupatikana. Andika geresho la ndiyo au hapana kwenye kisanduku. Iwapo Jibu ni hapana nenda sehemu inayofuata, na iwapo ni ndiyo endelea na Swali la 2.

## **Swali la 2: Jina la zao.**

Andika jina la zao ambalo limezalisha/kutoa bidhaa au mabaki. Onyesha geresho la zao linalostahili, halafu onyesha iwapo bidhaa au mabaki yamezalishwa.

## **Swali la 3: Ni bidhaa/mabaki gani ya zao hili yalizalishwa?**

Andika bidhaa/mabaki yaliyozalishwa, kwa kutumia mageresho yaliyoorodheshwa kwenye dodoso ó uwe mwangarifu kutofautisha bidhaa na mabaki, Ikiwa mhojiwa ameorodhesha bidhaa ambayo haionekani kwenye dodoso, amua endapo kitu hicho ni bidhaa au mabaki na uchague geresho linalostahili öNYINGINEö na ndika jina la kitu kwa maneno.

## **Swali la 4: Ni kiasi gani cha bidhaa/mabaki kilizalishwa kwa miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa kiasi cha bidhaa/mabaki kilichozalishwa miezi 12 iliyopita kisha andika uzito wake katika kilo/lita. Uwe mwangalifu katika kubadili vipimo vya kilo au lita. Kwa mfano, ikiwa mhojiwa amezalisha tani moja ya vyakula vya mifugo (fodder), andika kilo 1000.

## **Swali la 5: Ni [MAZAO] kiasi gani yalitumika kwa ajili ya kutengeneza/kuzalisha [MABAKI/BIDHAA] katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Uliza ni kiasi gani kilitumika kuzalisha bidhaa, mabaki mfano; kaya ilitumia kilo 100 za mahindi kusaga unga wa kilo 100, hivyo kilo 100 ndio ziandikwe kwenye swali hili. Andika kiasi katika kilo na badili vipimo vyote vya kienyeji kuwa kilo.

## **Swali la 6: Je, kuna [BIDHAA/MABAKI] yaliyouzwa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa kama kuna [BIDHAA/MABAKI] yaliyouzwa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Ikiwa jibu ni ndiyo endelea na Swali la 7 kama ni hapana nenda Swali la 13.

## **Swali la 7: Kiasi gani kiliuzwa?**

Uliza kiasi cha bidhaa/mabaki kilichouzwa na mhojiwa. Andika geresho la kiasi na kipimo katika kilogramu au lita kilichouzwa katika miezi 12 iliyopita. Kuwa makini katika kubadili vipimo kwenda kwenye kilo au lita.

#### **Swali la 8: Je, ni kiasi gani cha [ZAO] kilitumika katika uzalishaji huo?**

Uliza kujua kiasi gani cha zao kilichotumika, mfano kilo 60 za mahindi zilitumika kuzalisha kilo 20 za unga ambaio uliuzwa, onyesha hicho kiasi cha kilo 60 kwenye swali hili.

#### **Swali la 9: Nani katika kaya aliquwa na jukumu la kutoa maamuzi ya mauzo ya [BIDHAA/MABAKI]?**

Uliza nani katika kaya aliquwa na maamuzi ya mauzo ya bidhaa, andika namba yake kutoka kwenye orodha ya wanakaya, orodhesha hadi wanakaya wawili.

#### **Swali la 10: Nani katika kaya alitoa maamuzi ya nini kifanyike kwa kilichopatikana (baada ya mauzo)?**

Uliza nani katika kaya alitoa maamuzi ya nanmana ya kutumia mapato yaliyopatikana baada ya mauzo. Baadhi ya kaya maamuzi hufanywa kwa kushirikiana, mkuu wa kaya na mwenzi (ikiwa ni hivyo utaandika wote 01 na 02), kaya nyingine maamuzi hufanywa na mkuu wa kaya tu -01<sup>ø</sup>na zingine hufanywa na mwenza tu -02<sup>ø</sup> au na mwanakaya mwingine. Andika namba ya mwanakaya toka kwenye orodha ya wanakaya, orodhesha hadi wanakaya wawili.

#### **Swali la 11: Bidhaa/mabaki hayo yaliuzwa kwa thamani gani?**

Uliza mabaki ama bidhaa ziliuzwa kwa kiasi gani, andika kiasi katika shilingi.

#### **Swali la 12: Mliuza wapi sehemu kubwa ya [BIDHAA/MABAKI] hayo?**

Muulize mhojiwa wapi waliuza sehemu kubwa ya [BIDHAA/MABAKI]. Tumia orodha ya watoa huduma kutoka ukurasa wa mwisho wa dodoso. Jaza watoa huduma wasiozidi wawili.

#### **Swali la 13: Je, kulikuwa na gharama nyingine za kazi, pembejeo za ziada n.k. katika uzalishaji wa [BIDHAA/MABAKI]?**

Swali hili linataka kupata gharama ambazo zilitumika katika kuzalisha bidhaa/mabaki hayo. Mfano mishahara ya wafanyakazi, au mafuta ya kuendeshea mitambo n.k. Iwapo jibu ni ndiyo endelea na Swali la 14, kama jibu ni hapana nenda bidhaa/mabaki mengine.

#### **Swali la 14: Gharama zake zilikuwa kiasi gani?**

Muulize mhojiwa gharama za ziada zilizoorodheshwa katika swali la 14 na andika kiasi katika shilingi.

## **Sehemu 11. Vifaa na Mitambo ya Kilimo**

**Katika sehemu hii kuna orodha ya vifaa na mitambo ya kilimo. Muulize mhojiwa kama walitumia au kumiliki vifaa hivi kwa miezi 12 iliyopita ambavyo viro katika hali ya kufanya kazi. Msomee mhojiwa vifaa vyote.**

#### **Swali la 1: Mnamiliki idadi gani ya [VIFAA]?**

Muulize mhojiwa kama kaya inamiliki [VIFAA], kama kaya inamiliki andika idadi ya kila KIFAA kinachomilikiwa, na kama HAKUNA andika 00 kisha nenda Swali la 3.

#### **Swali la 2: [VIFAA] vikiuzwa vinathamani gani?**

Swali hili linataka mhojiwa kukadiria thamani ya kifaa kwa sasa, sio kipindi kifaa kimenunuliwa. Kwa mfano, kama kaya inamiliki kifaa kwa muda mrefu, thamani yake inaweza kuwa ndogo sana sasa hivi kuliko kipindi kaya imekinunua kifaa hicho. Swali hili linataka mhojiwa akadirie thamani ya kifaa sasa hivi kama kikiuzwa.

#### **Swali la 3: Je, kaya ilimiliki [VIFAA] katika miezi 12 iliyopita?**

Swali hili linaulizwa hata kama kaya haimiliki [KIFAA] kwa sasa, Je walimiliki KIFAA chochote katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Vifaa vingine vilinunuliwa au kuuzwa katika kipindi cha mwaka, lakini ni

muhimu kujua kama kaya ilimiki kifaa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, kama jibu ni NDIYO geresho  $\frac{1}{4}$  na uliza swali linalofuata. Kama HAPANA geresho ni  $\frac{2}{3}$  kisha nenda Swali la 6.

#### **Swali la 4: Mlitumia [KIFAA] katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Sawa na swali la 3, swali hili liuliza kama kaya ilitumia kifaa. Kaya inaweza ikamiliki mitambo na vifaa vya kilimo lakini isivitumie, au kaya inaweza isimiliki vifaa na mitambo ya kilimo, lakini ikatumia vifaa hivyo katika shughuli zake za kilimo. Ni muhimu kujua aidha kaya ilipata au kukitumia kifaa. Kama jibu ni ndiyo nenda Swali la 6, na kama jibu ni hapana endelea Swali la linalofuata.

#### **Swali la 5: Kwa sababu gani hamkutumia [KIFAA]?**

Muulize mhojiwa sababu gani hawakutumia [KIFAA] wanachokimiliki katika shughuli za kilimo kwa miezi 12 iliyopita. Angalia mageresho, kama mhojiwa ametoa sababu ambayo haipo kwenye orodha husika, andika 5 öNYINGINE TAJAö na andika sababu kwa maneno.

*Maswali ya 6 - 9. Maswali haya manne, yanazungumzia vifaa vya kilimo vilivyokodiwa na kaya katika miezi 12 iliyopita.*

#### **Swali la 6: Je, mlikodi au kuazima [KIFAA] katika miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa kama walikodi au kuazima [KIFAA] katika miezi 12 iliyopita. Kama jibu ni NDIYO geresho  $\frac{1}{4}$ , endelea na swali linalofuata. kama HAPANA geresho  $\frac{2}{3}$  nenda kifaa kinachofuata/kingine.

#### **Swali la 7: Je, ni [KIFAA] vingapi mlikodi/kuazima katika miezi 12 iliyopita?**

Andika idadi ya vifaa walivyokodi/kuazima katika miezi 12 iliyopita.

#### **Swali la 8: Ni wapi mlikodi/kuazima [KIFAA] mlitchotumia katika miezi 12 iliyopita?**

Andika mahali ambapo walikodi/kuazima kifaa. Tumia Orodha ya watoa huduma.

#### **Swali la 9: Mlilipa kiasi gani kukodi [KIFAA] mlitchotumia katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Uliza kiasi cha fedha kilicholipwa kwa kukodi kifaa katika miezi 12 iliyopita. Kama mhojiwa amefanya malipo yasiyo ya fedha (malipo kwa njia ya vitu) kwa ajili ya matumizi ya kifaa, kadiria thamani ya malipo hayo na uandike jumla katika shilingi ya kitanzania.

## **Sehemu 12. Huduma za Ushauri wa Kilimo**

Kuna orodha ya vyanzo vya ushauri wa kilimo cha mazao katika safuwima ya kwanza.

#### **Swali la 1: Je, katika miezi 12 iliyopita, ulipokea ushauri kutoka [CHANZO] juu ya ...?**

Swali hili linauliza aina mbalimbali za ushauri ambazo kaya ilipata kutoka katika chanzo. Kama jibu ni ndiyo, andika geresho  $\frac{1}{4}$  na, iwapo jibu ni hapana, andika  $\frac{2}{3}$  Kwa mfano, kaya ilipata ushauri kutoka katika ushirika wa wakulima kuhusu aina ya mbegu na mbolea za kutumia ili kuongeza uzalishaji wa mahindi. Kwa kuongeza, kaya pia ilipata ushauri kuhusu chanjo za misfugo kutoka katika Mashirika yasiyo ya kiserikali. Kwa mantiki hii, safumlalo 2 öMashirika yasiyo ya serikali ö inapaswa kuwa na  $\frac{1}{4}$  itaandikwa katika safuwima E, na safumlalo 3 öUshirika/mwungano wa wakulima ö inapaswa kuwa na  $\frac{1}{4}$  itaandikwa katika safuwima A1 na A2. Ikiwa mhojiwa atataja chanzo ambacho hakipo katika orodha, weka geresho 5 öOTHERö na andika chanzo kwa maneno.

#### **Swali la 2: MDADISI, MHOJIWA AMEJIBU "NDIYO" KWA AINA YOYOTE YA USHAURI KATIKA SWALI LA 1?**

Usimuulize mhojiwa swali hili. Angalia kwa kila safumlalo kuona kama angalau kuna jibu la moja  $\frac{1}{4}$  lililoandkwa katka safuwima yoyote. Ikiwa kuna  $\frac{1}{4}$  ilioandikwa kwenye safuwima yoyote katika

safumlalo, hapo andika  $\rightarrow$ Økwa swali hili. Ikiwa  $\leftarrow$ Øiliandikwa kwa kila safuwima kwenye safumlalo, hapo andika  $\leftarrow$ Økwa swali hili.

**Swali la 3: Nani katika kaya alipata ushauri toka [CHANZO].**

Muulize mhojiwa ni mwanakaya yupi alipata ushauri kutoka kwenye chanzo. Tumia orodha ya Wanakaya kuorodhesha wanakaya waliopata ushauri. Orodhesha mpaka wanakaya 4.

**Swali la 4: Ubora wa huduma ya ushauri.**

Muulize mhojiwa aonavyo ubora wa ushauri alioupata. Angalia mageresho.

**Swali la 5: Je, ulilipa chochote ili kupewa ushauri?**

Muulize mhojiwa ni kiasi gani alilipa ilikupata ushauri toka chanzo. Kama NDIYO geresho ni  $\tilde{1}\tilde{0}$  na kama HAPANA geresho  $\tilde{0}\tilde{2}\tilde{0}$  kisha nenda Swali la 7.

**Swali la 6: Ulilipa shilingi ngapi?**

Andika kiasi cha fedha alicholipa mhojiwa/kaya kwa ajili ya kupata ushauri huo

**Swali la 7: Ni mara ngapi mshauri toka [CHANZO] alitembelea shamba lenu katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa ni mara ngapi mshauri amewahi kutembelea kaya/shamba la kaya katika miezi 12 iliyopita. Usihusishe ziara zilizofanywa na mshauri kwa ujumla kijijini au ushauri uliotolewa kwa makundi. Andika  $\rightarrow$ Økama hukuna mshauri aliyetembelea kwenye kaya.

## **CHANZO CHA TAARIFA (SWALI LA 8 –10)**

**Swali la 8: Je, katika miezi 12 iliyopita mmewahi kupata taarifa yoyote kuhusu bei za mazao/mifugo/uvuvi kutoka [CHANZO]?**

Muulize mhojiwa kama amewahi kupata taarifa yoyote kuhusu bei za mazao kutoka chanzo chochote. Msomee orodha ya vyanzo hivyo. Andika  $\rightarrow$ Ø kama jibu ni ndiyo, iwapo jibu ni hapana, andika  $\leftarrow$ Ø kisha nenda mstari mwngine.

**Swali la 9: Je, ulilipa chochote ili kupewa taarifa?**

Uliza kama alilipa gharama yoyote ili aweze kupata taarifa zozote zinazohusiana na mazao/mifugo/uvuvi. kama jibu ni ndiyo endelea na Swali la 10 vinginevyo nenda mstari mwngine. Sehemu iliyotiwa kivuli usijaze chochote.

**Swali la 10: Ulilipa shilingi ngapi?**

Swali hili ni sawa na swali la 6 unatakiwa kuuliza kiasi alicholipia kwa ajili ya kupata taarifa tu. Uliza kiasi cha fedha kilicholipwa ili kaya/mhojiwa apewe taarifa. Sehemu iliyotiwa kivuli usijaze chochote.

***MAHOJIANO YATAKUWA SASA YAMEKAMILIKA LABDA TU KAMA KUNAHITAJIKA  
MAHOJIANO KWA DODOSO LA MIFUGO/UVUVI. TAFADHALI MSHUKURU MHOJIWA  
NAKUMBUKA KUANDIKA MUDA WA KUMALIZA MAHOJIANO.***

### **III. Dodoso La Mifugo na Uvuvi**

---

# SEHEMU YA 1-A: UTAMBULISHO WA KAYA

---

Utapata mageresho ya mkoa, Wilaya, Kata, Kijiji/Eneo la kuhesabia kutoka kwa Msamamizi wako. Andika mageresho ya namba ya kaya kama ilivyoandikwa kwenye dodoso la kaya na dodoso la kilimo, **hakikisha kuwa mageresho ya namba ya kaya ni sawa na kabisa na madodoso ya kaya na kilimo**. Pia jaza jina lako, namba ya mdadisi, tarehe na muda wa kuanza kuhoji kama ulivyofanya kwenye madodoso ya kaya na kilimo. Ukurasa wa 2 pia una nafasi ya kuandika maoni au vidokezo muhimu juu ya mahojiano.

Swali la 22 na 23 yaliyopo ukurasa wa 2 yatakusaidia kujua ni sehemu ipi ya dodoso hili yatatakiwa kujazwa kwenye kaya hii. Kaya ambazo zinamiliki mifugo katika kipindi cha miezi 12 iliyopita zilijibu NDIYOØ katika sehemu ya U-2, swali la 6. Na kaya zinazojihusisha na uvuvi au uuzaaji wa samaki katika kipindi cha miezi 12 iliyopita zilijibu NDIYOØ sehemu ya U-2 swali la 7 na 8. Sehemu ya 1-8 inahusiana na Mifugo na Sehemu ya 9-13 inahusiana na uvuvi.

## Sehemu ya 1: Taarifa za Mwanakaya

---

Nakili taarifa zote za mwanakaya kutoka dodoso la kaya. Ni MUHIMU kuhakikisha kuwa kila namba ya mwanakaya ni sawa kwa madodoso yote yanayohusiana na kaya hiyo. Swali la 4, unatakiwa kuweka alama ya -XØ kwa mwanakaya anayejibu dodoso hili. Ikiwa kuna wanakaya wengine wanaotoa taarifa hizi kwa pamoja, weka alama kwa wote waliohusika na utoaji wa taarifa katika sehemu hii.

## ORODHA YA WATOA HUDUMA

---

Orodha ya watoa huduma ni orodha ya watu (ambao si wanakaya), kampuni au taasisi ambapo mhojiwa alishirikiana nao katika kipindi fulani. Orodha ya watoa huduma inatengenezwa na mdadisi wakati wa mahojiano kwa kadri mhojiwa anavyoajibu maswali kuhusiana na vyanzo au sehemu anayopata mahitaji yanayohusiana na shughuli zao. Orodha ya watoa katika dodoso hili inatakiwa ijazwe sawa na orodha ya watoa huduma kwenye dodoso la kilimo. Kwa maelekezo zaidi juu ya kujaza kwa ufasaha orodha ya watoa huduma, rejea dodoso la kilimo sehemu ya watoa huduma.

## Sehemu ya 2: Mifugo

---

Sehemu hii inaelezea umiliki wa mifugo kwa kipindi hiki na kipindi cha miezi 12 iliyopita, isipokwa kwa swali la 2 ambalo linahitaji öidadi ya (MNYAMA) iliyomilikiwa miaka miwili iliyopitaö. Katika sehemu hii uliza maswali kwa kila mnyama ili kufuatilia mabadiliko pamoja na kujua sababu za mabadiliko hayo.

Ukiangalia kwenye safu wimu na vyumba vilivyowekwa kivuli, utaona kuwa kwa baadhi ya makundi ya wanyama hutatakiwa kujaza. Kwa mfano, sehemu ya 1 safuwima ya 5, inahusiana na wanyama waliozaliwa, haitakiwi kujazwa kwa wanyama wakubwa kama ng'ombe dume, ng'ombe jike, ng'ombe dume aliyehasiwa, mbwa n.k. Mbwa ameongezwa kwa makusudi kwenye mstari wake hasa kwa kuhofia kuwa angeongezwa katika kundi la ḍwanyama wengineö. Ni swali la 1 tu ambalo linauliza kama kaya ilifuga mbwa, sehemu nyingine zote zinazofuata zimetiwa kivuli. Ikiwa kaya inamiliki mbwa tu, nenda sehemu inayofuata.

*Angalizo: Kuna Waislamu wanaomiliki/kufuga wanyama maeneo mengi ya Tanzania ambao kwa namna moja au nyingine wanaweza kukerwa na maswali yanayohusiana na nguruwe. Kwa ujumla Waislam hawafugi wala kumiliki nguruwe. Wadadisi wanatakiwa kutumia hekima za kidini na kitamaduni katika kuuliza maswali haya. Kwa umakini zaidi, ni vizuri mdadisi akaomba msamaha mapema kwa maswali yanayohusiana na nguruwe kama ataona mhojiwa ana mashaka.*

**Anza kwa kujaza karatasi la kukunja (flap).** Tumia karatasi ya kukunja ili kuhakikisha kuwa wanyama wote wanaomilikiwa na kaya wanafutilia kwa umakini.

## UMILIKI

### **Swali la 1: Je, kaya yenu ilimiliki [MNYAMA] yoyote katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Kwa kila [MNYAMA] aliyeorodheshwa kwenye dodoso, muulize mhojiwa kama kuna mwanakaya yeote alimiliki [MNYAMA] katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Mifugo au wanyama hawa ni wale tu aliokuwa anamiliki au kutunza kwenye kaya husika. Mifugo midogo/vifaranga inatakiwa ijumuishwe ( kama vifaranga vya kuku kwenye jamii ya kuku, watoto wa nguruwe katika jamii ya nguruwe, watoto wa mbuzi kwenye jamii ya mbuzi, n.k.) Utufauti upo kwa ndama tu, ambao wana kundi lao. Kama jibu ni ndiyo, andika geresho ḍø kisha endelea na Swali la 2. Kama mhojiwa ametaja jina la mnyama ambalo halipo kwenye orodha, andika jina la mnyama kwa maneno katika kundi la wanyama wengine safu mlalo ya 16 na kisha nenda swali la 2.

**Zingatia:** *Hapa ina maana kuwa mifugo au wanyama hawa ni wale tu aliokuwa anamiliki au kuwatunza kwenye kaya husika.*

### **Swali la 2: Idadi ya [MNYAMA] iliyomilikiwa miaka miwili iliyopita.**

Muulize mhojiwa idadi ya wanyama waliomilikiwa na kaya kipindi cha miaka miwili iliyopita. Idadi hii ni muhimu ili kujua/kupima mabadiliko ya ongezeko la wanyama toka wafutiliaji wa kaya walipopita kwenye kaya. Weka geresho la 99 kwa kaya mpya.

### **Swali la 3: Idadi ya [MNYAMA] iliyomilikiwa miezi 12 iliyopita.**

Muulize mhojiwa idadi ya wanyama walikuwa wanamilikiwa na kaya katika kipindi cha miezi 12 iiyopita. Ni muhimu kudadisi zaidi na kupata idadi sahihi kwa sababu itakuwa muhimu sana katika kuangalia uwiano wa taarifa (unapojaza Sehemu ya 1 kwa kila mnyama, hakikisha kuwa idadi ya wanyama wanaoingia/kupatikana katika kaya na ambao wanaondoka kwenye kaya inakuwa sawa na idadi ya wanyama waliokuwa wanamilikiwa na kaya miezi 12 iliyopita na idadi inayomiliki kwa sasa).

### **Swali la 4: Ni [WANYAMA] wangapi ambao kaya hii inamiliki/kutunza kwa sasa?**

Swalli hili linamtaka mhojiwa ataje idadi ya [MNYAMA] ambao kaya inamiliki katika makundi mawili, ambazo ni ḍkiasili/wa-kienyejiö na ḍwalioboreshwa/wa-kisasaö. ḍIndigenous/localö ni mifugo iliyotokana na uzalishaji wa kiasili, kama Zebu (ng'ombe) wa pembe fupi; ḍexoticö inahusiana na uzalishaji wa mifugo kwa kutumia njia za kigeni, mfano ng'ombe aina ya Holstein Fresian; ḍwalioboreshwaö ni aina na mifugo

ambayo uzalishaji wake ni wa kuchanganya mifugo ya kisasa na kienyeji. Andika idadi kulingana na kundi lake. Angalia kuna sehemu zimetiya kivuli katika kundi la wanyama walioboreshw/wa kisasa; usiandike kwenye visanduku vilivyotiwa kivuli.

## **UZALISHAJI**

### **Swali la 5: Ni [MNYAMA] wangapi waliozaliwa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Uliza wanyama waliozaliwa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Sehemu zilizotiwa kivuli usiulize. (Ikiwa wanyama wakubwa ni chini ya mwaka mmoja tutawahesabu kama ni ndama, kama inavyojieleza kwenye chumba cha 1-4 ambazo zimetiya kivuli.)

## **MANUNUZI**

### **Swali la 6: Je, ulinunua [MNYAMA] hai katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa kama alinunua mnyama yoyote katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Ni mnyama yoyote awe mkubwa au mdogo/ndama. Usijumishe wanyama walionunuliwa hai lakini walichinjwa baada ya muda mfupi kwa ajili ya matumizi ya kaya na wanyama walioletwa kwenye kaya na kuachwa wanenepe kwa muda mfupi na kuchinjwa.

### **Swali la 7: Ni [ MNYAMA] wangapi hai kaya ilinunua katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Andika idadi ya [MNYAMA/WANYAMA] walionunuliwa, ukijumuisha na wanyama wadogo.

### **Swali la 8: Thamani ya manunuvi yote ni kiasi gani?**

Andika thamani ya [MNYAMA/WANYAMA] walionunuliwa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita katika TSHS.

## **ZAWADI**

### **Swali la 9: Je, ulipokea [MNYAMA] kama zawadi au malipo kwa huduma uliyotoa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Zawadi inaweza ikatoka kaya nyingine na zile zinazoweza kutolewa na mashirika kama chama cha wafugaji, taasisi zisizo za serikari na miradi mbalimbali. Pia jumuisha wanyama waliopokelewa kwenye kaya kama malipo au malipo ya huduma iliyotolewa kutoka kwa rafiki au mmoja wa familia na mashirika au NGO.

### **Swali la 10: Ni [MNYAMA] wangapi ulipokea kama zawadi katika miezi 12 iliyopita?**

Andika idadi ya ya Mnyama/wanyama aliopokea kama zawadi au malipo ya huduma, jumuisha wanyama wadogo.

### **Swali la 11: Idadi kubwa ya [MNYAMA] ilipokelewa kutoka kwa nani?**

Mdodose mhojiwa zawadi ilitoka kwa nani na angalia geresho linalostahili kutoka kwenye dodoso

### **Swali la 12: Je, ulitoa [MNYAMA] kama zawadi au malipo ya huduma mliyopata miezi 12 iliyopita?**

Mdodose mhojiwa kama alitoa zawadiya [MNYAMA] yeoyote au malipo ya mnyama kwa huduma aliyopewa kwa kipindi cha miezi 12 iliyopita. Zawadi inajumuisha mnyama aliyetolewa kwa mtu ambaye si mwanakaya, kama kaya nyingine au kwa jumuia.

### **Swali la 13: Je, ni idadi gani ya [MNYAMA] mliyotoa kama zawadi au malipo ya huduma mliyopata katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Andika idadi ya Mnyama/wanyama uliota kama zawadi au malipo ya huduma, jumuisha wanyama wadogo.

### **Swali la 14: Je, ni nani mlimpatia [MNYAMA] walio wengi?**

Mdodose mhojiwa kuhusu zawadi aliyota alimpa nani na angalia geresho kutoka kwenye dodoso.

## **MAGONJWA**

### **Swali la 15: Je, kuna [MNYAMA] aliyekufa kwa UGONJWA kwa miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa kama kuna mnyama aliyekufa kwa ugonjwa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, usijumuishe wanyama waliochinjwa kwa kusudio maalum. Kama jibu ni hapana andika →ø kisha nenda Swali la 18, iwapo jibu ni ndiyo, andika geresho →ø kisha endelea na Swali linalofuata.

### **Swali la 16: Ni [MNYAMA] wangapi waliokufa kwa ugonjwa kwa miezi 12 iliyopita?**

Andika idadi ya wanyama waliokufa kwa ugonjwa katika miezi 12 iliyopita.

### **Swali la 17: Je, nini thamani ya [MNYAMA] wote waliokufa kwa UGONJWA.**

Muulize mhojiwa kukadiria thamani ya wanyama waliokufa kwa ugonjwa katika miezi 12 iliyopita. Kiasi cha fedha kiandikwe katika shilingi ya Tanzania.

## **WIZI**

### **Swali la 18: Mmeibiwa [MNYAMA] ye yote kwa miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa kama kuna mnyama aliyeibwa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Kama jibu ni hapana geresho →ø kisha nenda Swali la 21, na kama jibu ni ndiyo, geresho →ø kisha nenda swali linalofuata.

### **Swali la 19: Je mmeibiwa [MNYAMA] wangapi kwa miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa ni [MNYAMA] wangapi walioibiwa katika miezi 12 iliyopita na andika idadi yake.

### **Swali la 20: Thamani ya [MNYAMA] wote walioibiwa.**

Muulize mhojiwa akadirie jumla ya thamani ya [MNYAMA] walioibiwa na andika kiasi cha fedha katika shilingi.

## **MAJERAHA**

### **Swali la 21: Je, mliwahi kupoteza [MNYAMA] ye yote kuitia MAJERAHA / AJALI / MAJANGA YA ASILI katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa kama kuna mnyama ye yote aliywahi kupoteza kutokana na majeraha au ajali au majanga ya asili katika kipindi cha miezi 12 iliyopoita. Ni muhimu kuandika wale wanyama tu aliopoteza kutokana na majeraha, ajali na majanga ya asili na sio kwa magonjwa. Kama wanyama wamekufa kwasababu ya kukosa chakula (malisho) au maji wanajumuishwa hapa. Kama jibu ni hapana, geresho →ø na nenda swali la 24. Kama jibu ndiyo, geresho →ø na endelea na swali linalofuata.

### **Swali la 22: Je, ni idadi gani ya [MNYAMA] mliopoteza kuitia MAJERAHA / AJALI / MAJANGA YA ASILI katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa akutajie idadi ya [MNYAMA] aliowapoteza kuitia majeraha, ajali au majanga ya asili katika kipindi cha miezi 12 iliyopita.

### **Swali la 23: Ni nini ilikuwa thamani ya [MNYAMA] waliokufa kutokana na MAJERAHA/AJALI/MAJANGA YA ASILI?**

Muulize mhojiwa kukadiria jumla ya thamani ya [MNYAMA] waliokufa kutokana na majeraha, ajali au majanga ya asili, na andika kiasi hicho cha fedha katika shilingi ya Tanzania.

## **MAUZO**

### **Swali la 24: Je, umeuza [MNYAMA] hai kwa miezi 12 iliyopita?**

Swali hili linataka kujua iwapo kaya imeuza [MNYAMA] hai katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Usijumuushe wanyama ambao wamechinjwa kabla ya kuuzwa katika swali hili. Ikiwa jibu ni ndiyo, jaza geresho -1Ø endelea na swali la 25, ikiwa jibu ni hapana, weka geresho -2Ø kisha nenda Swali la 29.

**Swali la 25: [MNYAMA] hai wangapi uliuza kwa miezi 12 iliyopita?**

Andika idadi ya [MNYAMA] hai waliouzwa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita.

**Swali la 26: [MNYAMA] hai aliuzwa kwa kiasi gani?**

Muulize Mhojiwa kiasi cha fedha alichopata kwa kuuza kila aina ya mnyama hai.

**Swali la 27: Nani katika kaya yako aliamua juu ya matumizi ya mapato haya?**

Swali hili linamuuliza mhojiwa ni nani katika kaya alitoa maamuzi kutokana na matumizi ya mapato yaliyopatikana. Kumbuka kwamba wanyama wanaweza kuuzwa na mwanakaya mmoja lakini wanakaya wengine wanatoa maamuzi ya matumizi ya mapato. Taarifa zinazokusanywa hapa ni kuhusu mtu/watu wanaoamua juu ya matumizi ya mapato hayo. Unatakiwa kutumia mageresho yaliyorodheshwa kwenye orodha ya wanakaya. Baadhi ya kaya maamuzi yanafanywa pamoja kutoka kwa mume na mke (kwa hiyo geresho itakuwa 01Ø naø 02Ø), na baadhi ni mkuu wa kaya tu (01) au ni mke geresho (02), au na mwanakaya mwengine. Orodhesha mpaka watu 2 katika kaya kwa usahihi.

**Swali la 28: Ni wapi mliuza sehemu kubwa ya [MNYAMA] hai?**

Swali hili linataka kujua mnunuzi wa wanyama hai waliouzwa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita (pale ambapo sehemu kubwa ya wanyama hai waliuzwa). Tumia orodha ya watoa huduma kutoka ukurasa wa mwisho wa dodoso la mifugo na uvuvi kuandika namba (ID) za wanunuzi.

## UCHINJAJI

**Swali la 29. Je, mlichinja [MNYAMA] wowote katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Swali hili linahusu wanyama wa aina tofauti waliochinjwa ambao wapo kwenye orodha (isipokua mbwa ambao hakuna taarifa inayoulizwa zaidi ya ile ya sehemu ya 1, swali la 1). Jumuisha wanyama wanaochinjwa shambani na nje ya shambani (Mfano, wamepelekwa machinjioni). Usijumuushe wanyama walionunuliwa sokoni na kisha kuchinjwa kwa matayarisho ya chakula na wale wanyama walioletwa kwenye kaya kwa kipindi kifupi kwa ajili ya malisho na kuchinjwa. Kama hapana [MNYAMA] hakuchinjwa, andika 2 na nenda [MNYAMA] anayefuata.

**Swali la 30: Ni [MNYAMA] wangapi ulichinja katika miezi 12 iliyopita?**

Andika idadi ya wanyama waliochinjwa katika kaya miezi 12 iliyopita. Jumuisha pia wanyama wadogo katika idadi hiyo.

**Swali la 31: Je, nini ulikuwa wastani wa uzito wa [MNYAMA] hai kabla ya kuchinjwa?**

Muulize mhojiwa kukadiria wastani wa uzito wa [MNYAMA] hai kabla ya kuchinjwa, na andika jibu katika kilogramu na sio katika vipimo vya kiasili au kienyeji.

**Swali la 32: Je, Mliuza [MNYAMA] wangapi kati ya mlnochinja?**

Kwa kila aina ya mnyama ambae amechinjwa, andika idadi ya wanyama waliouzwa. Swali hili linahusu wanyama ambao walichinjwa kwa ajili ya kuuzwa tu. Usijumuushe wanyama ambao walichinjwa kwa madhumuni mengine (kama vile mazishi, sherehe, n.k.) Kama hakuna mnyama aliyechinjwa, andika -Ø kisha nenda mnyama mwengine/sehemu nyingine.

**Swali la 33: Jumla ya thamani [MNYAMA] mlionchinja na kuuza ni kiasi gani?**

Andika thamani ya mnyama aliyechnjwa na kuuzwa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita katika shilingi ya Tanzania.

**Swali la 34: Je, ni wapi uliuzia sehemu kubwa ya [MNYAMA] ambao mlichinja?**

Muulize mhojiwa akutajie ni wapi uliuzia [MNYAMA] ambao alichinja. Tumia mageresho kutoka katika orodha ya watoa huduma katika ukurasa wa mwisho wa dodoso la mifugo na uvuvi ili kuandika hadi watoa huduma 2 pale ambapo mhojiwa uliuzia sehemu kubwa ya [MNYAMA] aliyechnjwa.

**Swali la 35: Nani katika kaya yako aliamua juu ya matumizi ya mapato haya?**

Swali hili linamuuliza mhojiwa ni nani katika kaya alitoa maamuzi kutokana na matumizi ya mapato yaliyopatikana. Kumbuka kwamba wanyama wanaweza kuuzwa na mwanakaya mmoja lakini wanakaya wengine wanatoa maamuzi ya matumizi ya mapato. Taarifa zinazokusanya hapa ni kuhusu mtu/watu wanaoamua juu ya matumizi ya mapato hayo. Unatakiwa kutumia mageresho yaliyorodheshwa kwenye orodha ya wanakaya. Angalia mfano unaofuata:

Endapo mkuu wa kaya ana id namba 01 na mke wake id namba 02. Kama maamuzi ya matumizi ya kaya yanafanywa kwa pamoja na mkuu wa kaya na mke wake, weka geresho 01 na 02. Kama maamuzi yanafanywa na mkuu wa kaya tu au mke wake tu, geresho 01 au 02. Kama mwanakaya mwingine anafanya maamuzi, tumia mageresho ya orodha ya wanakaya husika kwa usahihi.

## Sehemu ya 3: Afya ya Wanyama

---

*Kumbuka: Maswali katika sehemu hii yanauliza kuhusu makundi ya wanyama, kama vile Wanyama wakubwa (Ng'ombe), Wanyama wadogo (Mbuzi, kondoo), Nguruwe na Jamii ya Ndege (Kuku na Bata), na sio kwa mnyama mmoja mmoja. Kama kaya inatoa taarifa/takwimu kwa kila mnyama peke yake, ni muhimu kupata jumla ya thamani tofauti pembeni mwa dodoso/kurasa husika wewe mwenyewe kabla hujuandika jibu katika sehemu husika. Mhojiwa hataulizwa kufanya mahesabu ye ye mwenyewe kama hayupo tayari.*

*Kumbuka: Kuna wafugaji/wakulima wengi wakiislamu Tanzania nzima ambao wanaweza kukerwa na maswali yanayohusiana na nguruwe. Kwa ujumla wafugaji wa kiislam hawafugi wala hawamiliki nguruwe. Khahiyo wadadisi watumie hekima za kidini na kitamaduni wakati wanauliza maswali haya. Kwa uangalifu, mdadisi anaweza kuomba samahani mapema kwa maswali yahusuyo nguruwe kama ataona mhojiwa anakerwa nayo.*

**Swali la 1: Rejea sehemu ya 2, swali la 1: Kaya ilimiliki aina yoyote ya wanyama hawa?**

Mdadisi anatakiwa kuangalia sehemu ya 2, swali 1 kuona kama kaya inamiliki mnyama yeyote katika kila kundi. Mdadisi hatakiwi kuuliza swali hili kwa mhojiwa. Maswali katika sehemu hii yanauliza kwa makundi ya wanyama na swali hili linahakikisha kwamba hakuna kundi la mnyama lililoachwa kwa bahati mbaya.

**Jaza kikaratasi cha kukunja cha wanyama (flap).** Rejea swali la 1, sehemu hii ili kujaza kwa usahihi flap. Tumia flap kuhakikisha unafuatilia wanyama wanaomilikiwa na kaya kwa ajili ya sehemu zinazofuata katika sehemu ya mifugo ya dodoso hili.

## Chanjo

### Swali la 2: Je, [MNYAMA] aliugua magonjwa gani katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?

Muulize Mhojiwa iwapo [MNYAMA] aliugua ugonjwa wowote katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Tumia mageresho yaliyorodheshwa kwenye dodoso kujaza aina ya magonjwa, jaza hadi magonjwa makubwa 2. Kumbuka swali linauliza ugonjwa kwa kila kundi la wanyama kama vile Wanyama wakubwa (Ngøombe na Punda), Wanyama wadogo (Mbuzi, Kondoo), Nguruwe na Jamii ya Ndege (Kuku na Bata). Mfano, kama baadhi ya Ngøombe wanaumwa ugonjwa wa kutupa mimba (Brucellosis) na baadhi wanaumwa homa ya mapafu (CBPP), mageresho yote 1 na 2 yanatakiwa kujazwa katika safuwima husika.

### Swali la 3: Je, uliwachanja [MNYAMA] wako katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?

Muulize mhojiwa kama [MNYAMA] amechanjwa. Kwa kila safu mlalo, andika geresho kulingana na maelezo katika dodoso. Kama [MNYAMA] wote walichanjwa jaza geresho →1 Iwapo walichanjwa baadhi ya [MNYAMA] jaza geresho →2 Kama walichanjwa wote au baadhi endelea na sawali linalofuata. Ikiwa hakuna wanyama waliochanjwa, andika geresho 3 kisha nenda swali la 6.

### Swali 4: Nani aliwapatia chanjo [MNYAMA] wako?

Onyesha nani aliwachanja (au kuwapatia chanjo) [MNYAMA], tumia mageresho yaliyorodheshwa kwenye dodoso. Kama mhojiwa kasema mtu/shirika/mtoya huduma amba hawapo kwenye orodha ya mageresho, andika 4 öPENGINE TAJAö na andika jina la mtoaji chanjo kwa maneno. Kama kaya ya mhojiwa ilipokea na iliweza kuwapatia chanjo yenye, orodhesha mtu/shirika lililotoa dawa ya chanjo.

### Swali la 5: Je, [MNYAMA] alipata chanjo ya magonjwa gani?

Muulize mhojiwa aina yachanjo ya ugonjwa aliyopewa [MNYAMA]. Andika mageresho yaliyorodheshwa katika dodoso, andika hadi majibu 2.

Ifuatayo ni orodha ya magonjwa makubwa ambayo chanjo zake zinapatikana, pamoja na maelezo ya kina ya magonjwa na maneno muhimu yapo katika jedwali lifuatalo:

- Ngøombe dume ni ambaye hajahasiwa anatumia kwa kuzalisha mbegu.
- Ngøombe jike ni ambaye amewahi kuzaa angalau mara moja.
- Maksai ni ngøombe dume aliyehasiwa mwenye umri zaidi ya mwaka mmoja.
- Mtamba ni ngøombe jike mwenye umri wa miaka kati ya mmoja na mitatu ambaye hajazaa.

JINA LA UGONJWA	MIFUGO INAYOATHIRIKA	DALILI ZA UGONJWA
Homa ya Mapafu (CBPP)	Ngøombe	Ngøombe hufa kwa wingi. Mnyama hupumua kwa shida na wakati mwingine hupanua miguu ya mbele. Hunyoosha shingo na kupumua kwa shida
Homa ya Mapafu kwa mbuzi (CCPP)	Mbuzi	Homa, Vifo hutokea kati ya siku 7 ó 10 baada ya kuonyesha dalili za ugonjwakupumua kwa shida
Mapelengozi (Lumpy Skin Disease)	Ngøombe	Homa ya muda mrefu, ngozi inakua na mapele kama majipu, ngozi kunyonyoka nywele.
Ndigana Kali (East Coast Fever)	Ngøombe	Homa kali inayofikia nyuzi joto 42 centigradi, Kutokwa na machozi mara kwa mara, kutopenda kutembea au kutafuta

		chakula,kuvimba matezi hasa chini ya masikio, kukohoa kidogo na kupumua kwa shida, kutoa mate mengi na povu puan na mdomoni, kuharisha katika hatua za mwisho
Ndigana baridi (Anaplasmosis)	Ngøombe	Joto la mwili kuongezeka, kupungukiwa na damu mwilini, kujikamua na kutoa choo kigumu, kwa ngombe wanaokamuliwa, utoaji wa maziwa kupungua, macho na utando wa mdomo kuwa mweupe au njano
Kichaa cha Mbwa (Rabies)	Wanyama wote wafugwao na binadamu	Mnyama kubadilika tabia, kuwa na hasira (kunguruma), kuuma ovyo, kubweka ovyo, kuogopa mwanga na kujificha, kuogopa maji, kutoa mate mdomoni, kuacha kula na mwisho mnyama huanguka chini na kufa
<b>JINA LA UGONJWA</b>	<b>MIFUGO INAYOATHIRIKA</b>	<b>DALILI ZA UGONJWA</b>
Ugonjwa wa Miguu na Midomo(FMD)	Ngøombe, kondoo, mbuzi, nguruwe na wanyama wengine wenye kwato	Homa, vidonda kwenye midomo, pua, miguu, chuchu. muzzle, kuchuruzika mate, kushindwa kula, vidonda mdomoni na kwenye kwato
Kimeta (Anthrax)	Wanyama wote wanaofugwa pamoja na Nyati	Homa kali , Mnyama anakufa ghafla, kutokwa na damu kwenye matundu yote ya mwilini.
Chambavu (BQ)	Ngombe	kupoteza hamu ya kula, kupumua kwa haraka, mnyama kuwa mnyonge na homa kali. Anavimba maeneo yenye nyama nyingi, bega, kifua, mgongo, shingo na maeneo mengine
Kideli / Mdondo (New castle Disease)	Kuku na jamii ya ndege	Kutokwa na ute mzito mdomoni Kushindwa kupumua, kuharisha mharo wa kijani, kupinda shingo,kushusha mabawa na vifo vingi
Gomboro (Gumboro)	Kuku	Huathiri kuku walio na umri chini ya wiki sita, vifaranga wanajikusanya na kushindwa kula, kuharisha na hatimaye kufa ghafla.
Minyoo(Helminthiosis)	Ngombe,Kondoo mbuzi, Nguruwe mbwa,kuku	Kupungua uzito na kupunguza kula chakula Manyoya kusimama hasa kwa wanyama wadogo kama vile ndama, upungufu wa damu, kuharisha, kujaa tumbo.kuku wanaotaga kupunguza utagaji
ASF (Homa yaNguruwe)	Nguruwe	Homa kali, wanyama hujikusanya pamoja wanashindwa kula, masikio na sehemu ya tumbo huwa nyekundu na baadaye kubadilika na kuwa rangi ya zambarau, kupumua kwa shida, kufa ngazi sehemu ya kiuno na baadaye kulemaa miguu ya nyuma hatimaye kushindwa kutembea, mimba kuharibika.

Nagana(Typanosomiasis)	Ng'ombe	Wanyama hukonda kwa muda mrefu, kukatika mkia, kuacha kula hatimaye kifo
Kuoza kwato (Foot Rot)	Wanyama wenge kwato	Kwato huoza na hatimaye wanyama kushindwa kutembea hivyo kushindwa kutafuta chakula.
Tetenasi (Tetanus)	Wanyama wote na binadamu	Joto la mwili hupanda, katika hatua za mwisho mnyama hupumua kwa shida, misuli hukaza na hatimaye hufa
Mabaka/mba katika ngozi (Mange)	Wanyama wote	Husababishwa na Wadudu wanaoishi kwenye <b>hair follicles</b> na hatimaye husababisha kunyonyoka manyoya na kusababisha mnyama kujikusugua kwenye miti na kusababisha mabaka kwenye ngozi
Upungufu wa damu (Anaemia)	Wanyama wote	Husababishwa na <b>parasite</b> (bacteria, protozoa na virusi) ambao hushambulia <b>red blood cells</b> na kunyonya damu au vimelea.
Surua ya mbwa (Canine Distemper)	Mbwa na paka	Homa kali, kupoteza hamu ya kula, kuharisha damu na mwisho kifo

## DAWA ZA MINYOO

**Swali la 6: Katika miezi 12 iliyopita umewahi kuwapa [MNYAMA] dawa za minyoo?**

Muulize mhojiwa kama alitumia dawa za minyoo kwa [MNYAMA]. Kama wanyama wote wamepewa dawa za minyoo, andika 1. Kwa kila safumlalo, nakili majibu kulingana na maelekezo katika dodoso. Kama baadhi ya [MNYAMA] wamepewa dawa za minyoo, andika 2. Kama wote au baadhi ya wanyama wamepewa dawa za minyoo endelea swali linalofuata. Kama hakuna wanyama waliopewa dawa za minyoo, andika 3 na nenda swali la 8

**Swali la 7: Ni nani aliwapatia [MNYAMA] dawa za minyoo?**

Onyesha nani aliwapatia (au alitoa) dawa za minyoo kwa [MNYAMA], tumia mageresho yaliyoorodheshwa kwenye dodoso. Kama mhojiwa ameordhesha mtoaji dawa ambaye hayupo katika orodha, andika 4 ōNYINGINE TAJAö na andika jina la mtoaji kwa maneno.

## KUPE

**Swali la 8: Katika kipindi cha miezi 12 iliyopita umewahi kuchukua hatua yoyote kwa [MNYAMA] kwa ajili ya kuzuia magonjwa yaenezwayo na kupe?**

Muulize mhojiwa kama wanyama wana/wamepata kinga zidi ya ugonjwa wa ndigana baridi. Kwa kila safu mlalo, andika majibu kulingana na maelekezo katika dodoso. Kama wanyama wote wana kinga, andika 1, kama baadhi tu ya wanyama wana kinga, andika 2. Kama hakuna wanyama wenye kinga, andika 3 na nenda swali la 10.

**Swali la 9: Ni hatua gani ulichukua kwa ajili ya kinga ya [MNYAMA]?**

Muulize mhojiwa kuhusu hatua alizochukua kuwakinga wanyama zidi ya ugonjwa wa ndigana baridi. Kwa kila safumlalo, nakili majibu kulingana na maelekezo katika dodoso. Kama kuwazamisha kwenye joshio, geresho 1, kwa kuwapulizia (dawa) geresho 2 na kwa hatua nyininge, andika 3 na utaje.

**Swali la 10: Je, katika miezi 12 iliyopita umewahi kuwapatia [WANYAMA] tiba dhidi ya magonjwa yaenezwayo na kupe?**

Muulize mhojiwa kama aliwapatia [MNYAMA] tiba dhidi ya magonjwa yaenezwayo na kupe.Kama [MNYAMA] wote wamepatiwa tiba dhidi ya magonjwa yaenezwayo na kupe, andika 1. Kwa kila safumlalo, nakili majibu kulingana na maelekezo katika dodoso, kama vile baadhi ya [MNYAMA] wamepatiwa tiba, andika 2.Kama wote au baadhi wamepatiwa tiba, endelea na swali linalofuata.Kama hakuna wanyama waliopatiwa tiba, andika 3 na nenda swali la 12.

**Swlila 11: Ni nani aliwapatia [MNYAMA] tiba dhidi ya magonjwa yaenezwayo na kupe?**

Onyesha nani aliwapatia (au alitoa) tiba dhidi ya magonjwa yaenezwayo na kupe kwa [MNYAMA], tumia mageresho yaliyoorodheshwa kwenye dodoso. Kama mhojiwa ameorodhesha mtoaji tiba ambaye hayupo katika orodha, andika 4 ðNYINGINE TAJAö na andika jina la mtoaji kwa maneno.

## **MATIBABU YA MAGONJWA MENGINE ZAIDI YAKUPE**

**Swali la 12: Je, katika miezi 12 iliyopita [MNYAMA] wako walipatiwa tiba?**

Muulize mhojiwa kama tiba yoyote ilitolewa kwa [MNYAMA]. Kwa kila safumlalo, nakili majibu kulingana na maelekezo katika dodoso, kama vile [MNYAMA] wote wamepatiwa tiba, andika 1. Kama baadhi ya [MNYAMA] wamepatiwa tiba, andika 2. Kama wote au baadhi ya wanyama wamepatiwa tiba, endelea na swali linalofuata. Kama hakuna wanyama waliopatiwa tiba, andika 3 na nenda swali la 14.

**Swali la 13: Ni nani aliwapatia [MNYAMA] wako tiba hiyo?**

Onyesha nani aliwapatia (au alitoa) tiba [MNYAMA], tumia mageresho yaliyoorodheshwa kwenye dodoso. Kama mhojiwa ameorodhesha mtoaji tiba ambaye hayupo katika orodha, andika 4 ðNYINGINE TAJAö na andika jina la mtoaji kwa maneno.

## **MATUMIZI**

**Swali la 14: Je, kwa ujumla ultumia kiasi gani katika chanjo, kinga, matibabu na gharama zingine za kitabibu katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa kukadiria jumla ya gharama zinazohusiana na afya ya mnyama, jumuisha malipo ya huduma iliyotolewa, gharama ya madawa, chanjo na gharama nyinginezo. Andika jibu katika shilingi ya Tanzania. Kama malipo yamefanyika kwa njia ya vitu, muulize mhojiwa athaminishe malipo hayo kwa njia ya vitu katika shilingi na andika kwenye dodoso.

## **Sehemu 4: Chakula cha Mifugo, Maji, Makazi na Uzalishaji**

Kumbuka: Maswali katika sehemu hii (Swali la 1-11) yanauliza kwa makundi ya wanyama kama vile Wanyama wakubwa (Ng'ombe na Punda), Wanyama wadogo (Mbuzi, Kondoo), Nguruwe na Jamii ya ndege (Kuku na Bata), na sio mnyama mmoja mmoja.Tumia flap kuhakikisha kwamba kaya inamiliki aina hiyo ya wanyama.

## **VYAKULA VYA MIFUGO**

**Swali la 1: Je, ni njia gani kuu ya ulishaji wa [MNYAMA] katika kaya hii katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa akutajie njia kuu ya ulishaji [MNYAMA]. Tumia mageresho yaliyoorodheshwa, kuonyesha hadi njia kuu 2 za ulishaji wa [MNYAMA]. Angalau njia moja na idadi ya juu ni njia mbili za ulishaji zinazotakiwa kuandikwa.

**Swali la 2: Je, mliwahi kununua chakula cha mifugo kwa ajili ya [MNYAMA] katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa kama chakula chochote cha mifugo kilinunuliwa kwa ajili ya [MNYAMA]. Kama hapana, geresho 2, na nenda swali la 5. Kama ndiyo, geresho 1 na endelea na swali linalofuata.

**Swali la 3: Ni miezi ipi mnanunua chakula cha mifugo katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Kila herufi inawakilisha mwezi katika mwaka. Zungushia herufi kwa kila mwezi ambao chakula cha mifugo kilinunuliwa katika miezi 12 iliyopita.

**Swali la 4: Je, ni kiasi gani kaya hii imelipa kwa ajili ya kulisha [MNYAMA] katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa kukadiria kiasi cha fedha kilichotumika kulisha mnyama katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Andika majibu katika shilingi. Hii ni jumla ya fedha kwa kipindi cha miezi 12.

## **MAJI**

**Swali la 5: Ni mara ngapi, kwa wastani, kwa siku kaya hii imewapa maji [MNYAMA] katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa kuonyesha ni mara ngapi kwa wastani, kwa siku aliwapa maji {MNYAMA}. Andika majibu kulingana na mageresho yaliyoorodheshwa kwenye dodoso. Kama wanyama wanafata maji wenyewe kutoka vyanzo vilivypo, andika 1 na nenda swali la 11.

**Swali 6: Je, nini kimekuwa chanzo kikuu cha maji kwa ajili ya [MNYAMA] katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa akutajie chanzo kikuu cha maji kwa ajili ya [MNYAMA]. Tumia mageresho yaliyoorodheshwa kuandika jibu. Kama kaya inatumia maji kutoka chanzo zaidi ya kimoja (vyanzo mbali mbali), andika chanzo kikuu na chanzo cha pili kilichofuatia katika majibu. Andika angalau chanzo kimoja (Isipokuwa kama kaya ilijibu geresho 1 katika swali la 5

**Swali la 7: Je, kaya hii imewahi kulipia maji kwa ajili ya [MNYAMA] katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa kama kuna malipo yoyote yaliyolipwa ili [MNYAMA] wawezi kuputa maji au kama maji yalinunuliwa kwa ajili ya [MNYAMA]. Kama hapana, andika 2, na nenda swali la 10. Kama ndiyo, andika 1 na nenda swali linalofuata.

**Swali la 9: Ni kiasi gani kaya hii imelipa kwa ajili ya kupata maji kutoka vyanzo vikuu kwa ajili ya [MNYAMA] katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa kukadiria kiasi cha fedha kilicholipwa kwa ajili ya kupata maji ya [MNYAMA] kutoka chanzo kikuu. Kama kaya ilifanya malipo kwa njia ya vitu, muulize mhojiwa akadirie/athaminishe thamani

ya soko kwa wakati huo kwa malipo hayo kwa njia ya vitu na andika jibu katika shilingi ya Tanzania. Hii ni jumla ya fedha kwa kipindi cha miezi 12.

## MAKAZI

**Swali la 11: Ni njia gani kuu ya kutunzia [MNYAMA] kaya hii imetumia katika miezi 12 iliyopita?**

Tumia mageresho yaliyooodheshwa kwenye dodoso kuonyesha njia inayotumika na kaya kutunzia [MNYAMA]. Andika 1 kama hakuna njia iliyotumika kutunzia wanyama au [MNYAMA] asiyefungwa (aliyearchiwa huru).

## UZALISHAJI

**Swali 12: Je, kaya hii imefanya njia zozote maalumu za kupandisha wanyama au njia nyingine za uzalishaji wa [WANYAMA] miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa kama kaya ilitumia njia ya kupandisha wanyama. Kama hakuna njia ya kupandisha wanyama iliyotumika, andika 2, na nenda mstari unaofuata.

**Swali 13: Ni nini imekuwa njia kuu ya kupandishia wanyama au njia nyinginezo zilizotumiwa na kaya hii kwa ajili ya [WANYAMA] miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa akutajie njia kuu ya kupandishia wanyama au njia nyinginezo za uzalishaji kwa [MNYAMA]. Tumia mageresho yaliyooodheshwa katika dodoso kuandika jibu. Kama kaya imetumia njia zaidi ya moja, orodhesha njia kuu mbili.

Lifuatalo ni jedwali pamoja na orodha ya maelezo ya kila aina ya njia ya upandishaji (uzalishaji) wa mifugo:

NAMBA	AINA YA UZALISHAJI	MAELEZO
1	<b>Hakuna</b>	Hakuna njia maalum ya upandishaji (uzalishaji) wanyama inayofuatwa. Wanyama wanaruhusiwa kupandana kwa wakati wao.
2	<b>Upandishaji (Uzalishaji) wa njia ya asili, dume lililochaguliwa kutoka ndani ya.</b>	Upandishaji wa wanyama kiasili kwa dume maalum lililochaguliwa kutoka kundini kwa ajili ya upandishaji/uzalishaji.
3	<b>Upandishaji (Uzalishaji) wa njia ya asili, kwa Ununuaji wa dume.</b>	Upandishaji wa wanyama kiasili kwa dume maalum lililonunuliwa kwa ajili ya upandishaji/uzalishaji.
4	<b>Upandishaji (Uzalishaji) wa njia ya asili, kwa Kubadilishana dume.</b>	Upandishaji wa wanyama kiasili kwa dume maalum kwa kubadilishana na kaya nyingine kwa ajili ya upandishaji/uzalishaji.
5	<b>Uhamilishaji</b>	Njia ya kuweka mbegu kutoka kwa dume la [MNYAMA] katika sehemu za uzazi wa jike la [MNYAMA] kwa njia za kisayansi zaidi ya zile za kupandisha kiasili.
6	<b>Jike la Ng'ombe lililonunuliwa</b>	Upandishaji wa wanyama kiasili kwa ng'ombe jike maalum lililonunuliwa. Kwa ajili ya upandishaji/uzalishaji.
7	<b>Jike la ng'ombe la kubadilishana</b>	Upandishaji wa wanyama kiasili kwa ng'ombe jike maalum kwa kubadilishana na kaya nyingine kwa ajili ya upandishaji/uzalishaji.
8	<b>Madume yaliyohasiwa.</b>	Madume ambayo hayatakiwi katika upandishaji/uzalishaji, wanahasiwa ili kuwazua katika upandishaji.

# Sehemu ya 5: Nguvukazi kwa Wanyama

---

Angalizo: Sehemu hii inauliza maswali kuhusu kundi la Wanyama wakubwa kama (ng'ombe na pack animals), wanyama wadogo (Mbuzi, kondoo), Nguruwe, na ndege(Kuku na Bata) na siyo kila mnyama. Tumia karatasi ya kukunja (flap) ya wanyama kuhakikisha kuwa kaya inamiliki aina hii ya wanyama.

## Swali la 1: Kimsingi, nani anawajibika kutunza/kuangalia [MNYAMA] hawa?

Muulize mhojiwa idadi ya wanakaya ambao kimsingi wanawajibika kutunza kila aina ya mnyama. Katika sehemu hii tunazingatia zaidi kwa wanakaya ambao wanatumia muda wao mwingi zaidi ya wengine kutunza wanyama ( na sio wale wanatoa maamuzi juu ya mauzo au mapato, ambao tutakutana nao sehemu nyininge). Kama kuna wanakaya wengi walishiriki swali hili linataka uorodheshe wawili tu ambao walitumia muda mwingi zaidi ya wengine kutunza [MNYAMA]. Maswali yanayofuata yatauliza kuhusu muda uliotumika kwenye kazi husika. Tumia namba za wanakaya mpaka wawili kutoka kwenye orodha ya wanakaya kulingana na umuhimu wao.

## Swali la 2: Nani katika kaya yako alitumia muda wake mwingi kulisha/kunywesha [MNYAMA]?

Tumia namba za wanakaya kuorodhesha wanakaya hadi wawili walioshiriki katika kulisha/kunywesha [MNYAMA] kulingana na umuhimu wao.

## Swali la 3: Nani katika kaya yako alitumia muda wake mwingi kuuza wanyama na mazao/bidhaa yatokanayo na wanyama?

Tumia namba za wanakaya kuorodhesha wanakaya walitumia nguvu/muda wao mwingi katika kuuza mnyama au mazao ya mnyama. Orodhesha wanakaya hadi wawili kulingana na umuhimu wao.

## Swali la 4: Ni nani katika kaya yako, alitumia muda mwingi kwa ajili ya kuchunga [MNYAMA]?

Tumia namba za wanakaya kuorodhesha wanakaya waliochunga wanyama. Orodhesha wanakaya hadi wawili kulingana na umuhimu wao. Kwa mnyama ambaye hachungwi mfano, kuku, bata, sungura, n.k andika 99.

## Swali la 5: Je, mliajiri mtu wa kusaidia kutunza [MNYAMA] katika miezi 12 iliyopita?

Lengo la swali hili ni kuuliza iwapo mhojiwa aliajiri vibarua kutoka nje ya kaya kwa ajili ya kutunza [MNYAMA] katika miezi 12 iliyopita. Jumuisha vibarua waliolipwa fedha na wale waliolipwa kwa vitu (inkind). Iwapo kuna vibarua walijiriwa, jaza geresho 1 kisha endelea Swali linalofuata. Kama hakuna kibarua aliyeajiliwa jaza geresho la 2 na kwenda kwenye kundi la wanyama wengine.

## Swali la 7: Gharama ya kazi hiyo kwa kipindi cha miezi 12 iliyopita ni kiasi gani?

Andika kiasi cha fedha kilichotumika kumlipa mtu uliyemuajiri kutoka nje ya kaya ambaye alisaidia kutunza kila aina ya mnyama. Kiasi cha fedha kiandikwe katika shilingi, kwa hiyo thamani ya malipo ya vitu yakadirie katika shilingi. Hii ni jumla kwa kipindi cha miezi 12.

# Sehemu ya 6: Maziwa

---

Angalizo: Sehemu hii inauliza maswali kuhusu kundi la Wanyama wakubwa kama (ng'ombe) na Wanyama wadogo (Mbuzi, kondoo). Hakikisha kuwa majibu ya mhojiwa yanajumuisha wanyama wote kwenye kundi

la wanyama wakubwa na wanyama wadogo. Tumia karatasi ya kukunja(flap) ya wanyama kuhakikisha kuwa kaya inamili aina hii ya wanyama.

**Swali la 1: Ni [WANYAMA] wangapi walikamuliwa maziwa miezi 12 iliyopita?**

Muombe mhojiwa ajumuise wanyama wote waliokamuliwa, jumuisha hata wale ambao walikamuliwa masaa ambayo si ya kukamua katika mahesabu ya mwisho. Kama hakuna [MNYAMA] aliyekamuliwa, andika 0, nenda mstari unaofuata.

**Swali la 2: Kwa wastani ni miezi mingapi mlikamua maziwa [WANYAMA]?**

Andika namba ya miezi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita ambapo kila aina ya mnyama aliyekamuliwa.

**Swali la 3: Je, kwa wastani mlizalisha maziwa kiasi gani kwa siku kwa [MNYAMA] aliyekamuliwa katika kipindi hiki?**

Muombe mhojiwa akadirie wastani wa maziwa yaliyokamuliwa kwa kila aina ya mnyama kwa siku. Mfano, kama Mbuzi na Kondoo wanazalisha kiwango tofauti cha maziwa kwa siku, kadiria wastani wa maziwa yaliyokamuliwa kwa wote kwa kuangalia idadi ya wanyama wa kila kundi. Katika mazingira fulani hili linaweza kuwa na utata/gumu (kama kaya inamili na kukamua kondoo na mbuzi). Ukiangalia taarifa za tafiti zilizopita hali hii inatakiwa kujitokeza kwa kiwango kidogo sana, inatakiwa kumdodosa mhojiwa kwa kadri ya uwezo wako ili kupata taarifa/madirio yaliyo sahihi.

**Swali la 4: Katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, ni mwezi upi uzalishaji wa maziwa kwa mnyama ulikuwa mkubwa?**

Kwa miezi ambayo kila mnyama alikamuliwa, mhojiwa anatakiwa akutajie mwezi ambapo uzalishaji wa maziwa ulikuwa mkubwa. Pia mhojiwa anatakiwa akutajie kiwango cha maziwa kilichozalizwa kwa **siku** katika **lita** na kwa **kila mnyama** katika mwezi huo.

**Swali la 5: Katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, ni mwezi upi uzalishaji wa maziwa kwa mnyama ulikuwa mdogo sana?**

Kwa miezi ambayo kila mnyama alikamuliwa, mhojiwa anatakiwa akutajie mwezi ambapo uzalishaji wa maziwa ulikuwa kwa kiwango kidogo. Pia mhojiwa anatakiwa akutajie kiwango cha maziwa kilichozalizwa kwa **siku** katika **lita** na kwa **kila mnyama** katika mwezi huo.

**Swali la 6: Kwa ujumla, [WANYAMA] walikuwa wananyonyesha wakati mlipokuwa mnakamua maziwa?**

Muulize mhojiwa endapo wanyama waliozaliwa walinyonyeshwa kipindi ambacho [MNYAMA] anakamuliwa. Kama hakuzuiliwa kunyonya/alinyonyeshwa sana, andika 2, kama alinyonyweshwa kiasi andika 1

**Swali la 7: Katikaki pindi cha miezi 12 iliyopita, ni kiasi gani cha maziwa kilichozalishwa na [MNYAMA] kilitumiwa na kaya kila siku yakiwa katika hali ya kimiminika (freshi)?**

Swali hili linauliza kuhusu maziwa yaliyozalishwa kwa kila kundi la mnyama na kutumiwa na wanakaya. Mdadisi mhojiwa ili uweze kupata makadirio ya maziwa yaliyotumiwa mojakwamoja na wanakaya yakiwa katika hali ya kimiminika tu. Andika jibu katika lita kwa siku. Usijumuise maziwa yaliyotoka/kuzalishwa nje ya kaya wala maziwa yaliyosindikwa.

**Swali la 8: Katika kipindi hiki, uliuza kiasi cha lita za maziwa zilizouzwa kwa siku zilizozalishwa na [MNYAMA]?**

Muulize mhojiwa akadirie kiwango cha maziwa katika hali ya kimiminika kilichouzwa kwa kila kundi la wanyama. Andika jibu katika lita kwa siku. Swali hili linauliza kuhusu yale maziwa yaliyozalishwa na kaya

na ambayo taarifa zake zimetolewa swali la 3. Kiasi kwa swali hili hakipaswi kuwa kikubwa kuliko kiasi katika swali la 3. Ikiwa kaya iliuzi maziwa ambayo hayakuzalishwa na wanyama wao, hapo jaza -0ø kwa swali hili.

**Swali la 9: Katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, ni kiasi gani cha maziwa kilisindikwa kila siku?**

Swali hili linamtaka mhojiwa akadirie kiwango cha mazima kilichosindikwa na kupata vitu kama samli, jibini au mtindi, kwa kila mnyama. Jumuisha maziwa yaliyosindikwa kwa ajili ya matumizi ya kaya pamoja na yaliyosindikwa kwa ajili ya kuuza. Andika jibu katika lita kwa siku. Kiasi kwa swali hili hakipaswi kuwa kikubwa kuliko kiasi katika swali la 3. Ikiwa kaya ilisindika maziwa ambayo hayakuzalishwa na wanyama wao hapo jaza -0ø. Kama maziwa hayakusindikwa, andika 0 na nenda swali la 11.

*Angalizo: Mdadisi anatakiwa kuhakiki kama kiwango cha maziwa kilichozalishwa(swali la 3) ni kikubwa au ni sawa na maziwa yakiwa katika hali ya kimiminika yaliyotumiwa na kaya (swali la 7) + maziwa ya kimiminika yaliyouzwa (swali la 8) + maziwa yaliyosindikwa(swali la 9). Swali la 3 linatakiwa kuwa kubwa kuliko swali la 7 + swali la 8 + swali la 9.*

**Swali la 10: Ni kiasi gani cha maziwa yaliyosindikwa kiliuzwa kwa siku?**

Swali hili linamtaka mhojiwa akadirie kiwango cha maziwa yaliyosindikwa kilichouzwa kwa kila kundi la wanyama. Andika jibu katika lita kwa siku.

**Swali la 11: Kwa wastani ulipata kiasi gani kwa siku kwa kuza maziwa/maziwa yaliyosindikwa?**

Muulize wastani wa mapato kutokana na maziwa kwa siku kwa kila kundi la mnyama. Mdadisi zaidi na akutajie wastani wa mapato kwa siku ambazo aliuza maziwa. Andika mapato katika shilingi kwa siku.

**Swali la 12: Uliuza wapi sehemu kubwa ya maziwa/maziwa yaliyosindikwa kutoka kwa [MNYAMA]?**  
Mhojiwa anatakikiwa kueleza ni wapi anapouzia maziwa kutokana na [MNYAMA]. Tumia mageresho kutoka kwenye Orodha ya watoa huduma katika dodoso la mifugo na uvuvi, orodhesha mpaka 2 ambao waliuziwa maziwa kwa kiasi kikubwa kwa kila kundi la wanyama .Ikiwa kaya haikuza maziwa yoyote au kusindika, andika -99ø

**Swali la 13: Ni nani katika kaya mwenye maamuzi juu ya matumizi ya mapato hayo?**

Muulize ni nani anatoa maamuzi ya matumizi ya mapato kutokana na uuzaji wa maziwa kwa kutofautisha kila kundi la wanyama. Tumia namba za wanakaya kutoka kwenye orodha ya wanakaya orodhesha mpaka 2 kulingana na umuhimu wao.

**Angalia mfano huu:** Endapo mkuu wa kaya ana namba 01 and mke wake ana namba 02. Kama maamuzi ya matumizi ya mapato wanafanya kwa pamoja yaani mkuu wa kaya na mke wake, utatumia namba 01 na 02. Kama maamuzi yanafanya na mkuu wa kaya mwenyewe au mke mwenyewe, andika namba 01 au 02. Ikiwa mwanakaya mwagine anafanya maamuzi, tumia namba zao kama zilivyoorodhewa kwenye orodha ya wanakaya.

## **Sehemu ya 7: Wanyama Kazi na Kinyesi cha Wanyama**

---

**Zingatia:** Maswali ya sehemu hii yanaulizia kundi la wanyama na si kwa mnyama mmoja mmoja mfano; kundi la wanyama wakubwa (ng'ombe na Pack animals), kundi la wanyama wadogo (mbuzi na kondoo), nguruwe na wanyama jamii ya ndege (kuku na bata). Punda wanahusika katika katika sehemu hii, tumia #flapø ya wanyama kujua kama kaya inamiliki aina hii ya wanyama.

**Swali la 1: Je, kaya hii imefanya matumizi ya kinyesi kilichoalishwa na [WANYAMA] ktika kipindi cha miezi 12 iliyopita?** Uliza kama kaya ilitumia kinyesi cha wanyama. Ikiwa hakuna kinyesi kilichotumika jaza ≈2Ø na nenda swali la 5.

**Swali la 2: Ni aina gani ya matumizi ya kinyesi cha [WANYAMA] yaliyofanyika katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?** Muulize mhojiwa, akutajie matumizi makuu mawili ya mbolea iliyozalishwa na kundi la wanyama, jaza jibu kulingana na majibu yaliyopo kwenye dodoso. Kama mhojiwa atakutajia aina ya matumizi ambayo hayajaorodheshwa kwenye dodoso andika geresho ≈6Ø na andika aina hiyo kwa maneno. Andika mpaka matumizi mawili, kama mhojiwa aliuza kinyesi, andika 5 kisha nenda swali la 3, na kwa majibu yote nenda swali la 4.

**Swali la 3: Nini thamani ya mauzo ya kinyesi cha [MNYAMA] katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?** Muombe mhojiwa akadirie thamani ya mauzo ya kinyesi. Kama kaya ilipokea malipo kwa njia ya kitu/vitu ≈in-kindØ muombe akadirie kitu hicho katikathamani ya soko na andika jibu katika shilingi ya kitanzania.

**Swali la 4: Ni kiasi gani cha kinyesi kilichoalishwa na [WANYAMA] katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?** Muulize mhojiwa akupe makadirio ya kinyesi kilichoalishwa kwa kila kundi la wanyama kwa mwezi. Kama kinyesi kinapimwa kwa kilogramu, andika 1, kama kinapimwa kwa lita andika 2.

**Swali la 5: Je, kaya hii imewahi kutumia [WANYAMA] wake wowote kwa ajili ya usafiri wa kaya (kwa watu, mazao n.k.) katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?** Muulize mhojiwa kujua kama kaya ilitumia mnyama yeyote kwaajili ya usafiri. Usafirishaji unajumuisha watu, usafirishaji wa mazao na bidhaa nyingine.

**Swali la 6: Je, kaya hii imewahi kuwatumia [WANYAMA] wake kwa kulimia shamba la kaya katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?** Muulize mhojiwa kujua kama kaya ilitumia mnyama yoyote kulima shamaba la kaya. Thibitisha hili kwakuangalia sehemu za kilimo (Dodoso la Kilimo) kujua kama kaya ililima shamba lolote, dadisi zaidi kama itawezekana. Usihushe wanyama walioazimwa kwa watu wengine kwa ajili ya kulimia, zingatia kwamba kuna baadhi ya sehemu zimebekwa kimvuli, usijaze kitu chochote katika sehemu hizi.

## **Sehemu ya 8: Bidhaa/Mazao Mengine Yatokanayo na Wanyama**

---

Sehemu hii inaulizia bidhaa/mazao yanayotokana na aina mbalimbali ya wanyama wanaofugwa. Kwakuwa kuna bidhaa mbalimbali zinazoweza kuzalishwa na wanyama, na zinaweza kutofautiana mkoa hadi mkoa,

bidhaa nyingi zinaweza zisiwepo kwenye orodha, safu mlalo ya 3 ipo kwa ajili ya kuorodhesha bidhaa ambayo haipo kwenye orodha, andika kwa maneno na endelea na maswali. Sehemu hii iorodheshe uzalishaji wa bidhaa nyingine tofauti na maziwa, nyama, ambazo zimeshaandikwa kwenye sehemu zilizopita. Sehemu hii inatakiwa kuhusisha uzalishaji unaotokana na wanyama wa kaya: Kama kaya huwa inanunua mfano, ngozi au asali na inauza (ikiwa hivyo hivyo au baada ya kutengeneza bidhaa nyingine) shughuli hizi ziandikwe kwenye sehemu ya biashara ya kaya.

**Swali la 1: Je, mlizalisha [BIDHAA] kutoka mifugo yenu katika miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa kila bidhaa iliyoorodhesha kujua kama kaya ilizalisha.

**Swali la 2: Katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, miezi mingapi mlizalisha [BIDHAA]?** Swali linauliza kujua ni miezi mingapi katika mwaka kaya ilizalisha bidhaa. Mfano kama kuku walitaga mayai kwa miezi 8 kati ya miezi 12, jibu la swali hili litakuwa miezi 8. Au kama kaya ilitumia miezi miwili katika mwaka kushuhulika na ngozi na kwato, jibu litakuwa 2.

**Swali la 3: Kwa wastani ni kiasi gani cha [BIDHAA] mlizalisha kwa mwezi?**

Swali hili linafanya makadirio ya uzalishaji kwa mwezi, vipimo hivi viwe katika vipimo (kama lita au kilogram), na si katika vipimo vya kiasili/kienyeji, zingatia kwamba kuna kipimo kimeandikwa  $\frac{1}{2}$ kipande $\frac{1}{2}$ . Hii itumike tu pale ambapo ni lazima. Mfano; kaya ilizalisha ngozi 6 (au vipande 6), lakini haiwezi kuzalisha vipande 6 vya asali, vitu vya kimiminika viandikwe katika lita.

**Swali la 4: Je, mliuza [BIDHAA] mliyozalisha katika miezi 12 iliyopita?**

Andika 1 kama kaya iliuzwa bidhaa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, andika 2 kama hakuna bidhaa iliyouzwa na nenda safu mlalo inayofuata.

**Swali la 5: Kiasi gani cha [BIDHAA] mliyozalisha kiliuzwa katika miezi 12 iliyopita?**

Swali hili linafanya makadirio ya bidhaa zilizouzwa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Vipimo hivi viwe katika vipimo (kama lita au kilogram), na si katika vipimo vya kiasili/kienyeji, zingatia kwamba kuna kipimo kimeandikwa  $\frac{1}{2}$ kipande $\frac{1}{2}$ . Hii itumike tu pale ambapo ni lazima. Mfano: kaya ilizalisha ngozi 6 (au vipande 6), lakini haiwezi kuzalisha vipande 6 vya asali, vitu vya kimiminika viandikwe katika lita. Kwa kufuata kanuni, unatakiwa/shauriwa kujaribu kutumia vipimo hivyo hivyo viliviyotumika katika swali la 3 kama itawezekana.

**Swali la 6: [BIDHAA] mlizozalisha kwa miezi 12 iliyopita ziliwu na thamani gani?**

Muulize mhojiwa thamani ya jumla ya mauzo ya kila bidhaa katika kipindi cha miezi 12.Thamani hii iandikwe katika shilingi.

**Swali la 7: Mliuza wapi sehemu kubwa ya [BIDHAA]?**

Muulize mhojiwa, nani walimuuzia kiasi kikubwa cha bidhaa. Tumia orodha ya watoa huduma iliyopo kwenye dodoso la mifugo na uvuvi, orodhesha mpaka watoa huduma wawili kwa kuzingatia umuhimu wake.

**Swali la 8: Nani katika kaya aliamua juu ya matumizi ya haya mapato?**

Swali hili muulize mhojiwa kujua nani huwa anafanya maamuzi juu ya matumizi ya mapato ya yatokanayo na mauzo ya bidhaa. Kumbuka kwamba baadhi ya bidhaa zinaweza kuuzwa na mwanakaya mmoja na wanakaya wengine wakaamua nini kifanyike kwa kilichopatikana. Unatakiwa kutumia mageresho yaliyoorodhesha kwenye geresho la kaya. Kuna baadhi ya kaya maamuzi hufanywa kwa pammoja, mkuu wa kaya na mwenza (hivyo utatumia geresho 01, na 02), baadhi ya maamuzi hufanywa na mmoja tu anaweza kuwa mkuu wa kaya (01) au mwenza (02) au hufanywa na mwanakaya mwengine, tumia mageresho kwa kadiri itakavyohitajika.

**Swali la 9: JE, KUNA MWANAKAYA YEYOTE ALIYEJISHUGHULISHA NA UVUVI,  
BIASHARA YA SAMAKI, AU USINDIKAJI WA SAMAKI KATIKA KIPINDI CHA MIEZI 12  
ILIYOPITA?**

Usiulize swali hili kwa mhojiwa. Swali hii litakufahamisha kama kaya itahitaji kuulizwa dodoso la uvuvi. Rejea swali la 23 katika sehemu A kujua kama kaya ilijihuisha na uvuvi, biashara ya uvuvi au uandaaji wa samaki katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Kama jibu ni **ENDIYOØ** endelea na sehemu 9-13. Kama **HAPANAØ** dodoso la mifugo na uvuvi litakuwa limekwisha na hivyo itakupasa kujaza muda wa kumaliza dodoso kwenye kisanduku cha muda.

## **Sehemu 9-13: Uvuvu**

---

Sehemu ya 9-12 inahusiana na shughuli za uvuvi. Kaya ambazo zilijihuisha katika shughuli za uvuvi wa aina yoyote au kufanya biashara ya samaki katika miezi 12 iliyopita zilizotambuliwa katika sehemu **U-2Ø** (Swali 9) katika dodoso la kaya, ni **LAZIMA** zihojiwe katika dodoso la mifugo/uvuvi.

Unahitaji Orodha Kamili ya Wanakaya (Sehemu **BØ**) ili uweze kukamilisha dodoso la mifugoUvuvu

## **Sehemu ya 9: Wanakaya Walioshiriki Katika Uvuvu**

---

Orodhesha kila mwanakaya aliyejihuisha katika shughuli zinazohusiana na uvuvi (kuvua samaki, kuandaa samaki, au biashara ya samaki) katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Katika sehemu hii uliza maswali yote kwa mstari (1 ó 4) maliza mstari wa 1 kabla yakwenda mstari wa 2.

**Swali 1: Katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, ni mezi mingapi wewe au mwanakaya ye yote alijihuisha na uvuvi, biashara ya samaki au shughuli za uandaaji wa samaki?**

Mhojiwa anatakiwa akadirie kiasi cha miezi ambayo mwanakaya ye yote alitumia katika uvuvi, biashara ya samaki au shughuli za uandaaji wa samaki. Andika jumla ya miezi ambayo shughuli za uvuvi, biashara ya samaki au shughuli za uandaaji wa samaki zilifanyika kama ilivyokuwa kwenye dodoso la kaya. **Mfano:** ikiwa mwanakaya alivua kwa miezi 4, na pia aliuza samaki waliovuliwa na wenginekwa kwa muda wa miezi 2, jibu lake litakuwa ni miezi 6. **Angalizo:** *Jibu lake halitakiwi kuwa zaidi miezi 12.*

**Maelezo ya Swali 2.** Maswali haya yanafanana na yale ya sehemu ya wafanyakazi katika dodoso la Kaya kwa ajili ya kukadiria kiasi cha muda ambacho mwanakaya hutumia katika shughuli za uvuvi. Unapaswa utumie akili/ufahamu na utumie mbinu za kudadisi makadirio kuhakikisha mhojiwa anaelewa swali vizuri. Kwa mfano, kama mhojiwa ameonyesha kwamba alifanya shughuli za uvuvi kwa miezi 5, haiwezekani mwanakaya akafanya kazi wiki 50 katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Kwa kutumia njia za kuhakiki makadirio haya, unaweza kukusanya taarifa sahihi kwa kuhakikisha mhojiwa anaelewa vizuri. Angalia kama kila mwanakaya aliyeorodheshwa katika sehemu hii muda anaotumia, awe ameshiriki muda wote au kwa muda mchache katika uvuvi.

**Swali la 2: Ni wiki ngapi kwa jumla (JINA) alikuwa mvuvi wa muda wote katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

**Wakati wa wiki hizo, kadiria ni siku ngapi kwa wiki (JINA) alivua?**

**Katika siku hizo, kadiria (JINA) alitumia masaa mangapi kwa siku kuvua?**

Muulize muhojiwa kwa wastani idadi ya WIKI, idadi ya SIKU KATIKA WIKI na idadi ya MASAA KWA SIKU mwanakaya amefanya kazi za uvuvi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Andika idadi ya wiki, idadi ya siku katika wiki mmoja, na idadi ya masaa katika siku moja kwa kawaida mwanakaya alifanya. Andika sifuri katika safu wima zote kama(JINA) hakuvua katika kipindi hicho na uliza swali linalofuata.

**Maswali ya 3 – 4.** Maana ya *uandaaji* wa samaki na *biashara* ya samaki imeandikwa kwenye dodoso na inapaswa mhojiwa kuelezwu kabla ya kujibu swali hili. Kitu mhimu kinachotofautisha maana hizi ni kuwa uandaaji wa samaki unahusu samaki waliovuliwa moja kwa moja na wanakaya na biashara ya samaki inahusu samaki waliovuliwa na watu nje ya kaya lakini huuzwa na wanakaya. Kumbuka kaya inaweza kujihusisha na shughuli zote hizi kama, kwa **mfano**: wanakaya wana sehemu sokoni na wanaauza samaki waliovuliwa na kaya na waliovuliwa na watu wengine nje ya kaya.

**Swali la 3: Ni wiki ngapi kwa ujumla (JINA) alishiriki katika utayarishaji wa samaki katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Katika wiki hizo, kadiria ni siku ngapi kwa wiki (JINA) alitayarisha samaki? Katika siku hizo, kadiria (JINA) alitumia masaa mangapi kutayarisha samaki?

Muulize muhojiwa kwa wastani idadi ya WIKI, idadi ya SIKU KATIKA WIKI na idadi ya MASAA KWA SIKU mwanakaya alizoshiriki kwenye utayarishaji wa samaki katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Andika idadi ya wiki, idadi ya siku katika wiki mmoja, na idadi ya masaa katika siku mmoja kwa kawaida mwanakaya ameshiriki katika utayarishaji wa samaki. Angalia, utayarishaji wa samaki unaweza kuelezwu kuwa ni kuuza samaki moja kwa moja kwa watumiaji/walaji au kwa wachuuzi wa samaki (i) samaki mbichi aliyevuliwa na kaya na (ii) samaki aliyetayarishwa na kuvuliwa na kaya, ambao wanaweza kuwa wamepitishwa katika njia kama kukaushwa kwa moshi, juu au kwa chumvi. Andika  $\text{f}0\phi$  katika safu wima zote kama (JINA) hakushiriki katika utayarishaji wa samaki katika kipindi cha miezi 12 iliyopita na uliza swali linalofuata.

**Swali la 4: Ni wiki ngapi kwa ujumla (JINA) alishiriki katika biashara ya samaki katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Katika wiki hizo, kadiria ni siku ngapi kwa wiki (JINA) aliuza samaki? Katika siku hizo, kadiria (JINA) alitumia masaa mangapi kuuza samaki?

Muulize muhojiwa kwa wastani idadi ya WIKI, idadi ya SIKU KATIKA WIKI na idadi ya MASAA KWA SIKU mwanakaya ameshiriki kwenye biashara ya samaki muda wote katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Andika idadi ya wiki, idadi ya siku katika wiki mmoja, na idadi ya masaa katika siku mmoja kwa kawaida mwanakaya anatumia katika biashara ya samaki. Angalia, biashara ya samaki ni kuuza (jumla au rejareja) samaki wabichi au waliotayarishwa, wanaweza kununuliwa na wavuvi au watayarishaji. Kuuza samaki waliovuliwa na kaya kwa matumizi ya kaya nyingine isichukuliwe kama biashara ya samaki bali utayarishaji wa samaki. Andika  $\text{f}0\phi$  katika safu wima zote kama (JINA) hakushiriki katika uuzaji wa samaki katika Kipindi cha miezi 12 iliyopita na uliza swali linalofuata.

## Sehemu ya 10: Nguvu Kazi ya Uvuvi

**Swali la 1: Ni wavuvi wanaume na/watoto wangapi uliwakodi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita? Ni wiki ngapi kila kibarua alikufanya kazi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Maswali haya yanahusiana na nguvu kazi ya kukodi. Muulize mhojiwa ni watu wazima wangapi na watoto wangapi walikodiwa kufanya shughuli za uvuvi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Andika idadi ya watu wazima na watoto walikodiwa na idadi ya wiki aliyofanya mtu mzima mmoja na mtoto mmoja. Kama kuna

makundi yaliyokodiwa, andika makundi katika safu mlalo tofauti na andika idadi ya wiki kwa kila kundi. Unaweza kuandika makundi mpaka 5 yaliyofanya kazi katika wiki tofauti. Kama walifanya kazi pamoja na mbia, andika idadi ya waliokodiwa kwa boti zima, sio sehemu tu ya mhojiwa. Kama hakuna waliokodiwa andika õö na kisha nenda sehemu inayofuata.

**Mfano 1:** Kama kaya iliajiri wanaume 3 kufanya kazi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita kwenye zana/chombo (kwa kufikiria miezi 5 katika miezi 12), kwahiyu safu mlalo ya kwaza itakuwa na -3ø katika safu wima ya -watu wazimaø na safu wima ya pili itakuwa na -20ø(idadi ya wiki katika miezi 5).

Kwa nyongeza ya hawa wanaume 3, kaya pia ilikodi wanaume 4 na mvulana mwenye miaka 13 (tunamweka kwenye kundi la watoto) kwa wiki moja kurekebisha nyavu za uvuvi. Kwa kuwa kundi hili la wanaume 4 na mvulana walifanya kazi kwa muda tofauti na wanaume 3 waliokodiwa, tunatumia mstari unaofuata kuandika muda wao. Wanaume 4 watahusishwa kwenye mstari unaofuata, -4ø kwenye safu wima ya kwanza, na -1ø (wiki moja) kwenye safu wima ya pili, ikifuatiwa na mvulana -1ø(mmoja) katika safu wima ya tatu na -1ø (wiki moja) katika safu wima ya nne.

Majibu ya Swali la 6 yanapaswa kuonekana kama ifuatavyo:

<b>WAFANYAKAZI WALIOAJIRIWA</b>			
IDADI YA WATU WAZIMA	IDADI YA WIKI/WATU MZIMA	IDADI YA WATOTO	IDADI YA WIKI/MTOTO
<b>3</b>	<b>20</b>		
<b>4</b>	<b>1</b>	<b>1</b>	<b>1</b>

### **Swali la 2: Uliwalipa vibarua hawa ujira maalum?**

Muulize mhojiwa kama aliwalipa vibarua ujira maalum. Kama NDIYO geresho õ1ö na uliza swali linalofuata. Kama HAPANA geresho õ2ö kisha nenda Swali la 4.

### **Swali la 3: Kila kibarua alilipwaje kwa wiki?**

Muulize mhojiwa mfumo wa malipo kwa Mtu mzima na mtoto KWA WIKI. Andika malipo kwa wiki na tofautisha mtu mzima na mtoto katika safu wima tofauti. Kama ujira ulikuwa maalumu kila siku, msaidie mhojiwa kukadiria kwa wiki au muulize ni siku ngapi kwa kawaada anafanya kwa wiki kisha zidisha. Ni gharama ya wiki tu inayotakiwa .

### **Swali la 4: Kama mojawapo ya malipo kwa vibarua, uliwalipa vibarua samaki kama gawio la mavuno ya chombo cha kuvulia?**

Uliza kwa mhojiwa kama vibarua walipewa samaki kama gawio la mavuno ya chombo cha kuvulia. Kama NDIYO geresho õ1ö na uliza swali linalofuata, kama HAPANA geresho õ2ö nenda Swali la 6.

### **Swali la 5: Kwa wastani kwa kila wiki, ni kiasi gani cha samaki ulilipa kila kibarua katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa kwa wastani ni kiasi gani cha samaki kwa wiki alilipa vibarua katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Andika kiasi kwa wiki na tofautisha kwa mtu mzima na mtoto katika safu wima husika. Andika kipimo husika kama ilivyo kwenye orodha kwenye dodoso. Kama mhojiwa hawezu kukadiria kiwango cha samaki alichowapa kila kibarua, muulize kwa UJUMLA aliwapa kiasi gani kwa watu wazima na kiasi kwa UJUMLA alichowapa watoto, na gawanya kwa idadi ya vibarua, kama ilivyo onyeshwa Swali la 1. Kama

mhojiwa hawezi kukadiria walicholipa watu wazima na watoto, muulize kiasi alicholipa vibarua WOTE yaani watu wazima na watoto kisha gawanya na idadi yao toka Swali la 1. Andika wastani kwa makundi yote katika safu wima husika.

**Swali la 6: Kama mojawapo ya malipo kwa vibarua, je uliwalipa vibarua hao pesa taasilimu kama gawio la mapato ya chombo cha uvuvi?**

Muulize mhojiwa kama alilipa pesa taslim kwa vibarua kama sehemu ya gawio. Kama NDIYO geresho ö1ö nenda swali linalofuata, na kama HAPANA geresho ö2ö kisha nenda Swali la 8.

**Swali la 7: Kwa wastani, kwa wiki uliwalipa shilingi ngapi kama gawio la mapato ya chombo cha uvuvi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa kwa wastani, kwa wiki uliwalipa shilingi ngapi kama gawio la mapato ya chombo cha uvuvi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Andika kiwango cha wiki kwa watu wazima na watoto katika safu wima husika. Kama mhojiwa ameshindwa kutoa kiasi alicholipa kwa kila kibarua. Muulize kwa UJUMLA alilipa shilingi ngapi kwa watu wazima na JUMLA aliyolipa watoto, na gawanya kwa idadi ya watu wazima na watoto kupata kilicholipa kwa kila mmoja. Kama mhojiwa ameshindwa kutofautisha kilicholipa watu wazima na watoto, muulize JUMLA aliyolipa na gawanya jumla ya watu wazima na watoto kama ilivyo katika Swali la 1. Andika kiasi katika safu wima ya watu wazima na watoto.

**Swali la 8: Katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, uliwalipa vibarua aina nyingine ya malipo yasiyo ya kifedha kama chakula, sigara, n.k?**

Kama kuna malipo mengine yalifanyika yasiyo ya fedha, kwa vibarua kwa wiki. Andika kiasi kwa wiki kwa watu wazima na watoto tofauti katika safu wima husika.

## Sehemu ya 11: Zana za Uvuvi

---

Katika sehemu hii muulize mhojiwa maswali yote katika safu wima (Zana za uvuvi,boti/injini, au gharama nyingine), kwa safu mlalo 1 kabla ya kwenda 8. Safu mlalo 1-8 inahusiana na aina mbalimbali za vifaa vya uvuvi wakati safu mlalo 9-12 inauliza taarifa za boti na injini.Kumbuka kuwa swali la 7 haliulizwi kwa safu mlalo 1-9 na 13-14, linahitaji tu kuulizwa kwa boti na injini.

Maswali ya 1 ó 6, sehemu hii yanauliza mfululizo wa maswali kuhusu aina mbalimbali za uvuvi zinazoendeshwa hapa Tanzania. Kumbuka sehemu tofauti zinaweza kuwa na majina yake ya njia hizi za uvuvi na mdadisi anapaswa kutambua njia hizo zinazotumiwa na mhojiwa. Jedwali lifuatalo linaweza kusaidia kutambua zana za uvuvi:

## **Jedwali 11.1: ZANA ZA UVUVI ZINAZOTUMIWA TANZANIA**

Zana geresho 1 &2: **Jarife.** Hii inajumuisha chandarua, Chambo seine, Kambuzi seine, and Matemba seine. Vinafanana katika uundwaji tofauti ni urefu na ukubwa wa nyavu. *Ni aina ya nyavu ambayo huwa na tundu kubwa kwa ajili ya kuvua samaki wakubwa, kawaida hutumika katika kina kirefu cha maji. Upande wa juu wa nyavu huwa na maboya na kamba ya kuvutia nyavu na chini huwa na nanga kubwa na ndogo ambazo huiwezesha nyavu kunyooka inapokuwa baharinii.*

Zana geresho 3: **Ndoana:** Hii inajumuisha ndoana/zana yenye kamba ndefu na imara ambayo chambo huvalishwa na huwekwa kwa kuachanishwa. Ndoana huvishwa na vipande vya samaki. Kamba hiyo ndefu yenye uzito hudumbukizwa chini na kwa kawaida inaachwa usiku kucha na kutolewa asubuhi.Ndoana ya namna hii ni kubwa kuliko ile ya handlines. **Handlines**-Hii inajumuisha ndoana yenye kamba nyororo ambayo huvishwa kwenye ndoana, na chini ya kamba hiyo uzito huwekwa. Ndoana huvishwa na chambo pamoja na au Usipa kutegemeana na aina ya samaki wanaolengwa.

Zana geresho 4: **Nyavu kubwa.** Hii ni zana yenye umbo la mstatili ambalo kwa kawaida nje au chini panatengenezwa na hutumiwa kwa uvuvi wa kawaida. Inawekwa asubuhi na kuchukuliwa asubuhi inayofuata.Wakati mwininge, nyavu hizi huweza kutumiwa katika maji wazi ambapo hufanya kazi kama Chilimira net, kwa taratibu huvutwa nyuma ya vyombo/mota mbili, hutegwa katika maji ya kina kifupi na samaki kufukuzwa ndani kwa kutikisa maji-Chiombera. *Kwa kawaida inafanana sana na jarife na inakuwa na matundu yenye ukubwa usiozidi sentimita 6.*

Zana geresho 5: **Mitego ya samaki** - Kwa ujumla hii imetengenezwa na mwanzi ambayo hutegwa kwenye mto/ziwa fupi kwa ajili ya kukamata chambo na samaki kama *Mlamba* usiku kucha. Mtego wa samaki unaweza kutumika na uzio ambao unaongoza samaki kuingia kwenye mtego.

Zana geresho 6: **Nyavu za kuvulia pwani (Chavi/Kokoro)**-Hizi zina umbo kama la *cone* lenye kamba iliyofungwa na mawe madogo. Kwa ujumla hutumiwa na watu wawili, mmoja akisukuma nyavu wakati mwenzake amesimama mbele ya chombo/mota kuongoza uelekeo ambao angependa kuelekea .Mapema kabla ya nyavu kurushwa, chombo/mota husimamishwa. Baada ya kuzamishwa kwa nyavu mpaka chini, chombo/mota huongozwa kwenda mbele ili nyavu ziweze kwenda wima.

Zana geresho 7: **Madema:** Sanduku la mbao na nyavu (mtego wa kuvulia samaki) ambalo huruhusu maji kupita. Sanduku lina sehemu moja ya kuingilia, ambalo huwezesha samaki kuingia, lakini huwazuia kutoka. Kitu kizito kinawekwa kwenye sanduku kulipa uzito na chakula cha samaki huwekwa ndani ili kuwavutia kuingia.

Zana geresho 8: **Mtando wa usiku:** Mtumbwi mkubwa unazungukwa na mitumbwi midogo midogo. Mitumbwi midogo hutoa mwanga ambao huwavutia samaki kuingia kwenye mtumbwi mkubwa ambapo hukamatwa. *Mashua kubwa hubeba nyavu, wavuvi na boti ndogo, wakati wa kuvua, nyavu ya mtando hushushwa kwenye maji na mashua na kufanya umbo la herufi ‘c’. Vihori hutumika kuwashaa taa ya karabai pamoja na kutupa chambo (chakula cha samaki), wakati samaki wanafuata mwanga na chakula mashua huendelea kutupa nyavu na kuifanya umbo la duara. Kwa kutumia kamba zilizopo katika upande wa chini nyavu hujifunga na kutoruhusu samaki kutoka, hapo wavuvi hutumia senga kuchota samaki kutoka katika nyavu.*

**Swali la 1: Kuna mwanakaya yejote aliyejihuisha na shughuli za uvuvi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita? kwa kutumia [ZANA YA UVUVI]?**

Muulize mhojiwa Kama kuna mwanakaya yoyote anayeweza kutumia zana za uvuvi zilizo orodheshwa (16 8). Kama NDIYO geresho ölö na uliza swali linalofuata, kama HAPANA geresho ö2ökishwa nenda safu mlalo nyingine. Kama kuna zana ya uvuvi iliyotumika ambayo haipo kwenye orodha, andika zana hiyo katika safu mlalo (13-14)

**Swali la 2: Ni [ZANA ZA UVUVI] ngapi zilitumiwa na kaya yako katika kipindi cha miezi 12 iliyopita? Muulize mhojiwa ni zana ngapi za uvuvi zilitumika katika kipindi cha miezi 12 iliyopita.**

**Swali la 3: Ni kwa wiki ngapi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita ultumia [ZANA ZA UVUVI]?**

Muulize mhojiwa kukadiria namba ya wiki kwa kila zana ya uvuvi iliyotumika kwa kipindi cha miezi 12 iliyopita.

**Swali la 4: Ni [ZANA ZA UVUVI] ngapi zinamilikiwa na kaya yako?**

Uliza zana ngapi za uvuvi zinamilikiwa na kaya katika kipindi cha miezi 12 iliyopita.

**Swali la 5: Kama wewe au mwanakaya yeote aliyejihusisha na uvuvi angenunu [ZANA ZA UVUVI], angelipa kiasi gani cha fedha katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**  
Muulize mhojiwa ni kiasi gani zana moja ingegharimu katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Andika katika shilingi za kitanzania kwa zana.

**Swali la 6: Ni [ZANA ZA UVUVI] ngapi ilinunuliwa na wewe au mwanakaya yeote katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**  
Muulize mhojiwa ni zana ngapi zilizonunuliwa na kaya katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Andika -Ø kama hakuna kilichonunuliwa.

**Swali la 7: Nini ilikuwa jumla ya gharama kwa ajili ya mafuta, mafuta ya kulainishia mitambo na gharama za matengenezo kwa wiki kwa ajili ya [ZANA YA UVUVI] iliyotumika katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa ni kiasi gani kwa ujumla walilipia mafuta, mafuta ya kulainishia mitambo na gharama ya matengenezo kwa ajili ya zana zote za boti/injini zilizotumika katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Andika gharama katika shilingi za kitanzania katika safuwima husika. Hakikisha unaonyesha gharama kwa wiki. Andika -Ø kama hakuna. Kumbuka kuwa swali la hili linahitaji kujibiwa katika safu mlalo 1-12.

**Swali la 8: Ni kiasi gani cha fedha kaya yako ililipa kukodi [ZANA ZA UVUVI/ MOTA] kwa matumizi katika kipindi miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa kwa ujumla ni kiasi gani kaya ililipa kukodi zana hizi za uvuvi kwa ajili ya kutumiwa katika kipindi miezi 12 iliyopita? Zingatia kuwa swali hili linaluzia jumla ya pesa zilizolipwa kwa zana zote zilizokodishwa, na sio gharama kwa zana moja. Andika -Ø kama hakuna kilichokodiwa. Baada ya kumaliza swali hili endelea na safu mlalo inayofuatia na uliza Swali la 1.

**Maswali ya 9 – 10** yanahusiana na gharama za pembejeo nyingine. Baada ya kujaza taarifa kwa safu mlalo zote zilizoorodheshwa (1-12), dadisi gharama nyinginez, lakini usihusishe gharama za manunu, ukodishaji au uendeshaji wa zana za uvuvi/mota/ na matumizi ya vibarua wa shughuli za uvuvi, ambazo tayari zimeshaulizwa katika maswali yaliyotangulia. Kama kuna gharama mpya za pembejeo/zana, andika katika safu mlalo ya -MØ ambayo ni Øzana nyingine, zitaje na ujaze kiasi kilicholipwa katika safu wima husika.

**Swali la 9: Je, mlinunua au kulpia vitu vifuatavyo katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa kama walinunua au walilipia zana zilizoorodheshwa, katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Kama Ndiyo, andika -1Ø na uliza swali linalofuatia, kama ni Hapana, andika -2Ø na nenda safu mlalo inayofuatia.

**Swali la 10: Je, mlitumia gharama kiasi gani kwa [VIFAA] miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa ni kiasi gani walilipia pembejeo katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Andika gharama katika Tsh kwenye safu wima husika. Katika safu wima ya KIPIMO, andika -1Ø kama gharama ya pembejeo ni kwa SIKU, andika -2Ø kama gharama ni kwa WIKI, andika -3Ø kama gharama ni kwa MSIMU, na andika -4Ø kama gharama ni kwa MWAKA. Baada ya kumaliza, nenda safu mlalo inayofuatia na uliza Swali la 9.

## Sehemu ya 12: Uzalishaji wa Samaki

**Swali la 1: Angalia sehemu ya 9. Je, kulikuwa na mwanakaya yeote aliyejihusisha na uvuvi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, kutokana na swali la 1 au la 2?**

Mdadisi anapaswa kuangalia maswali ya 1 na 2 katika sehemu ya -9Ø ili kujua kama kuna wanakaya wowotewaliojishughulisha na uvuvi muda wote au sehemu ya muda katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Kama Ndiyo, andika -1Ø na uliza swali la 2, kama Hapana, nenda sehemu inayofuata.

**Swali la 2: Tafadhali orodhesha mpaka aina tano ya samaki amba wewe au mwanakaya yeote alivua katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Swali hili linaorodhesha aina tofauti ya samaki waliovuliwa. Kumbuka baadhi ya samaki wanaweza kuwa na majina ya mtaani na ni mhimu mhojiwa kuelewa vizuri aina gani ya samaki anaulizwa. Kumbuka kuwa -kundi la samaki ni sahihi kama kaya ilivua samaki tofauti wengi pamoja kwa wakati mmoja. Muulize mhojiwa ni aina gani ya samaki kaya yao ilivua na andika mpaka aina 5 kati ya hizo, ukianza na zile aina kubwa. Andika jina la samaki na geresho lake katika safu wima husika.

**Swali la 3: Je, kwa kiasi kikubwa, ni wapi ambapo unavua [AINA YA SAMAKI]?**

Muulize mhojiwa mahali ambapo kwa kawaida wanavua samaki kwa kila aina ya samaki. Andika majina ya sehemu hizo, na angalia orodha ya mageresho yake ili kuandika geresho lake sahihi.

**Swali 4: Je, Ni njia gani ya uvuvi ultumia kuvulia [AINA YA SAMAKI] katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa mbinu au njia walizotumia kuvulia samaki kwa kila aina ya samaki. Andika geresho la njia walijotumia kutoka katika mageresho yaliyoorodheshwa katika swali katika kila mstari.

**Swali la 5: Je, Kwa jumla, ni kiasi gani cha [AINA YA SAMAKI] ambacho wewe, wanakaya wengine au mtu yeote aliyekodishwa alivua katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa ni kiasi gani cha samaki wanaovua, kwa msaada wa wanakaya wengine na wengine waliokodiwa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Andika idadi wanaovuliwa na geresho lake husika la KIPIMO. Kama hakuna samaki waliovuliwa, andika -Øø

**Swali la 6: Je, kwa jumla, katika kipindi miezi 12 iliyopita, ni kiasi gani cha [AINA YA SAMAKI] ambacho wewe au/na wanakaya wengine mlihifadhi kwa ajili ya kuza baadae? Ni njia gani mlitumia kuhifadhi [AINA YA SAMAKI]?**

Muombe mhojiwa afanye makisio ya JUMLA ya kiasi cha samaki waliohifadhi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita kwa ajili ya kuza baadae, na njia gani za kuhifadhi zilitumika kwa ajili ya kuwatunza samaki. Andika jumla ya kiasi cha samaki waliotunzwa na mageresho yake husika ya KIPIMO mpaka njia 2 tofauti. Andika geresho husika la njia ya kuhifadhi. Kama kulikuwa na aina moja ya namna ya kuhifadhi, acha WAZI safu wima za njia ya pili. Zingatia kuwa takwimu hizi zinapaswa tu kuhusisha samaki wabichi na amba walihofadhiwa amba walivuliwa na wanakaya, au vibarua walikodiwa na kaya.

**Swali la 7: Ni wiki ngapi wewe au mwanakaya yeote alivua [AINA YA SAMAKI] katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Muombe mhojiwa akadirie idadi ya wiki ambapo yeye au wanakaya wengine walivua aina hii ya samaki katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?

**Swali la 8: Ni kiasi gani cha [AINA YA SAMAKI] wewe, wanakaya wengine na/au mvuvi yeote aliyekodishwa, walivua kwa wastani kwa wiki katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Muombe mhojiwa afanye makadirio ya WASTANI wa kiasi cha aina hii ya samaki ambapo yeye au mwanakaya mwingine walivua katika kipindi cha wiki moja katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Andika geresho sahihi kwa ajili ya KIPIMO na KIASI cha samaki.

**Swali la 9: Ni wiki ngapi, wewe au mwanakaya yeote alisindika (kwa moshi, kukausha kwenye juu, kugandisha) [AINA YA SAMAKI] katika katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Muombe mhojiwa akadirie idadi ya wiki ambapo yeye au mwanakaya mwingine alitumia kutayarisha aina hii ya samaki katika kipindi cha miezi 12 iliyopita.

**Swali la 10: Je, kwa jumla, katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, ni kiasi gani cha [AINA YA SAMAKI] ambacho wewe au/na wanakaya wengine mlihifadhi kwa ajili ya kuza baadae kwa wastani kwa wiki?**

### **Ni njia gani mlitumia kuhifadhia [AINA YA SAMAKI]?**

Muombe mhojiwa akadirie WASTANI wa kiasi cha samaki waliohifadhi KWA WIKI kwa ajili ya kuuza baadae katika kipindi cha miezi 12 iliyopita na Ni njia gani walitumia kuhifadhia. Andika wastani wa kiasi cha samaki waliohifadhiwa kwa wiki na mageresho yake ya KIASI kwa mpaka njia 2 za kuhifadhi. Andika geresho husika la njia ya kuhifadhi. Kama kulikuwa na aina moja ya namna ya kuhifadhi, acha WAZI safu wima za njia ya pili. Zingatia kuwa takwimu hizi zinapaswa tu kuhusisha samaki wabichi na ambao walihifadhiwa ambaeo walivuliwa na wanakaya, au vibarua walikodiwa na kaya.

### **Swali la 11: Ni kwa wiki ngapi mliuza [AINA YA SAMAKI] katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Muombe mhojiwa akadirie idadi ya wiki ambapo yeye au wanakaya wengine waliuuza aina hii ya samaki katika kipindi cha miezi 12 iliyopita.

### **Swali la 12: Ni kiasi gani cha (AINA YA SAMAKI) wewe na/mwanakaya yeote aliuza, kwa wastani, kwa wiki katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

**Katika kipindi cha wiki za kufanya kazi, kwa wastani, bei ya kila fungu/KIPIMO ilikuwa shilingi ngapi?**

Muombe mhojiwa kukadiria WASTANI wa kiasi cha samaki waliouzwa KWA WIKI, wastani wa bei, na njia za kuhifadhi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Andika wastani wa kiasi cha samaki waliouzwa kwa wiki na mageresho yake husika ya KIPIMO mpaka njia 2 tofauti. Andika geresho husika la njia ya kuhifadhi na wastani wa bei kwa kiasi cha KIPIMO cha samaki waliouzwa. Kama kulikuwa na aina moja ya namna ya kuhifadhi, acha WAZI safu wima za njia ya pili. Zingatia kuwa takwimu hizi zinapaswa tu kuhusisha samaki wabichi na ambao walihifadhiwa ambaeo walivuliwa na wanakaya, au vibarua walikodiwa na kaya.

### **Swali la 13: Ni kiasi gani cha (AINA YA SAMAKI) walivuliwa na wewe na/ mwanakaya yeote katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, kwa wastani walitunzwa kwa wiki kwa ajili ya matumizi ya kaya?**

Muombe mhojiwa kukadiria WASTANI wa kiasi cha samaki walitonza KWA WIKI kwa ajili ya matumizi kaya katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, na njia walizotumia kuwatunzia samaki hao. Andika wastani wa kiasi cha samaki walitonza kwa wiki, tumia mageresho husika ya KIPIMO andika mpaka njia mbili za utunzaji walizotumia. Andika geresho husika la njia ya kuhifadhi iliyotumika. Kama kulikuwa na aina moja ya namna ya kuhifadhi, acha WAZI safu wima za njia ya pili. Zingatia kuwa takwimu hizi zinapaswa tu kuhusisha samaki wabichi na ambao walihifadhiwa ambaeo walivuliwa na wanakaya, au vibarua walikodiwa na kaya.

### **Swali la 14: Kwa ujumla, katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, ni gawio kiasi gani cha [AINA YA SAMAKI] waliovuliwa, kilitunzwa kwa ajili ya matumizi ya kaya?**

Muombe mhojiwa kufanya makadirio ya kiasi cha samaki waliovuliwa ili kufahamu kiasi kilichotunzwa kwa ajili ya matumizi ya kaya katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Hakikisha mhojiwa unamsomea majibu matano yaliyoorodheshwa.

### **Swali la 15: MDADISI: KWA KILA AINA YA SAMAKI, KIASI KILICHOVULIWA KWA WIKI, LAZIMA KIWE KARIBU SAWA NA KIASI KILICHOZWA KWA WIKI + KIASI KILICHOTUNZWA + KIASI KILICHOTUMIWA NA KAYA YENYEWE KWA WIKI. KAMA SIO HIVYO, MUULIZE MHOJIWA ILI AWEZE KUREKEBISHA MAKISIO YAKE NA ELEZA HAPO CHINI SABABU ZA TOFAUTI KATI YA MAKADIRIO HAYO MAWILI YA KIASI KILICHOVULIWA.**

Swali hili linatoa nafasi ya kuhakiki majibu yaliyojazwa katika Swali la 8 na jumla ya maswali ya 10, 12, na 13. Swali ni kwa ajili ya Mdadisi na hatakiwi kuulizwa mhojiwa. Mdadisi anapaswa kuhakikisha kuwa kwa kila aina ya samaki, mlinganyo ufuatao unakuwa sahihi:

<b>Swali la 8</b>	<b>=</b>	<b>Swali la 10</b>	<b>+</b>	<b>Swali la 12</b>	<b>+</b>	<b>Swali la 13</b>
KIASI KILICHOVULI WA / WIKI		KIASI KILICHOUZW A / WIKI		KIASI KILICHOTUNZW A / WIKI		KIASI KILICHOTUMIWA NYUMBANI(KAYA ) / WIKI

Kama takwimu hizi kwa aina zote za samaki zinakaribia kuleta mlinganyo sahihi, andika  $\frac{1}{\phi}$  na nenda sehemu inayofuatia. Kama takwimu haziwiani katika mlinganyo huu, andika  $\frac{2}{\phi}$  muulize mhojiwa kwanini takwimu hazijumlishiki kiusahihi, na waombe warekebishe mahesabu yao. Andika mabadiliko na sababu za kutofautiana kwa mahesabu katika kisanduku chenyeye jina la ñMaelezoö.

## Sehemu ya 13: Biashara ya Samaki

---

**Swali la 1: Je, wewe au mwanakaya mwengine yejote alijishughulisha na biashara ya samaki yaani kununu na kuuza samaki katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Uliza ili kujua kama kuna wakaya wowote waliokuwa wanajishughulisha na uuzaaji wa samaki katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Kama Ndiyo, andika  $\frac{1}{\phi}$  na nenda swali linalofuatia, kama Hapana, andika  $\frac{2}{\phi}$  mwisho wa mahojiano.

**Swali la 2: Tafadhali orodhesha mpaka aina tano ya samaki ambao wewe au mwanakaya yejote aliuzza Kama njia mojawapo ya biashara yako ya samaki.**

Swali hili linafanana na Swali la 2 katika sehemu  $\frac{1}{1}\phi$ Muulize mhojiwa ni aina gani ya samaki ambayo kaya iliuzza katika kipindi cha miezi 12 iliyopita na andika mpaka aina 5, ukizingatia zile kuu. Andika jina la samaki pamoja na geresho lake katika safu wima husika.

**Swali la 3: Katika miezi 12 iliyopita, ni kiasi gani [AINA YA SAMAKI], wewe au mwanakaya yejote alinunua kutoka kwa wavuvi wengine na au waandaaji wengine kwa wiki kwa ajili ya biashara ya samaki yako? Katika wiki za kazi, nini ilikuwa wastani wa bei kwa kila fungu?**

Muombe mhojiwa akadirie WASTANI wa kiasi cha samaki KWA WIKI walichonunua ili kuuza katika biashara yao na wastani wa bei ya kuuzia kwa fungu/KIPIMO. Hakikisha unatenganisha kati ya njia tofauti za utayarishaji kwa kila aina ya samaki na andika mpaka njia 2 za utayarishaji. Andika wastani wa kiasi cha samaki walionunuliwa kwa wiki na mageresho yake ya KIPIMO. Pia, andika mageresho sahihi ya njia za utayarishajina andika wastani wa bei kwa kiasi kilichonunuliwa. Kama kulikuwa na aina moja ya namna ya utayarishaji, acha WAZI safu wima za njia ya pili

**Swali la 4: Katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, kwa wastani ni kiasi gani (AINA YA SAMAKI) wewe au mwanakaya yejote aliuzza kwa wiki kama mojawapo ya biashara yako ya samaki?**

Katika wiki za kazi, nini ilikuwa wastani wa bei kwa kila fungu?

Muombe mhojiwa akadirie WASTANI wa kiasi cha samaki KWA WIKI waliouzwa katika biashara yao na wastani wa bei ya kuuzia kwa fungu/KIPIMO. Hakikisha unatenganisha njia tofauti za utayarishaji kwa kila aina ya samaki na andika mpaka njia 2 za utayarishaji. Andika wastani wa kiasi cha samaki waliouzwa kwa wiki na mageresho yake ya KIPIMO. Pia, andika mageresho sahihi ya njia za utayarishajina andika wastani wa bei kwa kiasi kilichouzwa. Kama kulikuwa na aina moja ya namna ya utayarishaji, acha WAZI safu wima za njia ya pili

**Swali la 5: Je, kaya yako iliingia gharama zozote za (GHARAMA ZA KITU) kuhusiana na shughuli za biashara ya samaki katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Muulize mhojiwa kama iliwapasa kulipia aina yejote ya gharama kati ya gharama zilizoorodheshwa 1-6 ili waweze kuendesha biashara yao ya samaki katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Kama Ndiyo, andika  $\frac{1}{\phi}$  na uende swali linalofuatia na kama Hapana, andika  $\frac{2}{\phi}$  na uende kipengele kingine cha gharama. Kama kwa vipengele vyote vya gharama jibu ni Hapana, nenda sehemu inayofuata. Kama kuna gharama ya kitu kingine ambacho hakikuorodheshwa, kinapaswa kuonyeshwa katika safu mlalo ya 6, andika geresho öngine, tajaö

Usijumuuishe gharama za kuvua samaki katika swali hili, gharama hizi zipo katika sehemu ya 11 swali la 9-10.

**Swali la 6: Ni kiasi gani cha fedha kililipwa na kaya yako kwa ajili ya [GHARAMA ZA KITU] kwa wiki katika kipindi cha miezi 12 iliyopita?**

Muombe mhojiwa kukadiria kiasi kilicholipwa KWA WIKI kwa kila kifaa katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Andika jibu katika shilingi za kiatanzania kwa wiki.

## **Sehemu ya IV: Fomu za Ufutiliaji**

### **Itifaki za Ufutiliaji**

---

Shughuli ya ufutiliaji kwenye eneo la kazi la NPS inahusisha hatua zifuatazo:

1. Kurudia kila kaya ya NPS mwaka wa 3, ilioandaliwa kwenye Fomu ya T-0 yenyе Orodha ya Wanakaya. Fomu ya T-0 ina orodha ya majina ya wanakaya iliyopatikana kutokana na Utafiti wa tatu wa NPS wa 2012/2013, na taarifa za kuwezesha kufanya mawasiliano na kaya kutoka mwaka wa tatu wa NPS katika sehemu ya U-1, na taarifa za mashamba yaliyoorodheshwa na kaya katika utafiti huo uliopita.
2. Tambua kama kaya yote imehama kutoka katika makazi yake ya awali na wanakaya wake wote kwa pamoja. Kama kaya yote imehama, ni lazima ujaze fomu ya ufutiliaji wa kaya T-1. Fomu ya T-1 ni fomu inayotumika kukusanya taarifa kuhusu makazi mapya ya kaya.
3. Tambua kama kuna mwanakaya ye yote aliye hama kutoka kwenye kaya ya awali. Kwa mwanakaya ye yote aliye hama, ni lazima ujaze fomu ya binafsi T-2. Fomu ya T-2 inatumika kukusanya taarifa za mahali alipo mwanakaya aliye hama.
4. Tafuta makazi mapya ya kaya au mwanakaya kwa kutumia taarifa zinazopatikana kwenye fomu T-1, T-2, na taarifa nyingine za nyongeza kutoka kwa msimamizi/muwezesaji wa mambo ya ufutiliaji kutoka makao makuu.
5. Kuhoji wanakaya/mwanakaya aliye fuatiliwa na kupatikana kwenye makazi mapya.

## **Fomu ya T-0 Iliyochapishwa Orodha ya Wanakaya**

---

Fomu ya T-0 iliyochapishwa yenyе orodha ya wanakaya imejazwa taarifa toka NPS ya mwaka wa 3 na taarifa za mawasiliano toka NPS mwaka wa 3 sehemu ya U-1.

### **Mhojiwa wa Fomu ya T-0**

Mhojiwa wa fomu ya T-0 ni mtu ye yote anayeweza kujibu sehemu ya orodha ya wanakaya. Mkuu wa kaya ndiye mhojiwa anayehitajika zaidi. Kama mkuu wa kaya hayupo, mwenza (mke wake) au mtu mzima ye yote ambaye ni mwanakaya anaweza kuhojiwa. Kuna sehemu iliyopo juu kulia mwa fomu ya T-0 kwa ajili ya kuorodhesha namba ya mwanakaya anayepaswa kuhojiwa fomu hii. Unapaswa kutumia namba ya mwanakaya kutoka utafiti uliopita (yaani wa 2012/2013 ambayo imenorodheshwa hapo chini). Katika fomu hii na katika Swali la 6, sehemu B ni sehemu pekee unazoweza kuandika namba hii ó katika sehemu nyingine zote katika dodoso la kaya unapaswa kutumia namba mpya za wanakaya. Katika mazingira machache, kama vile katika kaya ambayo watu wazima wote wamefariki, fomu ya T-0 inawezwa kuulizwa kwa mtu mwingine mwenye ufahamu wa kutosha katika kijiji. Katika hali hii, andika -99% katika kisanduku na andika maelezo ya kina katika kisanduku cha maoni katika ukurasa wa pili wa T-0. Kwa mfano, taarifa zimetolewa na Mr. Matumbo anayeishi katika kaya mlango wa pili katika sehemu ya awali.

**Taarifa zifuatayo zimechapishwa kwenye fomu ya T-0, kutokana na taarifa kutoka NPS mwaka wa tatu.**

**1. Taarifa za kijiografia**

Taarifa hizi zinatakiwa zifanane na taarifa za sasa hivi za mahali ulipo na sio za mahali pa utafiti wa awali. Kama, kwa mfano kaya imehamia EA/kijiji jirani, unapaswa kujaza namba ya ya EA/kijiji ambacho kwa sasa hivi unafanya mahojiano, na sio eneo la utafiti uliopita.

Hizi ni taarifa za kijiografia (kama vile mkoa, EA/kijiji, kata) kwa kaya ambayo iliorodheshwa mwaka wa 3. Kaya inaweza isiwepo tena kwenye sehemu ya awali ilioonyeshwa kwenye fomu hii, ila ni mwanzo wa kuifuatilia/kuitafuta kaya katika mwaka wa 4.

**2. Jina la Mkuu wa kaya kutoka kwenye NPS 3**

Ni muhimu kutambua kuwa unapotembelea kaya kwa ajili ya utafiti wa sasa (NPS 2014/2015), kaya inaweza kuwa na mkuu wa kaya tofauti na yule wa utafiti wa mwaka wa 3.

**3. Utambulisho kamili wa kaya kutoka NPS ya mwaka wa tatu**

Huu ni utambulisho wa tarakimu 7 uliopewa kaya katika utafiti wa mwaka wa 3.

**4. Namba ya simu ya mkuu wa kaya**

Hii ni namba ya simu inayoweza kutumika kuwasiliana na mkuu wa kaya kabla ya kumtembelea au ikiwa unapata tatizo kuipata kaya.

**5. Maelezo mahali/sehemu**

Haya ni maelezo ya nyumba au mahali kaya ilipo, yaliyoandikwa na mdadisi alipotembelea kaya wakati wa NPS ya mwaka wa 3. Maelezo haya yapo kwenye fomu ya T-0 hivyo inakurahisishia kuitambua kaya.

**6. Namba ya Fomu**

Taarifa hizi zilijazwa kwenye dodoso. Inahusisha na idadi ya fomu za T-0. Karibu katika kila kaya kutakuwa na wanakaya pungufu ya 14 na hii itaeleza -Fomu ya 1 kati ya 1 $\varnothing$  Kwa kaya yenyé wanakaya 16, kunatakiwa kuwa na fomu 2 za T-0. Fomu ya 1 kati 2, itakua na taarifa za wanakaya 1 mpaka 12. Mwanakaya wa 15 na 16 wataonekana kwenye fomu ya 2, -fomu ya 2 kati ya 2 $\varnothing$  Sehemu hii inakufanya ufahamu idadi ya fomu unazozitarajia na fomu ambayo inakosekana kama hutakuwa na zote.

**7. Mtu mwingine wa karibu katika jamii**

Huyu ni mtu mwingine ndani ya jamii anayeweza kutumiwa kumsaidia mdadisi kuipata kaya. Ni lazima uwasiliane na mtu huyu kama unapata tatizo kuipata kaya na mtu huyu anaweza kukusaidia.

**8. Mtu mwingine nje ya jamii**

Huyu ni mtu mwingine nje ya jamii unayeweza kuwasiliana naye kama mtu wa karibu katika jamii hapatikani au hawezu kukupa msaada wa kutosha.

**9. Namba za simu za wanakaya wengine**

Hizi namba za simu zinaweza kutumika kuwatafuta wanakaya wengine kama unapata tatizo kuipata kaya.

*Kama mojawapo ya maswali ya hapo juu yapo wazi, ni kwa sababu hayakuandikwa na wadadisi katika mwaka wa utafiti uliopita. Hivyo, inakupasa uendelee na taarifa zinazopatikana. Kama inawezekana, jaza maswali yaliyo wazi wakati wa kujaza fomu ya T-0 kwa sababu taarifa inaweza kuwa msaada kwa timu ya kuifuatilia kaya (tracking team).*

## 10. Orodha iliyojazwa majina ya wanakaya na namba zao za mstari

Orodha hii imejazwa taarifa binafsi za waliokuwa wanakaya katika NPS ya mwaka wa 3. Taarifa zilizojazwa ni kama: Jina, jinsia, mwezi na mwaka wa kuzaliwa, umri katika NPS 2014/2015, na uhusiano na mkuu wa kaya kwa mwaka wa 3 wa utafiti, na kama mwanakaya alikuwa katika mwaka wa 3.

## 11. Taarifa za mashamba zilizojazwa

Sehemu ya orodha ya mashamba ina taarifa za mashamba yaliyoorodheshwa na kaya katika utafiti wa NPS mwaka wa 3. Taarifa hizi zilizojazwa ni: jina la shamba, maelezo ya sehemu lilipo shamba, na namba ya shamba katika utafiti uliopita.

Mfano hapo chini ni wa fomu ya T-0 ambayo zhaijajazwa kama ambavyo utaipata kutoka kwa msimamizi wako. Sehemu zilizo na kivuli, ndizo ambazo unatakiwa kuzijaza kutohakana na taarifa utakazopita kutoka kwenye kaya.

### KURASA YA 1

Utafiti wa Kufuatilia Kaya Tanzania (2014/2015)												FOMU YA KUFUATILIA KAYA (T-0)												Formu ya																											
MKOA				WILAYA				KATA				EA/KUJI				HHID				JINA LA MKUU WA KAYA KUTOKA MWAKA WA 3 WA NPS:				KITONGOJI/ MTAAS				VISEGESE				SIMU YA KUFUATILIA KAYA				MHOJIWA T-0															
0	5			5				0	9	3		3	2	1		0	0	6	2	JINA LA MKUU WA KAYA KUTOKA MWAKA WA 3 WA NPS: CLEMENT ALOYCE	UTAMBULISHO KAMILI WA KAYA KUTOKA MWAKA WA 3 WA NPS:																														
0	5			5				0	9	3		1	3	1	7	-	0	0	1	NAMBA YA SIMU YA MKUU WA KAYA: NAMBA YA SIMU YA MKUU WA KAYA: 0 7 6 4 9 4 0 7 4 5																															
1. JINA	2. JINSI	3. MWEZI NA MWAKA WA KUZALIWA	4. UMRI	5. UHUSIANO	6. HALI YA MWAKA WA NA MKUU	7. Je [JINA] kwa ssesi ni mwaniakaya?	8. Kwa sa [JINA] analishi wap?	9. GERESHO YA UFUATILIAJI	10. HALIYA UFUATILIAJI																																										
1 CLEMENT ALOYCE	1	3	1968	44	1	1	NDIYO...1 ► 9	ANGALIA GERECHO	WEKA 'X' KAMA MITU AMEPATIKANA																																										
2 BAHATI ALLY	2	4	1976	36	2	1																																													
3 ELIZABETH CLEMENWNT	2	7	1995	17	3	2																																													
4 NASRA HAMISI	2	10	1997	14	4	1																																													
5 JOHN ALOYCE	1	9	1974	37	8	2																																													
6 JOYCE FROLIANI	2	6	1988	24	8	2																																													
7 DANIEL ALOYCE	1	99	1938	74	7	1																																													
105 JAMES ALOYCE	1	99	1979	33	5	2																																													
9																																																			
10																																																			
11																																																			
12																																																			

## KURASA YA 2

MASHAMBA											
11. NAMBA YA SHAMBA MWAKA 2012/2013	12. JINA LA SHAMBA	13. MAELEZO YA SEHEMU LILIPU SHAMBA	14. Bado kaya ina mamlaka juu ya shamba hill?	15. Kwanini shamba hill halikulimwa/kulimikiwa tena na kaya? LILIJUWA.....1 LILITELKEZWA.....2 ►SHAMBA LINGINE LILICHUKULIWA.....3 ►17 LILIGAWIWA NA KILIGI.....4 ►17 LILITIWUA KWIA MTE MILIMWIWA.....5 ►17 LILIRACHWA KUKODIMA/ KUWANA NAVUNO...6 ► SHAMBA LINGINE	16. Ulipata kiasi gani ulipouza hill shamba?	17. Ulipokea fidia ya kiasi gani?  KAMA HAKUNA, ANDIKA '0'					
NDIYO...1 ►SHAMBA LINGINE	HAPANA..2	►SHAMBA LINGINE	TSH	►SHAMBA LINGINE	TSH						
1 M1 KASANGA	BARABARA KUU KWENDA KULIA										
2 M2 MANGOBANE	LIKO MAGOMBANE										
3 M3 MISONGENI	LIKO MISONGENI										
4											
5											
6											
7											
8											
9											
10											
11											
12											
MAONI											

### Ujazaji wa Fomu ya T-0

Ukiwa na fomu ya T-0, unapaswa kutembelea kaya makazi ya mwaka wa 3 ya kaya ya NPS na kuona kama kuna mwanakaya yeote wa NPS ambaye bado anaishi kwenye makazi hayo. Wakati mwingine mwenyekiti wa kijiji au viongozi wengine wanaweza kukuambia kuwa kila mtu katika kaya hiyo amehama. Kama watakuwa hawajakuelekeza makazi mapya ya kaya na kufanya mawasiliano nao, unapaswa kusisitiza kuwa unataka kutembelea makazi ya kaya ya mwaka wa 3 wa NPS ya kaya hii ili kujihakikishia kuwa hakuna mwanakaya ambaye bado anayeishi pale.

Kama ni kweli wanakaya wote wamehama kwa **pamoja**, kwenda kwenye makazi mapya, usijaze fomu ya T-0 na badala yake endelea na fomu ya T-1.

### ORODHA YA WANAKAYA

Ikiwa angalau mwanakaya mmoja aliye kwenye fomu ya T-0 amepatikana, basi fomu T-0 itatakiwa kujazwa kwenye kaya ambayo mwanakaya huyo anaishi. Safuwima ya 1-6 katika fomu ya T-0 zinahitaji kuthibitishwa na safuwima 7-10 zinahitaji kujazwa ili kujua ni watu gani bado ni wanakaya (öwa kaya ya sasa hiviö) na wanakaya wapi wameondoka, na kama fomu ya T-2 inahitajika kujazwa kwa ajili ya baadhi ya wanakaya.

### Safuwima 1-5

Mara tu baada ya mtu aliyeorodheshwa katika orodha ya wanakaya ilijojazwa kuthibitishwa kuwa bado ni mwanakaya, unapaswa kuanza kujaza fomu T-0. Kumbuka kujaza mstari/mtu kwa mstari/mtu, ukianzia na mtu wa kwanza kwenye orodha ya wanakaya. Safuwima ya 1-5 lazima zithibitishwe. Chukua taarifa zozote zilizotofautiana za majina, jinsia, mwezi na mwaka wa kuzaliwa. Kumbuka kwamba safuwima ya 4 ni umri kwa mwaka 2014, kulingana na taarifa zilizokusanywa kwenye NPS ya mwaka wa tatu. Usihamishe tu taarifa hizi kama zilivyo katika dodoso la kaya. Wakati mwingine, jina liliandikwa visivyo, au umri utakuwa si sahihi, na hata katika mazingira machache jinsi ya mtu yaweza kuwa si sahihi. Unapaswa kuandika taarifa sahihi katika sehemu ya orodha ya wanakaya. Unapaswa pia kutambua kuwa mabadiliko haya, yataonekana kwenye taarifa ya öuwiano wa taarifaö (consistency check) katika programu ya kuingizia taarifa. Unapaswa kuelezea kwenye ösehemu ya maoniö kwenye dodoso la kaya kuwa kulikuwa na makosa ambayo umeyasahihisha ili msimamizi wako ajue kuwa hujafanya makosa.

## **Safuwima 6**

Katika utafiti wa mwaka huu, pia tunajaribu kuwatafuta wanakaya ambao hawakupatikana mwaka wa 3. Safuwima ya 6 ina taarifa za wanakaya wa utafiti uliopita na itaonyesha kama mwanakaya alipatikana katika mwaka wa 3. Kama mwanakaya alikuwa ni sehemu ya utafiti wa pili wa NPS na alipatikana mwaka wa 3, safuwima ya 6 itakua na geresho -1 $\varnothing$  kuonyesha kuwa mwanakaya alipatikana mwaka wa 3. Kama mwanakaya alikuwa ni sehemu ya utafiti wa pili wa NPS lakini hakupatikana mwaka wa 3, safuwima ya 6 itakua na geresho -2 $\varnothing$  kuonyesha kuwa mwanakaya huyo hakupatikana mwaka wa 3 wa utafiti. Kama mwanakaya alikuwa mpya katika kaya mwaka wa 3, safuwima ya 6 itakua na geresho -3 $\varnothing$  kuonyesha kuwa mwanakaya huyo hakuwa mwanakaya mwaka wa 2 wa utafiti na ni mwanakaya mpya katika mwaka 3.

## **Safuwima 7**

Baada ya ya kudhibitisha taarifa za mwanakaya kwa safuwima 1-6 , Swalil 7 linauliza kama mtu huyo ni mwanakaya. Dadisi ili kuhakikisha kuwa mtu huyo kwa hakika bado ni mwanakaya, kwa kufuata maana ya mwanakaya kama inavyotumika katika NPS. Kama jibu ni öndiyoö fuata maelekezo na uende Swalil 9. Kama mtu huyo si mwanakaya tena kwenye kaya hiyo, endelea na Swalil 8.

## **Safuwima 8**

Swali katika safuwima ya 8, linauliza sehemu anayoishi mtu huyo kwa sasa. Kama amefariki, chagua geresho 8 na nenda kwa mtu anayefuata.

Mageresho mengine yanayohusiana na kiasi cha umbali ambapo mtu aliyehama yupo. Mageresho kamili ni kama yafuatayo:

- 1 EA/Kijiji kile kile ó kama mtu anaishi EA/kijiji kile kile cha mwaka wa 2
- 2 Kata ile ile ó kama mtu anaishi kijiji kingine tofauti ila kata ile ile
- 3 Wilaya ile ile ó kama mtu anaishi kata nyingine tofauti ila wilaya ile ile
- 4 Mkao ule ule ó kama mtu anaishi wilaya tofauti ila mkao ule ule
- 5 Tanzania ó kama mtu anaishi mkao tofauti ila bado yupo Tanzania
- 6 Nchi jiranió kama mtu anaishi nchi jirani
- 7 Nchi nyingine ó kama mtu anaishi nchi ya mbali sana na sio jirani
- 8 Amefariki ó kama mtu huyu amefariki

## **Safuwima 9**

Safu wima 9 ni angalizo kwa mdadisi kuangalia kama mtu anatakiwa kuorodheshwa kwenye orodha ya majina ya wanakaya katika dodoso la kaya, au kama fomu T-2 inatakiwa kujazwa, na baada ya kujaza fomu ya T-2 na kama mtu anatakiwa kufuatiliwa palepale kwenye eneo la kazi.

Mageresho kamili ni kama yafuatayo.

1. Kama mtu bado ni mwanakaya. Fomu T-2 haitahitajika kwa mtu huyu.
2. Kama mtu ameondoka kwenye kaya, ana zaidi ya miaka 15, na anaishi ndani ya saa moja katika EA/kijiji cha awali. Jaza fomu T-2 kuhusu mtu huyu. Mtu huyu lazima afuatiliwe na kuhojiwa kabla timu haijondoka kwenye EA/kijiji hiki.
3. Kama mtu ameondoka kwenye kaya, ana miaka zaidi ya 15, na anaishi zaidi ya saa moja kwenye eneo la awali, jaza T-2 kuhusu mtu huyu. Mtu huyu atafuatiliwa baadae.
- 4 . Kama mtu huyu ameondoka kwenye kaya, lakini ana miaka chini ya 15. Hutakiwi kujaza fomu T-2 kwa kuhusu mtu huyu. Kama ameondoka na mtu mzima ambaye ni mwanakaya atakayefuatiliwa, itawasaidia timu ya kufuatilia kujumuisha taarifa za mtoto huyo kwenye fomu ya kufuatilia ya mwanakaya huyo ambaye ni mtu mzima.

Baada ya kujaza fomu T-0, kila mwanakaya mwenye zaidi ya miaka 15 aliyejazwa kwenye T-0 anapaswa kukidhi kimojawapo kati ya yafuatayo:

1. Awepo kwenye kaya na ataaingizwa kwenye orodha ya wanakaya iliyo wazi katika dodoso la kaya.
2. Awe na fomu T-2 iliyojazwa taarifa zake.
3. Amefariki.

Hakutakuwa na mazingira yoyote ambapo mtu mzima ambaye ameordheshwa kwenye T-0 ambaye hajafariki, ambaye haonekani kwenye orodha yoyote ya wanakaya na fomu ya T-2 yoyote. Kama mtu mzima huyo haingii katika kipengele kimojawapo kati ya hivi, hii itaonekana kwenye program ya kuingiza taarifa na itabidi kurudi kwenye kaya.

### **Safuwima ya 10**

Safuwima ya 10 inasaidia kujua ni mwanakaya gani wa mwaka wa 3 bado anahitaji kufuatiliwa. Mdadisi aweke alama →XØ katika safuwima kama mwanakaya amepatikana. Kama mwanakaya bado yupo kwenye kaya ya awali katika sehemu ile ile, kwahiyo mdadisi aweke alama →XØ katika safuwima ya 10 hata kama mdadisi hajamuona ana kwa ana au hajakutana na mwanakaya. Kama mwanakaya ameondoka katika kaya kwenda makazi mapya na baadae akapatikana na kuhojiwa, Msimamzi wa kundi/timu anatakiwa kuchukua fomu husika ya T-0 na kuweka alama ya →XØ katika safuwima ya 10 kwa mwanakaya husika. Safuwima ya 10 inadhamiria kuawasaidia watu wa makao makuu na timu ya kufuatilia kaya kujua ni wanakaya gani bado wanatakiwa kufuatiliwa kwa hiyo timu ya kufuatilia haitatumia muda wake kutafuta wanakaya ambao tayari wameshahojiwa na timu nyingine. Ni muhimu sana kwa mdadisi kumtaarifu msimamizi wake pindi wanapokuwa wamempata mhojiwa anayefuatiliwa ili msimamizi aweke taarifa katika safuwima ya 10 kila wakati.

### **KUKATAA**

Ikiwa wanakaya wamekataa kuhojiwa jaza alama ya →XØ kwenye kisanduku husika

***Angalia kurasa inayofuata kwa mfano wa jinsi yakujaza kwa usahihi safuwima ya 7-10.***

### **KWA MFANO:**

Wakati wa utafiti wa pili, kaya hii ilikuwa na wanakaya sita. Mkuu wa kaya alikuwa bwana Clement Aloyce, mke wake alikuwa Bahati Ally, watoto wake wawili, Elizabeth na Nasra, kaka yake James, na baba yake Daniel. Katika mwaka wa 3, wanakaya wote walikuwepo kwenye kaya kasoro Daniel ambaye alikua mbali na kaya kwa miezi michache kwa kazi za msimu. Ndugu wawili wa Clement, John na Joyce wanaishi pia kwenye kaya hiyo.

Wakati unaporudi kwenye kaya unagundua kuwa kumekuwa na mabadiliko. Mtoto wake mkubwa wa kike, Elizabeth ameolewa na anaishi na mumewe kwenye kaya yake katika EA ile ile (kijiji kile kile) ya kaya yake ya zamani. Mtoto wake mwingine wa kike, Nasra, bado anaishi ndani ya kaya. James kwa sasa hafanyi kazi kwahiyo amerudi kwenye kaya. Baba yake, Daniel amefariki. Ndugu zake wengine, John na Joyce, wameenda kwa pamoja Dar es Salaam kutafuta kazi. Fomu ya T-0 iliyojazwa itakuwa na taarifa zifuatazo kwenye sehemu ya orodha ya wanakaya. Sasa, utahitaji kujaza fomu ya T-2 kwa ajili ya Elizabeth na upange taratibu za kumhoji pamoja na kaya yake kabla ya kuondoka kwenye EA. Utahitaji pia kujaza fomu T-2 kwa ajili ya John na Joyce. Utakapomaliza kujaza sehemu ya orodha ya wanakaya, unapaswa kuhakikisha kuwa Clement Aloyce, Bahati Ally, Nasra Hamisi na James Aloyce wote wanaonekana kwenye orodha ya wanakaya, na Daniel Aloyce anaonekana kwenye sehemu S, ya Vifo kwenye kaya katika dodoso la kaya. Sehemu ya Orodha ya wanakaya ya fomu ya T-0 inatakiwa kujazwa kama inavyoonekana hapo chini.

**Utafiti wa Kufuatilia Kaya Tanzania (2014/2015)**

MIKO	0	5	JINA LA MKUU WA KAYA KUTOKA MWAKA WA 3 WA NPS:
WILAYA		5	<b>CLEMENT ALOYCE</b>
KATA	0	9	3
EAKIJUJI	3	2	1
HHID	0	0	6
	6	2	NAMBA YA SIMU YA MKUU WA KAYA: 0 7 6 4 9 4 0 7 4 5

MWAKILISHI (NDANI YA JAMI)

JINA MWAKILISHI (NJE YA JAMI)

JINA MZEE MOHAMMED

UHUSIANO JIRANI

KAZI MKULIMA

MAHALI CHAMWINO

KWINGINE MAKAZI ZAIKI YA KILIMO

SIMU SIMU

MWAKILISHI (NDANI YA JAMI)

JINA MR CLEMENT KATUA

UHUSIANO SHEMEJI YAKE

KAZI DEREVA

MAHALI MASIIKA

KWINGINE

SIMU

7153839404

**FOMU YA KUFUATILIA KAYA (T-0)**

KITONGOJI/ MTAA

**VISEGESE**

SEHEMU ILIPOKUWA KAYA WAKATI WA MWAKA WA 3 WA NPS:

UNITOKA BARABARA KUU NYUMBA YA PILI UPANDE WA KULIA  
KUNA MASHINE YA KUSAGA KUSHOTO MWALIMU MANGO DIWA  
KICHOCHORO KATIKATI

Formu ya 1 Katu ya 1

MHOJIWA T-0

1

(INGIZA NAMBA YA MWANAKAYA RUTOKA KWENYE ORODA  
YA WANAKAYA 2010/11 KAMA LIVYORODHESHA HAPA  
CHINI KAMA MHOJIWA HAKUWA MWANAKAYA ANDIKA '9'  
NA ELEZA UHUANO WAKE NA MWANAKAYA KWENYE  
KISANDUKU CHA MAONI KILCHOPA CHINI KWENYE  
UKURASA UNAOFUATA MUOJU).

1. JINA	2. JINSI	3. MWEZI NA MWAKA WA KUZALIWA	4. UMPRI	5. UHUSIANO NA MKUU WA KAYA	6. HALI YA MWAKA WA 2	7. Je [JINA] kwa sasa ni mwankay?	8. Kwa sa [JINA] analishi wapi?	9. GERESHO YA UFUATILAJI	10. HALI YA UFUATILAJI	MAGERESHO YA SWALI LA 5
ME.1	KE.2	MWEZI MWAKA MIAKA				NDIYO...1 ► 9	ANGALIA GERESHO	WEKA 'X' KAMA MTU AMEPATIKANA		MAGERESHO YA SWALI LA 6
1 CLEMENT ALOYCE	1 3 1968	44	1	1	1	1		1	X	MGERESHO YA SWALI LA 7
2 BAHATI ALLY	2 4 1976	36	2	1	1	1		1	X	MGERESHO YA SWALI LA 8
3 ELIZABETH CLEMENWNT	2 7 1995	17	3	2	2	2	2	2		MGERESHO YA SWALI LA 9
4 NASRA HAMISI	2 10 1997	14	4	1	1	1		1	X	MGERESHO YA SWALI LA 10
5 JOHN ALOYCE	1 9 1974	37	8	2	2	2	5	3		MGERESHO YA SWALI LA 11
6 JOYCE FROLIANI	2 6 1988	24	8	2	2	2	5	3		MGERESHO YA SWALI LA 12
7 DANIEL ALOYCE	1 99 1938	74	7	1	2	2	8			MGERESHO YA SWALI LA 13
105 JAMES ALOYCE	1 99 1979	33	5	2	1	1		1	X	MGERESHO YA SWALI LA 14
9										MGERESHO YA SWALI LA 15
10										MGERESHO YA SWALI LA 16
11										MGERESHO YA SWALI LA 17
12										MGERESHO YA SWALI LA 18

## MASHAMBA

Sehemu ya mwisho ya fomu ya T-0 ni sehemu ya kufuatilia mashamba. Sehemu hii inapaswa kujazwa sawa na sehemu ya kufuatilia mwanakaya hapo juu wakati unapoanza dodoso la kilimo. Safuwima ya 11-13 zinakupa taarifa za kutambua mashamba na zitakuwa zimeshajazwa. Kama mojawapo ya sehemu hizi itakuwa haijajazwa itakuwa ni kwa sababu mdadisi katika utafiti uliopita hakuwa amejaza hizi taarifa. Unapaswa kujaza safu wima ya 14-17 kwa kila shamba. Kama itatokea mhojiwa hafahamu, andika -99% na weka maoni katika kisanduku maalumu chini ya ukurasa.

### Safu wima ya 14

Kama kaya bado ina mamlaka juu ya shamba hili, weka -10% katika dodoso. Huna haja ya kuuliza taarifa zaidi kuhusiana na shamba hili lakini unapaswa tu kuhakikisha kuwa umeliorodhesha kwenye dodoso jipya la kilimo. Usipofanya hivi itakubidi kurudi kwenye kaya baadae

### Safu wima ya 15

Swali hili linafanana na Swali la 84 sehemu ya 3A katika dodoso la Kilimo. Linaulizia sababu ya kaya kutomiliki au kutolima tena shamba ambalo katika utafiti uliopita ilikuwa ikilimiliki/ikililima.

### Safu wima ya 16

Kama shamba liliuzwa, andika kiasi ambacho shamba hili liliuzwa. Badilisha malipo yoyote yasiyo katika fedha taslimu na andika jumla yake.

### Safu wima ya 17

Kama shamba lilichukuliwa, liligawiwa na mamlaka ya kijiji, au lilitolewa kwa mtu mwengine andika jumla ya thamani yoyote ya fidia ambayo kaya ilipokea. Badilisha kuwa katika fedha malipo yote ambayo hayakuwa katika pesa taslimu.

**Angalia kurasa inayofuata kwa mfano wa jinsi yakujaza kwa usahihi safuwima ya 14-17.**

### KWA MFANO

Hali ya umiliki/utuamiaji wa mashamba kwenye kaya Clement Aloyce imebadilika pia. Wakati wa utafiti uliopita, alikuwa na mashamba matatu, -Shamba la Kasanga, -Shamba la Mangobane, na -Shamba la Misongeni. Mwishoni mwa mwaka 2011, aliuza -Shamba la Misongeni kwa shilingi 350,000. Kwa kutumia pesa hizi alinunua shamba lingine, ambalo analiita -Shamba la Mkole Zaidi ya hiyo, kama sehemu ya zawadi ya harusi, alimpa mume wa mtoto wake wa kike -Shamba la Mangobane. Fomu ya T-0

iliyoyojazwa inaonekana hapo chini. Utagundua shamba jipy, ḍShamba la Mkoleø halikuorodheshwa. Na litaonekana tu katika dodoso jipy la Kilimo.

MASHAMBA																
11. NAMBA YA SHAMBA MWAKA 2010/2011	12. JINA LA SHAMBA	13. MAELEZO YA SEHEMU LILIPU SHAMBA	14. Bado keya ina mamileka juu ya shamba hil?	15. Kwanini shamba hili halikulimwa/kulimikiwa tena na kaya? LILIUMWA.....1 LILITOLEKA KWA MTU LILIGAWINDWA.....3 ►17 LILIGAWINDWA.....4 ►17 LILITOLEKA KWA MTU LILIGAWINDWA.....5 ►17 LILIACHWA KUKODIWA/ KUWANA MAVUNO...6 ► SHAMBA LINGINE	16. Ulipeta kiasi gani ulipouza hili shamba?	17. Ulipokea fidia ya kiasi gani?	KAMA HAKUNA, ANDIKA '0' ►SHAMBA LINGINE TSR	►SHAMBA LINGINE TSR								
1 M1 2 M2 3 M3	KASANGA MANGOBANE MISONGENI	BARABARA KUU KWENDA KULIA LIKO MAGOMBANE LIKO MISONGENI	1 2 2	5 1		0 350,000										
4																
5																
6																
7																
8																
9																
10																
11																
12																
MAONI																

## Fomu ya Kufuatilia Kaya, T-1

Fomu ya T-1 inatumika kukusanya taarifa zinazohusiana na makazi mapya ya kaya, kama kaya yote imehama kutoka kwenye makazi ya awali (kama wanakaya wote kwa pamoja wamehama).

**Maswali ya 1-3:** Maswali haya yanakusanya taarifa za kutambua kaya inayofuatiliwa. Unapaswa kuandika jina la mkuu wa kaya kama lilivyokua katika utafiti wa 2012/2013 hata kama mtu huyu amefariki au ameondoka nchini. Jina lake litatumika kuthibitisha tarakimu 7 ambazo zimetumika kuunganishia kaya na taarifa zake.

**Maswali ya 4-7 (TAARIFA KWA AJILI YA MDADISI):** Maswali haya yanakusanya taarifa juu ya mdadisi. Zingatia kuwa Swali la 7 ambalo linaluzia namba ya fomu kati ya jumla ya fomu zote zilizotumika. Kama fomu moja tu imejazwa, jibu la swali hilo litakuwa ḍFomu ya 1 kati ya 1ø Kwa mfano: kama fomu mbili au zaidi zimejazwa, inapaswa kuwa ḍFomu ya 1 kati ya Jumla ya Fomu 2ø au ḍFomu ya 2 kati ya 2ø Utapaswa kubadilisha idadi ya fomu baada ya kumaliza kujaza fomu zako kama inabidi ujaze fomu zaidi.

### Mhojiwa wa fomu T-1

Mhojiwa wa fomu T-1, **mtoe taarifa**, anaweza kuwa mtu yejote ambaye ana uelewa mzuri kuhusu makazi mapya ya kaya. Anaweza kuwa ndugu, jirani, rafiki, mwajiri wa zamani wa mwanakaya, au mwalimu wa zamani, au kiongozi wa jamii. Tafuta taarifa nzuri na kama kuna ulazima hoji zaidi ya mtu mmoja kupata picha kamili ya sehemu ilipo kaya. Katika mazingira mengine kunaweza kuwa na mtoe taarifa zaidi ya mmoja na (na T-1 zaidi ya moja) kwa kila kaya iliylengwa au inayofuatiliwa.

### Maswali ya 8-21 (UTAMBULISHO WA MTOA TAARIFA)

Maswali haya yanakusanya taarifa kuhusu mtoe taarifa ambaye anahojiwa kwa fomu T-1. Taarifa zinazokusanywa ni: jina, anuani, mahali, namba za simu, kijiji/mtaa, tarafa, wilaya na mkoa anakoishi mtoe taarifa. Hakuna sababu yoyote ya taarifa yoyote kukosekana kwa sababu inamuhusu mtoe taarifa

anayehojoja na mdadisi. Swali la 21 linaulizia uhusiano kati ya mto taarifa na mkuu wa kaya au na mwanakaya mwingine yejote.

#### **Dondoo jinsi ya kujaza taarifa zinazohusu mahali ilipo kaya / mwanakaya katika T-1 na T-2:**

1. Kama inawezekana, **anuani** inapaswa kuwa na mtaa (ikihusisha jengo au namba ya jengo), jina la EA/kijiji au mji.
2. **Taarifa za mahali** zielezee nyumba au mahali (mfano, "mita 100 kaskazini toka ofisi ya kijiji, au nyumba yenye mlango wa kijani")
3. **Sehemu ya kazi** (kama inawezekana) nakili jina la shirika, ofisi, stoo, taasisi n.k ambapo anafanya kazi. Kama mtu ni mfanyakazi wa kuhamahama (mfano mfanyakabiashara) sehemu ya kazi ielezewe yale maeneo ambayo mara nyingi huwa akienda.
4. **Namba ya simu** inaweza kuwa simu ya mezani au ya mkononi, namba za simu zithibitishwe, kuhakiki kuwa zipo hewani. Uthibitishaji ufanyike kwa uangalifu ili kutoharibu utaratibu wa mahojiano au kujenga dhana ya kutomwamini mhojiwa. Zungushia "1" baada ya kuthibitisha namba ya simu na "2" kama namba haikuthibitishwa.
5. Majina ya **EA/kijiji, kata, wilaya na mkoa** yanapaswa kuulizwa na kuandikwa, ingawaje unaweza usiwe unafahamu mageresho yake rasmi.

**Maswali ya 22-35 (ANUANI YA SASA YA KAYA INAYOFUATILIWA):** Maswali haya yanaulizia kuhusu eneo jipya la makazi ya kaya. Hii itakuwa ndiyo taarifa ya kwanza kutumiwa na mdadisi/mfuatiliaji ambaye ataenda kuwasiliana na kaya kwenye makazi mapya. Ni muhimu sana kupata kila taarifa hii kwa undani kadri mto taarifa atakavyojibu. Fuata dondoo zilizolezewa awali kupata taarifa za mahali.

**Maswali ya 36-49 (MAHALI PA SASA WALIPO WANAKAYA WENGINE):** Maswali haya yanaulizia anuani na mahali alipo mwanakaya mwingine. Swali hili litahusika kama baadhi ya wanakaya wanafahamika wameenda sehemu nyingine tofauti. Fuata dondoo/maelekezo yaliyoelezewa mwanzoni kupata taarifa za mahali za wanakaya wengine. Maswali haya pia yanaulizia kama mahali alipo mwanakaya mwingine ni katika EA/kijiji hicho hicho alipo mkuu wa kaya.

**Maswali ya 50-63 (TAARIFA ZA MAWASILIANO KWA MTOA TAARIFA KATIKA ENEO JIPYA):** Maswali haya yanakusanya taarifa za mtu mwingine ambaye anaweza kuwa ni mto taarifa aliye katika eneo la makazi mapya ya mwanakaya: **mto taarifa katika eneo la makazi mapya**. Kwa mfano kaya husika inayotafutwa imehamia Dar es Salaam. Hivyo, swali hili pia linakusanya taarifa za mtu ambaye pia yupo Dar es Salaam ambaye anaweza kuwa na ufhamu mzuri kuhusu yalipo makazi mapya ya kaya. Dhumuni la swali hili ni kwamba mdadisi anapokwenda Dar es salaam kujaribu kutafuta kaya, anaweza kuwasiliana na mahali alipo mto taarifa katika eneo jipya la kaya ambaye anaweza kumsaidia mdadisi kuipata kaya.

**Maswali ya 64-78 (TAARIFA ZA MAWASILIANO SEHEMU YA KAZI/SHULE KATIKA ENEO JIPYA):** Maswali haya yanakusanya taarifa za mahali anapofanya kazi au shulen kwa mto taarifa katika eneo jipya la anayetafutwa. Fuata maelekezo yaliyoelezewa awali ili kupata taarifa za mahali. Kupata taarifa kuhusu sehemu anapofanya kazi au shulen ni muhimu sana kwa sababu wakati mwingine ni rahisi kwa mfuatiliaji kumpata mto taarifa katika sehemu hizi kuliko nyumbani.

**Mawali ya 79-93 (TAARIFA ZA MAWASILIANO SEHEMU YA KAZI/SHULE KATIKA ENEO JIPYA):** Maswali haya yanakusanya taarifa juu ya mtu mwingine yejote katika eneo jipya ambaye anafanya kazi au anasoma na mwakaya anayefuatiliwa katika eneo jipya, na anaweza kumpatia mdadisi taarifa zake, mahali ilipo kaya. Fuata maelekezo yaliyoelezewa awali kupata taarifa ya mahali pa kazi pa mwanakaya.

**Maswali ya 94-107 (TAARIFA ZA MAWASILIANO KWA MTOA TAARIFA KATIKA ENEO LA AWALI):** Maswali haya yanakusanya taarifa za kuhusiana na mtu mwingine katika eneo ambaye anaweza kumpatia mdadisi taarifa za mahali ilipo kaya. Fuata maelekezo ya awali kupata taarifa muhimu za alipo mtoa taarifa huyu muhimu.

**Swali la 108 (RAMANI):** Tumia nafasi katika Swali la 108 kuchora ramani itakayotuwezesha kuitafuta kaya katika eneo jipya ilipohamia. Ramani hiyo inatakiwa iwe rahisi kusomeka, na inayoweza kutumika. Kwa mfano, njia ya kwenda ilipohamia kaya inachorwa, si lazima ianze toka katika EA/kijiji cha awali, inaweza kuonyesha njia ya kuelekea kwenye kaya kutoka sehemu yoyote yenye alama inayofahamika vizuri.

### **Swali la 109**

Tumia nafasi katika swali la 109 kuandika uelekeo wa makazi mapya ya kaya, au maelezo kuhusu eneo ambalo lipo karibu na makazi mapya ya kaya, maelezo yatakayoandikwa katika nafasi hii yafanane na ramani iliyochorwa katika swali la 108. Maelezo yahusishe alama muhimu zilizo karibu, taarifa za kijiografia, mitaa iliyo karibu (kama ni eneo la mjini) na taarifa nyingine ambazo mtoa taarifa ataona ni za muhimu na zitamsaidia mdadisi/mfatiliaji kuipata kaya.

## **TATHMINI YA TAARIFA**

Mwisho wa mahojiano ya fomu ya T-1, msimamizi wako atapaswa kwanza kufanya tathmini iwapo taarifa zilizotolewa ni za kutosheleza kuipata kaya. Mageresho ni kama ifuatavyo:

1. Kama taarifa ni za kutosheleza kupata yalipo makazi mapya ya kaya, na kaya imehamia mwendo wa saa moja toka EA/kijiji cha awali. Mdadisi au timu inapaswa kuwasiliana na kuihoji kaya kabla timu haijaondoka kwenye EA/kijiji.
2. Kama taarifa ni za kutosheleza kupata yalipo makazi mapya ya kaya, na kaya imehamia mwendo wa zaidi ya saa moja toka EA/kijiji cha awali. Katika hali hii, msimamizi anapaswa kuamua kati ya yafuataao:
  - a) Taarifa kwa hakika zinatosheleza. Kama sio, unapaswa kujaza fomu nyingine ya T-1 kwa kumhoji mtoa taarifa mwingine wa uhakika .
  - b) Eneo jipya kaya la kaya kwa hakika lipo umbali wa zaidi ya saa moja kutoka EA/kijiji cha awali (pasipoendeka kwa ufuatiliaji wa ndani ya eneo). Kama sio, lazima ufanye mawasiliano na kaya na kuihoji kabla timu haijaondoka kwenye EA/kijiji.
- 3 Kama taarifa za mahali yalipo makazi mapya ya kaya hazitoshelezi kuweza kuipata kaya. Katika hali hii unatakiwa kuhoji fomu nyingine ya T-1 kwa kuwahoji watoa taarifa wengine muhimu .

## **KUKATAA**

Ikiwa T-1 kaya inayofatiliwa imepatikana katika eneo jipya lakini wakakataa kuhojiwa, weka alama ya ~~XØ~~ kwenye kisanduku husika.

Utapaswa kujaza fomu T-1 kadri itakavyowezekana kupata taarifa zinazotosheleza kuipata kaya katika eneo lake jipya. Kumbuka, inawezekana ikawa ni timu yako itakayowajibika kuwafatilia wahojiwa katika maeneo yao mapya.

## **Fomu ya Kufuatilia Wanakaya, T-2**

Fomu T-2 ni fomu inayotumika kukusanya taarifa kuhusu eneo jipya alipohamia **mwanakaya**, aliyejewa kwenye kaya ya awali ya NPS2 (Mtu anayefuatiliwa). Fomu hii hapaswi kujaziwa mwanakaya mwenye umri chini ya miaka 15. Tambua kwamba inaweza kutokea kwamba umri wa mtoto uliotajiwa na mtoa taarifa haulingani na umri uliopo kwanye fomu ya T-0. Kama mtoa taarifa atakwambia mwanakaya huyo ana

umri chini ya miaka 15, lakini fomu ya ufuutiliaji inaonyesha ana miaka 15 au zaidi, utahitaji kujaza fomu ya T-2. Viongozi kutoka makao makuu watafanya maamuzi kama mtoto huyo anastahili kufuatiliwa au hapana. Kama haukumjazia fomu za T-2 mtoto wa miaka 15, utahitajika kurudi kwenye eneo kujaza fomu hizo.

### **Fomu za T-2 zinapaswa kujazwa kabla timu haijaondoka kwenye EA/Kijiji.**

**Maswali ya 1-4:** Maswali haya yanakusanya taarifa za kuitambua kaya. Unapaswa kuandika majina yao, tarakimu 16 za mageresho ya utambulisho na tarakimu mbili za namba za mstari kwenye orodha ya wanakaya kwa mwaka 2008/2009. Taarifa zote hizi zitapatikana katika fomu ya T-0.

**Maswali ya 5-8 (TAARIZA ZA MDADISI):** **Maswali haya yanakusanya taarifa za mdadisi.** Zingatia kuwa Swali la 8 ambalo linaulizia namba ya fomu kati ya jumla ya fomu zote zilizotumika. Kama fomu moja tu imejazwa, jibu la swali hilo litakuwa  $\frac{1}{\text{Fomu ya 1 kati ya 1}}$  Kwa mfano: kama fomu mbili au zaidi zimejazwa, inapaswa kuwa  $\frac{1}{\text{Fomu ya 1 kati ya Jumla ya Fomu 2}}$  au  $\frac{2}{\text{Fomu ya 2 kati ya 2}}$  Utapaswa kubadilisha idadi ya fomu baada ya kumaliza kujaza fomu zako kama inabidi ujaze fomu zaidi.

### **Mhojiwa kwa Fomu ya T-2**

Mhojiwa wa fomu ya T-2, yaani **mtoya taarifa**, anaweza kuwa mtu yoyote mwenye taarifa za uhakika kuhusu eneo jipya alipohamia anayefuatiliwa. Anaweza kuwa ndugu wa anayefuatiliwa, jirani, rafiki, mwajiri wa zamani, mwalimu wake wa zamani, au mwenyekiti wa kijiji/mtaa alipokuwa anaishi anayefuatiliwa. Unatakiwa kukusanya taarifa sahihi na kama unaweza wahoji watu kadhaa ili kupata taarifa kamili juu ya sehemu alipo mtu anayefuatiliwa. Katika mazingira mengine unaweza ukawa na mtoya taarifa zaidi ya mmoja (na zaidi ya fomu moja ya T-2) ya kila anayefuatiliwa.

**Maswali 9-22 (UTAMBULISHO WA MTOYA TAARIFA):** Sehemu hii inakusanya taarifa kuhusu **mtoya taarifa** anayehojiwa kwa fomu ya T-2. Taarifa zinazokusanywa ni: jina, anuani, maelezo alipo mtoya taarifa, namba ya simu, mtaa/kijiji, kata, wilaya na mkoa anapoishi mtoya taarifa. Hakuna sababu yoyote itakayofanya sehemu ya taarifa hii ikosekane kwani mtoya taarifa mwenyewe ndiye anayehojiwa na mdadisi. Swali la 22 linaulizia uhusiano kati ya mtoya taarifa na mtu anayefuatiliwa.

**Maswali ya 23-25 (MAWASILIANO YA AWALI YA ANAYEFUATILIWA):** Maswali haya yanaulizia kuhusu mara ya mwisho ambapo mtoya taarifa alikuwa na mawasiliano na mtu anayefuatiliwa. Taarifa hii ni muhimu katika kujua ni kwa kiasi gani taarifa zilizopatikana ni za hivi karibuni. Pia yanaulizia njia iliyotumika katika mawasiliano kati ya mtoya taarifa na mtu anayefuatiliwa. Mara ambazo mtoya taarifa amewasiliana na anayefuatiliwa tangu amehama eneo la awali pia inauliziwa. Kama mtoya taarifa ana mawasiliano ya mara kwa mara anayefuatiliwa (zaidi ya mara moja kwa mwezi), chagua  $\frac{1}{\text{Kama wanawasiliana, lakini chini ya mara moja kwa mwezi}}$  (labda mara moja kwa mwezi), chagua  $\frac{2}{\text{Kama mtoya taarifa na anayefuatiliwa, hawana mawasiliano ya mara kwa mara (inawezekana mara moja kwa mwaka)}}$  chagua  $\frac{3}{\text{Kama hawana mawasiliano kabisa tangu ahame eneo la awali, chagua 4}}$

**Maswali ya 26-46 (MAHALI ALIPO KWASASA ANAYEFUATILIWA):** Maswali haya yanaulizia kuhusu sehemu anayoishi mtu anayefuatiliwa. Taarifa hizi zitakuwa ni za kwanza zitakazotumiwa na mdadisi/mfuutiliaji ambaye atawasiliana na anayefuatiliwa katika eneo lake jipya la makazi. Ni muhimu sana kupata hata taarifa kidogo za undani kwa kadiri mtoya taarifa anavyoweza kutoa. Kwa mfano, unaweza kumuuliza mtoya taarifa angefanya nini kama atahitaji kuwasiliana na huyu mtu anayefuatiliwa. Kuna namba ya simu yoyote, anuani ya barua pepe, n.k. Fuata maelekezo uliyopewa awali kupata taarifa za sehemu alipo anayefuatiliwa. Swali la 30 linamtaka mtoya taarifa kuelezea baadhi ya vitu muhimu/maarufu vilivyo karibu na eneo la mtu anayefuatiliwa ambavyo vitawenza kurahisisha upatikanaji wa anayefuatiliwa. Inaweza kuwa kiwanda mashuhuri katika eneo hilo, msikiti, kanisa, shule, alama za asili kama (mto, makutano ya barabara kuu n.k.). Swali la 43 linauliza sababu ya anayefuatiliwa kuhama meneo/makazi yake ya awali. Swali la 44 linaulizia lini mtu anayefuatiliwa aliondoka kwenye maeneo ya makazi yake ya awali na Swali la 45 linaulizia ni lini anayefuatiliwa alihamia kwenye makazi mapya. Swali la 46 linamtaka mtoya taarifa kuorodhesha sehemu ambazo mtu anayefuatiliwa alishi baada ya kuondoka sehemu yake ya awali (wakati wa NPS 2) na kabla hajahamia makazi yake mapya ya sasa hivi. Kwa mfano, labda mtu anayefuatiliwa

aliishi kwa ndugu yake kabla ya kupata sehemu yake binafsi ya kuishi. Hivyo, huyu ndugu atakuwa ni mtoa taarifa muhimu.

**Maswali ya 47-56 (UTAMBULISHO MWINGINE WA ANAYEFUATILIWA):** Maswali ya 47-56 yanaulizia sehemu zinazopendelewa na mtu anayefuatiliwa, inawezakwa ikawa ni palipokuwepo makazi yake ya awali au palipo na makazi yake mapya. Ni msikiti au kanisa gani ambalo anayefuatiliwa alikuwa anakwenda katika makazi yake ya awali, au anapokwenda katika eneo la makazi yake mapya? Je, kuna migahawa yoyote, vibanda vya chakula, baa, klabu, vikundi vya maombi ambavyo anayefuatiliwa huhudhuria? Je, kuna saluni za kike zozote, au kwa kinyozi alipokuwa akienda? Andika majina na anuani za sehemu hizi kwa undani. Hizi ndizo sehemu zote ambapo wewe au mfuatiliaji anaweza kupata mtoa taarifa muhimu ambaye anafahamu mtu anayefuatiliwa. Swali la 48 linaulizia majina mengine yanayotumiwa na mtu anayefuatiliwa kama vile jina la ukoo, jina la kikristo, jina la utani. Watoa taarifa tofauti wanaweza kumfahamu anayefuatiliwa kwa majina tofauti. Swali la 49 linaulizia sifa nyingine zinazoweza kusaidia kumtambua mtu anayefuatiliwa. Kwa mfano aina gani ya michoro (tattoos) alizonazo anayefuatiliwa na ziko sehemu gani? Je, mtu anayefuatiliwa ana mtindo gani wa nywele, miwani ya macho? Je, kuna miondoko/kutembea maalum au uongeaji wa namna fulani. Mtoa taarifa anaweza kumuelezea vipi mtu anayefuatiliwa kwa mtu ambaye hajawahi kukutana na huyu anayefuatiliwa? Swali la 50 linaulizia lini, kwa ufahamu wa mtoa taarifa, mtu anayefuatiliwa ametembelea eneo/kijiji? Ni nini lengo la kutembelea eneo/kijiji? Biashara? Kutembelea familia? Likizo za kidini? Nani alikutana na anayefuatiliwa alipotembelea eneo/kijiji? Taarifa hizi ni muhimu katika kupata watoa taarifa wengine. Maswali ya 52-53 yanaulizia ni lini, kwa uelewa wa mtoa taarifa mtu anayefuatiliwa atatembelea tena eneo/kijijini. Nini yatakuwa madhumuni ya matembezi yake kwenye eneo/kijijini, biashara? Familia? Likizo za kidini? Atakutana na nani atakapokuja? Swali la 53 linaulizia jina la mwenza wa mtu anayefuatiliwa, kama mlengwa ameo/ameolewa. Kama inawezekana, lipatikane jina kamili la mwenza kabla hawajaoana ili kupata jina lake ukoo. Inawezekana kuwa watu katika eneo jipya la anayefuatiliwa, hawamjui mtu huyo na badala yake wanamfahamu mwenza wake au ndugu wa mwenza.

**Maswali ya 57-69 (TAARIFA ZA MAWASILIANO YA SHULE/ SEHEMU YA KAZI MAHALI ALIPOHAMIA):** Maswali haya yanaulizia kama mtu anayefuatiliwa kwa sasa yupo shule au kazini. Kama anayefuatiliwa kwa sasa yupo shule, na kama jibu ni ḋndiyoꝝ kusanya taarifa kuhusiana na shule. Lazima uulize jina kamili la shule kwa kadri inavyowezekana. Ulizia jina la mwalimu/mwalimu mkuu, namba za simu za shule au za mwalimu/mwalimu mkuu na anuani ya shule. Kama anayefuatiliwa hayupo shule, fuata maelekezo na nenda Swali la 63. Kama anayefuatiliwa kwa sasa anafanya kazi (yupo kazini sehemu ingine), na jibu ni ḋndiyoꝝ chukua taarifa za mahali pa kazi. Ulnapaswa kuulizia kazi ya sasa/weledi wa mtu anayefuatiliwa, jina la sehemu ya kazi, jina la msimamizi wake (kama inawezekana), namba ya simu ya mahali pa kazi, na anuani. Kama anayefuatiliwa kwa sasa hafanyi kazi , fuata maelekezo uende Swali la 70.

**Maswali ya 70-98 (TAARIFA ZA MAWASILIANO KWA WATOA TAARIFA MUHIMU):** Maswali haya yanaulizia mpaka majina matatu ya watu wenye ushawishi mkubwa, aidha katika EA/kijiji cha zamani au kipyu ambazo zinaweza kumuongoza anaehoji kumpata mtu anayefuatiliwa. (Majina ya watoa taarifa muhimu yanaulizwa katika maswali ya 71, 80 na 90). Kwa mfano, je, kuna mtu ambaye mtu anayeheshimiwa sana na anayefuatiliwa katika eneo la makazi ya zamani au mapya. Unaweza kumuuliza mtu huyu juu ya yule anayefuatiliwa, au ye ye mwenyewe anaweza kuwasiliana na anayetafutwa na kumshawishi anayefuatiliwa kuwasiliana na wewe au na timu.

**Maswali ya 99-100 (WANAKAYA WALIOONDOKA NA ANAYEFUATILIWA):** Maswali haya yanauliza kuhusu wanakaya walioondoka na anayefuatiliwa ambao walikuwa wakiishi pamoja wakati wa utafiti uliopita. Mfano Mtu na kaka yake waliondoka pamoja kwenda Dar es salaam kutafutakazi. Swali la 99 linauliza kama kuna mwanakaya ye yote aliondoka na anayefuatiliwa. Kama ndiyo jaza swali la 100 kwa majina na namba zao za kaya za mwaka wa 2 wa utafiti. Fomu za T-2 zinahitajika kujazwa kwa kila mwanakaya ambaye ameondoka na anayefuatiliwa, lakini taarifa imuwezeshe mdadisi/ mfuatiliaji kufahamu kwamba wanakaya kadhaa wanaweza kupatika eneo moja. Hii itamsaidia mdadisi/ mfuatiliaji kujumuisha taarifa hizo ili kuweza kumpata anayefuatiliwa.

**Swali la 101 (RAMANI):** Tumia nafasi katika Swali la 101 kuchora ramani itakayosaidia kupata mahali yalipo makazi mapya ya kaya. Ramani hiyo inatakiwa iwe rahisi kusomeka na yenyekusaidia. Kwa mfano, kama njia ya kwenda kwenye kaya inachorwa, sio lazima ianzie kwenye EA/kijiji cha awali, inaweza kuonyesha njia ya kuelekea kwenye kaya kutoka kwenye sehemu yoyote inayofahamika vizuri kama vile kanisa, msikiti n.k.

**Swali la 102 (UELEKEO):** Tumia nafasi katika swali la 102 kuandika uelekeo wa makazi mapya ya kaya, au maelezo kuhusu eneo ambalo lipo karibu na makazi mapya ya kaya, maelezo yatakayoandikwa katika nafasi hii yafanane na ramani iliyochorwa katika swali la 101. Maelezo yahushe alama muhimu zilizo karibu, taarifa za kijiografia, mitaa iliyo karibu (kama ni eneo la mjini) na taarifa nyingine ambazo mtoa taarifa ataona ni za muhimu na zitamsaidia mdadisi/mfatiliaji kuipata kaya.

### Muhimu kwa Msimamizi

Mwishoni mwa mahojiano ya T-2, msimamizi wako atahitajika kufanya tathimini kuona kama taarifa zinatosheleza kumpata mwanakaya anayefuatihi. Mageresho ni kama ifuatavyo:

1. Kama taarifa zinatosheleza kumpata mtu anayefuatihi, na kama mlengwa amehamia sehemu ingine iliyo na umbali wa ndani ya saa moja kutoka EA/kijiji cha awali, wewe au timu yako mnalazimika kumhoji anayefuatihi kabla timu haijaondoka kwenye eneo hilo.
2. Kama taarifa zinatosheleza kumpata mtu anayefuatihi, na kama mlengwa amehamia sehemu ingine iliyo na umbali wa zaidi ya saa moja kutoka EA/kijiji cha awali. Katika hali hiyo kiongozi wako unapaswa kufanya kuamua kati ya yafuatayo:
  - a. Taarifa kwa hakika zinatosheleza. Kama sio, unapaswa kujaza fomu nyingine ya T-2 kwa kuwahoji watoa taarifa wengine.
  - b. Eneo jipya kaya la kaya kwa hakika lipo umbali wa zaidi ya saa moja kutoka EA/kijiji cha awali (pasipoendeka kwa ufuatiliaji wa ndani ya eneo). Kama sio, lazima ufanye mawasiliano na anayefuatihi na ahojiwe kabla timu haijaondoka kwenye EA/kijiji.
3. Kama taarifa hazitoshelezi kumpata mlengwa, katika hali hii unapaswa kujaza fomu nyingine ya T-2, kwa kuwahoji watoa taarifa wengine wa uhakika.

### KUKATAA

Ikiwa T-2 mlengwa amepatikana katika eneo jipya lakini wakakataa kuhojiwa, weka alama ya X kwenye kisanduku husika.

*Fomu T-1 na T-2, ni zana kuu zinazotumika kutafuta mahali kaya na wanakaya walipohamia. Unapaswa kujaza fomu hizi ukiwa na wazo moja kichwani: kuhakikisha kwamba taarifa zinazokusanywa zitatosheleza kuwapata waliohamu tu. Fikiria kama miezi miwili kuanzia sasa utaombwa kutafuta kaya/mwanakaya kwa kutumia fomu hizi tu. Utakuwa tayari kufanya kazi hii kwa kutumia fomu hizi? Kama hapana, basi kazi yako ya ujazaji wa fomu hizi utakuwa hujaifanya vizuri.*

## Mifano ya Ufuatiliaji wa Kaya / Wanakaya

*Yafuatayo ni mambo unayoweza kukutana nayo, na mifano ya namna ya kushughulika nayo kwa kila jambo.*

Hali ya 1: Angalau mwanakaya mmoja amepatikana anaishi kwenye makazi ya utafiti uliopita.

1. Jaza Fomu T-0 kuona kama kuna mwanakaya yeyote aliyezama au kufariki.
2. Kwa yeyote aliyezama, fanya mahojiano kwenye fomu ya T-2, na fuata maelekezo kwenye safu wima 8 ya T-0.
3. Endelea na Dodoso la Kaya.

## MFANO WA 1

*Kaya ya NPS ya mwaka wa 3 ilikuwa:* John (ID 01), Christina (ID 02, mke wake), na Michael (ID 03, mtoto wao wa kiume, mwenye miaka 9). Mwaka 2014, wanakaya wote watatu bado wanaishi kwenye makazi yale yale na wanakaya 5 walioingia kwenye kaya yao kuishi nao.

1. Jaza Fomu T-0. John ni mhojiwa (au Christina).
2. Huhitaji kujaza Fomu T-1 au T-2 kwa kuwa wanakaya wote wa awali bado wapo kwenye kaya.
3. Endelea kujaza dodoso la kaya, na John akiwa kama mkuu wa kaya.

## MFANO WA 2

*Kaya ya NPS ya mwaka wa 3 ilikuwa:* Ali (ID 01), Amina (ID 02, mke wake), na Khamis (ID 03, mtoto wao wa kiume, mwenye miaka 17). Mwaka 2013, Ali na Amina wamehamia mkoa mwingine. Khamis bado anaishi makazi yale yale.

1. Jaza Fomu T-0. Khamis atakuwa mhojiwa.
2. Jaza Fomu T-2 kwa ajili ya Ali. Andika katika swalii la 98 kwenye fomu ya T-2 ya Ali kuwa aliondoka na Amina.
3. Jaza Fomu T-2 kwa ajili ya Amina. Andika katika swalii la 98 kwenye fomu ya T-2 ya Amina kuwa aliondoka na Ali.
4. Endelea na mahojiano ya dodoso la kaya. Khamis anaweza au anaweza asiwe mkuu wa kaya. Tumia utaratibu ule ule ambaa ungetumika kujaza orodha ya wanakaya.

## MFANO WA 3

*Kaya ya NPS ya mwaka wa 3 ilikuwa:* Frank (ID 01) na Joyce (ID 02, dada yake). Mwaka 2014, Frank bado anaishi kwenye makazi yale yale na mke wake mpya na mtoto. Joyce ameenda jijini kufanya kazi benki.

1. Jaza Fomu T-0. Frank atakuwa ni mhojiwa.
2. Jaza Fomu T-2 kwa ajili ya Joyce.
3. .... Endelea na dodoso la kaya na Frank kama mkuu wa kaya.

## MFANO WA 4

*Kaya ya NPS ya mwaka wa 3 ilikuwa:* Juma (ID 01), mke wake Mariamu (ID 02), na mtoto wao Hassan (ID 03, mwenye miaka 15). Mwaka 2014, wakati timu inafika kijijini, walimkuta Mariam na Hassan kwenye kaya ya awali lakini Juma hakuwepo kwa mwezi mmoja kwa ajili ya kazi yake ya udereva.

1. Jaza Fomu T-0. Mariam atakuwa ni mhojiwa.
2. Endelea na dodoso la kaya na Mariam kama mhojiwa. Juma bado ni mkuu wa kaya hata kama hakuwepo kwa muda. Inatakiwa anakiliwe hakuwepo kwa muda katika orodha ya wanakaya (Sehemu B). Hutakiwi kujaza fomu ya T-2 kwa ajili ya Juma kwasababu hayupo tu kwa muda na atarudi katika kaya ndani ya majuma machache.

**Hali ya 2: Hakuna mwanakaya aliyepatikana kwenye makazi ya awali. Wanakaya wote wanaishi pamoja (hawajabadilika) kwenye makazi mapya yaliyopo zaidi ya saa 1 kutoka kwenye makazi yao ya awali.**

1. Usijaze fomu ya T-0.
2. Endelea na mahojiano kwa kutumia Fomu ya T-1.

## **MFANO WA 5**

*Kaya ya NPS ya mwaka wa 3 ilikuwa:* Juma (ID 01), Mariam (ID 02, mke wake), Rehema (ID 03 mtoto wao), Happy (ID 04 mtoto wao). Mwaka 2014, Juma na Mariam na watoto wao walihamia kijiji kingine katika wilaya nyingine (masaa 5 kwa gari) baada ya Juma kurithishwa ardhi huko.

1. Jaza Fomu T-1 kwa kaya.
2. Usiwasiliane na kaya wakati timu ikiwa kwenye EA/Kijiji hicho cha awali kwa kuwa walipohamia ni mbali sana. Timu nyingine ya NPS iliyo katika maeneo waliyohamia kaya hii watajaza fomu ya T-0 na kufanya mahojiano haya.

**Hali ya 3: Hakuna mwanakaya aliyepatikana kwenye makazi ya awali. Wanakaya wote wanaishi pamoja (hawajabadilika) kwenye makazi mapya, na makazi mapya bado yapo mwendo wa saa 1 kutoka kwenye EA/kijiji kwenye makazi yao ya awali.**

1. Usijaze fomu ya T-0 kwenye makazi ya awali. Utaijaza fomu hii utakapofika kwenye makazi mapya.
2. Jaza Fomu ya T-1 kwa kufanya mahojiano na mtoa taarifa wa uhakika. Kama inawezekana, muombe huyu mhojiwa akupeleke kwenye kaya hiyo. (Ingawa hata katika hali hii **unapaswa** kujaza fomu T-1, hata kama ina taarifa chache sana).
3. Fanya mawasiliano na ihoji kaya mkiwa bado kwenye EA/kijiji.

## **MFANO WA 6**

*Kaya ya NPS ya mwaka wa 3 ilikuwa:* Mohamed (ID 01), Salum (ID 02, kaka yake). Mwaka 2014, Mohamed na Salum wamehamia sehemu nyingine kwenye kijiji kile kile.

1. Jaza Fomu T-1 kwa ajili ya kaya.
2. Wasiliana na ihoji kaya wakati timu ikiwa bado kwenye kijiji.

**Hali ya 4: Hakuna mwanakaya aliyepatikana kwenye makazi ya awali ya kaya. Wanakaya wote hawaishi tena pamoja. Angalau mwanakaya mmoja wa miaka zaidi ya 15 anaishi sehemu nyingine ambayo ipo mwendo wa saa 1 kutoka EA/kijiji cha awali.**

1. Jaza Fomu T-1 kwa sehemu ambayo wanakaya wengi wanaishi kwa sasa. Kama wote wanaishi sehemu tofauti tofauti, jaza fomu ya T-2 kwa kila mwanakaya.
2. Wasiliana na ufanye mahojiano na kaya ambayo bado ipo mwendo wa saa 1 kutoka kwenye EA/Kijiji cha awali. Unapaswa kujaza Fomu ya T-0 na mwanakaya huyu ( wa kaya ya awali).

## **MFANO WA 7**

*Kaya ya NPS ya mwaka wa 3 ilikuwa:* David (ID 01), Grace (ID 02, mke wake), Aaron (ID 03, mtoto wa kiume, miaka 18), James (ID 04, mtoto wa kiume, miaka 14), Adia (ID 05, mtoto wa kike, miaka 10) . Mwaka 2014, Aaron amehamia mkoaa mwingine kwa ajili ya kazi, David, Grace, James na Adia wamehamia kijiji cha jirani/karibu.

1. Jaza Fomu ya T-1 kwa ajili ya kaya.
2. Jaza fomu ya T-2 kwa ajili ya Aaron.
3. Wasiliana na kaya na jaza fomu ya T-0 (pengine na David) .
4. Hoji kaya ya David wakati timu ikiwa bado kwenye kijiji.

## **MFANO WA 8**

*Kaya ya NPS ya mwaka wa 3 ilikuwa:* Samuel (ID 01), Anna (ID 02, mke wake), James (ID 03, mtoto wa kiume, miaka 20), Peter (ID 04, mtoto wa kiume, miaka 14). Mwaka 2014, Samuel amehamia mji mwingine, Anna amerudi kwa mama yake mkoaa mwingine, James ameondoka nyumbani lakini bado anaishi kwenye au karibu na EA/kijiji cha awali. Peter ameondoka na Anna.

1. Jaza Fomu ya T-2 kwa ajili ya James.
2. Jaza Fomu ya T-2 kwa ajili ya Samuel.
3. Jaza Fomu ya T-2 kwa ajili ya Anna. Nakili katika swalii la 99 kwenye fomu ya T-2 ya Anna kuwa ameondoka na Peter.
4. Huitaji kujaza fomu ya T-2 kwa ajili ya Peter kwasababu ana miaka chini ya 15.
5. Wasiliana na kaya na jaza fomu ya T-0 (pengine na James)
6. Hoji kaya ya James wakati timu ikiwa bado kwenye kijiji.

## **MFANO WA 9**

*Kaya ya NPS ya mwaka wa 3 ilikuwa:* Said (ID 01), Aisha (ID 02, mke wake), Musa (ID 03, mtoto wa kiume, umri miaka 28), Aziz (ID 04, mtoto wa kime, umri miaka 12). Mwaka 2014, Said na Aisha wamehamia mji mwingine. Musa alihama na mjomba wake lakini bado yupo kwenye EA/kijiji au katika EA/kijiji cha karibu. Martin alihama na babu yake lakini bado yupo kwenye EA/kijiji au katika EA/kijiji cha karibu.

1. Jaza Fomu ya T-0 kwa ajili ya Musa.
2. Jaza Fomu ya T-1 kwa ajili ya Said.
3. Jaza fomu ya T-2 kwa ajili ya Aisha. Nakili katika swalii la 99 kwenye fomu ya T-2 ya Aisha kuwa ameondoka na Aziz.
4. Huitaji kujaza fomu ya T-2 kwa ajili ya Aziz kwasababu ana miaka chini ya 15.
5. Wasiliana na kaya na jaza fomu ya T-0 (pengine na Musa).
6. Hoji kaya ya Musa wakati timu ikiwa bado kwenye kijiji/EA Mjomba wa Musa sasa atakuwa mkuu wa kaya ya Musa ya sasa.

**Hali ya 5: Hakuna mwanakaya anayekutwa kwenye makazi ya awali.** Wanakaya wote hawaishi pamoja. Hakuna mwanaka mwenye miaka zaidi ya 15 anayeishi katika sehemu mpya ambayo bado ni sehemu inayofikika ndani ya EA/kijiji. Angalau mwanakaya mmoja mwenye miaka chini ya 15 anaishi sehemu mpya ambayo bado inafikika.

1. Jaza Fomu ya T-1 kwa sehemu ambayo wanakaya walio wengi wanaishi kwa sasa. Kama kila mmoja anaishi sehemu tofauti, jaza fomu ya T-2 kwa kila mwanakaya. Jaza katika swalii la 98

- kwenye fomu ya T-2 kama kuna wanakaya wowote walioondoka pamoja. Tumia kaya mpya ya watoto au vyanzo vingine vya uhakika kutoa taarifa.
- 2 Jaza fomu ya T-0 kwenye kaya ya mtoto.
  - 3 Usijaze dodoso la kaya kwenye kaya ya mtoto. Ni kwa kaya tu ambazo zina angalau mwanakaya mmoja mwenye miaka 15 au zaidi ndizo zitakazostahili kufuatiliwa ndani ya eneo.

## MFANO WA 10

*Kaya ya NPS ya mwaka wa 3 ilikuwa:* Emmanuel (ID 01), Grace (ID 02, mke), Agnes (ID 03, mtoto wa kike, umri miaka 8). Mwaka 2014, Emmanuel na Grace wamekwendwa Dar es Salaam kutafuta kazi zenyenye kulipa zaidi. Agnes amebakia na bibi yake kijijini na anahudhuria shule.

- 1. Jaza Fomu ya T-1 kwa Emmanuel na Grace.
- 2. Hauhitaji kujaza fomu ya T-2 kwa ajili ya Agnes kwa sababu anaumri chini ya miaka 15.
- 3. Jaza Fomu ya T-0 kwa Agnes. Usihoji dodoso la kaya kwenye kaya mpya ya Agnes.

## MFANO WA 11

*Kaya ya NPS ya mwaka wa 3 ilikuwa:* Godfrey (ID 01), Zuhura (ID 02, mke wake), William (ID 03, mtoto wa kiume, miaka 2). Mwaka 2014, Godfrey na Zuhura wote wamefariki, na mtoto ameenda kuishi na bibi yake katika kaya nyingine hapo hapo kwenye EA/kijiji.

- 1. Hata kama William ndiye mwanakaya pekee aliyebakia kutoka kaya ya awali, hauhitaji kujaza fomu ya T-2 kwa ajili ya William kwa sababu ana umri chini ya miaka 15.
- 2. Jaza Fomu ya T-0 na mwenyekiti wa mtaa/kijiji, bibi yake William au mtu ye yeyote mwenye taarifa za uhakina.

**Usijaze dodoso la kaya kwenye kaya hii mpya ya mtoto.**

**Hali ya 6:** Hakuna mwanakaya aliyekutwa kwenye makazi ya kaya ya awali. Wanakaya wote hawaishi pamoja. Hakuna mwanakaya mwenye miaka zaidi ya 15+ anayeishi katika sehemu mpya ya makazi inayofikika ndani ya EA/eneo.

- 1. Jaza Fomu ya T-0 kwa kutumia chanzo cha uhakika kwenye EA/kijijini.

## MFANO WA 12

*Kaya ya NPS ya mwaka wa 3 ilikuwa:* Hassan (ID 01), Fatuma (ID 02, mke wake), Baraka (ID 03, mtoto wa kiume, miaka 25), Ismali (ID 04, mtoto wa kiume, miaka 24). Mwaka 2014, Hassan mefariki, Fatuma amerudi kijijini kwake kuishi na mmojawapo wa watoto wake wa kike, Baraka ameoza na kwenda mkoaa mwingine, na Ismali amepata ufadilili kwenda kusoma Uingereza.

- 1. Jaza Fomu ya T-0 kwa kumtumia mwenyekiti wa mtaa/kijiji.
- 2. Jaza Fomu T-2 ya Fatuma.
- 3. Jaza Fomu T-2 ya Baraka.
- 4. Jaza Fomu T-2 ya Ismali.

## Hali ya 7: Wanakaya wote wamefariki.

Hii hutokea mara chache sana, na zaidi kwa wahojiba wenyewe umri mkubwa wanaoishi wenye. Kuwa mwangalifu sana na watoa taarifa wanaokuambia kuwa wanakaya wote wamefariki. Katika majaribio ya zoezi la ufuatiliaji kaya/wanakaya, Ilitokea mhojaji kuambiwa wanakaya wote watatu wamefariki, wakati ukweli ulikuwa kuwa walikuwa wanaishi sehemu ingine ya kijiji. Peleleza kwa kina na majirani mbali mbali na wanafamilia wengine wanaoishi nje ya kaya kabla hujafanya majumuisho kuwa wanakaya wote wamefariki.

1. Jaza Fomu ya T-0 kwa kumhoji mwenyekiti wa mtaa/kijiji au mtoa taarifa mwengine wa uhakika.

## V. Dodoso la Jamii

# Utangulizi

---

Dodoso la Jamii linakusanya taarifa ambazo kaya zote katika jamii hiyo inahusika nazo. Dodoso hili linapaswa kuhojiwa muda ule ule ambao madodoso mengine ya kaya pia yanahojiwa.

○Jamiiö inatafsiriwa kama **kijiji** katika maeneo ya vijijini na **mtaa** kama EA ipo maeneo ya mjini. Unapaswa kuuliza maswali yaliyopo kwenye dodoso hili kwa viongozi mbali mbali wa kijiji/mtaa. Katika maeneo ya vijijini miongoni mwa viongozi hawa watakuwa mwenyekiti wa kijiji na mtendaji wa kijiji (VEO), na pia viongozi wengine wa baraza la kijiji. Katika maeneo ya mijini unapaswa kumhoji mwenyekiti wa mtaa na pengine viongozi wengine wa mtaa. Katika maeneo yote ya mjini na vijijini utapaswa kumhoji mtendaji wa kijiji au mtaa.

## Sehemu CB: Upatikanaji wa Huduma Muhimu

---

**Swali la 1:** Kwa kila huduma ilioorodheshwa (a-x; aa-ag), ulizia kama inapatikana katika jamii hiyo. Andika gharama za usafiri kwa usafiri wa umma kutoka katikati ya mtaa/kijijini kwenda sehemu inakopatikana huduma katika shilingi za kitanzania katika **swali la 2**. **Swali la 3**, andika umbali katika kilomita kutoka katikati ya mtaa/kijijini kwenda sehemu inakopatikana huduma. Mwisho andika jina la mto huduma/taasisi katika **swali la 4**.

## Sehemu CC: Miradi ya Uwekezaji

---

Katika **swali la 1**, kwa kila mradi ulioorodheshwa (*a-n*) uliza ili ufahamu kama mradi huo ulitekelezwa katika mwaka 2013 au 2014. Hakikisha kuwa hii ni jumla ya fedha kwa ajili ya mradi husika katika **swali la 2**. Hakikisha kiasi cha fedha kilichochangwa na wanajamii kwa mradi husika katika **swali la 3** na jinsi fedha hizo zilivyochangishwa kwa wanajamii katika **swali la 4**. Kama fedha zilipatikana kutoka kwenye mpango/taasisi yoyote ilioorodhesha kwenye kisanduku cha mageresho, zungushia duara geresho linalohusika katika **swali la 5**.

## Sehemu CD: Matumizi ya Ardhi

---

Katika **swali 1**, andika kiasi cha ekari za ardhi na asilimia ya ardhi yote inayotumika kwa kila kipengele kilichoordheshwa. Kwa **swali la 2** na **la 3**, uliza kama kijiji kina hati za ardhi za kijiji na kama ni hivyo ni lini hati ilitolewa. **Maswali ya 4-7** yanuhusu matukio makubwa ya ardhi. Uliza kama matukio yoyote yaliyoorodheshwa yalitokea na kama ni hivyo ni lini yalitokea. Andika IDADI ya kaya zilizoathirika na matukio na kiasi cha fedha kilicholipwa kama fidia kaya zote zilizoathirika na matukio.

# **Sehemu CE: Demografia, Ardhi na Mifugo Kilimo**

---

Andika idadi, wanachama, na shughuli za vikundi vyovyothe vya ushirika vya wakulima ambavyo vipo katika jamii husika katika **swali la 1-4**. Katika **swali la 5-8**, andika uwepo na bei za mbegu za mahindi zilizoboreshwa ndani na nje ya kijiji. Katika **swali la 9 na 10**, andika idadi ya kaya ambazo zimehamia katika jamii au zimehamia kutoka katika jamii husika katika kipindi cha miezi 12 iliyopita. Katika **swali la 11-13**, andika idadi na wanachamawa SACCOS ndani ya jamii husika. Katika **swali la 14-17**, muulize mhojiwa kutoa tathmini ya matokeo juu ya mvua za vuli zilizopita na za masika ya mwaka 2013. Mwisho **swali la 18-21** yanahusiana na uhamaji/uhamishaji wa mifugo.

## **Sehemu CF: Bei za Bidhaa**

---

Katika sehemu hii andika taarifa za bei za bidhaa zilizoorodheshwa kutoka eneo la utafiti na makao makuu ya wilaya. Ikiwa bei za wilayani zimekwisha kuchukuliwa kwenye dodoso lingine la jamii katika wilaya hiyo, unapaswa kuandika utambulisho wa eneo kwenye dodoso hilo juu ya visanduku husika vya bei za bidhaa na kisha nenda sehemu ya bei za kijijini/mtaani. Hakikisha unaonyesha sehemu unayochukulia taarifa za pamoja na kuchukua vipimo vya GPS.

## **Sehemu CG: Vipimo vya Kienyeji**

---

Sehemu hii inataka kupata vipimo vya kienyeji vinavyotumika kupima baadhi ya bidhaa mbali mbali za chakula katika eneo la kazi/kijiji/mtaa na makao makuu ya Wilaya.

## VI. Vipimo Vya GPS

---

# Jinsi ya Kuwasha na Kutumia GPS

## Kupata Vipimo vya Uelekeo

### Vidokezo Muhimu na Njia za Mkato

- Kurudi kwenye Menu kutoka sehemu yoyote, bonyeza kitufe cha **MENU** mara mbili.
- Kuongeza uhai wa betri, zima GPS yako wakati ambapo hutumii eTrex. Punguza kiasi mwanga wa cha skirini (kioo) bonyeza haraka na kuachia kitufe cha kuwashia (POWER).

### Kuweka Betri

Machine ya eTrex inaganya kazi kwa kutumia beri mbili ndogo za  $\pm$ AA $\phi$  (ambazo haziji pamoja na mashine). Tumia betri za Alkaline, NiMH, au Lithium.

1. Ondo a kasha ya betri kwa kuzungusha kibangili cha kubania kwa kiasi cha robo (1/4) mzunguko (mwelekeo wa saa) na vuta mfuniko wa nyuma.
2. Weka betri, ukizingatia mwelekeo sahihi (chanya na hasi).

Toa betri kama huhitaji kutumia mashine kwa miezi kadhaa. Data zilizohifadhiwa haziwezi kupotea kwa kutoa betri.

### Hatua za Kuweka Kamba

1. Weka kitanzi (loop) cha kamba kwenye kisehemu maalumu kwenye kitako cha mashine.
2. Pitisha mkanda kwenye loop na kuvuta kukaza.

### Utumiaji wa e-Trex

#### Vitu vya kufahamu:

- **Uchaguzi** - Sogea sehemu yenyewe kuakisi mwanga kwenye skrini kwenda juu, kushoto au kulia kwa kutumia **ENTER/ROCKER** ili kuchagua sehemu mojawapo.
- **Kitufe (key)** - Unapohitajika kubonyeza kitufe, bonyeza kwa haraka na kiacie.
- **Field** - Ni sehemu ambayo data au maoni yanaweza kuonekana au kuingizwa.
- **On screen button** - Tumia **ENTER/ROCKER** kuchagua kitufe na kasha bonyeza kitufe kuifungua. (**ENTER**)
- **Scroll bar** - Unapotazama orodha ya vitu vingi ambavyo haviwezi kuonekana vyote kwenye skrini, scroll bar inatokea baada ya orodha ya vitu hivyo, bonyeza juu au chini kwenye **ROCKER** au tumia kitufe cha **Ndani na Nje (In and Out)**.
- **Default** – Mpangilio wa vitu kwenye mashine kama ilivyotoka kiwandani umewekwa kwenye kumbu kumbu ya mashine. Unaweza kuubadilisha, na unaweza kuurudisha kwa kuchagua **Restore Defaults**.

#### Taratibu za Kutumia Maelekezo Yaliyotolewa

Katika maelekezo yaliyopo ya namna ya kutumia mashine, unapoelekezwa kuchagua kitu, mshale mdogo utaonekana (>) katika maandishi. Inaashiria kuwa unapaswa ku-highlight vitu katika skrini kwa kutumia **ROCKER**, na ubonyeze  **$\pm$ ENTER** kwa kila kitu unachochagua. Kwa mfano,  $\ddot{\text{u}}$ nachagua **Service>Show Info**,  $\ddot{\text{u}}$ unapaswa ku-highlight Service, na ubonyeza  **$\ddot{\text{o}}\text{ENTER}$** . Then highlight Show Info, na bonyeza  **$\ddot{\text{o}}\text{ENTER}$**  tena.

## Kazi za Vitufe

- **IN/OUT Zoom key** - kutoka kwenye ukurasa wa ramani, bonyeza kukuza ramani ndani au nje.
- **MENU/FIND key** - bonyeza na kuachia kitufe kuangalia machaguo kwenye ukurasa.
- **ENTER/ROCKER key** - chezesha juu au chini au kulia au kushoto kuangalia orodha, highlight fields, on screen button au icons, enter data au move the map panning arrow.
- **QUIT/PAGE key** - bonyeza kurudi kwenye peji ya awali. Bonyeza na shikilia kurudisha compass on au of (Vista HCx and Summit HC only)
- **POWER KEY** - bonyeza na shikilia ukihitaji kuwashia au kuzima. Bonyeza na kuachia kwa kurekebisha mwanga au kuangalia muda,tarehe na uwezo wa betri.

## Kuwasha e-Trex

### Kuwasha na kuzima e-Trex:

Bonyeza na shikilia kitufe cha kuwashia (**POWER**).

## Kubadili Mwanga

### Kubadili kiasi cha mwanga:

1. Bonyeza na achia kwa haraka kitufe cha kuwashia (**POWER**).
2. Bonyeza kwa juu **ROCKER** kuongeza kiasi cha mwanga na kuelekea chini kupunguza mwanga.
3. Bonyeza kitufe cha ðENTERö au ðQUITö kufunga.

## Kuanzisha GPS Receiver

Kwa mara ya kwanza unapowasha e-Trex, GPS yako, GPS receiver lazima kwanza ikusanye data za sateliti na kutambua na kuonyesha mahali ulipo.

Ili kupokea signo za satellite ni lazima uwe nje kwenye anga iliyo wazi (clear).

## The status bar na Tarehe na Muda

Kidirisha cha Status bar na tarehe/muda huonekana chini ya kitufe cha kurekebishi mwanga unapobonyenza na kuachia kitufe cha **POWER**. Nguvu (umeme) kwenye kifaa unatokana na betri au kutoka chanzo saidizi. Hali ya nguvu (power) ya mashine inaonekana kwenye Menu kubwa (Main Menu) na Status Bar. Kialama cha umeme kinaonyesha kiasi cha nguvu iliyobakia kadri betri unavyopungua nguvu, na kialama cha chanzo cha nje cha nguvu kinayooonekana wakati mashine inapopata chaji/nguvu kutoka kifaa kingine cha nje.

Signal za satellite zinaonekana pale ambapo mashine inatafuta signal au inapopata satellite, a2D imepatikana na 3D imepatikana.

## Matumizi ya Msingi

Sehemu hii inaelezea baadhi ya vitu unavyoweza kufanya kwa kutumia e-Trex ikihusisha kutengeneza na kutumia waypoints, kutumia orodha ya vitu (menu) na jinsi ya kutengeneza na kutumia *tracts* na *routes*.

## Kutengeneza na Kutumia Waypoint

Waypoint ni mahali au pointi unazohitaji kurekodi na kuhifadhi katika GPS, unaweza kuongeza waypoint Kwa njia “*routes*” na hata kutengeneza njia ya mkato ya kwenda moja kwa moja kwenye waypoint iliyochaguliwa.

Unaweza kutengeneza waypoints kwa kutumia njia tatu. Bonyeza kitufe cha õENTERö unapokuwa katika hiyo sehemu, tengeneza waypoint kwenye ukurasa wa ramani, au ingiza pointi (coordinates) za waypoint wewe mwenyewe (manually) mpya na bonyeza õENTERö

## Kutumia Njia/Track

Sehemu ya njia/track hutengeneza ramani ya njia õtrack log” kwenye ukurasa wa ramani kadri unavyotembea. Hii track long ina taarifa zinazohusu points kwa sehemu ulizotembea.

Track long inaanza kurekodi mapema pale tu kifaa kitakapopata mahali, asilimia ya kumbukubuku

Track log inaanza kurekodi mara tuyotumika kwenye õcurrent track longö hutokea juu ya tracks page.

### Kufuta track log

1. Bonyeza õMENUö mara mbili ili kufungua main menu.
2. Chagua õTRACKSö
3. Chagua kitufe cha õCLEARö. Ujumbe wa udhibitisho utatokea.

### Kupata track log

1. Bonyeza õMENUö mara mbili> TRACK
2. Chagua õSETUPö
  - a. “**Wrap When Full**” ótrack log itaweka kumbukumbu za sasa na kufuta data za zamani.
  - b. “**Record Method**” ó distance records track points after a specified distance is traveled. Time creates track points after a specified time has elapsed. Auto (inayoshauriwa) inakuruhusu kuchagua kutoka kwenye vipindi →intervalsøtano.

### Kuhifadhi track log yote

1. Bonyeza õMENUö mara mbili> TRACK
2. Chagua õSAVEö ujumbe utatokea kukuuliza kama unahitaji kuhifadhi enter track
3. Chagua ndiyo kuhifadhi →trackø

### Kuhifadhi sehemu ya track log:

1. Bonyeza MENU mara mbili >**Tracks**.
2. Chagua õSave”.
3. Chagua õNo” ili kuhifadhi sehemu tu ya track log.
4. Tumia **ROCKER** kusogeza pointer kwenye point katika mstari wa õtrackö ambapo unataka pawe pointi ya kuanzia, na bonyeza **ENTER**.
5. Rudia ili kuchagua pointi ya kumalizia. Chagua **OK**.

### Kuangalia track kwenye ramani

Kwenye track uliyoihifadhi, chagua ramani, ramani itaonyesha track/njia nzima ulipoanzia Hadi ulipoishia na waypoints zitaonekana kwenye track.

### Kukokotoa eneo la track

1. Kwenye ukurasa wa track long fungua track on, bonyeza õMENUö
2. Chaguaa õkokotoa eneoö na bonyeza õENTERö
3. Bonyeza õENTERö kuanza kukokotoa eneo, kadri unavyozidi kutembea unatambua mipakana kitufe cha õSTOPö kitaonekana kwenye ukurasa.
4. Ukimaliza kutambua eneo, bonyeza õENTERö na chagua hifadhi/SAVE.

# Jinsi ya Kuandika Majina ya Faili Kwenye GPS

Ni muhimu kwa namba/tarakimu za GPS na za mashamba zipewe majina yenyе kufanana ili mtaalam aweze kuziweka hizo  $\Rightarrow$  point $\circ$  kwenye ramani.  $\Rightarrow$ Mafaili $\circ$  haya yanahitaji kuwa na majina ya kipekee ili kuweza kutambua zinafanana na kaya zipi. Katika utafiti uliopita tulitumia utambulisho wa kaya , lakini namba zimekuwa nyingi na kufanya utambulisho kuwa mrefu sana kuutumia tena kwa mwaka wa tatu, badala ya kutumia utambulisho huu mrefu ,sasa tutatumia utambulisho mfupi ambao badea utalinganishwa na ule wa awali wenyе tarakimu nyingi. Kama ilivyokuwa awali ni muhimu kunakili namba kwa umakini kama zilivyoandikwa ili iwe rahisi katika kulinganisha.

Kuna aina mbili za kaya ambazo tunahitaji kuzipa majina katika mafaili ya GPS ó Kaya za awali na kaya zilizogawanyika

**Kaya za awali:** Katika kaya za awali tunatumia namba za kaya za awali kutoka kwenye fomu ya T-0 (ambayo utakuwa umeinakili kwenye ukurasa wa mwanzo wa utambulisho wa dodoso na  $\approx$ 00 $\circ$  kuonyesha kuwa ni kaya ya awali. Mfano huu hapo chini unaonyesha namba ya kaya ya awali 1471, kwa kuwa ni kaya ya awali unaongeza  $\approx$ 00 $\circ$  kwa hiyo itakuwa 147100. Kutoka katika namba hiyo utanaongeza utambulisho kwenye GPS

 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ofisi ya Taifa ya Takwimu		SIRI
UTAFITI WA KUFUATILIA KAYA TANZANIA (NPS 2012/2013) UTAHTI HUU UNAFANYWA KWA KUZINGATIA SHERIA NAMBA I YA TAKWIMU YA MWAKA 2002 TAARIFA HIZI NI SIRI NA ZITATUMIKA KITAUKWIMU TU		
DODOSO LA TAARIFA ZA KAYA, MAPATO NA MATUMIZI (NPS - HhQ)		
SEHEMU A-1: UTAMBULISHO WA KAYA		
1. MKOA:	GERESHO	JINA
2. MILAYA:	0   1	Dodoma
3. KATASHEHIA:	4	Dodoma rural
4. KUJI / ENEO LA KUHESABIA:	1   2   1	
5. KITONGOJI / MTAAL:	0   0   6	
7. NANBA YA KAYA (ORODHA):	1   4   7   1	ANDIKA X' KATIKA CHUMBA NA IDADI YA FOMU HAPO CHINI IVAPO UTATUMA FOMU ZADI YA HII KUANDIKA TAARIFA ZA KAYA. HAKIKISHA UNAANDIKA VIVYO HIYO KWENYE FOMU ZOTE ZITAKAZOTUMIKA KWAKAYA HII.
8. JINA LA MKUU WAKAYA:		FOMU YA _____ KATI YA
9. JINA LA MKUU WAKAYA KUTOKA NPS MWAKA WA 2:		JUMLA YA FOMU _____
10. UTAMBULISHO WA KAYA KUTOKA NPS MWAKA WA 2:	1	
11. KAYA HIT:	KAYA ILE ILE, ..... NI KAYA ILLIYOGAWANYIKA, .....	0   1   0   4   0   1   2   0   0   6   0   0   2   3   0   1
12. MAHALI KAYA ILIPO:	IPO KATIKA ENEO LA AWALI ..... NI KAYA YA KUFUATILIA NIANI YA ENEO ..... NI KAYA YA KUFUATILIA MBALI NA ENEO ..... ILIPEKUZA AWALI ..... .....	15   1
13. JINA LA ANAYEFUATILWA:		
14. ROSTER ID YA ANAYEFUATILWA KUTOKA NPS MWAKA WA 2:		

utakayoirekodi. Mfano kama unanakili namba za GPS za kaya utaandika 147100\_HH, na kama unaandika namba za shamba M1 ,faili yake utalipa jina la 147100\_M1 katika hali hii itakuwa rahisi kuoanisha namba kwenye dodoso husika, kumbuka kuangalia kuwa kaya ni ya awali na sio kaya iliyogawanyika kabla ya kutumia namba  $\approx$ 00 $\circ$

**Kaya zilizogawanyika:** hii kidogo inachaganya kwani kaya inaweza kuwa imegawanyika na kutoa kaya mpya nyingi yaani kaya zaidi ya moja, katika kaya zilizogawanyika badala ya kutumia namba -00øbaada ya zile tarakimu nne za mwanzo, utatumia namba ya utambulisho ya mwanakaya anayefuatiiliwa.

 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ofisi ya Taifa ya Takwimu	<b>SIRI</b>  <b>UTAFITI WA KUFUATILIA KAYA TANZANIA (NPS 2012/2013)</b> <small>UTAFITI HU UNAFANYWA KW A KUZINGATIA SHERIA NAMBA 1 YA TAKWIMU YA MWAKA 2002 TAARIFA HIZI NI SHI NA ZITATUMIKA KITAKWIMU TU</small> <b>DODOSO LA TAARIFA ZA KAYA, MAPATO NA MATUMIZI (NPS - HHQ)</b>																																																																											
<b>SEHEMU A-1:UTAMBULISHO WA KAYA</b> <table border="1" style="width: 100%; border-collapse: collapse;"> <tr> <td style="width: 30%;">GERESHO</td> <td style="width: 30%;">JINA</td> <td style="width: 40%;">ANDIKA X' KATIKA CHUMBA NA IDADI YA FOMU HAPO CHINI IWAPO UTATUMIA FOMU ZADI YA HII KUANDIKA TAARIFA ZA KAYA. HAKIKISHA UNAANDIKA VIVYO HIVO KWENYE FOMU ZOTE ZITAKAZOTUMKA KWA KAYA HII.</td> </tr> <tr> <td>1. MKOA: <table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>0</td><td>1</td></tr></table></td> <td>Dodoma ----- Dodoma rural -----</td> <td><input type="checkbox"/></td> </tr> <tr> <td>2. WILAYA: <table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>4</td></tr></table></td> <td></td> <td></td> </tr> <tr> <td>3. KATA'SHEHIA: <table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>1</td><td>2</td><td>1</td></tr></table></td> <td></td> <td></td> </tr> <tr> <td>4. KUJU/ENEO LA KUHESABIA: <table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>0</td><td>0</td><td>6</td></tr></table></td> <td></td> <td></td> </tr> <tr> <td>5. KITONGOJI / MTAAS:</td> <td></td> <td></td> </tr> <tr> <td>7. NAMBA YA KAYA (ORODHA): <table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>1</td><td>4</td><td>7</td><td>1</td></tr></table></td> <td></td> <td>FOMU YA ____ KATI YA JUMLA YA FOMU _____</td> </tr> <tr> <td>8. JINA LA MKUU WA KAYA:</td> <td></td> <td></td> </tr> <tr> <td>9. JINA LA MKUU WA KAYA KUTOKA NPS MWAKA WA 2:</td> <td></td> <td></td> </tr> <tr> <td>10. UTAMBULISHO WA KAYA KUTOKA NPS MWAKA WA 2: <small>KAYA ILE ILE.....1 NI KAYA ILIYOGAWANYIKA...2</small></td> <td><table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>0</td><td>1</td><td>0</td><td>4</td><td>0</td><td>1</td><td>2</td><td>0</td><td>0</td><td>6</td><td>0</td><td>0</td><td>2</td><td>3</td><td>0</td><td>1</td></tr></table></td> <td></td> </tr> <tr> <td>11. KAYA HII:</td> <td><table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>2</td></tr></table></td> <td></td> </tr> <tr> <td>12. MAHALI KAYA ILIPO: <small>IPO KATIKA ENEO LA AWALI.....1 NI KAYA YA KUFUATILIA NDANI YA ENEO LILE LILE.....2 NI KAYA YA KUFUATILIA MEALI YA ENEO LILI POMBA AWALI.....3</small></td> <td><table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>2</td></tr></table></td> <td></td> </tr> <tr> <td>13. JINA LA ANAYEFUATILIWA:</td> <td>Juma Ally ----- Juma Hassan -----</td> <td></td> </tr> <tr> <td>14. ROSTER ID YA ANAEFATILIWA KUTOKA NPS MWAKA WA 2:</td> <td><table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>0</td><td>3</td></tr></table></td> <td></td> </tr> </table>		GERESHO	JINA	ANDIKA X' KATIKA CHUMBA NA IDADI YA FOMU HAPO CHINI IWAPO UTATUMIA FOMU ZADI YA HII KUANDIKA TAARIFA ZA KAYA. HAKIKISHA UNAANDIKA VIVYO HIVO KWENYE FOMU ZOTE ZITAKAZOTUMKA KWA KAYA HII.	1. MKOA: <table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>0</td><td>1</td></tr></table>	0	1	Dodoma ----- Dodoma rural -----	<input type="checkbox"/>	2. WILAYA: <table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>4</td></tr></table>	4			3. KATA'SHEHIA: <table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>1</td><td>2</td><td>1</td></tr></table>	1	2	1			4. KUJU/ENEO LA KUHESABIA: <table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>0</td><td>0</td><td>6</td></tr></table>	0	0	6			5. KITONGOJI / MTAAS:			7. NAMBA YA KAYA (ORODHA): <table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>1</td><td>4</td><td>7</td><td>1</td></tr></table>	1	4	7	1		FOMU YA ____ KATI YA JUMLA YA FOMU _____	8. JINA LA MKUU WA KAYA:			9. JINA LA MKUU WA KAYA KUTOKA NPS MWAKA WA 2:			10. UTAMBULISHO WA KAYA KUTOKA NPS MWAKA WA 2: <small>KAYA ILE ILE.....1 NI KAYA ILIYOGAWANYIKA...2</small>	<table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>0</td><td>1</td><td>0</td><td>4</td><td>0</td><td>1</td><td>2</td><td>0</td><td>0</td><td>6</td><td>0</td><td>0</td><td>2</td><td>3</td><td>0</td><td>1</td></tr></table>	0	1	0	4	0	1	2	0	0	6	0	0	2	3	0	1		11. KAYA HII:	<table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>2</td></tr></table>	2		12. MAHALI KAYA ILIPO: <small>IPO KATIKA ENEO LA AWALI.....1 NI KAYA YA KUFUATILIA NDANI YA ENEO LILE LILE.....2 NI KAYA YA KUFUATILIA MEALI YA ENEO LILI POMBA AWALI.....3</small>	<table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>2</td></tr></table>	2		13. JINA LA ANAYEFUATILIWA:	Juma Ally ----- Juma Hassan -----		14. ROSTER ID YA ANAEFATILIWA KUTOKA NPS MWAKA WA 2:	<table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>0</td><td>3</td></tr></table>	0	3	
GERESHO	JINA	ANDIKA X' KATIKA CHUMBA NA IDADI YA FOMU HAPO CHINI IWAPO UTATUMIA FOMU ZADI YA HII KUANDIKA TAARIFA ZA KAYA. HAKIKISHA UNAANDIKA VIVYO HIVO KWENYE FOMU ZOTE ZITAKAZOTUMKA KWA KAYA HII.																																																																										
1. MKOA: <table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>0</td><td>1</td></tr></table>	0	1	Dodoma ----- Dodoma rural -----	<input type="checkbox"/>																																																																								
0	1																																																																											
2. WILAYA: <table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>4</td></tr></table>	4																																																																											
4																																																																												
3. KATA'SHEHIA: <table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>1</td><td>2</td><td>1</td></tr></table>	1	2	1																																																																									
1	2	1																																																																										
4. KUJU/ENEO LA KUHESABIA: <table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>0</td><td>0</td><td>6</td></tr></table>	0	0	6																																																																									
0	0	6																																																																										
5. KITONGOJI / MTAAS:																																																																												
7. NAMBA YA KAYA (ORODHA): <table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>1</td><td>4</td><td>7</td><td>1</td></tr></table>	1	4	7	1		FOMU YA ____ KATI YA JUMLA YA FOMU _____																																																																						
1	4	7	1																																																																									
8. JINA LA MKUU WA KAYA:																																																																												
9. JINA LA MKUU WA KAYA KUTOKA NPS MWAKA WA 2:																																																																												
10. UTAMBULISHO WA KAYA KUTOKA NPS MWAKA WA 2: <small>KAYA ILE ILE.....1 NI KAYA ILIYOGAWANYIKA...2</small>	<table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>0</td><td>1</td><td>0</td><td>4</td><td>0</td><td>1</td><td>2</td><td>0</td><td>0</td><td>6</td><td>0</td><td>0</td><td>2</td><td>3</td><td>0</td><td>1</td></tr></table>	0	1	0	4	0	1	2	0	0	6	0	0	2	3	0	1																																																											
0	1	0	4	0	1	2	0	0	6	0	0	2	3	0	1																																																													
11. KAYA HII:	<table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>2</td></tr></table>	2																																																																										
2																																																																												
12. MAHALI KAYA ILIPO: <small>IPO KATIKA ENEO LA AWALI.....1 NI KAYA YA KUFUATILIA NDANI YA ENEO LILE LILE.....2 NI KAYA YA KUFUATILIA MEALI YA ENEO LILI POMBA AWALI.....3</small>	<table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>2</td></tr></table>	2																																																																										
2																																																																												
13. JINA LA ANAYEFUATILIWA:	Juma Ally ----- Juma Hassan -----																																																																											
14. ROSTER ID YA ANAEFATILIWA KUTOKA NPS MWAKA WA 2:	<table border="1" style="display: inline-table;"><tr><td>0</td><td>3</td></tr></table>	0	3																																																																									
0	3																																																																											

Katika mfano huu, kijana ameondoka na kuanzisha kaya mpya. Namba yake ya kaya toka katika utafiti uliopita ni -03ø na imeshaandikwa katika mstari wa mwisho wa sehemu ya utambulisho wa dodoso, bado utatumia tarakimu nne kama kawaida lakini badala ya kuandika -00ø utandika namba ya mwanakaya aliyerema kwa kuwa ni kaya iliyogawanyika, kwahiyoo itakuwa 1471 ikifuatiwa na namba ya kaya ya Hassani -03øitakuwa 147103 itakuwa ndiyo jina la faili. Kwahiyoo point za kaya zitaandikwa 147103\_HH na shamba itakuwa 147103\_M1.

## VII. Viambatanishi

---

# Mageresho ya TASCO

---

*Kwa Sehemu E, Maswali 16, 31, na 45:*

## **MAJOR GROUP 1: LEGISLATORS, ADMINISTRATORS AND MANAGERS**

### 11 LEGISLATORS AND ADMINISTRATORS

111 LEGISLATORS

112 SENIOR GOVERNMENT EXECUTIVE

113 VILLAGE LEADERS

114 SENIOR ADMINISTRATORS OF SPECIAL-INTEREST ORGANISATIONS

### 12 COMPANY DIRECTORS AND CORPORATE MANAGERS

121 COMPANY DIRECTORS AND NON-GOVERNMENT CHIEF EXECUTIVES

122 SPECIALISED MANAGERS AND SENIOR ADMINISTRATORS

123 PRODUCTION AND OPERATIONS MANAGERS AND SENIOR ADMINISTRATORS

### 13 SMALL BUSINESS MANAGERS AND MANAGING SUPERVISORS

131 SMALL BUSINESS MANAGERS AND MANAGING SUPERVISORS

## **MAJOR GROUP 2: PROFESSIONALS**

### 21 PHYSICAL, MATHEMATICAL AND ENGINEERING SCIENCE PROFESSIONALS

211 PHYSICAL SCIENTISTS AND RELATED PROFESSIONALS

212 MATHEMATICIANS, STATISTICIANS AND RELATED PROFESSIONALS

213 COMPUTING PROFESSIONALS

214 ARCHITECTS, ENGINEERS AND RELATED PROFESSIONALS

### 22 LIFE SCIENCE AND HEALTH PROFESSIONALS

221 LIFE SCIENCE PROFESSIONALS

222 MEDICAL AND HEALTH PROFESSIONALS, EXCEPT NURSES

223 NURSING PROFESSIONALS

### 23 TEACHING PROFESSIONALS

231 COLLEGE, UNIVERSITY AND HIGHER EDUCATION TEACHING PROFESSIONALS

232 SECONDARY EDUCATION TEACHING PROFESSIONALS

239 OTHER TEACHING AND RELATED PROFESSIONALS

### 24 OTHER PROFESSIONALS

241 BUSINESS AND ADMINISTRATIVE PROFESSIONALS

242 LEGAL PROFESSIONALS

243 ARCHIVISTS, LIBRARIANS AND RELATED INFORMATION PROFESSIONALS

244 SOCIAL AND RELATED SCIENCE PROFESSIONALS

245 ARTISTIC PROFESSIONALS

246 RELIGIOUS PROFESSIONALS

## **MAJOR GROUP 3: TECHNICIANS AND RELATED PROFESSIONALS**

### 31 PHYSICAL, MATHEMATICAL AND ENGINEERING SCIENCE ASSOCIATE PROFESSIONALS

311 PHYSICAL SCIENCE AND ENGINEERING TECHNICIANS

312 COMPUTER ASSISTANTS AND EQUIPMENT CONTROLLERS

313 OPTICAL AND ELECTRONIC EQUIPMENT CONTROLLERS

314 SHIP AND AIRCRAFT CONTROLLERS AND TECHNICIANS

315 BUILDING, SAFETY, HEALTH AND QUALITY INSPECTORS

### 32 LIFE SCIENCE AND HEALTH ASSOCIATE PROFESSIONALS

321 LIFE SCIENCE TECHNICIANS AND RELATED WORKERS

322 MODERN MEDICINE AND HEALTH ASSOCIATE PROFESSIONALS (EXCEPT NURSES)

323 NURSING AND MIDWIFERY ASSOCIATE PROFESSIONALS

324 TRADITIONAL MEDICINE PRACTITIONERS AND FAITH HEALERS

### 33 TEACHING ASSOCIATE PROFESSIONALS

- 331 SECONDARY EDUCATION TEACHERS, ASSOCIATE PROFESSIONALS
- 332 TECHNICAL/VOCATIONAL EDUCATION TEACHERS
- 333 PRIMARY EDUCATION TEACHERS
- 334 PRE-PRIMARY EDUCATION TEACHERS
- 335 SPECIAL EDUCATION TEACHERS, ASSOCIATE PROFESSIONALS
- 339 OTHER TEACHING ASSOCIATE PROFESSIONALS
- 34 OTHER ASSOCIATE PROFESSIONALS
  - 341 FINANCE AND SALES ASSOCIATE PROFESSIONALS
  - 342 TRADE BROKERS AND BUSINESS SERVICES AGENTS
  - 343 ADMINISTRATIVE ASSOCIATE PROFESSIONALS
  - 344 GOVERNMENT ASSOCIATE PROFESSIONALS
  - 345 SOCIAL WORK ASSOCIATE PROFESSIONALS
  - 346 CREATIVE AND PERFORMING ART, AND ARTISTIC ENTERTAINMENT, AND SPORTS ASSOCIATE PROFESSIONALS
  - 347 RELIGIOUS ASSOCIATE PROFESSIONALS
  - 348 OTHER ASSOCIATE PROFESSIONALS

#### **MAJOR GROUP 4: CLERKS**

- 41 OFFICE CLERKS
  - 411 SECRETARIES, KEYBOARD OPERATORS AND REGISTRY ASSISTANTS
  - 412 NUMERICAL CLERKS
  - 413 MATERIAL RECORDING AND TRANSPORT CLERKS
  - 414 LIBRARY, MAIL AND RELATED CLERKS
  - 415 OTHER OFFICE CLERKS
- 42 CUSTOMER SERVICE CLERKS
  - 421 CASHIERS, TELLERS AND RELATED CLERKS
  - 422 CLIENT INFORMATION CLERKS AND TELEPHONE OPERATORS

#### **MAJOR GROUP 5: SERVICE WORKERS AND SHOP SALES WORKERS**

- 51 PERSONAL SERVICE WORKERS
  - 511 TRAVEL ATTENDANTS AND GUIDES
  - 512 HOUSEKEEPING AND RESTAURANT SERVICES WORKERS, INSTITUTIONAL
  - 513 HOUSEKEEPING AND RELATED SERVICE WORKERS, DOMESTIC
  - 514 PERSONAL CARE WORKERS
  - 515 ASTROLOGERS, FORTUNE-TELLERS AND RELATED WORKERS
  - 516 OTHER PERSONAL SERVICE WORKERS
- 52 PROTECTIVE SERVICE WORKERS
  - 520 PROTECTIVE SERVICE WORKERS
  - 53 SALESPERSONS, DEMONSTRATORS AND MODELS
    - 531 SALESPERSONS AND DEMONSTRATORS
    - 532 STALL AND MARKET SALESPERSONS
    - 533 FASHION AND OTHER MODELS

#### **MAJOR GROUP 6: SKILLED AGRICULTURAL AND FISHERY WORKERS**

- 61 SKILLED AGRICULTURAL AND FISHERY WORKERS
  - 611 FARMERS AND CROP SKILLED WORKERS
  - 612 ANIMAL PRODUCERS AND SKILLED WORKERS
  - 613 FORESTRY AND RELATED SKILLED WORKERS
  - 614 FISHERY WORKERS, HUNTERS AND TRAPPERS
- 62 SUBSISTENCE AGRICULTURAL, FORESTRY, FISHERY AND RELATED WORKERS
  - 621 SUBSISTENCE AGRICULTURAL, FORESTRY, FISHERY AND RELATED WORKERS

#### **MAJOR GROUP 7: CRAFT AND RELATED WORKERS**

- 71 EXTRACTION AND BUILDING TRADES WORKERS

- 711 MINERS AND BLASTERS, STONE CUTTERS AND CARVERS
- 712 BUILDING FRAME AND RELATED TRADES WORKERS
- 713 BUILDING FINISHERS AND RELATED TRADES WORKERS
- 714 PAINTERS, STRUCTURAL CLEANERS AND RELATED WORKERS
- 72 METAL AND MACHINERY TRADES WORKERS
  - 721 METAL MOULDERS, WELDERS, SHEET - METAL WORKERS AND STRUCTURAL METAL PREPARERS AND RELATED WORKERS
  - 722 BLACKSMITHS, TOOLMAKERS AND RELATED WORKERS
  - 723 MACHINERY MECHANICS AND FITTERS
  - 724 ELECTRICAL AND ELECTRONIC EQUIPMENT FITTERS, INSTALLERS AND REPAIRERS
- 73 PRECISION, HANDICRAFT, PRINTING AND RELATED TRADES WORKERS
  - 731 PRECISION WORKERS IN METAL, DIAMONDS, PLASTICS, RUBBER, PAPER AND OTHER RELATED MATERIALS
  - 732 POTTERS, GLASS FORMERS AND RELATED WORKERS
  - 734 HANDICRAFT WORKERS IN WOOD, TEXTILE, LEATHER AND RELATED MATERIALS
  - 735 PRINTING AND RELATED TRADES WORKERS
- 74 OTHER CRAFTS AND RELATED TRADES WORKERS
  - 741 FOOD AND RELATED PRODUCTS PROCESSING TRADES WORKERS
  - 742 CABINET MAKERS, WOOD TREATERS AND
  - 743 RELATED TRADES WORKERS TEXTILE AND GARMENT TRADES
  - 744 WORKERS PELT, LEATHER AND SHOEMAKING TRADES
  - 749 WORKERS OTHER CRAFT AND RELATED TRADES WORKERS, NEC

#### **MAJOR GROUP 8: PLANT AND MACHINE OPERATORS AND ASSEMBLERS**

- 81 INDUSTRIAL PLANT OPERATORS
  - 811 MINING AND MINERAL-PROCESSING PLANT OPERATORS
  - 812 METAL-PROCESSING PLANT OPERATORS
  - 813 GLASS AND CERAMICS KILN AND RELATED PLANT OPERATORS
  - 814 WOOD-PROCESSING AND PAPERMAKING PLANT OPERATORS
  - 815 CHEMICAL-PROCESSING PLANT OPERATORS
  - 816 POWER-GENERATING AND RELATED PLANT OPERATORS
- 82 STATIONARY MACHINE OPERATORS AND ASSEMBLERS
  - 821 METAL AND MINERAL PRODUCTS PROCESSING MACHINE OPERATORS
  - 822 CHEMICAL PRODUCTS MACHINE OPERATORS
  - 823 RUBBER, PLASTICS AND LEATHER PRODUCTS MACHINE OPERATORS
  - 824 WOOD PRODUCTS MACHINE OPERATORS
  - 825 PRINTING, BINDING AND PAPER PRODUCTS MACHINE OPERATORS
  - 826 TEXTILE PRODUCTS MACHINE OPERATORS
  - 827 FOOD AND RELATED PRODUCTS PROCESSING MACHINE OPERATORS
  - 828 ASSEMBLERS
  - 829 OTHER STATIONARY MACHINE OPERATORS AND ASSEMBLERS
- 83 DRIVERS AND MOBILE MACHINERY OPERATORS
  - 831 RAILWAY ENGINE DRIVERS AND RELATED WORKERS
  - 832 MOTOR VEHICLE DRIVERS AND RIDERS
  - 833 AGRICULTURAL, EARTHMOVING, LIFTING AND OTHER MOBILE MATERIALS-HANDLING EQUIPMENT OPERATORS
  - 834 SHIPS DECK CREWS AND RELATED WORKERS

#### **MAJOR GROUP 9: ELEMENTARY OCCUPATIONS**

- 91 SALES AND SERVICES ELEMENTARY OCCUPATIONS
  - 911 STREET VENDORS AND RELATED WORKERS
  - 912 SHOE CLEANING AND OTHER STREET SERVICES ELEMENTARY OCCUPATIONS

913 DOMESTIC HELPERS AND CLEANERS AND RELATED WORKERS  
914 BUILDING CARETAKERS AND WINDOW CLEANERS  
915 MESSENGERS, WATCHERS AND RELATED WORKERS  
916 GARBAGE COLLECTORS AND RELATED LABOURERS  
919 OTHER SALES AND SERVICES ELEMENTARY OCCUPATIONS  
92 AGRICULTURAL, FORESTRY FISHERY AND RELATED LABOURERS  
    921 AGRICULTURAL, FORESTRY AND FISHERY LABOURERS  
    93 LABOURERS IN MINING, CONSTRUCTION, MANUFACTURING AND TRANSPORT  
        931 MINING AND CONSTRUCTION LABOURER  
        932 MANUFACTURING LABOURERS  
        933 TRANSPORT LABOURERS  
        934 HAND PACKERS, WEIGHERS AND RELATED ELEMENTARY WORKERS

**MAJOR GROUP 0: DEFENCE FORCES**

01 DEFENCE FORCES  
    011 TANZANIA PEOPLE'S DEFENCE FORCES  
    012 NATIONAL SERVICE (JKT)

**MAJOR GROUP X: WORKERS NOT CLASSIFIED BY OCCUPATIONS**

XI NEW WORKERS SEEKING EMPLOYMENT  
    X11 FRESH GRADUATES AND UNDER-GRADUATES SEEKING EMPLOYMENT  
    X12 FRESH SECONDARY SCHOOL LEAVERS AND DROPOUTS SEEKING EMPLOYMENT  
    X13 FRESH PRIMARY SCHOOL LEAVERS AND DROPOUTS SEEKING EMPLOYMENT  
    X14 FRESH LITERATES SEEKING EMPLOYMENT  
X2 WORKERS REPORTING OCCUPATIONS UNIDENTIFIABLE OR INADEQUATELY DESCRIBED  
    X21 WORKERS REPORTING OCCUPATIONS UNIDENTIFIABLE OR INADEQUATELY DESCRIBED  
X3 WORKERS NOT REPORTING ANY OCCUPATION  
    X31 WORKERS NOT REPORTING ANY OCCUPATION

# Mageresho ya ISIC

---

Mageresho yafuatayo yanapaswa kujazwa katika Swali la 24 katika sehemu E ya dodoso la kaya.

Mageresho haya yanapaswa kujazwa na msimamizi baada ya kumalizika mahojiano. Majibu yanaweza kuwa katika tarakimu 2 au 3. Inapohusu tumia tarakimu 3 kwa ajili ya maelezo ya kina. Vipengele vinavyotumika mara kwa mara vimekolezwa wino kwa ajili ya urahisi wa kutumia.

## ISIC Codes (Rev. 4) for Section E, Questions 13 & 24

### A - Agriculture, forestry and fishing

- 01 - Crop and animal production, hunting and related service activities
- 02 - Forestry and logging
- 03 - Fishing and aquaculture

### B - Mining and quarrying

- 05 - Mining of coal and lignite
- 06 - Extraction of crude petroleum and natural gas
- 07 - Mining of metal ores
- 08 - Other mining and quarrying
- 09 - Mining support service activities

### C ó Manufacturing

- 10 - Manufacture of food products
  - 101 ó Processing and preserving of meat
  - 102 – Processing and preserving of fish, crustaceans and mollusks**
  - 103 ó Processing and preserving of fruit and vegetables
  - 104 - Manufacture of vegetable and animal oils and fats
  - 105 - Manufacture of dairy products
  - 106 - Manufacture of grain mill products, starches and starch products**
  - 107 - Manufacture of other food products
  - 108 - Manufacture of prepared animal feeds
- 11 - Manufacture of beverages
- 12 - Manufacture of tobacco products
- 13 - Manufacture of textiles
- 14 - Manufacture of wearing apparel**
- 15 - Manufacture of leather and related products
- 16 - Manufacture of wood and of products of wood and cork, except furniture; manufacture of articles of straw and plaiting materials
- 17 - Manufacture of paper and paper products
- 18 - Printing and reproduction of recorded media
- 19 - Manufacture of coke and refined petroleum products
- 20 - Manufacture of chemicals and chemical products
- 21 - Manufacture of basic pharmaceutical products and pharmaceutical preparations
- 22 - Manufacture of rubber and plastics products
- 23 - Manufacture of other non-metallic mineral products
- 24 - Manufacture of basic metals
- 25 - Manufacture of fabricated metal products, except machinery and equipment
- 26 - Manufacture of computer, electronic and optical products
- 27 - Manufacture of electrical equipment
- 28 - Manufacture of machinery and equipment n.e.c.
- 29 - Manufacture of motor vehicles, trailers and semi-trailers
- 30 - Manufacture of other transport equipment
- 31 - Manufacture of furniture**
- 32 - Other manufacturing

- 33 - Repair and installation of machinery and equipment
- D - Electricity, gas, steam and air conditioning supply
  - 35 - Electricity, gas, steam and air conditioning supply
- E - Water supply; sewerage, waste management and remediation activities
  - 36 - Water collection, treatment and supply
  - 37 ó Sewerage
  - 38 - Waste collection, treatment and disposal activities; materials recovery
  - 39 - Remediation activities and other waste management services
- F ó Construction
  - 41 - Construction of buildings
  - 42 - Civil engineering
  - 43 - Specialized construction activities
- G - Wholesale and retail trade; repair of motor vehicles and motorcycles
  - 45 - Wholesale and retail trade and repair of motor vehicles and motorcycles
  - 46 - Wholesale trade, except of motor vehicles and motorcycles
  - 47 - Retail trade, except of motor vehicles and motorcycles
    - 471 - Retail sale in non-specialized stores**
    - 472 - Retail sale of food, beverages and tobacco in specialized stores
    - 473 - Retail sale of automotive fuel in specialized stores
    - 474 - Retail sale of information and communications equipment in specialized stores
    - 475 - Retail sale of other household equipment in specialized stores
    - 476 - Retail sale of cultural and recreation goods in specialized stores
    - 477 - Retail sale of other goods in specialized stores
    - 478 - Retail sale via stalls and markets**
    - 479 - Retail trade not in stores, stalls or markets**
- H - Transportation and storage
  - 49 - Land transport and transport via pipelines
    - 491 - Transport via railways
    - 492 - Other land transport
      - 4921 - Urban and suburban passenger land transport**
      - 4922 - Other passenger land transport**
      - 4923 - Freight transport by road**
    - 493 - Transport via pipeline
  - 50 - Water transport
  - 51 - Air transport
  - 52 - Warehousing and support activities for transportation
  - 53 - Postal and courier activities
- I - Accommodation and food service activities
  - 55 ó Accommodation
  - 56 - Food and beverage service activities
    - 561 - Restaurants and mobile food service activities**
    - 562 - Event catering and other food service activities
    - 563 - Beverage serving activities**
- J - Information and communication
  - 58 - Publishing activities
  - 59 - Motion picture, video and television programme production, sound recording and music publishing activities
  - 60 - Programming and broadcasting activities
  - 61 ó Telecommunications
  - 62 - Computer programming, consultancy and related activities
  - 63 - Information service activities
- K - Financial and insurance activities
  - 64 - Financial service activities, except insurance and pension funding
  - 65 - Insurance, reinsurance and pension funding, except compulsory social security
  - 66 - Activities auxiliary to financial service and insurance activities

- L - Real estate activities
  - 68 - Real estate activities
- M - Professional, scientific and technical activities
  - 69 - Legal and accounting activities
  - 70 - Activities of head offices; management consultancy activities
  - 71 - Architectural and engineering activities; technical testing and analysis
  - 72 - Scientific research and development
  - 73 - Advertising and market research
  - 74 - Other professional, scientific and technical activities
  - 75 - Veterinary activities
- N - Administrative and support service activities
  - 77 - Rental and leasing activities
  - 78 - Employment activities
  - 79 - Travel agency, tour operator, reservation service and related activities
  - 80 - Security and investigation activities
  - 81 - Services to buildings and landscape activities
  - 82 - Office administrative, office support and other business support activities
- O - Public administration and defence; compulsory social security
  - 84 - Public administration and defence; compulsory social security
- P ó Education
  - 85 ó Education
- Q ó Human health and social work activities
  - 86 - Human health activities
  - 87 - Residential care activities
  - 88 - Social work activities without accommodation
- R - Arts, entertainment and recreation
  - 90 - Creative, arts and entertainment activities
  - 91 - Libraries, archives, museums and other cultural activities
  - 92 - Gambling and betting activities
  - 93 - Sports activities and amusement and recreation activities
- S - Other service activities
  - 94 - Activities of membership organizations
  - 95 - Repair of computers and personal and household goods
  - 96 - Other personal service activities
- T - Activities of households as employers; undifferentiated goods- and services-producing activities of households for own use
  - 97 - Activities of households as employers of domestic personnel
  - 98 - Undifferentiated goods- and services-producing activities of private households for own use
- U - Activities of extraterritorial organizations and bodies
  - 99 - Activities of extraterritorial organizations and bodies

# Ubadilishaji wa Vipimo

## Ubadilishaji wa Vipimo vya

### Kimataifa

1 hectare	10,000 sq meters	(100 x 100 meters)
1 hectare	2.47 acres	
1 kilometer	1000 meters	
1 acre	4840 square yards	110 x 44 yards
1 mile	1.61 kilometers	

## Ubadilishaji Vipimo vya Kienyeji

		Kubadilisha kwenda kwenye kilogram		
Geresho la zao	Jina la Zao	Gunia	Kopo	Rumbesi
11	Mahindi	100	18	140
12	Mpunga	75	15	
13	Mtama	100	18	
14	Uwele	100	18	
15	Ulezi	120	20	
16	Ngano	75	15	
17	Shayiri	75	15	
21	Mhogo	60	12	
22	Viazi vitamu	80	16	
23	Viazi ulaya	80	16	
24	Viazi vikuu	80	16	
25	Magimbi	80	16	
26	Vitunguu	80	16	
27	Tangawizi	75	15	

31	Maharage	100	20	
32	Kunde	100	20	
33	Choroko	100	20	
34	Mbaazi	100	20	
35	Dengu	100	20	
36	Njugu mawe	100	20	
41	Alizeti	60	12	
42	Ufuta	100	20	
43	Karanga	50	10	
47	Soya	100	20	
48	Nyonyo	100	20	
75	Nanasi	90	18	
50	Pamba	50	10	
51	Tumbaku	70	14	
52	Pareto	60	12	
62	Jute	50	10	



Kubadilisha kwenda kwenye Kilograms		
<i>Geresho la zao</i>	<i>Jina la zao</i>	<i>Gunia</i>
44	Chikichi	100
45	Nazi	75
46	Korosho	80
86	Kabichi	50
87	Nyanya	90
88	Spinachi	45
89	Karoti	110


90	Pilipili	85
91	Mchicha	50
92	Boga	60
93	Matango	80
94	Bilinganya	70
95	Matikiti maji	80
96	Cauliflower	50
52	Mkonge	130
54	Kahawa	55
55	Chai	60
56	Kakao	60
58	Miwati	90
60	Miwa	120
61	Iliki	100
71	Ndizi	120
72	Parachichi	140
73	Embe	130
74	Papai	100
76	Machungwa	130
77	Madalanzi	120
78	Zabibu	80
79	Mchenza / Tangerine	110
80	Pera	110
81	Matunda damu	110
82	Apples	110
83	Peasi	110
84	Mafyoks	110

# Picha za Aina ya Vyoo

Picha zifuatazo zinaonyesha aina tofauti ya vyoo ambavyo vinazungumziwa katika sehemu ya Makazi, Maji na Usafi.

Choo cha kuvuta (chenye tenki la maji)		
Choo cha kumwaga maji		 (Photo: Anet Anton, Shinyanga)


<p>Choo cha shimo cha kisasa (VIP)</p>	 <p>Unaweza kuona bomba kona ya kushoto juu.</p> <p>(Photo by: EEPCO )</p>	 <p>Unaweza kuona bomba likiwa limefunikwa kwa waya wa kashata wa kuzuia wadudu</p> <p>(Photo: UNICEF)</p>
<p>Choo cha Ekolojia (Ecosan)</p>	 <p>Unaweza kuona milango ya kuondolea kinyesi na kifaa (drum) cha kuchukulia mkojo amba unaelekezwa huko na bomba</p> <p>(Photo: EEPCO)</p>	
<p>Choo cha shimo kilichoboreshw a (sakafu inasafishika)</p>	 <p>(Photo: EEPCO)</p>	 <p>(Photo: EEPCO)</p>


<p>Choo cha shimo kilichoboreshw a (Sakafu inasafishika)</p>	 <p>Sakafu inayosafishika iko ndani</p> <p>(Photo by: EEPSCO )</p>	 <p>(Photo by: EEPSCO)</p>
<p>Choo cha shimo cha kawaida (sakafu isiyosafishika)</p>	 <p>(Photo: WaterAid)</p>	 <p>(Photo: WaterAid)</p> 

	 <p>Shimo la wazi lisilo na mfuniko</p>
	<p>Choo cha shimo kisicho na mfuniko (kisichosakafisha)</p>

## Picha za Namna ya Kuandaa Maji Salama ya Kunywa ya Kaya

Picha zinazofuatia zinaonyesha njia mbali mbali za kuhakikisha kuwa maji yanakuwa salama kwa kunywa ambazo zinazungumziwa katika sehemu ya Makazi, Maji na USafi.

KUCHEMSHA	KUWEKA MADAWA
	
<b>KUTUMIA KICHUJA MAJI</b>	



## Picha za Namna ya Kudhibiti Mmomonyoko wa Udongo / Njia za Uvunaji wa Maji



Matuta



Erosion Control Bunds



Gabions



Vertiver Grass



Water Harvest Bunds



Drainage Ditches

## Picha za Aina ya Visima(Tubewell/Borehole)



Tubewell



Borehole

## Nembo za urutubishaji



